# UKWELI KUHUSU MALAIKA



Ellen White

**Uhamishoni. Ughaibuni .**
**Mtandaoni .Majumbani.**

# Enendeni Mitandaoni Kote

Mwito kwa Mpendwa Msomaji

Jiunge na darasa la Uandishi, Ukalimani, Kutafsiri na Uhariri WhatsApp!

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu , ushauri, na kisha Maombi yako msomaji. Kumbuka pia huduma zingine za machapisho kwa kila lugha, taifa na jamaa. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window' Sambaza Biblia popote ndiyo kauli mbiu ya muumini, Sambaza Neno la Mungu kote. Jiunge nasi katika kuandika vitabu vya kuboresha watu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ombi letu, ni unapochapa, usibadilishe chochote labda typos tu, tuwasilane kama kuna kosa la dhana au lugha! Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa rasilimali, mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Ila hapa Kwetu Afrika Mashariki, sisi tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu kwenye mada za afya, lishe, mahusiano kati ya wazazi au ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake, haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandano ya magharibi na ni mema tu, ila kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwasababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine. Kwanini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe. Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu, kwanini tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu ya nyingine, vizuri vingine, tuna wataalamu wengi wa nyimbo sasa.

Na hata vitabu vya watoto, tunahitaji watu wanaopenda watoto kufanya kazi hii kwa kushirikiana. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata, Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Wauminin wengi kuliko Amerika ya kusini, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au wawe na mwenendo kama ule, mfano mdogo sana utakuwa, wanafikiri sisi ni lazima tule kimchi, taco, panzit, empanada, manicotti, tortellini, sushi, falafel, je viwanda vyetu vinatengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana, Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk. Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! Naelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya! Nategemea tunaiga mazuri tu! Na si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii, wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu, vingine vitakudodea. Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio taasisi. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao vya kuboresha jamii mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake, tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwa mamilioni kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani tafadhali usisite kutufikia na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, tuwasiliane, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa ***Maandishi*** yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku, tunaomba mashauri pia kwa kutumia email UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au simu -1 -908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, "Njoo!" Kila mtu asikiaye hili, na aseme, "Njoo!" Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo BWANA!

## Waliofanikisha Kazi Hii

**Tunamshukuru Mwenyezi Mungu na wengi ambao wamehusika katika kazi hii, Watafsiri, Wasomaji Waombezi, Wahariri, Washauri, Wahakiki, Wataalamu wa Teknolojia, na watia moyo wote -wapita njia, Marafiki na Ndugu, na hakika wasomaji wote, kwa vile najua mnaendelea kuombea huduma ya machapisho duniani kote, maana tunaambiwa 'Watu 1000 siku moja wataamini kwa ujumbe wa kimya'. Endeleeni kuombea huduma hii na zingine zote zinazosambaza machapisho kwa kila lugha, jamaa taifa**

Grace Momadi-Masaka, New Jersey, Marekani
Daniel Masaka- Kisii, Kenya,
Christian Mugasa Gideon- Ukerewe, Tanzania
Sandra Barron- Kentucky, Marekani
Musa Budodi- Shinyanga, Tanzania
Niwaeli Mburuja- Pwani, Tanzania
Mbusi Mpagalushu- Bariadi, Tanzania
David Jabez Masaka- Pennsylvania, Marekani
Paul Momadi Masaka- New Jersey, Marekani
Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
Innocent Wayoga- Mbweni, Tanzania
Gerard Saakumi Nyafanga- Rorya Tanzania

*UhamishoniUghaibuniMtandaoniMajumbani*

Katika toleo la Kiswahili la kitabu hiki, mpangilio wa namba za Aya uko hivi; ukiachana na maelezo mengine bali kwa kuanzia hasa kwenye sura zenyewe za kitabu, kila Sura ina idadi ya Aya ambapo mwishoni mwa kila Aya kuna mafungu mawili ya namba:

- Fungu la awali ni namba ya Aya kulingana na mpangilio wa Aya katika toleo la Kiingereza (mfano; TA 132.3) na
- Fungu la pili ni namba ya Aya kulingana na mfuatano wa Aya toka mwanzo wa Sura hadi mwisho wa Sura hiyo (mfano; UM Aya ya 8).

Hivyo, ukiwa unataka kunukuu aya yo yote, anza na jina la kitabu, inafuata sura ya kitabu ilipo aya hiyo na kisha anza kuhesabu aya zote toka mwanzoni mwa sura mpaka utakapoifikia aya unayotaka kuinukuu. Hii itarahisisha kuhifadhi kumbukumbu na itakuwa rahisi kumshirikisha mtu kuhusiana na aya hiyo.

Mpangilio huu ni tofauti na kunukuu kwa kufuata ukurasa kwani utafsiri hutofautiana kwa mtu mmoja na mwingine, lakini pia uongezeaji wa maelezo fulani hufanya yaliyomo kutofautiana katika kurasa yalipo.

Katika toleo hili, neno “volume” limetafsiriwa kama ‘gombo,” na wakati mwingine limetumika kwa kubadilishana na neno “juzuu”

**Vifupisho**

UM—Ukweli kuhusu Malaika
TA—The Truth About Angels

## YALIYOMO

Waliofanikisha Kazi Hii ..... i
Kwa Msomaji ..... VIII

SURA YA 1
MALAIKA NA WEWE—MUHTASARI MFUPI
**Idadi na Uweza wa Malaika** ..... 1
**Malaika Huwasaidia Watoto wa Mungu** ..... 2
**Shetani na Malaika waovu** ..... 2
**Wafuasi wa Kristo Wako Salama** ..... 3

SURA YA 2

HUDUMA YA MALAIKA LEO
Malaika Hutulinda 4
Malaika Wanahusika Katika Maisha ya Familia 5
Malaika Huangazia Akili Zetu 6
Malaika Hutusaidia Kutenda Mema 6
Malaika Hushughulika kwa ajili ya Waliopotea 7
Malaika Huimarisha Imani Yetu 9

SURA YA 3
MALAIKA MBINGUNI, KABLA YA UASI
Kristo Kama Mungu Muumbaji. 10
Kabla Dhambi Haijainuka, Mungu Alikuwa na Mpango. 11
Kuumbwa kwa Malaika 11
Kuumbwa Kwa Lusifa 12
Nafasi ya Juu Zaidi ya Lusifa 12
Kabla Uovu Haujainuka 13

SURA YA 4
CHANZI CHA UOVU
Asili ya Uovu ni Siri/Fumbo 15
Fununu Za Awali Za Uovu 15
Mungu Aweka Rasmi Nafasi Halisi Ya Kristo 16
Lusifa Aanza Kampeni Yake Dhidi Ya Kristo 17
Lusifa Apewa Muda Kuendeleza Kanuni Zake 19
Malaika Wajadili Masuala Haya 20
Mungu Akabiliana Na Badiliko La Shetani 22
Lusifa Awa Shetani 22
Malaika Waonekana Mbele Ya Baba 23

SURA YA 5
MALAIKA WAASI WATUPWA NJE, NA ADAMU NA HAWA WAANGUKA
Vita Mbinguni 25
Matokeo ya Uasi. 25
Uumbaji wa Dunia na Wanadamu. 26
Adamu na Hawa Edeni 27
Shetani Apanga Kusababisha Anguko la Mwanadamu 28
Shetani Azungumza na Hawa Kupitia Nyoka 30
Hawa Ala Tunda na Amjaribu Adamu 32
Baraza la Amani 34
Adamu na Hawa Wafukuzwa Edeni 36

SURA YA 6

MALAIKA KABLA NA BAADA YA GHARIKA YA NUHU
Mpango wa Wokovu Waelezwa Zaidi 38
Ibada Iliyofanyika Kwenye Lango Lililolindwa na Makerubi 38
Adamu na Malaika Waliwafundisha Watu wa Kabla ya Gharika 39
Henoko 40
Nuhu 42
Gharika Yaja. 42
Baada Ya Gharika 43
Wajenzi wa Babeli 43

SURA YA 7
MALAIKA KATIKA NYAKATI ZA WAZEE WA IMANI
Ibrahimu 45
Kuangamizwa kwa Sodoma na Gomora 46
Malaika Wawili Wamtembelea Lutu 46
Ibrahimu Apimwa 47
Ndoa ya Isaka 50
Yakobo na Esau 51

SURA YA 8
MALAIKA WAKATI WA KUTOKA
Kuzaliwa Kwa Musa 55
Musa Akiwa Midiani 56
Mapigo ya Misri 57
Kristo, Kiongozi Asiyeonekana wa Israeli 59

SURA YA 9
MALAIKA KUTOKA SINAI HADI KUANGUKA KWA YERIKO
Malaika Katika Kuzunguka-zunguka kwa Israeli Jangwani 61
Israeli Huko Sinai 61
"Na Wanifanye Patakatifu" 62
Kufa na Kufufuka kwa Musa 64
Balaamu, Nabii Aliyekosea 66
Yoshua Awaongoza Israeli Kwenda Kanaani 68
Kutekwa Kwa Yeriko 69

SURA YA 10
MALAIKA KUTOKA KIPINDI CHA WAAMUZI HADI UFALME WA AWALI
Kristo Kama "Malaika Wa Bwana" 71
Gideoni 71
Samsoni 72
Samweli na Eli 74
Sauli na Yonathani 75
Miaka Ya Awali Ya Daudi 76

Sauli Apingana Na Malaika 76
Ibada Ya Umizimu Ya Sauli Huko Endori Na Kifo Chake 77

SURA YA 11
MALAIKA TANGU ENZI ZA DAUDI HADI KUTEKWA NA BABELI
Utawala Wa Daudi 80
Sulemani 82
Eliya 82
Elisha 85
Isaya 85
Ezekieli 87

SURA YA 12
MALAIKA TANGU UHAMISHONI KAMA MATEKA HADI KWA YOHANA MBATIZAJI
Danieli na Wenzake Watatu 88
Tanuru La Moto La Nebukadneza 88
Karamu ya Belshaza 88
Danieli Kwenye Tundu La Simba 89
Gabrieli Atumwa kufafanua Maono ya Danieli 8 90
Pambano Katika Kuwaongoa Wafalme Wa Uajemi 91
Hekalu la Pili 91
Ezra 92
Nehemia 92
Maono ya Zekaria 92
Maono ya Yoshua na Malaika 92
Maono ya Taa Saba na Mizeituni Miwili 94
Malaika Wakati wa Esta 95
Baba wa Yohana Mbatizaji 96

SURA YA 13
KUFANYIKA MWILI NA MAISHA YA AWALI YA KRISTO
Kufanyika Mwili ni Fumbo lenye Kina 98
Malimwengu Yote Yalitazama Tukio Hili. 98
Kwa Nini Kristo Alichukua Asili ya Mwanadamu 98
Asili ya Kibinadamu ya Kristo 99
Gabrieli Ampasha Habari Bikira Mariamu 100
Kabla ya Kuzaliwa kwa Kristo 101
Mamajusi 102
Miaka ya Ukimya 106

SURA YA 14
MALAIKA KWENYE UBATIZO WA KRISTO NA JANGWANI
Kubatizwa Kwa Kristo 107

Kujaribiwa kwa Kristo Mara tatu Jangwani 108
Jaribu la Kwanza 109
Jaribu la Pili 110
Jaribu la Tatu 112
Malaika wa Mbinguni Walimtazama Kristo Akijaribiwa 113
Baada ya Jaribu la Tatu 114

SURA YA 15
MALAIKA WEMA NA WAOVU WAKATI WA HUDUMA YA KRISTO
Kupagawa na Mapepo katika Siku za Yesu. 115
Kukataliwa kule Nazareti 115
Mtu Aliyepagawa Katika Sinagogi Kule Kapernaumu 117
Kuponywa kwa Mtumishi wa Akida 118
Watu wa Gadara Waliopagawa na Mapepo 118
Kuponywa kwa Mwana Aliyepagawa 120
Yesu Anashutumiwa Kuwa Ana Pepo 120
Malaika Waovu Katika Umbo La Mwanadamu Walikuwa Miongoni Mwa Wasikilizaji Wa Kristo. 121
Ufufuo wa Lazaro 121
Yesu Aliwindwa toka Mji na Mji Wakati wa Huduma Yake. 122

SURA YA 16
MALAIKA TOKA KATIKA MATESO YA KRISTO HADI KIFO CHAKE
Yesu Na Wanafunzi Wake Waenda Gethsemane 123
Malaika Katika Gethsemane 124
Mbele ya behewa la Anasi na Kayafa 127
Mbele ya Pilato 127
Kusulibiwa kwa Kristo 129

SURA YA 17
MALAIKA TOKA KUFUFUKA KWA YESU MPAKA KUPAA KWAKE
Asubuhi ya Kufufuka Kwake 133
Baada Tu Ya Kufufuka Kwa Yesu 135
Wanawake Waja Kaburini 136
Kupaa kwa Yesu kwa Baba Yake 137
Kuonekana Kwingine Baada Ya Kufufuka Kwake 139
Kuonekana Kwa Kristo Mara Ya Mwisho Katika Kupaa Kwake. 141
Kristo Anasindikizwa Mahali Alipo Baba. 143

SURA YA 18
MALAIKA TANGU PENTEKOSTE HADI SIKU ZA MWISHO
Malaika Hulinda Kweli za Thamani za Biblia 145
Petro na Yohana Watolewa Gerezani 145
Filipo na Towashi Mkushi 147

Wongofu wa Paulo 147
Paulo Aondoka Dameski 148
Kornelio na Petro 149
Petro Atolewa Gerezani 150
Kupigwa Mawe kwa Stefano 151
Malaika Wakati wa Huduma ya Paulo 151
Kuzingirwa kwa Yerusalemu 155
Yohana wa Ufunuo 156
Malaika katika Zama za Kati 157
Matengenezo ya Kiprotestanti 158
Luther 158
Melancthoni 159
Wazee Mahujaji na wasafiri 159
Malaika Watatu wa Ufunuo 14 160
William Miller 160

SURA YA 19
MALAIKA KATIKA UZOEFU WA ELLEN WHITE
Wito Wa Ellen White Kuwa Nabii 162
Sanduku la Agano Mbinguni 162
Shetani Kabla Hajaanguka, na Alivyo Sasa 163
Malaika Aliowaona Ellen White Katika Maono na Ndoto 164
Vita vya Manassas 165
Msimamizi wa Kituo cha tiba mbadala au tiba rahisi (Sanitarium) 166
Familia ya Brown 166
N. D. Faulkhead na Ishara ya Siri 167
Uwepo wa Malaika Ellen White Alipokuwa Macho 169

SURA YA 20
MALAIKA KATIKA PAMBANO KUU LA MWISHO
Malaika Wema na Waovu Watatokea 171
Kazi ya Malaika Wabaya Kupitia Umizimu 171
Miujiza Katika Wakati wa Mwisho 173
Pepo Wabaya Wakitenda Miongoni mwa Masalia 173
Malaika Watafanya Kazi iliyopuuzwa na Wanadamu 175
Malaika Watatoa ugavi wa Mahitaji ya Watu wa Mungu 175
Kujigeuza kwa Shetani 176
Malaika Waovu Wachochea Mateso 177
Utendaji Wa Shetani Wa Maigizo Baada Ya Kufungwa Kwa Mlango Wa Rehema 179
Malaika na Amri ya Kifo kwa Ulimwengu wote 180
Mungu Aingilia Pale Waovu Wanapojaribu Kuwaua Watu wa Mungu 181
Ujio wa Pili wa Kristo 182

Shetani na Malaika Wake Wabaya Kufungwa Katika Dunia Hii 184

SURA YA 21
MALAIKA KATIKA ULIMWENGU UJAO MBINGUNI
Tujapofika Mbinguni 185
Hukumu ya Miaka Elfu Moja 188
Ujio wa Tatu wa Kristo 188
Hukumu ya Mwisho 190
Dunia kufanywa upya 194
Dunia Mpya na Urithi Wetu wa Milele 194
Hitimisho 196

## Kwa Msomaji

Kitabu hiki kinashughulikia mada inayovutia ulimwenguni kote. Katika idadi isiyokuwa ya kawaida, vipindi vya televisheni vinaangazia juu ya mada zinazodaiwa za uhusika wa malaika katika mambo ya wanadamu. Magazeti ya udaku huchapisha hadithi kuhusu mionekano mingi iliyoripotiwa ya viumbe wa nje ya anga. Maduka ya vitabu yamesheheni safu kwa baada ya safu ya juzuu zinazohusika na viumbe visivyovya kawaida, na mauzo ni ya haraka. Katika kila nchi watu wanauliza maswali kama vile, ikiwa malaika kweli wapo, wao ni nani? Je! wao ni roho za wafu? Je, ni marafiki au maadui? Je, wanaweza kuwasiliana nasi?

Majibu mengi yaliyotolewa na "mamlaka" hayawaridhishi watafutaji wanyoofu wa ukweli. Majibu mengi yanawakilisha uvumi tu. Baadhi ni hisia za makusudi. Mengine yanatokana na tafsiri za uwongo za Maandiko.

Kinyume chake, juzuu hii imejaa habari iliyovuviwa. Inatoa majibu yenye msingi thabiti katika Neno la Mungu. Siyo tu inaeleza ukweli kuhusu malaika, lakini, tunaamini, itamwongoza msomaji katika uzoefu wa kina wa kiroho.

Sura ya kwanza inatoa muhtasari wa jumla wa uwepo na shughuli za viumbe katika ulimwengu usioonekana. Sura ya pili inaonyesha njia chache kati ya nyingi ambazo malaika wanahusika katika maisha ya binafsi ya wanadamu. Kuanzia na Sura ya 3, kitabu kinaweka katika mlolongo wa kihistoria ya ulimwengu matukio na uzoefu ambapo malaika wamekuwa wahusika wakuu. Huanza na uasi wa Lusifa mbinguni kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu huu na inamalizia katika nafasi ya Malaika katika ulimwengu ujao.

Juzuu hii ni kitabu cha thamani isiyokifani, lakini ni zaidi ya hilo; ni kitabu kinachoinua pazia kati ya ulimwengu unaoonekana na usioonekana. Kinafunua uhusika wa malaika katika matukio ambayo wanahistoria wa kiulimwengu waliyahifadhi lakini hawakuweza kuyaeleza, na humpa msomaji kuhisi kwamba yeye ni shahidi alinayejionea matukio hayo—jambo lenye kusisimua kwa hakika!

Tunaamini kwamba kitabu hiki kitathaminiwa na wote wanaotafuta ukweli duniani kote, kwamba kitawasaidia kutambua udhihirisho bandia wa roho, na kwamba katika kutembea kwao kila siku na Mungu kitawaongoza kutafuta na kufurahia ushirika wa malaika watakatifu.

Wadhamini wa Ellen G. White Estate, Inc.
Silver Spring, Maryland 20904

## SURA YA 1

## MALAIKA NA WEWE—MUHTASARI MFUPI

Uhusiano wa ulimwengu unaoonekana na usioonekana, utendaji wa malaika wa Mungu, na utendaji wa pepo wabaya, vimefunuliwa waziwazi katika Maandiko, na kufungamanishwa bila kutenganishwa na historia ya wanadamu. [TAsw 9.1; UM Aya ya 1]

Kabla ya kuumbwa kwa mwanadamu, malaika walikuwapo; kwa maana pale misingi ya nchi ilipowekwa, “nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, Na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha.” Ayubu 38:7. Malaika kwa asili ni wakuu kuliko wanadamu, kwani mtunga zaburi anasema kuwa mwanadamu aliumbwa mdogo punde kuliko malaika (Zaburi 8:5). [TAsw 9.2; UM Aya ya 2]

### Idadi na Uweza wa Malaika

Tunafahamishwa katika Maandiko kuhusu hesabu, na uweza na utukufu, wa viumbe wa mbinguni, kuhusiana na uhusiano wao na serikali ya Mungu, na pia uhusiano wao na kazi ya ukombozi. “Bwana ameweka kiti chake cha enzi mbinguni, Na ufalme wake unavitawala vitu vyote.” Na, asema nabii, “nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi.” Katika chumba cha Mfalme wa wafalme wanangoja—“malaika, walio hodari,” “watumishi wake, wafanyao mapenzi yake,” “wakiisikiliza sauti ya neno lake.” Zaburi 103:19-21; Ufunuo 5:11. [TAsw 9.3; UM Aya ya 3]

Elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu, walikuwa ni wajumbe wa mbinguni aliowaona nabii Danieli. Mtume Paulo aliwatangaza kuwa “elfu nyingi.” Danieli 7:10; Waebrania 12:22. Wakiwa wajumbe wa Mungu wanatoka, kama “kuonekana kwa kumulika kwa umeme,” (Ezekieli 1:14), wakiangaza utukufu wao, na hivyo kupaa kwao kwa haraka. Malaika aliyetokea kwenye kaburi la Mwokozi, sura yake “ilikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji.,” kwa hofu juu yake ilisababisha walinzi kutetemeka, nao “wakawa kama wafu.” Mathayo 28:3, 4. [TAsw 10.1; UM Aya ya 4]

Senakeribu, Mwashuru mwenye majivuno, pale alipomtukana na kumkufuru Mungu, na kutishia Israeli kuwaangamiza, “Ikawa usiku uo huo malaika wa Bwana alitoka, akakiingia kituo cha Waashuri, akawapiga watu mia na themanini na tano elfu.” “walikatiliwa mbali mashujaa wote, na majemadari, na maakida,” kutoka katika jeshi la Senakeribu. “Basi akarudia nchi yake mwenye haya ya uso.” 2 Wafalme 19:35; 2 Mambo ya Nyakati 32:21. [TAsw 10.2; UM Aya ya 5]

### Malaika Huwasaidia Watoto wa Mungu

Malaika hutumwa kwa utume wa rehema kwa watoto wa Mungu. Kwa

Ibrahimu, wakiwa na ahadi za baraka; kwenye malango ya Sodoma, ili kumwokoa Lutu mwenye haki toka katika adhabu yake kali; kwa Eliya, alipokuwa karibu kuangamia kwa uchovu na njaa nyikani; kwa Elisha, wakiwa na magari ya vita na farasi wa moto wakiuzunguka mji huo mdogo ambapo alifungiwa ndani na maadui zake; kwa Danieli, wakati akitafuta hekima ya kimungu katika ua wa mfalme wa mataifa, au pale alipoachwa kuwa mawindo ya simba; kwa Petro, aliyehukumiwa kifo katika gereza la Herode; kwa wafungwa huko Filipi; kwa Paulo na wenzake katika usiku wa tufani baharini; katika kufungua akili ya Kornelio kupokea injili; kumtuma Petro na ujumbe wa wokovu kwa mgeni asiye Myahudi—hivyo malaika watakatifu wamewahudumia watu wa Mungu katika vizazi vyote. [TAsw 10.3; UM Aya ya 6]

Hivyo watu wa Mungu, wakiwa wameanikwa kwenye nguvu za udanganyifu na uovu wa kila kuchwapo wa mkuu wa giza, na katika mapambano na nguvu zote za uovu, wanahakikishiwa ulinzi usiokoma wa malaika wa mbinguni. Wala uhakikisho huo hautolewi pasipo uhitaji wa huduma ya malaika. Ikiwa Mungu amewapa watoto Wake ahadi ya neema na ulinzi, ni kwa sababu kuna mawakala wenye nguvu wa uovu wanaopaswa kukabiliwa—mawakala wengi, walionuia, na wasiochoka, ambao ubaya na uwezo wao hakuna hata mmoja anayeweza kuwa mjinga au asiyezingatia. [TAsw 11.1; UM Aya ya 7]

### Shetani na Malaika waovu

Pepo wachafu, hapo mwanzo waliumbwa wasio na dhambi, walikuwa sawa kwa asili, uwezo, na utukufu pamoja na viumbe watakatifu ambao sasa ni wajumbe wa Mungu. Lakini wakiwa wameanguka kwa sababu ya dhambi, wameunganishwa pamoja katika kumfedhehesha Mungu na uharibifu wa wanadamu. Wakiwa wameungana na Shetani katika uasi wake, na wakiwa wametupwa pamoja naye toka mbinguni, kupitia vizazi vyote vinavyofuata, wameshirikiana naye katika vita vyake dhidi ya mamlaka ya kimungu. Tunaambiwa katika Maandiko juu ya njama zao na utendaji, juu ya nafasi zao mbalimbali, juu ya akili na werevu wao, na juu ya matendo yao maovu dhidi ya amani na furaha ya wanadamu. [TAsw 11.2; UM Aya ya 8]

Hakuna walio katika hatari kubwa zaidi kutokana na ushawishi wa pepo wabaya kuliko wale ambao, ijapokuwa ushuhuda tele na wa moja kwa moja wa Maandiko, wanakana njia na kuwako kwa ibilisi na malaika zake. Kadiri tusivyotambua werevu wao, wana faida ambayo haiwaziki kirahisi; wengi hutii hila zao huku wakidhani wao wenyewe wanafuata maagizo ya hekima yao wenyewe. Hii ndiyo sababu, pale tukaribiapo mwisho wa wakati, pale ambapo Shetani hana budi kutenda kwa uwezo mkubwa zaidi kudanganya na kuharibu, anaeneza kila mahali imani kwamba yeye hayupo. Ni sera yake kujificha na namna yake ya utendaji. [TAsw 12.1; UM Aya ya 9]

Ni kwa sababu amejifunika uso kwa ustadi uliokamilika ndiyo maana swali huulizwa sana: “Je, ni kweli kiumbe kama hicho kipo?” Ni uthibitisho wa kufanikiwa kwake ya kwamba nadharia zinazotoa uongo dhidi ya ushuhuda ulio wazi zaidi wa Maandiko zinapokewa na wengi katika ulimwengu wa kidini. Na ni kwa sababu Shetani aweza kwa urahisi zaidi kudhibiti akili za wale wasiojua ushawishi wake, ndiyo maana Neno la Mungu linatupa mifano mingi sana ya utendaji wake mwovu, akifunua mbele yetu mamlaka zake za siri, na hivyo kutuweka macho juu ya mashambulizi yake dhidi yetu. [TAsw 12.2; UM Aya ya 10]

### Wafuasi wa Kristo Wako Salama

Uwezo na uovu wa Shetani na jeshi lake linaweza kututahadharisha ikiwa hatujahifadhiwa na kuokolewa katika uweza mkuu wa Mkombozi wetu. Twazilinda kwa uangalifu nyumba zetu kwa makomeo na makufuli ili kulinda mali zetu na maisha yetu dhidi ya watu waovu; lakini sisi kwa nadra sana huwa tunawafikiria malaika waovu ambao daima hutafuta njia ya kutufikia, na ambao kwa mashambulizi yetu dhidi yao, kwa nguvu zetu wenyewe, hatuwawezi. Endapo wakiruhusiwa, wanaweza kuvuruga akili zetu, kuvuruga na kutesa miili yetu, kuharibu mali zetu na maisha yetu. Furaha yao pekee ni katika taabu na uharibifu. [TAsw 12.3; UM Aya ya 11]

Ni ya kuogofya mno hali ya wale wanaopinga matakwa ya kimungu na kujianika kwenye majaribu ya Shetani, mpaka Mungu huwaacha chini ya utawala wa pepo wabaya. Lakini wale wanaomfuata Kristo daima wako salama chini ya ulinzi Wake. Malaika walio na nguvu nyingi hutumwa toka mbinguni ili kuwalinda. Mwovu hawezi kuvunja ukuta wa uangalizi ambao Mungu amewazungushia watu Wake. E. G. White, Pambano Kuu, 511-513, 516, 517. [TAsw 13.1; UM Aya ya 12]

## SURA YA 2

## HUDUMA YA MALAIKA LEO

### Malaika Hutulinda

Malaika mlinzi ameteuliwa kwa kila mfuasi wa Kristo. Walinzi hawa wa mbinguni huwakinga wenye haki dhidi ya nguvu za mwovu. Shetani mwenyewe alitambua aliposema: "Je! Huyo Ayubu yuamcha Bwana bure? Wewe hukumzingira kwa ukigo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Ayubu 1:9, 10. Njia ambayo kupitia hiyo Mungu huwalinda watu Wake inaonyeshwa katika maneno ya mtunga-zaburi: "Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa." Zaburi 34:7. Mwokozi alisema, akizungumzia wale wanaomwamini: "Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni" Mathayo 18:10. Malaika waliowekwa rasmi kuwahudumia watoto wa Mungu, katika nyakati zote wana fursa ya kufikia uwepo Wake. E. G. White, Pambano Kuu, 512, 513. [TAsw 14.1; UM Aya ya 1]

Hatujui ni matokeo gani kwa siku, saa, au kwa dakika yanaweza kuwa, na hatupaswi kamwe kuianza siku bila kukabidhi njia zetu kwa Baba yetu wa mbinguni. Malaika wake wamewekwa kutulinda, na kama tukijiweka chini ya ulinzi wao, ndipo katika kila wakati wa hatari watasimama mkono wetu wa kuume. Tunapokuwa katika hatari ya kuwa na mvuto mbaya pasipo sisi kuelewa, malaika watakuwa upande wetu, wakituchochea kuenenda katika njia bora zaidi, wakituchagulia maneno ya kunena, na kuyadhibiti matendo yetu. E. G. White, Vielelezo vya Mafundisho ya Kristo uk. 341, 342. [TAsw 14.2; UM Aya ya 2]

Malaika wa Mungu wametuzunguka.... Loo, tunataka kujua mambo haya, na kuogopa na kutetemeka, na kufikiria zaidi uwezo wa malaika wa Mungu watuangaliao na kutulinda kuliko tulivyowahi hadi sasa. Malaika wa Mungu huagizwa kutoka mbinguni kuwalinda watoto wa wanadamu, lakini bado wanadamu hujiondoa kutoka kwenye udhibiti wa malaika na kwenda mahali ambapo wanaweza kuwa na mawasiliano na malaika wabaya.... Lo, ili sote tutii agizo la mtume (Soma 2 Wakorintho 6:17, 18). E. G. White, Manuscript Releases, vol. 5, pg. 125. [TAsw 15.1; UM Aya ya 3]

Malaika hutumwa kuwahudumia watoto wa Mungu ambao ni vipofu kimwili. Malaika hulinda hatua zao na kuwaokoa toka kwenye hatari maelfu, ambazo, pasipo wao kuzitambua, huzingira njia yao. E. G. White, Welfare Ministry, p. 240. [TAsw 15.2; UM Aya ya 4]

Leo ilikuwa niandike juu ya Kristo akitembea juu ya bahari na kutuliza tufani. Loo, jinsi gani tukio hili lilivyovutia akilini mwangu.... Ukuu wa Mungu na kazi Zake ziliyateka mawazo yangu. Azishikilia pepo mikononi Mwake, ayadhibiti maji. Viumbe wenye ukomo, kama madoadoa tu juu ya maji mengi, yenye kina kirefu ya Pasifiki, tulikuwa machoni pa Mungu, hata hivyo malaika wa mbinguni walitumwa kutoka kwenye utukufu Wake bora ili kulinda mashua hiyo ndogo

iliyokuwa ikipinduliwa na mawimbi. E. G. White, This Day With God, 110. [TAsw 15.3; UM Aya ya 5]

### Malaika Wanahusika Katika Maisha ya Familia

Bwana hutumikiwa zaidi, naam, zaidi, na mtendakazi mwaminifu wa nyumbani kama na yule anayehubiri Neno. Baba na mama watambue kuwa wao ndio waelimishaji wa watoto wao. Watoto ndio urithi wa Bwana; na wanapaswa kufunzwa na kuadabishwa ili kutengeneza maumbile ya tabia ambayo Bwana anaweza kuiafiki. Kazi hii inapofanywa kwa busara na kwa uaminifu na sala, malaika wa Mungu watailinda familia, na maisha ya kawaida zaidi yatafanywa kuwa matakatifu. E. G. White, (Australasian) Union Conference Record, Septemba 6, 1909. [TAsw 16.1; UM Aya ya 6]

Kabla ya kuondoka nyumbani kwa ajili ya kazi, familia yote inapaswa kukutana; na baba, au mama pale baba hayupo, wanapaswa kumwomba Mungu kwa bidii ili awahifadhi katika siku nzima. Njooni kwa kujidhili, kwa moyo uliojaa huruma, na kwa utambuzi wa majaribu na hatari mbele yenu na watoto wenu; kwa imani waongoze madhabahuni, na kuwaombea ulinzi wa Bwana. Malaika wahudumu watawalinda watoto ambao wamejiweka wakfu kwa Mungu. E. G. White, Child Guidance, p. 519. [TAsw 16.2; UM Aya ya 7]

Malaika wa Mungu, maelfu kwa maelfu, hutulinda dhidi ya uovu na kuzirudisha nyuma nguvu za giza zinazotafuta kutuangamiza. Je, hatuna sababu ya kuwa wenye shukrani kila wakati, wenye shukrani hata kunapokuwa na magumu yanayoonekana katika njia yetu? E. G. White, My Life Today, 171. [TAsw 16.3; UM Aya ya 8]

Malaika wa Mungu hutuangalia. Duniani hapa kuna maelfu na makumi ya maelfu ya wajumbe wa mbinguni walioagizwa na Baba kumdhibiti Shetani asiwafikie kwa vyo vyote wale wasiofuata katika njia ya uovu. Na malaika hawa wanaowalinda watoto wa Mungu duniani wanawasiliana na Baba aliye mbinguni. E. G. White, In Heavenly Places, 99. [TAsw 16.4; UM Aya ya 9]

Tunahitaji kuelewa vizuri zaidi utume wa malaika kuliko vile tulivyo sasa. Itakuwa vyema kukumbuka kwamba kila mtoto wa kweli wa Mungu ana ushirikiano wa viumbe wa mbinguni. Majeshi yasiyoonekana ya nuru na nguvu huwahudumia wale walio wapole na wanyenyekevu wanaoamini na kudai ahadi za Mungu. Makerubi na maserafi, na malaika walio hodari, wanasimama katika mkono wa kuume wa Mungu, "Roho zote zitumikazo, hutumwa kuwahudumia wale watakaourithi wokovu." E. G. White, The Acts of the Apostles, 154. [TAsw 17.1; UM Aya ya 10]

### Malaika Huangazia Akili Zetu

Mungu huwaita viumbe Wake kurudisha usikivu wao toka katika mkanganyo na kutatizika kunakowazunguka na kugeukia kustaajabia na kupendezwa na utendakazi wa mikono Yake. Wakazi wa mbinguni ni stahili ya mwanadamu kuwatafakari. Mungu amewafanya kuwa faida kwa mwanadamu, na jinsi tunavyojifunza kazi Zake, malaika wa Mungu watakuwa upande wetu kuangaza katika akili zetu na kuzilinda dhidi ya ulaghai wa kishetani. E. G. White, The S.D.A. Bible Commentary juzuu ya 4, uk. 1145. [TAsw 17.2; UM Aya ya 11]

Malaika wa kimbingu huwatazama wale watafutao kuangaziwa. Hushirikiana na wale wanaojaribu kuziokoa roho kwa Kristo. E. G. White, The Bible Echo, December 10, 1900. [TAsw 17.3; UM Aya ya 12]

Huduma yako kwa wagonjwa ni mchakato unaochosha na unaweza kukausha taratibu chemchemi adhimu za uzima ikiwa hakuna badiliko, hakuna wasaa kwa ajili ya uhuisho, na ikiwa malaika wa Mungu si kinga na walinzi wako. Ikiwa ungeweza kuona hatari nyingi ambazo unaepushwa nazo kila siku kwa huduma ya wajumbe wa mbinguni, shukrani zingebubujika mioyoni mwenu na kudhihirika katika vinywa vyenu. Ikiwa unamfanya Mungu kuwa nguvu yako, chini ya hali zikatishazo tamaa, unaweza kuinuliwa na kuongezeka katika ukamilifu wa Kikristo ambao unafikiri ya kuwa ni vigumu kuufikia. Mawazo yako yanaweza kuinuliwa, unaweza kuwa na matumaini adili, mtazamo safi wa ile kweli, na makusudi ya utendaji ambavyo vitakuinua juu ya misukumo hafifu. E. G. White, Counsels on Health, 384. [TAsw 17.4; UM Aya ya 13]

Nimeonyeshwa hatari yako [Tabibu], na pia nimeonyeshwa malaika wako mlinzi akikuhifadhi tena na tena, akikudhibiti usivunjike imani. Ndugu yangu, uinue msingi, uinue juu, na usikate tamaa au kuvunjwa moyo. E. G. White, Shuhuda za Kanisa, juzuu ya 8, uk. 175. [TAsw 18.1; UM Aya ya 14]

### Malaika Hutusaidia Kutenda Mema

Jifunze kumtumaini Mungu. Jifunze kumwendea yeye aliye na uweza wa kuokoa. Mwambie Mwokozi mpendwa kile unachohitaji. Yeye aliyesema, “Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie,” hatakataa maombi yako. Lakini atawaagiza Malaika wake wakulindeni dhidi ya Malaika waovu, na atakufanyieni wepesi kutenda mema. Ndipo itakuwa rahisi zaidi kuliko vile ambavyo ungejaribu kwa nguvu zako mwenyewe. Huenda ukahisi hivi: “Nimemwomba Mungu anisaidie, na atafanya hivyo. Nitatenda mema kwa nguvu zake. Sitawahuzunisha malaika wapendwa ambao Mungu amewaweka ili kunilinda. Sitafuata mwelekeo wa kuwafukuza mbali nami.” E. G. White, An Appeal to the Youth, 55, 56. [TAsw 18.2; UM Aya ya 15]

Ikiwa utajaribu kuzuia kila wazo baya kwa siku nzima, basi malaika wa Mungu watakuja na kukaa nawe. Malaika hawa ni viumbe wenye nguvu nyingi.

Unakumbuka jinsi malaika alivyofika pale kaburini, na askari wa Kirumi wakaanguka kama wafu mbele ya utukufu wa uso wake; na endapo malaika mmoja angetenda kwa uwezo huo, ingekuwaje kama malaika wote walio pamoja nasi hapa wangekuwepo? Malaika wako pamoja nasi kila siku, ili kutulinda dhidi ya mashambulizi ya adui. E. G. White, The Review and Herald, Agosti 14, 1888. [TAsw 19.1; UM Aya ya 16]

Hauko peke yako katika vita dhidi ya makosa. Laiti pazia lingefunuliwa, ungeona malaika wa mbinguni wakipigana pamoja nawe. Sharti wafanye hili; ni kazi yao kuwalinda vijana. “Je, hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumia wale watakaourithi wokovu?” Malaika elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu ya malaika huwahudumia vijana. E. G. White, The Youth's Instructor, Januari 1, 1903. [TAsw 19.2; UM Aya ya 17]

Ninashukuru sana kwamba ningeweza kutembelea shule yako [sasa Chuo cha Oakwood]. Kwa miaka mingi nimefanya nilichoweza kusaidia watu weusi, na sijawahi kushuhudia kazi ambayo imeanza vizuri mahali popote kama ninavyoiona hapa wakati huu. Katika mapitio yako yote, kumbuka kwamba malaika wa Mungu wako upande wako. Wanatambua unachofanya; wapo kukulinda. Usifanye chochote chenye kuwachukiza. Unapofanya kazi nao wanapotenda kazi, shule hii itakuwa sehemu takatifu. Nitatamani kusikia jinsi unavyofanikiwa. Mbingu yote inapendezwa na hatua unazofanya. Tufanye kila tuwezalo kusaidiana ili kupata ushindi. Na tuishi hivyo ili nuru ya mbinguni iangaze ndani ya mioyo na akili zetu, ikituwezesha kushikilia hazina za mbinguni. E. G. White, Southern Field Echo, Juni 1, 1909. [TAsw 19.3; UM Aya ya 18]

### Malaika Hushughulika kwa ajili ya Waliopotea

Pale watukufu wa mbinguni wanapoona wale wanaodai kuwa wana na binti za Mungu wakifanya jitihada kama za Kristo kuwasaidia wakosaji, wakionyesha roho ya upole na huruma kwa waliotubu na walioanguka, malaika husogea karibu yao, na kuwakumbusha maneno hasa yale yatakayoituliza na kuiinua nafsi. Yesu ameyatoa maisha yake ya thamani, uangalizi Wake binafsi, kwa walio wadogo kabisa wa Mungu; na malaika walio hodari hupiga kambi kuwazunguka wamchao Mungu. E. G. White, Healthful Living, 277. [TAsw 20.1; UM Aya ya 19]

Malaika hutumwa kutoka katika nyua za mbinguni, si kuangamiza, bali kuangalia na kulinda roho zilizo hatarini, kuokoa waliopotea, kuwarudisha waliopotea kwenye zizi. “Sikuja kuhukumu, bali kuokoa,” Kristo alisema. Je, basi, huna maneno yenye huruma ya kuwaambia waliopotea? Je, utawaacha waangamie, au utawanyoshea mkono wa kusaidia? Karibu na wewe kuna roho ambazo ziko katika hatari ya kuangamia. Je, hutawavuta kwa kamba za

upendo kwa Mwokozi? Je, hutaacha lawama zako, na kusema maneno ambayo yatawatia imani na ujasiri? E. G. White, Review and Herald, Mei 10, 1906. [TAsw 20.2; UM Aya ya 20]

Ni fursa ya wote wanaotii masharti kujua kwa ajili yao wenyewe kwamba msamaha hutolewa bure kwa kila dhambi. Ondoa shaka kwamba ahadi za Mungu hazijakusudiwa kwako. Ziko kwa kila mvunjaji wa amri aliyetubu. Nguvu na neema vimetolewa kupitia Kristo ili kuletwa na malaika wahudumu kwa kila nafsi inayoamini. E. G. White, Steps to Christ, 52. [TAsw 21.1; UM Aya ya 21]

Wale wanaofanya kazi kwa manufaa ya wengine wanafanya kazi pamoja na malaika wa mbinguni. Wana ushirika wa daima na malaika na huduma yao isiyokoma. Malaika wa nuru na nguvu huwa karibu kila wakati, kulinda, kufariji, kuponya, kuelekeza, kutia moyo. Elimu ya juu zaidi, mtindo wa kweli zaidi wa maisha, utumishi uliotukuka zaidi unaowezekana kwa wanadamu katika ulimwengu huu, ni vyao. E. G. White, The Review and Herald, Julai 11, 1912. [TAsw 21.2; UM Aya ya 22]

Malaika wa mbinguni wanaingia katika akili za wanadamu ili kuamsha uchunguzi juu ya mada za Biblia. Kazi kubwa zaidi itafanywa kuliko ambayo bado haijafanywa na hakuna utukufu wake wowote utakaotiririka kwa wanadamu, kwa maana malaika wanaohudumia wale ambao watakuwa warithi wa wokovu wanafanya kazi usiku na mchana. E. G. White, Counsels to Writers and Editors, 140. [TA 21.3; UM Aya ya 23]

Mungu angeweza kuukabidhi ujumbe wa injili, na kazi yote ya huduma ya upendo, kwa malaika wa mbinguni. Angeweza kutumia njia nyingine ili kutimiza kusudi Lake. Lakini katika upendo Wake usio na kikomo alichagua kutufanya watendakazi pamoja naye, pamoja na Kristo na malaika, ili tuweze kushiriki baraka, furaha, kuinuliwa kiroho, ambako hutokana na huduma hii isiyo na ubinafsi. E. G. White, Steps to Christ, p 79. [TAsw 21.4; UM Aya ya 24]

### Malaika Huimarisha Imani Yetu

"Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa." Zaburi 34:7. Mungu huwaamuru malaika Zake kuwaokoa wateule Wake dhidi ya majanga, wakiwalinda dhidi ya "tauni ipitayo gizani, Wala uele uharibuo adhuhuri." Zaburi 91:6. Tena na tena malaika huzungumza na wanadamu kama vile mtu azungumzapo na rafiki, na huwaongoza katika pahali salama. Tena na tena maneno ya kutia moyo ya malaika huhuisha roho zilizofifia za waaminifu na, huyavuta mawazo yao hata juu zaidi ya dunia, na hufanya hivyo kutazama kwa imani mavazi meupe, taji, matawi ya ushindi ya mitende, ambayo washindi watayapokea pale watakapokizunguka kiti cheupe cha enzi. E. G. White,

Matendo ya Mitume, 153. [TAsw 22.1; UM Aya ya 25]

Miongoni mwa hawa wasimamao karibu—majeshi ya adui, wanaojaribu kuwaletea watu wa Mungu tabia ovu, na majeshi ya mbinguni, malaika elfu kumi mara elfu kumi, wanaowaangalia na kuwalinda watu wa Mungu waliojaribiwa, wakiwainua na kuwatia nguvu. Hawa ndio wasimamao karibu. Na Mungu anawaambia wanaomwamini, Mtatembea kati yao. Hamtashindwa na nguvu za giza. Mtasimama mbele Yangu machoni pa malaika watakatifu, watumwao kuhudumu kwa wale ambao watakuwa warithi wa wokovu. E. G. White, The General Conference Bulletin, Aprili 23, 1901. [TAsw 22.2; UM Aya ya 26]

## SURA YA 3

## MALAIKA MBINGUNI, KABLA YA UASI

### Kristo Kama Mungu Muumbaji.

Kabla wanadamu na malaika kuumbwa, Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. [TAsw 23.1; UM Aya ya 1]

Dunia iliumbwa na Yeye, "wala pasipo Yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika." Ikiwa Kristo aliyafanya yote, alikuwako kabla ya mambo yote. Maneno yaliyotamkwa kuhusiana na hili ni ya thabiti kiasi kwamba hakuna anayeweza kubaki na mashaka. Kristo alikuwa Mungu Mtakatifu, na katika

hadhi ya juu. Alikuwa na Mungu tangu milele zote, Mungu juu ya vyote, mbarikiwa milele daima. [TAsw 23.2; UM Aya ya 2]

Bwana Yesu Kristo, Mwana mtukufu wa Mungu, alikuwako tangu milele, nafsi iliyo pekee, angali yu pamoja na Baba. Alikuwa na utukufu mwingi wa kuzidi, huko mbinguni. Alikuwa amiri wa wakazi wa mbinguni, na heshima yenye kicho ya malaika ilipokelewa na Yeye kama haki Yake. E. G. White, The Review and Herald, April 5, 1906; [TAsw 23.3; UM Aya ya 3]

Kupitia Sulemani Kristo alitangaza: “Bwana alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, Kabla ya matendo yake ya kale. Nalitukuka tokea milele, tangu awali, Kabla haijawako dunia. Wakati visipokuwako vilindi nalizaliwa, Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji. Kabla milima haijawekwa imara, Kabla ya vilima nalizaliwa... Alipoipa bahari mpaka wake, Kwamba maji yake yasiasi amri yake; Alipoiagiza misingi ya nchi; Ndipo nilipokuwa pamoja naye, kama stadi wa kazi; Nikawa furaha yake kila siku; Nikifurahi daima mbele zake.” [Mithali 8:22-25, 29, 30.] [TAsw 23.4; UM Aya ya 4]

Katika kunena juu ya uwepo wake kabla, Kristo anaelekeza mawazo nyuma katika zama za zamani mno. Anatuhakikishia kuwa hakukuwako kamwe na wakati ambapo hakuwa pamoja katika ushirika wa karibu na Mungu wa milele. Amekuwa pamoja na Mungu kama mmoja aliyeinuka pamoja Naye. E. G. White, The Signs of the Times, August 29, 1900. [TAsw 24.1 ; UM Aya ya 5]

Ni nini kazi ya malaika kwa kulinganisha na ukuu wa Kristo? Kiti Chake cha enzi ki tangu milele. Ameshikilia kila tao na nguzo katika hekalu kuu la zamani. E. G. White, In Heavenly Places, 40. [TAsw 24.2; UM Aya ya 6]

Kristo Neno, Mzaliwa pekee wa Mungu, alikuwa pamoja na Baba wa milele—wakiwa sawa katika asili, tabia, na makusudi—nafsi pekee katika mbingu yote ambayo inaweza kushiriki katika mashauri na makusudi yote ya Mungu. E. G. White, The Great Controversy, 493. [TAsw 24.3; UM Aya ya 7]

**Kabla Dhambi Haijainuka, Mungu Alikuwa na Mpango.**

Mungu na Kristo walijua tokea mwanzo, juu ya uasi wa shetani na juu ya anguko la Adamu kupitia mamlaka laghai ya mwasi. Mpango wa wokovu ulikusudiwa kuikomboa jamii iliyoanguka, kuwapa kipimo kingine. Kristo aliteuliwa kuwa katika ofisi ya Mpatanishi tokea uumbaji wa Mungu, akiwekwa tangu milele kuwa mbadala na dhamana yetu. E. G. White, Selected Messages 1:250. [TAsw 24.4; UM Aya ya 8]

Yanayojulikana kwa Mungu ni kazi Zake, na tangu zamani za milele agano la neema (wema wa Mungu kwa mdhambi asiyestahili) lilikuwako katika mawazo ya Mungu. Linaitwa agano la milele; mpango wa wokovu haukutolewa baada ya

anguko la mwanadamu, bali ulikuwa ule ulio—"sitirika tangu zamani za milele,' uka—'dhihirishwa wakati huu kwa maandiko ya manabii,' uka—'julikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu wa milele, ili waitii Imani.'" Warumi 16:25, 26. E. G. White, The Signs of the Times, December 15, 1914. [TAsw 25.1; UM Aya ya 9]

Mpango kwa ajili ya ukombozi wetu haukuwa wazo la baadaye, kwamba mpango huu ulifanywa baada ya anguko la Adamu. Ulikuwa ni ufunuo wa " siri iliyositirika tangu zamani za milele." Warumi 16:25. Ilikuwa ni ufunuo wa misingi ambayo tokea zamani za milele imekuwa nguzo ya kiti cha enzi cha Mungu...Mungu hakuamuru kuwa dhambi iwepo, bali Aliuona uwepo wa dhambi kabla, na akatoa njia ya kukabiliana na badiliko hili la kutisha. E. G. White, The Desire of Ages, 22. [TAsw 25.2; UM Aya ya 10]

### Kuumbwa kwa Malaika

Baba alifanya kupitia Mwana Wake katika uumbaji wa viumbe wote wa mbinguni. "Katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake." E. G. White, Patriarchs and Prophets, 34. [TAsw 25.3; UM Aya ya 11]

Kabla ya uumbaji wa mwanadamu, malaika walikuwako; kwa maana pale misingi ya dunia ilipowekwa, "Nyota za asubuhi zili—imba pamoja, Na wana wote wa Mungu wali—piga kelele kwa furaha." Ayubu 38:7. Baada ya anguko la mwanadamu, malaika waliagizwa kuulinda mti wa uzima, na hili lilikuwa kabla ya mwanadamu kuwahi kupatwa na mauti. Malaika kwa asili ni wakuu kuliko wanadamu, kwani mtunga zaburi anasema kuwa mwanadamu aliumbwa "mdogo punde kuliko...malaika" Zaburi 8:5. E. G. White, The Great Controversy, 511. [TAsw 25.4; UM Aya ya 12]

Toka zamani za milele lilikuwa kusudi la Mungu kwamba kila kiumbe, kuanzia Serafi mtakatifu na mwenye kung'aa sana hadi kwa mwanadamu, awe hekalu pa makao ya Muumbaji. E. G. White, The Desire of Ages, 161. [TAsw 26.1; UM Aya ya 13]

Viumbe wote huishi kwa mapenzi na uweza wa Mungu. Wanategemea uzima wa Mungu. Kuanzia Serafi mkuu hadi kwa kiumbe mdogo na wa chini zaidi, wote wanajazwa uhai na Yeye aliye chanzi cha uzima. E. G. White, The Desire of Ages, 785. [TAsw 26.2; UM Aya ya 14]

Pale Mungu alipowaumba malaika kusimama mbele ya kiti Chake cha enzi, walikuwa na mwonekano mzuri na uliotukuka. Kupendana na utakatifu viliwiana sana kulingana na nafasi zao zilizotukuka. Walifurikwa na hekima ya Mungu, na walihimiliwa na deraya (armor) ya mbinguni. E. G. White, The Signs

of the Times, April 14, 1898. [TAsw 26.3; UM Aya ya 15]

**Kuumbwa Kwa Lusifa**

Mungu alimuumba (Lusifa) mwema na mwenye kupendeza, karibu na Yeye Mwenyewe. E. G. White, The Review and Herald, September 24, 1901. [TAsw 26.4; UM Aya ya 16]

Mungu alikuwa amemuumba msharafu (mwenye kuheshimiwa sana), alikuwa amemruzuku vipaji vingi. Alimpatia nafasi ya juu na yenye kuwajibika. Hakukosa lo lote ambalo lilikuwa linamfaa. Hakuwa na budi kuongoza katika tumaini alilopewa na Mungu katika roho ya upole na bidii, akitafuta kuuinua utukufu wa Mungu, aliyekuwa amempatia utukufu na uzuri na upendo." E. G. White, Sabbath-School Worker, March 1, 1893. [TAsw 26.5; UM Aya ya 17]

Ijapokuwa Mungu alimuumba Lusifa mwenye kuheshimiwa sana na mzuri kwa mwonekano, na kumtukuza katika heshima kuu miongoni mwa jeshi la malaika, bado alikuwa angali hajawekwa kupita mpaka wa uwezekano wa kutenda uovu. Ilikuwa ni uwezo wake shetani, kuchagua kufanya hivyo ili kuvipotosha vipaji hivi. E. G. White, The Spirit of Prophecy 4:317. [TAsw 27.1; UM Aya ya 18]

**Nafasi ya Juu Zaidi ya Lusifa**

Lusifa mbinguni, kabla ya uasi, alikuwa malaika wa juu aliyetukuka, akifuata nyuma ya Mwana mpendwa wa Mungu. Uso wake, ukiwa vile zilivyo nyuso za malaika wengine, alidhihirika mwenye furaha. Paji la uso wake lilikuwa juu na pana, likifunua akili kubwa mno. Umbo lake lilikuwa kamilifu; mwenye kutukuzwa sana na mkuu miongoni mwa malaika wote. Nuru ya pekee ilileta mwako katika sura yake na kung'aa kumfunika, nuru angavu na nzuri kuliko kwa malaika wengine; bado Kristo, Mwana mpendwa wa Mungu, angali akiwa anajua uwepo wa jeshi la malaika hata kabla ya kuumbwa kwao. E. G. White, The Story of Redemption, 13. [TAsw 27.2; UM Aya ya 19]

Lusifa alikuwa Kerubi afunikaye, mwenye kuheshimiwa zaidi miongoni mwa viumbe wa mbinguni; alisimama karibu na kiti cha enzi cha Mungu, na alikuwa ameunganishwa karibu na kuwa na utambulisho sawa na serikali ya Mungu, akiwa ameneemeshwa vipaji vingi vya utukufu wa Mkuu na Mweza wa yote. E. G. White, The Signs of the Times, April 28, 1890. [TAsw 27.3; UM Aya ya 20]

Bwana Mwenyewe alimpatia shetani utukufu na hekima Yake, na akamfanya kuwa Kerubi afunikaye, mwema, mashuhuri, na mwenye upendo mwingi. E. G. White, The Signs of the Times, September 18, 1893. [TAsw 28.1; UM Aya ya 21]

Miongoni mwa wakazi wa mbinguni , shetani, aliye nyuma ya Kristo, kuna wakati aliheshimiwa sana na Mungu, na alikuwa mkuu katika mamlaka na

utukufu. E. G. White, The Signs of the Times, July 23, 1902. [TAsw 28.2; UM Aya ya 22]

Lusifa “mwana wa asubuhi,” mwenye utukufu kuzidi malaika wote wazungukao kiti cha enzi.. alikuwa ameunganishwa karibu na Mwana wa Mungu. E. G. White, The Desire of Ages, 435. [TAsw 28.3; UM Aya ya 23]

Lusifa, “mwana wa asubuhi,” hapo awali alikuwa Kerubi afunikaye, mtakatifu na asiye na unajisi wo wote. Alisimama katika uwepo wa Muumbaji Mkuu, na miale yasiyofifia ya utukufu wake ikimfunika Mungu wa milele ilikaa juu yake (shetani). E. G. White, Patriarchs and Prophets, 35. [TAsw 28.4; UM Aya ya 24]

Lusifa alikuwa mkuu wa viumbe wote wa mbinguni, na alikuwa mbele katika kuyafunua makusudi ya Mungu kwa mbingu yote. E. G. White, The Desire of Ages, 758. [TAsw 28.5; UM Aya ya 25]

**Kabla Uovu Haujainuka**

Amani na furaha, katika kujisalimisha kikamilifu kwenye mapenzi ya mbinguni, vilidhihirika kwa jeshi la malaika. Upendo kwa Mungu ulitawala, upendo wa wao kwa wao ulikuwa adili. Hiyo ndiyo hali ilivyokuwa kwa miaka mingi kabla ya kuingia kwa dhambi. E. G. White, The Spirit of Prophecy 4:316, 317. [TA 28.6; UMsw Aya ya 26]

Lusifa alikuwa na maarifa ya thamani isiyopimika ya vipaji vya milele ambavyo mwanadamu hakuwa navyo. Alikuwa amezoea radhi kamili, amani, furaha iliyozidi na bashasha halisi, ya makao ya mbinguni. Kabla ya uasi wake alikuwa ametambua radhi ya kuwa na kibali kamili cha Mungu. Alikuwa na uelewa kamili wa utukufu uliokuwa ukimfunika Baba, na alitambua kuwa (Baba) hakuwa na mpaka wa uweza Wake. E. G. White, The Signs of the Times, August 4, 1887. [TAsw 29.1; UM Aya ya 27]

Kulikuwa na wakati ambapo ilikuwa ni furaha yake shetani kutekeleza amri za kiungu. Moyo wake ulijawa na upendo na bashasha katika kumtumikia Muumbaji. E. G. White, The Signs of the Times, September 18, 1893. [TAsw 29.2; UM Aya ya 28]

Shetani alikuwa mzuri, malaika aliyetukuzwa, na angelibaki hivyo daima ikiwa asingeliondoa utii kwa Mungu. E. G. White, The Signs of the Times, December 21, [TAsw 29.3; UM Aya ya 29]

## SURA YA 4

## CHANZI CHA UOVU

### Asili ya Uovu ni Siri/Fumbo

Malaika walikuwa wameumbwa na wema na upendo mkamilifu. Walipendana pasina budi na walimpenda Mungu wao, na walikumbushwa na pendo hili ili kuyatenda yanayompendeza Mungu. Sheria ya Mungu haikuwa nira yenye kuwahuzunisha, bali ilikuwa furaha yao kutii amri Zake, kusikia sauti ya neno Lake. Lakini katika hali hii ya amani na usafi, dhambi iliinuka pamoja na yeye aliyekuwa mkamilifu katika njia zote. Nabii anaandika kuhusu yeye, “Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako” (Ezekieli 28:17). Dhambi ni siri, kitu kisichoelezeka. Hakukuwa na sababu ya kuwepo kwake; kutaka kuielezea ni kutaka kuipa sababu, na hilo lingelikuwa kuihesabia haki. Dhambi ilionekana katika ulimwengu mkamilifu, kitu ambacho kilionyeshwa kuwa hakina kisingizio. E. G. White, The Signs of the Times, April 28, 1890. [TA 30.1; UM Aya

ya 1]

Mungu alikuwa na ujuzi wa matukio ya wakati ujao, hata kabla ya kuumbwa kwa dunia. Hakufanya makusudi yake kukidhi mabadiliko ya hali, bali aliruhusu yote yatendeke. Hakutenda ili kuleta hali fulani ya mambo, bali alijua kuwa hali kama hiyo ingelitukia. Mpango ambao unapaswa kutekelezwa juu ya kuasi kwa kiumbe yoyote wa mbinguni—hii ni siri, fumbo ambalo limefichwa tangu zamani. Na dhabihu ilitayarishwa katika makusudi ya milele ili kufanya kazi hasa ile ambayo Mungu amefanya kwa ajili ya wanadamu walioanguka. E. G. White, The Signs of the Times, March 25, 1897. [TA 30.2; UM Aya ya 2]

Kuingia kwa dhambi mbinguni hakuwezi kufafanuliwa. Ikiwa kungeweza kufafanuliwa, ingelionyesha kuwa kulikuwa na sababu fulani ya dhambi. Lakini kama ilivyokuwa kwamba hakuna kisingizio cha dhambi, chanzi chake daima kitabaki kufunikwa katika fumbo. E. G. White, The Review and Herald, March 9, 1886. [TA 31.1; UM Aya ya 3]

Mungu hakuumba uovu. Aliumba wema pekee, ambao ulikuwa vile Yeye alivyo...Uovu, dhambi, na mauti… vyote ni matokeo ya kutotii, ambako kuliasisiwa na Shetani. E. G. White, The Review and Herald, August 4, 1910. [TA 31.2; UM Aya ya 4]

### Fununu Za Awali Za Uovu

Kulikuwa na wakati ambapo Shetani alikuwa anatangamana na Mungu, na ilikuwa furaha yake kutekeleza amri za kiungu. Moyo wake ulijawa na pendo na bashasha katika kumtumikia Muumba wake, hadi alipoanza kufikiri kuwa hekima yake haikutokana na Mungu, bali ilirithiwa katika yeye, na ya kwamba alikuwa na haki kama vile Mungu alivyokuwa kupokea heshima na mamlaka. E. G. White, The Signs of the Times, September 18, 1893. [TA 31.3; UM Aya ya 5]

Ingawa Mungu alimuumba Lusifa mashuhuri na mzuri, na alimwinua katika heshima kuu miongoni mwa jeshi la malaika, bado angali hajawekwa kupita mpaka wa uwezekano wa kutenda uovu. Ilikuwa ni kutokana na Yeye, ambapo alichagua kutenda hivyo, kuvipotoa vipaji hivi. Angeliweza kubaki ndani ya kibali cha Mungu, akipendwa na kuheshimiwa na umati wa malaika wote, akiishi katika nafasi yake tukufu kwa ukarimu, upendo usio na ubinafsi, akiyatumia mamlaka yake makuu kuwabariki wengine na kumtukuza Muumba wake. Lakini kidogo kidogo, alianza kutaka heshima yake mwenyewe, na kutumia mamlaka yake kuvuta usikivu na kujisifia mwenyewe. Pia, taratibu aliwaongoza malaika ambapo aliwataka wamtumikie, badala ya kujitolea mamlaka yao yote kumtumikia Muumba wao. E. G. White, The Spirit of Prophecy 4:317. [TA 31.4; UM Aya ya 6]

Taratibu, Lusifa alianza kujiingiza katika tamaa ya kujitukuza…Ijapokuwa

utukufu wake wote ulitoka kwa Mungu, malaika huyu mwenye uwezo alianza kuuona kama vile utukufu huo umefungamanika kwake mwenyewe. E. G. White, Patriarchs and Prophets, 35. [TA 32.1; UM Aya ya 7]

### Mungu Aweka Rasmi Nafasi Halisi Ya Kristo

Kabla ya upinzani mkuu kutokea, wote hawakuwa na budi kudhihirisha mapenzi Yake, ambaye hekima na wema wake vilikuwa chemchemi ya furaha yao yote. [TA 32.2; UM Aya ya 7]

Mfalme wa mbingu alilialika jeshi la mbinguni mbele Yake, kwamba katika uwepo wao atangaze rasmi nafasi hasa ya Mwana wake, na kuwaonyesha uhusiano alioudumisha kwa viumbe wote…Mbele ya kutano la wakazi wa mbinguni Mfalme alitangaza kuwa hakuna ye yote ila Kristo, Mzaliwa pekee wa Mungu, mwenye stahiki ya kuingia katika makusudi Yake, na Kwake (Kristo) mashauri makuu ya mapenzi Yake (Baba) yalitekelezwa. E. G. White, Patriarchs and Prophets, 36. [TA 32.3; UM Aya ya 8]

Muumbaji mkuu alilikutanisha jeshi la mbinguni, kwamba katika uwepo wa malaika wote aweze kutunuku heshima ya kipekee juu ya Mwana Wake. Mwana alikuwa amekaa juu ya kiti cha enzi pamoja na Baba, na umati wa mbinguni wa malaika watakatifu uliwazunguka. Kisha Baba akajulisha kuwa ilikuwa ndani ya mamlaka Yake kwamba Kristo, Mwana Wake, anapaswa kuwa sawa na Yeye (Baba); ili kusudi po pote ulipo uwepo wa Mwana Wake, ilikuwa ndipo ulipo uwepo Wake. Neno la Mwana haikuwa budi kulitii kwa hiari kama neno la Baba. Mwana Wake alimpatia mamlaka kuamuru jeshi la mbinguni. Hasa hasa ilikuwa mamlaka ya Mwana Wake kutenda kwa umoja pamoja Naye (Baba) katika matazamio ya kuumba dunia. [TA 32.4; UM Aya ya 9]

Shetani alikuwa hasidi na mwenye wivu kwa Yesu Kristo. Pale malaika wote waliposujudu kwa Yesu kuutukuza ukuu Wake na mamlaka ya juu na utawala wa haki yake, Shetani naye alisujudu pamoja nao; lakini moyo wake ulijawa na wivu na chuki. Kristo alikuwa amechukuliwa katika mashauri mahususi juu ya mipango Yake (Baba), wakati shetani hakuyajua. Hakuelewa, wala hakuruhusiwa kujua, makusudi ya Mungu. Lakini Kristo alitambuliwa mkuu wa mbingu, uweza na mamlaka vyake kuwa sawa na Mungu Mwenyewe. [TA 33.1; UM Aya ya 10]

Shetani alidhani kuwa yeye mwenyewe alikuwa kipenzi mbinguni miongoni mwa malaika. Alikuwa ameinuliwa; lakini ... alitamani kimo sawa na Mungu Mwenyewe. Alijitukuza katika ufahari wake. Alijua kuwa alikuwa anaheshimiwa na malaika. Alikuwa na utume mahususi kuufanya. Alikuwa karibu na Muumba mkuu, na miale isiyokoma ya nuru tukufu iliyomfunika Mungu wa milele, ilikuwa inamwangaza yeye hasa. Shetani alifikiri jinsi malaika walivyotii amri yake kwa hima. Je! mavazi yake hayakuwa angavu na mazuri? Kwa nini basi Kristo

aheshimiwe mbele yake (shetani)? E. G. White, The Spirit of Prophecy 1:17, 18. [TA 33.2; UM Aya ya 11]

Malaika walikiri kwa furaha ukuu wa Kristo, na kumsujudia, wakamimina upendo na ibada yao. Lusifa alisujudu pamoja nao, lakini moyoni mwake kulikuwa na mzozo wa ajabu na katili. Kweli, haki, na ushikamanifu vilikuwa vikishindana dhidi ya husuda na wivu. Mvuto wa malaika kwa muda watakatifu ulionekana kumshawishi.... Lakini tena alijawa na kiburi katika utukufu wake mwenyewe. Tamaa yake ya ukuu ikarudi, na wivu juu ya Kristo ukaanikwa tena. E. G. White, Patriarchs and Prophets, 36, 37. [TA 34.1; UM Aya ya 12]

### Lusifa Aanza Kampeni Yake Dhidi Ya Kristo

Shetani ... alianza kazi yake ya uasi na malaika waliokuwa chini ya amri yake, akitafuta kueneza miongoni mwao roho ya kutoridhika. Na alitenda kwa njia ya udanganyifu sana kiasi kwamba wengi wa malaika walivutwa kwake kabla makusudi yake hayajajulikana kikamilifu. E. G. White, The Review and Herald, January 28, 1909. [TA 34.2; UM Aya ya 13]

Shetani ... alikuwa ametamani sana heshima iliyotukuka zaidi ambayo Mungu alikuwa ameitoa kwa Mwanawe. Alimwonea Kristo wivu, na kudhihirika kwa malaika waliomheshimu kama kerubi afunikaye kuwa hakuwa na heshima aliyopewa ambayo cheo chake kilidai. E. G. White, The Review and Herald, February 24, 1874. [TA 34.3; UM Aya ya 14]

Kwa shutuma zake, ambazo kwazo alifanya ionekane kwamba Kristo alikuwa amechukua nafasi iliyokuwa yake mwenyewe, Lusifa alipanda mbegu za kutilia shaka katika akili za malaika wengi. E. G. White, The Educational Messenger, September 11, 1908, par.1. [TA 34.4; UM Aya ya 15]

Kazi yake [Lusifa] ya udanganyifu ilifanywa kwa usiri mkubwa mno kiasi kwamba malaika waliokuwa na vyeo vya chini sana walifikiri kuwa yeye ndiye aliyekuwa Mtawala wa mbinguni. E. G. White, This Day With God, 256. [TA 35.1; UM Aya ya 16]

Malaika waliokuwa waaminifu na wa kweli walitaka malaika huyu mwenye nguvu na mwasi kumpatanisha na mapenzi ya Muumba wake. Walihalalisha tendo la Mungu la kumpa Yesu Kristo heshima, na kwa hoja zenye nguvu walitaka kumsadikisha Shetani kwamba heshima iliyokuwa kwake sasa si ndogo kuliko kabla Baba hajatangaza heshima ambayo Yeye alikuwa amempa Mwanawe. Walieleza waziwazi kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, aliyekuwako pamoja Naye kabla ya kuumbwa kwa malaika; na kwamba daima amesimama mkono wa kuume wa Mungu, na mamlaka yake ya upole na yenye upendo hayakuwa yametiliwa shaka hapo awali; na kwamba Hakuwa ametoa amri ila kile ambacho kilikuwa ni furaha kwa jeshi la mbinguni kutekelezwa. Walisihi kwamba Kristo kupokea heshima ya pekee kutoka kwa Baba, mbele ya

malaika, hakukupunguza heshima ambayo [Shetani] alikuwa nayo hapo kabla. E. G. White, The Spirit of Prophecy 1:19. [TA 35.2; UM Aya ya 17]

[Lusifa] alipata huruma ya baadhi ya washirika wake kwa kupendekeza mawazo ya ukosoaji kuhusiana na serikali ya Mungu. Mbegu hii mbaya ilitawanywa kwa njia ya ushawishi mno; na baada ya kuota na kukita mizizi katika akili za wengi, alikusanya mawazo ambayo yeye mwenyewe alikuwa ameyapandikiza kwanza katika akili za wengine, na kuyaleta mbele ya malaika wakuu kama mawazo ya wengine dhidi ya serikali ya Mungu. E. G. White, The S.D.A. Bible Commentary 4:1143. [TA 35.3; UM Aya ya 18]

Lusifa... awali alifanya majaribio yake ambayo yeye mwenyewe alijifanya kutoyatenda. Malaika ambao hangeweza kuwageuzia kikamilifu upande wake, aliwashutumu kwa kutojali maslahi ya malaika wengine. Kazi yenyewe hasa ambayo yeye mwenyewe alikuwa akiifanya, aliitupilia kwa malaika waaminifu. Ilikuwa ni sera yake kutatanisha kwa hoja za hila kuhusu makusudi ya Mungu. Kila kilichokuwa dhahiri alikifunika katika siri, na kwa upotovu wa hila alitia shaka juu ya kauli zilizo wazi kabisa za Yehova. Na cheo chake cha juu, kilichounganishwa kwa ukaribu sana na serikali ya kimungu, kilitia nguvu zaidi mipango yake. E. G. White, Patriarchs and Prophets, 41. [TA 36.1; UM Aya ya 19]

Jitihada ya kwanza kabisa ya Shetani kupindua sheria ya Mungu—iliyofanywa miongoni mwa wakazi wasio na dhambi wa mbinguni—kwa muda ilionekana kufanikiwa. Idadi kubwa ya malaika walishawishika. E. G. White, Patriarchs and Prophets, 331. [TA 36.2; UM Aya ya 20]

Serikali ya Mungu haikujumuisha wakazi wa mbinguni tu bali na malimwengu yote yalioumbwa; na Shetani alifikiri kwamba ikiwa angeweza kuwachukua wakazi wa mbinguni pamoja naye katika uasi, angeweza pia kuyachukua pamoja naye malimwengu mengine. E. G. White, The Review and Herald, March 9, 1886. [TA 36.3; UM Aya ya 21]

Hapa, kwa muda, Shetani alikuwa na fursa; naye alishangilia katika ukuu wake uliotukuka, katika jambo hili moja, kwa malaika wa mbinguni, na hata kwa Mungu mwenyewe.... [Lusifa] alikuwa amejivika katika vazi la uongo na kwa muda haikuwezekana kuliondoa, ili tabia yake lemavu iweze kuonekana. Sharti aachwe ajidhihirishe katika matendo yake ya kikatili, ya ustadi na maovu. E. G. White, The Spirit of Prophecy 4:319. [TA 36.4; UM Aya ya 22]

### Lusifa Apewa Muda Kuendeleza Kanuni Zake

Mungu katika hekima yake hakumfukuza Shetani mara moja kutoka mbinguni. Kitendo hiki kisingebadilisha kanuni zake, na kingeimarisha tu uasi wake, kwani kingemletea huruma kama anayetendewa isivyo haki; na

angebeba idadi kubwa zaidi pamoja naye. Sharti ahamishwe, na awe na muda wa kudumisha kanuni zake kikamilifu. E. G. White, The Review and Herald, March 9, 1886. [TA 37.1; UM Aya ya 23]

Shetani alilalamika juu ya kasoro zilizodhaniwa katika usimamizi wa mambo ya mbinguni, na kutopendezwa kwake akatafuta kujaza akili hito kwa malaika. Kwa sababu hakuwa mkuu, alipanda mbegu za mashaka na kutoamini. Kwa sababu hakuwa kama Mungu, alijitahidi kutia ndani ya akili za malaika wivu na kutoridhika kwake. Hivyo mbegu za mfarakano zilipandwa, baadaye zionyeshwe mbele ya mahakama za kimbingu zikitokana, si na Shetani, bali na malaika. Hivyo mdanganyifu angeonyesha kwamba malaika walifikiri kama yeye alivyofikiri. [TA 37.2; UM Aya ya 24]

Yale ambayo Shetani alikuwa ameingiza katika akili za malaika—neno hapa na neno pale—ilifungua njia kwa orodha ndefu ya mawazo ya mashaka. Kwa njia yake ya ustadi alidhihirisha mashaka kwao. Kisha, alipohojiwa, aliwashutumu wale aliowashawishi. Alitupia mabaya yote kwa wale aliowashawishi. E. G. White, The Review and Herald, September 7, 1897. [TA 37.3; UM Aya ya 25]

[Lusifa] alianza kutilia shaka sheria zilizowaongoza viumbe wa mbinguni, akidokeza kwamba ingawa sheria ni muhimu kwa wakazi wa malimwengu, malaika, wakiwa wameinuliwa zaidi, hawakuhitaji kizuizi hicho, kwa kuwa hekima yao wenyewe ilikuwa mwongozo tosha. E. G. White, Patriarchs and Prophets, 37. [TA 38.1; UM Aya ya 26]

Lusifa ... alitaka kukomesha sheria ya Mungu. Alidai kwamba viumbe wasioanguka wa mbingu takatifu hawakuhitaji sheria, bali walikuwa na uwezo wa kujiongoza na kudumisha uadilifu usio na doa. E. G. White, The Signs of the Times, April 28, 1890. [TA 38.2; UM Aya ya 27]

Hata malaika waaminifu hawakutambua kikamilifu tabia yake [Shetani]. Hii ndiyo sababu ya Mungu kutomwangamiza Shetani mara moja. Laiti kama angefanya hivyo, malaika watakatifu wasingetambua haki na pendo la Mungu. Kutilia shaka wema wa Mungu ingekuwa kama mbegu mbaya ambayo ingezaa matunda machungu ya dhambi na ole. Kwa hiyo mwanzilishi wa uovu alisitiriwa, ili aendeleze kikamilifu tabia yake. E. G. White, Christ's Object Lessons, 72. [TA 38.3; UM Aya ya 28]

### Malaika Wajadili Masuala Haya

Ingawa baadhi ya malaika walijiunga na Shetani katika uasi wake, wengine walimzuia asifanye makusudi yake, wakipigania heshima na hekima ya Mungu katika kumpa Mwana Wake mamlaka. Shetani aliwaza, ni kwa sababu gani Kristo alipewa uwezo usio na kikomo na amri ya juu kama hiyo juu yake

Shetani! E. G. White, Spiritual Gifts 3:37. [TA 38.4; UM Aya ya 29]

Shetani alikataa kusikiliza. Na kisha akageuka dhidi ya malaika waaminifu na wa kweli, akiwashutumu kama watumwa. Malaika hawa, wakiwa waaminifu kwa Mungu, walistaajabu walipoona kwamba Shetani amefaulu katika jitihada zake za kuchochea uasi. Aliwaahidi serikali mpya na bora kuliko waliyokuwa nayo wakati huo, ambayo yote yangekuwa uhuru. Idadi kubwa iliashiria kusudi lao la kumkubali Shetani kama kiongozi wao na amiri mkuu. Alipoona maendeleo yake yanafanikiwa, alijisifu kwamba bado angepaswa kuwa na malaika wote upande wake, na kwamba atakuwa sawa na Mungu Mwenyewe, na sauti yake ya mamlaka ingesikika katika kuliamuru jeshi lote la mbinguni. [TA 39.1; UM Aya ya 30]

Tena malaika washikamanifu walimwonya Shetani na kumhakikishia matokeo yatakavyokuwa ikiwa angeendelea; kwamba Yeye ambaye aliweza kuumba malaika, kwa uwezo Wake angeweza kupindua mamlaka yao yote na uasi wa kutisha. Kufikiri kwamba malaika angeleta upinzani dhidi ya sheria ya Mungu ambayo ilikuwa takatifu kama Yeye Mwenyewe! Waliwaonya waasi wazibe masikio yao wasisikie mawazo ya udanganyifu ya Shetani, na wakamshauri Shetani, na wote waliokuwa wameathiriwa naye, kumwendea Mungu na kukiri kosa lao hata kwa kuwa na wazo la kutilia shaka mamlaka Yake. E. G. White, The Spirit of Prophecy 1:20. [TA 39.2; UM Aya ya 31]

Shetani alikuwa mjanja katika kuwasilisha upande wake wa mashaka. Mara tu alipogundua kwamba mbinu hii imejulikana waziwazi, alitumia mbinu nyingine. Si hivyo kwa Mungu. [Mungu] Angetumia aina moja tu ya silaha—kweli na haki. Shetani angeweza kutumia kile ambacho Mungu hangeweza—upotovu na udanganyifu. E. G. White, The Review and Herald, March 9, 1886. [TA 39.3; UM Aya ya 32]

Utendakazi [wa Shetani] ulikuwa wa siri mno kiasi kwamba haungeweza kufanywa kuonekana mbele ya jeshi la mbinguni vile hasa ulivyokuwa.... Hali hii ya mambo ilidumu kuwepo kwa kipindi kirefu kabla Shetani hajaanikwa wazi. E. G. White, The S.D.A. Bible Commentary 4:1143. [TA 40.1; UM Aya ya 33]

Mungu katika rehema zake kuu alimvumilia Lusifa kwa muda mrefu. Mujarabu wa badiliko lake hilo hakukumshusha hadhi kutoka kwenye nafasi yake iliyotukuka pale aliporuhusu kwa mara ya kwanza roho ya kutoridhika, hata pale alipoanza kutoa madai yake ya uongo mbele ya malaika washikamanifu. Alihifadhiwa kwa muda mrefu mbinguni. Tena na tena alipewa msamaha kwa sharti la toba na kujisalimisha. E. G. White, The Great Controversy, 495, 496. [TA 40.2; UM Aya ya 34]

Roho ya kutoridhika na uadui haikuwahi kujulikana hapo awali mbinguni. Ilikuwa ni mbegu mpya, isiyojulikana, ya siri, isiyoweza kusimulika. Lusifa mwenyewe awali hakuwa anafahamu hali halisi ya mawazo yake; kwa muda

aliogopa kuweka wazi utendaji na mawazo ya akili yake; hata hivyo hakuyaondoa. Hakuona kuwa alikuwa akianguka. Lakini juhudi zile ambazo ni upendo usio na kikomo na hekima tu ndizo zingeweza kugundua, zilifanywa kumsadikisha juu ya kosa lake. Uadui wake ulithibitika kuwa bila sababu, na alifanywa aone ni nini kingekuwa matokeo ya kuendelea kufanya maasi. Lusifa alishawishika kwamba alikuwa katika makosa. Aliona kwamba amri za Mungu ni za haki, na kwamba inampasa kuzitambua hivyo mbele ya mbingu yote. [TA 40.3; UM Aya ya 35]

Kama angefanya hivi, angeweza kujiokoa yeye mwenyewe na malaika wengi. Wakati huo hakuwa ameacha kabisa uaminifu wake kwa Mungu. Ingawa alikuwa ameacha nafasi yake kama kerubi afunikaye, hata hivyo kama angekuwa tayari kumrudia Mungu, akikiri hekima ya Muumba, na kuridhika na nafasi aliyopewa katika mpango mkuu wa Mungu, angalirudishwa katika ofisi yake. Wakati uliwadia wa uamuzi wa mwisho; sharti ajisalimishe kikamilifu kwa ukuu wa kimungu au ajidhihirishe waziwazi katika uasi. Alikaribia kufikia uamuzi wa kurudi, lakini kiburi kilimzuia. E. G. White, Patriarchs and Prophets, 39. [TA 40.4; UM Aya ya 36]

### Mungu Akabiliana Na Badiliko La Shetani

Katika mabaraza ya mbinguni iliamuliwa kwamba kanuni sharti zitekelezwe ambazo hazingeharibu mara moja nguvu za Shetani; kwa maana lilikuwa ni kusudi la Mungu kuweka mambo juu ya msingi wa milele wa usalama. Muda lazima utolewe kwa Shetani kuendeleza kanuni ambazo zilikuwa msingi wa serikali yake. Ulimwengu wa kimbingu lazima uone jinsi kanuni ambazo Shetani alizitangaza kuwa bora kuliko kanuni za Mungu. Utaratibu wa Mungu sharti ulinganuliwe na utaratibu wa Shetani. Kanuni potovu za utawala wa Shetani sharti zifichuliwe. Kanuni za haki zinazoonyeshwa katika sheria ya Mungu sharti zidhihirishwe kuwa zisizobadilika, kamilifu, za milele. E. G. White, The Review and Herald, September 7, 1897. [TA 41.1; UM Aya ya 37]

Malaika waaminifu waharakisha kumwendea Mwana wa Mungu na kumjulisha yale yanayotendeka miongoni mwa malaika. Wanamkuta Baba katika shauri la pamoja na Mwanawe mpendwa, ili kuamua njia ambayo, kwa manufaa bora ya malaika waaminifu, mamlaka iliyochukuliwa ya Shetani iweze kuangamizwa milele. Mungu mkuu angeweza mara moja kumtupa mdanganyifu huyu mkuu kutoka mbinguni; lakini hili halikuwa kusudi Lake. Aliona vyema kumpatia mwasi nafasi sawa ya kupima nguvu na uwezo akiwa pamoja na Mwana Wake mwenyewe na malaika Wake washikamanifu. Katika pambano hili kila malaika angechagua upande wake mwenyewe, na kuonyeshwa kwa wote. E. G. White, The Spirit of Prophecy 1:21. [TA 41.2; UM Aya ya 38]

### Lusifa Awa Shetani

Shetani alinuia kujifanya mwenyewe kuwa kitovu cha ushawishi. Ikiwa hakuwa mwenye mamlaka kuu zaidi mbinguni, angelikuwa mwenye mamlaka kuu zaidi katika uasi dhidi ya serikali ya mbinguni. Angelikuwa mkuu, kuongoza, na siyo kuongozwa. E. G. White, The Review and Herald, April 16, 1901. [TA 42.1; UM Aya ya 39]

Wengi wa wale waliomhurumia Shetani walikuwa na mwelekeo wa kutii shauri la malaika waaminifu, na kuungama kutokuridhika kwao, na kupokelewa tena kwenye usahibu wa Baba na Mwanawe mpendwa. Kisha mwasi mkuu akatangaza kuwa anaelewa sheria ya Mungu, na kama akijisalimisha kunyenyekea katika kutii, heshima yake ingeondolewa kwake. Asingelikabidhiwa tena utume wake uliotukuka. Aliwaambia kuwa yeye mwenyewe na wao vilevile wametanga mbali mno kiasi cha kushindwa kurejea tena, na angelikabiliana na matokeo; kwa maana kusujudu katika ibada kwa Mwana wa Mungu hakuthubutu tena kamwe; kwamba Mungu asingelimsamehe, na sasa ni sharti wadai uhuru wao na kuipata kwa nguvu nafasi na mamlaka ambayo hayakukabidhiwa kwao. E. G. White, The Spirit of Prophecy 1:20, 21. [TA 42.2; UM Aya ya 40]

Kwa kadiri Shetani mwenyewe alivyohusika, ilikuwa kweli kuwa sasa ametanga mbali kuweza kurudi. Lakini si hivyo kwa wale waliokuwa wamepofushwa na madanganyo yake. Kwao shauri na maombi ya malaika waaminifu vilifungua mlango wa tumaini; na laiti kama wangelitii onyo, wangeliweza kujinasua katika mtego wa Shetani. Lakini majivuno, kumpenda kiongozi wao, na kutamani uhuru usiokuwa na masharti viliruhusiwa kuwapeperusha, na sala za pendo na rehema vya kiungu hatimaye vilikataliwa. E. G. White, Patriarchs and Prophets, 41. [TA 42.3; UM Aya ya 41]

### Malaika Waonekana Mbele Ya Baba

Jeshi lote la mbinguni liliitwa kuonekana mbele za Baba, ili kila kesi iamuliwe. Shetani bila haya alidhihirisha kutoridhika kwake kwamba Kristo anapaswa kuwekwa mbele yake. Alisimama kwa kiburi na kuhimiza kwamba awe sawa na Mungu, na aingie kwenye nia moja na Baba na kuelewa makusudi Yake (Baba). Mungu alimjulisha Shetani kwamba kwa Mwana Wake pekee Angelifunua makusudi Yake ya sirini, na Alihitaji familia yote mbinguni, hata Shetani, impe utii kamili na usiotiliwa shaka; Lakini yeye alikuwa amejionyesha kuwa hastahili mbinguni. Kisha Shetani akaonyesha kwa furaha wale waliomhurumia, wakiwa karibu nusu ya malaika wote, na kusema, hawa wako pamoja nami! Je! mtawafukuza hawa pia, na kufanya ukiwa kama huo mbinguni? Kisha akatangaza kwamba alikuwa tayari kupinga mamlaka ya Kristo, na kutetea mahali pake mbinguni kwa nguvu na uwezo, nguvu dhidi ya nguvu. E. G. White, The Spirit of Prophecy 1:22. [TA 43.1; UM Aya ya 42]

Karibia mwisho kabisa wa pambano la mbinguni, mnyang'anyi mkuu alidumu kujihesabia haki. Wakati ilipotangazwa kwamba pamoja na wenzake wote sharti afukuzwe kutoka kwenye makao ya furaha, kisha kiongozi wa waasi akaanika kwa ujasiri dharau yake kwa sheria ya Muumba. Alirudia madai yake kwamba malaika hawakuhitaji kuongozwa, bali wafuate hiari yao wenyewe, ambayo ingewaongoza kuwa sahihi. Alizishutumu amri za Mungu kama kizuizi cha uhuru wao, na akatangaza kwamba lilikuwa ni kusudi lake kuhakikisha ukomeshaji wa sheria; ili, wakiwa wamefunguliwa kutoka katika kizuizi hiki, majeshi ya mbinguni yapate kuingia kwenye hali iliyotukuka zaidi, na tukufu zaidi ya uwepo wao. [TA 43.2; UM Aya ya 43]

Kwa nia moja, Shetani na jeshi lake walimtupia Kristo kabisa lawama za uasi wao, wakitangaza kwamba ikiwa wasingelikaripiwa, wasingeliasi kamwe. E. G. White, The Great Controversy, 499, 500. [TA 44.1; UM Aya ya 44]

Ujuzi ambao Shetani na malaika walioanguka pamoja naye, kuhusiana na tabia ya Mungu, wema Wake, rehema Zake, hekima na utukufu Vyake, ujuzi huo uliifanya hatia yao isiweze kusameheka. E. G. White, The Review and Herald, February 24, 1874. [TA 44.2; UM Aya ya 45]

## SURA YA 5

## MALAIKA WAASI WATUPWA NJE, NA ADAMU NA HAWA WAANGUKA

### Vita Mbinguni

Kristo alikuwa amefanya kazi katika nyua za mbinguni ili kumshawishi Shetani juu ya kosa lake la kutisha, mpaka mwishowe yule mwovu na wasaidizi wake wakawa wameonekana katika uasi wa wazi dhidi ya Mungu Mwenyewe.—This Day with God, 256. TA 45.1; UM Aya ya 1]

Kristo, kama jemedari mkuu wa mbinguni, aliteuliwa kuwaangusha uasi.—The Review and Herald, Mei 30, 1899. [TA 45.2; UM Aya ya 2]

Ndipo kulikuwa na vita mbinguni. Mwana wa Mungu, Mfalme wa Mbingu, na malaika Zake waaminifu, walihusika katika pambano na mwasi mkuu na walioungana naye. Mwana wa Mungu na Malaika wakweli, na waaminifu walishinda; na Shetani na wasaidizi wake wakafukuzwa kutoka mbinguni.—The Spirit of Prophecy 1:23. [TA 45.3; UM Aya ya 3]

Malaika walihusika katika vita; Shetani alitaka kumshinda Mwana wa Mungu na wale waliokuwa wanyenyekevu kwa mapenzi Yake. Lakini malaika wema na wakweli walishinda, na Shetani, pamoja na wafuasi wake, walifukuzwa kutoka mbinguni.— Early Writings, 146. [TA 45.4; UM Aya ya 4]

### Matokeo ya Uasi.

Shetani alisimama kwa kustaajabu na hali yake mpya. Furaha yake ilitoweka. Aliwatazama malaika waliokuwa pamoja naye wakati fulani walikuwa na furaha sana, lakini ambao wamefukuzwa kutoka mbinguni...Sasa mambo yote yalionekana kubadilika. Muonekano ambao ulikuwa haukiakisi taswira ya Muumba wao alikuwa na huzuni na kukata tamaa. Ugomvi, migongano, na uchungu, vilikuwa miongoni mwao....Shetani sasa anaona yale matokeo ya kutisha ya uasi wake. Alitetemeka, na kuogopa kukabiliana na siku zijazo, na kutafakari mwisho wa mambo haya. [TA 46.1; UM Aya ya 5]

Saa ya nyimbo za furaha, za shangwe za sifa kwa Mungu na na Mwana

Wake mpendwa ilipokuwa ikifika. Shetani alikuwa akiongoza kwaya ya mbinguni. Alikuwa akianzisha nota/noti za kwanza, kisha jeshi lote la malaika liliungana naye, na muziki wenye utukufu ulivuma mbinguni kwa heshima ya Mungu na Mwanae mpendwa. Lakini sasa, badala ya muziki mtamu zaidi, mafarakano na maneno ya hasira yalianguka kwenye sikio la kiongozi mkuu wa waasi. Saa ya ibada ikawa inakaribia, wakati malaika wa nuru na watakatifu wanainama mbele za Baba. Yeye shetani hataungana nao tena katika wimbo wa mbinguni. Hatasujudu tena kwa kicho na kicho kitakatifu mbele ya uwepo Mungu wake wa milele [TA 46.2; UM Aya ya 6]

Shetani alitetemeka alipotazama kazi yake. Alikuwa peke yake katika kutafakari juu ya mikakati yake ya siku zilizopita, siku za sasa, na mipango yake ya baadaye. Mwili wake wenye nguvu ulitikisika kama tufani. Mara Malaika kutoka mbinguni alikuwa akipita. Naye adui huyu alimwita, na akaomba mahojiano na Kristo. Hili ombi alitunukiwa, yaani alikubaliwa. Kisha akamwambia Mwana wa Mungu kwamba alitubu uasi wake, na anataka tena fadhila za Mungu. Alikuwa tayari kuchukua mahali ambapo Mungu alikuwa amemwekea hapo awali, na kuwa chini ya amri Yake ya hekima. Kristo alilia kwa hatima ya ole wa Shetani, lakini akamwambia, kama nia ya Mungu (akili za Bwana), kwamba asingeweza kupokelewa mbinguni kamwe, kwani mbegu za uasi bado zilikuwa ndani yake. [TA 46.3; UM Aya ya 7]

Pale Shetani aliposadikishwa kabisa kwamba hakuna uwezekano ya kurudishwa kwake katika fadhila za Mungu, alidhihirisha uovu wake kwa kuongeza chuki na harara zenye moto mkali. TA 47.1; UM Aya ya 8]

Kwa vile hangeweza kupokelewa kuingia ndani ya malango ya mbinguni, angelingoja langoni, kuwadhihaki malaika na kutafuta ugomvi nao walipokuwa wakiingia na kutoka.—Spirit of Prophecy. 1:28-30. [TA 47.2; UM Aya ya 9]

**Uumbaji wa Dunia na Wanadamu.**

Malaika waaminifu waliomboleza hatima ya wale ambao walikuwa wenzao katika furaha na raha. Upotevu wao ulihisiwa mbinguni. Baba alishauriana na Yesu kuhusiana na kutekeleza mara moja kusudi lao la kumfanya mwanadamu akae duniani.— The Signs of the Times, Januari 9, 1879. [TA 47.3; UM Aya ya 10]

Wana wa nuru waliooinuliwa na wa asubuhi wenye kung'aa zaidi walitangaza... utukufu Wake [Kristo] katika uumbaji, na katika kuzaliwa Kwake kwa nyimbo za shangwe.— The Signs of the Times, Januari 4, 1883. [TA 47.2; UM Aya ya 11]

Wakati Mungu alipoiumba dunia, kulikuwa na milima, vilima, na tambarare, na kati yake kulikuwa na mito na bahari. Dunia haikuwa tambarare moja kubwa,

bali ni uwanda mmoja tu, bali mandhari ilikuwa na vilima na milima hapa na pale, sio milima iliyoinuka, na chakavu kama ilivyo sasa, bali yenye mpangilio na muonekano mzuri…Malaika walitazama na walishangilia kwa sababu ya kazi ya Mungu kazi iliyo ya ajabu na nzuri.— Spiritual Gifts 3:33. [TA 47.3; UM Aya ya 12]

Mbingu zote zilichukua shauku kubwa na ya shangwe katika uumbaji wa ulimwengu na mwanadamu. Wanadamu walikuwa kitu kipya na cha tofauti. Review and Herald, Februari 11, 1902. [TA 48.1; UM Aya ya 13]

Baada ya malaika, familia ya kibinadamu, iliyofanyizwa katika mfano wa Mungu, ndiyo kazi bora zaidi aliyoiumba.— The Review and Herald, Desemba 3, 1908. [TA 48.2; UM Aya ya 14]

Bwana ... alikuwa amemjalia Adamu nguvu za akili zilizo bora zaidi kuliko kiumbe hai chochote alichokuwa amekifanya. Uwezo wake wa kiakili ulikuwa chini kidogo kuliko ule wa Malaika.— The Review and Herald, Februari 24, 1874. [TA 48.3; UM Aya ya 15]

Mara tu BWANA kupitia Yesu Kristo alipoumba ulimwengu wetu, na kumweka Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni, Shetani alitangaza kusudi lake la kuwapatanisha na asili yake baba na mama wa ubinadamu wote (kuwapa taswira yake binadamu).— The Review and Herald, Aprili 14, 1896. [TA 48.4; UM Aya ya 16]

Pale Bwana alipomleta Hawa kwa Adamu, malaika wa Mungu walikuwa mashahidi kwenye sherehe hiyo.—In Heavenly Places, 203.. [TA 48.5; UM Aya ya 17]

Wanandoa hawa wasio na dhambi hawakuvaa mavazi ya bandia. Walikuwa wamefunikwa na nuru na utukufu, kama walivyo malaika.—The Signs of the Times, Januari 9, 1879.. [TA 48.6; UM Aya ya 18]

Mungu alimuumba mwanadamu kwa ajili ya utukufu Wake, kwamba baada ya kujaribiwa familia ya kibinadamu iweze kuwa moja na familia ya mbinguni. Ilikuwa Kusudi la Mungu la kujaza tena mbingu na familia ya wanadamu.— The S.D.A. Bible Commentary 1:1082.. [TA 48.7; UM Aya ya 19]

Nafasi zilizoachwa wazi mbinguni kwa kuanguka kwa Shetani na malaika zake zitajazwa na waliokombolewa na Bwana.— The Review and Herald, Mei 29, 1900. [TA 49.1; UM Aya ya 20]

### Adamu na Hawa Edeni

Ingawa kila kitu ambacho Mungu alikuwa ameumba kilikuwa katika utimilifu wa uzuri, na hakuna chochote kilichoonekana kupungua juu ya dunia ambacho Mungu alikuwa ameumba ili kuwafurahisha Adamu na Hawa, lakini bado

alidhihirisha Upendo Wake mkubwa kwao kwa kuandaa bustani maalumu haswa kwa ajili yao. Sehemu ya muda wao ilikuwa ya kutumiwa kwa kazi ya furaha katika kuitunza bustani, na sehemu ya kupata kutembelewa na Malaika, kusikiliza mafundisho yao, na katika tafakuri ya furaha. Kazi yao haikuwa ya kuchosha, bali ilikuwa ya kupendeza na yenye kutia nguvu.— The Signs of Times, Januari 9, 1879. [TA 49.2; UM Aya ya 21]

Malaika watakatifu ... walitoa maagizo kwa Adamu na Hawa kuhusu kazi zao, na pia kuwafundisha juu ya uasi wa Shetani na anguko lake.— The Spirit of Prophecy 1:20. [TA 49.3; UM Aya ya 22]

Adamu alisimama mbele za Mungu katika nguvu ya ubinadamu kamili, viungo vyote na uwezo wake ukiwa na uwiano mkamilifu; na alikuwa amezungukwa na mambo mazuri na mema tu, na alizungumza kila siku na malaika watakatifu.—The Spirit of Prophecy 2:88. [TA 49.4; UM Aya ya 23]

Sheria ya Mungu ilikuwepo kabla ya mwanadamu kuumbwa. Iliasiliwa kwa hali ya viumbe watakatifu; hata malaika walitawaliwa kwa hiyo.— The Signs of the Times, Aprili 15, 1886. [TA 49.5; UM Aya ya 24]

Mwanadamu alipaswa kujaribiwa na kuthibitishwa, na kama angehimili jaribu hilo la Mungu, na kubaki mwaminifu na mkweli baada ya jaribio la kwanza, hangekuwa na majaribu ya mara kwa mara; bali alipaswa kuinuliwa sawa pamoja na malaika, na hivyo kuishi milele. — The Review and Herald, Februari 24, 1874. [TA 50.1; UM Aya ya 25]

### Shetani Apanga Kusababisha Anguko la Mwanadamu

Shetani ... aliwajulisha malaika walio wafuasi wake juu ya mipango yake ya kumpokonya Mungu Adamu mtukufu na mwenzi wake Hawa. Kama angeweza, kwa njia yoyote ile, kuwadanganya ili waasi, Mungu angewafanyia fadhila nyingine ambayo kwayo wangepata kusamehewa, na kisha yeye mwenyewe na malaika wote walioanguka wangekuwa katika njia ya haki kushiriki nao rehema ya Mungu. Ikiwa hili likishindwa, wangeweza kuungana na Adamu na Hawa; kwani mara tu watakapoivunja sheria ya Mungu, wangekuwa chini ya ghadhabu ya Mungu, kama wao wenyewe. Uovu wao ungefanya wawe pia katika hali ya uasi; na wangeweza kuungana na Adamu na Hawa, kuimiliki Edeni, na kuishikilia kuwa makao yao. Na kama wangeweza kuufikia mti wa uzima katikati ya hiyo bustani, walidhani, uwezo wao ungekuwa sawa na ule wa malaika watakatifu, na hata Mungu Mwenyewe hangeweza kuwafukuza. [TA 50.2; UM Aya ya 26]

Shetani alifanya shauri na malaika zake waovu. Hawakuungana wote kwa urahisi kushiriki katika kazi hii hatari na ya kutisha. Alisema kwamba

asingemwamini hata mmoja wao kutimiza kazi hii; kwani alidhani ya kuwa yeye peke yake ndiye mwenye hekima ya kutosha kuifanikisha kazi hii muhimu sana. Aliwataka kuzingatia jambo hili wakati anapowaacha na kutafuta muda wa kupumzika ili kufanikisha, kutekeleza hilo mipango yake…….[TA 50.3; UM Aya ya 27]

Shetani alienda peke yake kupanga mipango iliyokomaa ambayo kwa hakika ingehakikisha anguko la Adamu na Hawa. Alijishughusha na mawazo ya kuighiribu jozi ya ndoa takatifu, na ya furaha kuingia katika taabu na majuto aliyokuwa nayo mwenyewe akiyavumilia. Alionekana katika hali ya kusita; kwa wakati mmoja alikuwa imara na kuamua, kisha muda mwingine akaingia kusitasita na kuyumba. Malaika zake walikuwa wakimtafuta, kiongozi wao, ili kuungana naye katika uamuzi wao. Wataungana na Shetani katika mipango yake, na pamoja naye kuwajibika na kushiriki matokeo. [TA 51.1; UM Aya ya 28]

Shetani alitupilia mbali hisia zake za kukata tamaa na udhaifu, na, kama kiongozi wao, alijiimarisha ili kulizuia jambo hilo, na kufanya kwa uwezo wake wote wa kuyapinga mamlaka ya Mungu na Mwanaye.—The Spirit of Prophecy 1:31-33. [TA 51.2; UM Aya ya 29]

Shetani alikusudia kuwa angethibitisha kwa malimwengu ambayo Mungu ameumbwa, na kwa viumbe wa mbinguni, kwamba ilikuwa ni jambo lisilowezekana kuishika sheria ya Mungu.— The Review and Herald, Septemba 3, 1901. [TA 51.3; UM Aya ya 30]

Mungu alikusanya jeshi la malaika kuchukua hatua za kuzuia tishio la uovu. Iliamuliwa katika baraza la Mbinguni kuwa Malaika waitembelee Edeni na kumwonya Adamu kuwa alikuwa hatari kutoka kwa adui. Kwa hiyo, malaika wawili walienda kwa kasi kwenda kuwatembelea wazazi wetu wa kwanza.— The Signs of the Times, Januari 16, 1879. [TA 51.4; UM Aya ya 31]

Wajumbe wa mbinguni waliwafungulia Adamu na Hawa kisa cha anguko la Shetani, na njama zake za kuwaangamiza, wakiwafunulia kwa wazi na kikamilifu zaidi juu asili ya serikali ya Mungu, ambayo mkuu uovu alikuwa anajaribu kuipindua……..[TA 51.5; UM Aya ya 32]

Malaika waliwaonya wajihadhari na hizo hila za Shetani; kwani juhudi zake za kuwatega na kuwanasa zingekuwa zisizokoma. Watakapokuwa watiifu kwa Mungu, yule mwovu asingeweza kuwadhuru; kwani, ikiwa ingelazimu, kila malaika mbinguni angetumwa kwa ajili ya msaada wao. Kama wao kwa uthabiti yaani mkazo, watakataa vidokezo vyake vya kwanza vya hila, wangekuwa salama kama walivyo wajumbe wa mbinguni. Lakini ikiwa hata mara moja tu wangekubali kushindwa na jaribu, asili yao ingepotoka kwa kuogopesha sana kiasi kwamba ndani yao wenyewe kusingekuwa na uwezo, wala mwelekeo wa kumpinga Shetani.— Patriachs and Prophets, 52, 53. [TA

51.6; UM Aya ya 33]

Malaika walimwonya Hawa asitengane na mume wake katika kazi yake; kwa maana anaweza kukutana na huyu adui aliyeanguka. Ikiwa wangetengana kila mmoja, wangekuwa katika hatari kubwa zaidi kuliko kama wote wawili wangekuwa pamoja. Malaika waliwaamuru kwa ukaribu kufuata maagizo ambayo Mungu alikuwa amewapa kuhusiana na mti ya ujuzi wa mema na mabaya; kwani katika utii mkamilifu walikuwa salama, na huyu adui aliyeanguka angeweza kuwafikia tu kupitia mti wa ujuzi wa mema na mabaya. [TA 52.1; UM Aya ya 34]

Adamu na Hawa waliwahakikishia malaika kwamba kamwe wasingeiuvunja amri ya Mungu; kwa kuwa ndiyo ilikuwa starehe na furaha yao ya juu kufanya mapenzi yake. Malaika waliungana na Adamu na Hawa katika muziki mtakatifu ulio na ulinganifu; na nyimbo zao zilipokuwa zikivuma kutoka Edeni yenye furaha, Shetani alisikia sauti zao za shangwe za ibada kwa Baba na Mwana. Na Shetani aliposikia, wivu wake, chuki, hiana na uovu, viliongezeka, na alionyesha wasiwasi wake kwa wafuasi wake wawachochee Adamu na Hawa waasi.— The Spirit of Prophecy 1:34, 35. [TA 52.2; UM Aya ya 35]

### Shetani Azungumza na Hawa Kupitia Nyoka

Ili kukamilisha kazi yake bila kujulikana, Shetani alichagua kumtumia nyoka kama chombo chake—njia iliyotumika kuficha vizuri kusudi lake la udanganyifu. Wakati huo nyoka alikuwa mmoja wa viumbe wenye hekima zaidi na viumbe wazuri zaidi duniani. Alikuwa na mabawa, na alipokuwa akiruka angani kulionyesha mwonekano wa kung'aa, wenye rangi na mng’ao wa dhahabu iliyosafishwa.— Patriachs and Prophets, 53. [TA 52.3; UM Aya ya 36]

Hawa alitoka upande wa mumewe, akitazama uzuri wa vitu vya asili katika uumbaji wa Mungu, na kufurahisha hisia zake kwa rangi na harufu ya maua na uzuri wa miti na vichaka. Alikuwa akifikiria juu ya katazo ambalo Mungu alikuwa ameliweka juu yao kwa habari ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Alifurahishwa na uzuri na fadhila ambazo Bwana alikuwa ametoa kwa ajili ya kujiridhisha katika kila hitaji. Haya yote, alisema Hawa, Mungu ametupa tufurahie. Yote ni yetu; kwa maana Mungu amesema, “Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula; bali wa mti wa ujuzi wa mema na mabaya, usile.” [TA 53.1; UM Aya ya 37]

Hawa alikuwa ametangatanga karibu na mti uliokatazwa, na udadisi wake uliamshwa kujua jinsi kifo kingeweza kufichwa katika matunda ya huu mti mzuri. Alishangaa kusikia maswali yake yakichukuliwa na kurudiwa kwa sauti ya ajabu. “Eti, hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda yote ya bustani?” Hawa hakujua kwamba alikuwa amefunua mawazo yake kwa kuzungumza mwenyewe kwa sauti (alipojiziuka), kwa hiyo alishangaa kusikia maswali yake

yakirudiwa na nyoka.— The Review na Herald, Februari 24, 1874. [TA 53.2; UM Aya ya 38]

Kwa maneno laini na ya kupendeza, na kwa sauti ya muziki, Shetani] alizungumza na Hawa anayeshangaa. Alishtuka kusikia nyoka akiwazungumza. Aliutukuza uzuri wake na uzuri wa kupita kiasi, ambao ulikuwa si wa kumchukiza Hawa. [TA 53.3; UM Aya ya 39]

Hawa alidanganywa, alibembelezwa, akasifiwa kwa udanganyifu (kwa kutia chumvi) na kuvutiwa. (alipakwa mafuta kwa chupa ya mgongo)— The Spirit of Prophecy 1:35, 36. [TA 54.1; UM Aya ya 40]

Hawa alifikiria kuwa ni kweli kwamba nyoka alikuwa na ujuzi juu ya mawazo yake, na kwamba lazima awe na hekima sana. Akamjibu, “Matunda yote ya miti ya bustani twaweza kula; bali matunda ya mti ulio katikati ya bustani, Mungu amesema, Msile, wala msiyaguse, msije mkafa. Na nyoka akasema akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa; kwa maana Mungu anajua ya kuwa siku mtakayokula, macho yenu yatafumbuliwa, nanyi mtakuwa kama mungu, mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:2-5. [TA 54.2; UM Aya ya 41]

Hapa baba wa uwongo alitoa madai yake kwa kupingana moja kwa moja na Neno la Mungu lilivyosema na kueleweza. Shetani alimhakikishia Hawa kwamba aliumbwa na uwezo wa kutokufa, na kwamba hakukuwa na uwezekano wa yeye kufa. Alimwambia kwamba Mungu alijua kwamba ikiwa wangekula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya ufahamu wao ungeangazwa, ungepanuliwa, kuboreshwa na kukuzwa, ikiwafanya waokuwa sawa na yeye Mwenyewe. Hawa alifikiri mazungumzo ya nyoka kwa busara sana. Aliutazama kwa hamu mti uliojaa matunda ambayo yalionekana kuwa ya kutamanika sana. Nyoka alikuwa akiyala kwa furaha dhahiri. [TA 54.3; UM Aya ya 42]

Hawa alikuwa amezidisha Maneno ya amri ya Mungu. Alikuwa amesema kwa Adamu na Hawa, “Lakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula utakufa hakika.” Katika mazungumzo ya Hawa na nyoka, aliongeza meneno, “Wala msiyaguse, msije mkafa. Hapa ujanja wa nyoka alionekana. Maneno hayo ya Hawa yalimpa adui faida.— The Review and Herald, February 24, 1874. [TA 54.4; UM Aya ya 43]

Kwa kula mti huu, Shetani alitangaza wangepata kuwa katika hadhi iliyotukuka zaidi, na kuingia katika uwanja mpana wa ujuzi. Yeye mwenyewe alikuwa amekula tunda lililokatazwa, na kama matokeo alikuwa amepata nguvu ya kuongea. Na alisisitiza kwamba Bwana kwa wivu alitamani kuwanyima, wasije wakainuliwa hadi kuwa sawa na Yeye Mwenyewe.—Patriarchs and Prophets, 54. [TA 55.1; UM Aya ya 44]

Udadisi wa Hawa uliamshwa. Badala ya kukimbia kutoka mahali hapo, aliendelea kusikia nyoka akiongea. Haikuingia akilini mwake kwamba anaweza kuwa adui aliyeanguka, akitmumia nyoka kama mpenyo/njia yake.—The Spirit of Prophecy 1:36. [TA 55.2; UM Aya ya 45]

Kwa shauku kubwa ya kiasi gani malimwengu (universe, galaksi zote) yote yalitazama pambano ambalo lilikuwa la kuamua nafasi ya Adamu na Hawa. Jinsi gani malaika walivyosikiliza kwa makini maneno ya Shetani, mwanzilishi wa dhambi, namna vile alivyoweka mawazo yake mwenyewe juu ya amri Zake Mungu, na akitaka kuitangua sheria ya Mungu kwa njia ya udanganyifu wake! Jinsi walivyongoja kwa hamu kuona kama wenzi hao watakatifu wangekubali kumomonyoshwa nakudanganywa na mjaribu, na kukubali na hila zake. [TA 55.3; UM Aya ya 46]

Shetani alimwakilisha Mungu kama mdanganyifu, kama Yule ambaye angeharibu Viumbe Wake kutokana na faida ya zawadi Yake kuu. Malaika walisikia kwa huzuni na mshangao kauli hii kuhusiana na tabia ya Mungu, kadiri Shetani alivyomwakilisha Mungu kama mwenye taabu; bado Hawa hakushtuka kusikia Mungu mkuu namna hiyo, akishtakiwa kwa uongo. Laiti angelikumbuka…. ishara zote za upendo Wake, laiti kama angemkimbilia mumewe, basi angalipata kuokolewa na majaribu ya hila ya yule mwovu.— The Signs la Times, May 12, 1890. [TA 55.4; UM Aya ya 47]

Mjaribu alichuma tunda na kumpa Hawa. Yeye alichukua mkononi mwake. Sasa, mjaribu alisema, ulikatazwa hata usiliguse usije ukafa. Alimwambia kwamba hatatambua tena hisia ya uovu na kifo katika kula kama ilivyo kugusa matunda. Hawa alitiwa moyo kwa sababu hakuhisi dalili za mara moja za kuchukiwa na Mungu. Aliyafikiria maneno ya mjaribu kuwa ya busara na sahihi. Alikula, akafurahishwa na tunda lile. Ilionekana lina ladha kwake, na kufikiri kwamba laiti angalitambua ndani yake matokeo ya ajabu ya tunda hilo.—The Spirit of Prophecy 1:38. [TA 56.1; UM Aya ya 48]

Hakukuwa na kitu chenye sumu katika tunda la mti wa ujuzi kwa lenyewe, hakuna kitu ambacho kingeweza kusababisha kifo katika kulila. Mti ulikuwa umewekwa katika bustani ili kuujaribu uaminifu wao kwa Mungu. —The Signs of la Times, February 13, 1896. [TA 56.2; UM Aya ya 49]

**Hawa Ala Tunda na Amjaribu Adamu**

Hawa alikula na kufikiria kwamba alihisi hisia mpya na maisha yaliyotukuka zaidi. Hakuhisi madhara yoyote kutokana na tunda hilo, hakuna chochote ambacho kinaweza kufasiriwa kuwa na maana ya kifo, lakini, ila kama vile nyoka alivyosema, hisia ya msisimko wa furana na utamu ambao yeye alifikiri ilikuwa kama malaika waliyohisi.—Testimonies for the Church 3:72. [TA 56.3; UM Aya ya 50]

Kisha akachuma tunda na kula, na kuwaza alihisi uwezo wa kuhuisha wa maisha mapya na ya hali ya juu kama matokeo ya ushawishi wa kusisimua wa matunda yaliyokatazwa. Alikuwa na msisimko wa ajabu na usio wa kawaida alipokuwa akimtafuta mumewe, huku mikono yake ikiwa imejaa tunda lililokatazwa. Alimsimulia kuhusu hotuba ya busara ya nyoka, na alitaka kuongozana naye mara moja hadi kwenye mti wa ujuzi wa mema na mabaya Akamwambia alikuwa amekula matunda, na badala ya kuhisi hisia zozote za kifo, alitambua hisia za mihemko yenye furaha nyingi, na kusisimua na hata kurukaruka. Mara tu Hawa alipokosa kutii, yeye akawa chombo chenye nguvu ambacho kingeweza kusababisha anguko la mume wake.— The Spirit of Prophecy 1:38, 39. [TA 56.4; UM Aya ya 51]

Udhihirisho wa huzuni ulikuja juu ya uso wa Adamu. Yeye alionekana kushangaa na kushtuka. Kwa maneno ya Hawa alijua kwamba huyu lazima awe adui ambaye walikuwa wameonywa dhidi yake; na kwa hukumu ya Mungu lazima afe. Hawa akamsihi ale, akirudia maneno ya nyoka, kwamba hawatakufa hakika. Alikuwa akipembua mambo kwa kufikiri kwamba hilo lazima liwe kweli, kwa kuwa hakuhisi uthibitisho wowote wa hasira ya Mungu….[TA 57.1; UM Aya ya 52]

Adamu alielewa wazi kuwa mwenzi wake alikuwa amevunja amri ya Mungu, akalipuuza katazo pekee lililowekwa juu yao kama mtihani wa uaminifu na upendo wao. Kulikuwa na mapambano ya kutisha ndani ya akili yake. Aliomboleza kwamba alikuwa amemruhusu Hawa kutangatanga kutoka kwake. Lakini sasa tendo limefanyika; na hivyo lazima yeye atengwe mbali na yule ambaye amekuwa akifurahia ushirika naye. Hili litawezekanaje kwake? Yeye aliamua kushiriki hatima yake; ikiwa ni lazima afe, atakufa pamoja naye. Baada ya yote, aliwaza, huenda maneno ya nyoka mwenye hekima yakawa ya kweli? Hawa alikuwa mbele yake, mrembo, na anaonekana kama asiye na hatia, kuliko kabla ya tendo hili la uasi. Alionyesha upendo mkubwa kwake kuliko hapo awali. Hakuna dalili ya kifo iliyoonekana ndani yake, na aliamua kuvumilia matokeo. Alinyakua matunda, na haraka akala. [TA 57.2; UM Aya ya 53]

Baada ya kosa lake, Adamu mwanzoni alijihisi anaingia katika hali ya juu ya maisha. Lakini muda mfupi mawazo ya dhambi yake yakamjaza hofu. Hewa, ambayo hadi sasa ilikuwa ya joto na hali ya kawaida, ilionekana kuwafanya wenzi hao kuwa na baridi na hatia. Upendo na amani iliyokuwa kwao ilitoweka, na mahali pake walihisi hisia ya dhambi, hofu ya wakati ujao, utupu wa nafsi.— Patriachs and Prophets, 56, 57. [TA 58.1; UM Aya ya 54]

Shetani alijigamba na kufurahia mafanikio yake. Sasa alikuwa amemjaribu mwanamke huyo kutomwamini Mungu, kuhoji hekima yake, na kutafuta kupenyeza kwake mipango ya busara yote. Na kupitia yeye pia alikuwa amesababisha kuangushwa kwa Adamu, ambaye, kwa matokeo ya upendo

wake kwa Hawa, hakuitii amri ya Mungu, kisha akaanguka pamoja naye.— The Spirit of Prophecy 1:42. [TA 58.2; UM Aya ya 55]

Shetani, malaika aliyeanguka, alikuwa ametangaza kwamba hakuna mtu angeweza kuishika sheria ya Mungu, na alielekeza kwenye kutotii kwa Adamu kuwa kunathibitisha tangazo lake.— The Signs of the Times, April 10, 1893. [TA 58.3; UM Aya ya 56]

Shetani ... kwa kiburi alijigamba kuwa ulimwengu ambao Mungu aliuumba ulikuwa utawala wake. Baada ya kumshinda Adamu, mfalme wa ulimwengu, alikuwa amepata jamii ya wanadamu kuwa raia wake, na alipaswa sasa kuimiliki Edeni, na kupafanya hapo kuwa makao yake makuu. Na angekisimamisha kiti chake cha enzi, na kuwa mfalme wa ulimwengu.— The Review and Herald, Februari 24, 1874. [TA 58.4; UM Aya ya 57]

### Baraza la Amani

Habari za anguko la mwanadamu zilienea mbinguni—kila kinubi kilitulia. Malaika walitupa taji zao kutoka katika vichwa vyao kwa huzuni. Mbinguni kulikuwa na msukosuko.—The Spirit of Prophecy 1:42. [TA 59.1; UM Aya ya 58]

Baraza lilifanyika kuamua ni nini kifanyike kwa wanandoa wenye hatia.— Spiritual Gifts 3:44. [TA 59.2; UM Aya ya 59]

Wasiwasi wa malaika ulionekana kuwa mzito wakati Yesu alipokuwa akizungumza na Baba yake. Mara tatu alijifungia ndani ya nuru ya utukufu wa Baba, na mara ya tatu alitoka kwa Baba, sasa aliweza kuonekana… Kisha akajulisha jeshi la malaika kwamba njia ya wokovu ilikuwa imepatikana kwa ajili ya mtu aliyepotea. Aliwaambia kwamba alikuwa akimsihi Baba Yake, na Yeye alikuwa amejitolea uhai Wake kuwa fidia, kuchukua hukumu ya kifo Kwake Mwenyewe, ili kwa Yeye mwanadamu apate msamaha. [TA 59.3; UM Aya ya 60]

Mara ya kwanza malaika hawakuweza kufurahi; kwani Jemedari wao hakuwaficha chochote, bali alifungua mbele yao mpango wa wokovu. Yesu aliwaambia kwamba ataacha utukufu Wake wote mbinguni, na kuonekana duniani kama mwanadamu, akijinyenyekeza kama mwanadamu,…na hivyo hatimaye, baada ya utume Wake kama Mwalimu kukamilika, angekabidhiwa mikononi mwa watu, na kustahimili karibu kila ukatili wa mtu na mateso ambayo Shetani na malaika Zake wangeweza kuwachochea wanadamu kupata kuyatenda; kwamba angekufa kifo cha kikatili zaidi, kilichowekwa kati ya mbingu na dunia kama mkosaji; kwamba atateseka saa za kutisha za uchungu, ambazo hata malaika hawangeweza kutazama, lakini wangefunika nyuso zao wasionekane. [TA 59.4; UM Aya ya 61]

Malaika wakainama mbele Zake na kumsujudia. Nao wakayatoa Maisha yao.

Yesu akawaambia kwamba kwa kifo Chake angewaokoa wengi; na kwamba maisha ya malaika yasingeweza kulilipa deni. Maisha Yake peke yake yanaweza yaliyokubaliwa na Baba kuwa fidia kwa ajili ya wanadamu.— Early Writings, 149,150. [TA 60.1; UM Aya ya 62]

Malaika wakaogopa kwamba Adam na Hawa wangenyoosha mkono, na kula matunda ya mti wa uzima, na kuwa wenye dhambi milele. Lakini Mungu akasema atawatoa wale wapotovu bustanini. Malaika waliagizwa mara moja kuilinda njia ya mti wa uzima.— Spiritual Gifts 1:22 .. [TA 60.2; UM Aya ya 63]

Malaika waliowekwa rasmi kumlinda Adamu katika Edeni nyumbani kwake, kabla ya uasi wake na kufukuzwa bustanini, sasa wakateuliwa kulinda milango ya bustani na njia ya mti wa uzima.— The Review and Herald, February 24, 1874. [TA 60.3; UM Aya ya 64]

Adamu na Hawa walipotambua jinsi sheria ya Mungu ilivyokuwa ya thamani ya juu na utakatifu, uasi/kosa ambalo lilifanya dhabihu kuwa ghali sana kuwaokoa wao na vizazi vyao kutokana na maangamizi makubwa, wao waliahidi kufa wenyewe, au Mungu aache wao na vizazi vyao wapate adhabu ya uasi wao, badala ya Mwana mpendwa wa Mungu kutoa dhabihu hiyo kubwa. [TA 60.4; UM Aya ya 65]

Adamu alijulishwa kwamba uhai wa malaika haungeweza kulilipa deni. Sheria ya Yehova, msingi wa serikali Yake mbinguni na duniani, ilikuwa takatifu kama Mungu Mwenyewe; na kwa sababu hii maisha ya malaika hayangeweza kukubaliwa na Mungu kama dhabihu kwa ajili kosa lake...Baba hangeweza kuitangua wala kuibadilisha amri ya sheria Yake kuendana na mwanadamu katika hali yake ya kuanguka. Lakini Mwana wa Mungu, ambaye alikuwa katika umoja na Baba alipomuumba mwanadamu, Ndiye pekee ambaye angeweza kufanya upatanisho kwa mwanadamu unaokubaliwa na Mungu…..[TA 60.5; UM Aya ya 66]

Wakati Adamu alipotoa sadaka, kulingana na maagizo mahsusi ya Mungu kwa ajili ya dhambi, kwa kuendana na maagizo, ilikuwa kwake adhimisho la uchungu sana. Mkono wake ulikuwa lazima uinuliwe kuutoa uhai ule ambao ni Mungu peke yake ndiye anayeweza kuutoa, na kufanya sadaka kwa ajili ya dhambi. Hiyo ikawa ni mara yake ya kwanza kushuhudia kifo. Wakati yeye alimtazama mhanga aliyetokwa na damu, aliugua kwa maumivu ya kifo, alipaswa kumtazamia kwa imani Mwana wa Mungu, ambaye mhanga huyo ulimwakilisha.—The Spirit of Prophecy 1:50-53. [TA 61.1; UM Aya ya 67]

### Adamu na Hawa Wafukuzwa Edeni

Adamu na Hawa walijulishwa kwamba itawapasa kupoteza makazi yao ya Edeni, kwani haikuwa salama kwao kubaki ndani ya bustani ya Edeni, ili wasije

katika hali yao ya dhambi, wakapata nafasi ya kuufikia mti huo ya uzima.—The Spirit of Prophecy 1:44. [TA 61.2; UM Aya ya 68]

Adamu na Hawa waliomba kwa dhati na bidii i kuendelee kubaki katika makazi ya kutokuwa na hatia na furaha yao. Walikiri kwamba wao walikuwa wamepoteza haki zote za makao hayo yenye furaha, lakini walijitolea wenyewe kwa siku zijazo kutoa utii kamili kwa Mungu. Lakini waliambiwa kwamba asili yao ilikuwa imepotoka kwa dhambi; walikuwa wamejipunguzia nguvu zao za kupinga uovu, nao walikuwa wamefungua njia kwa Shetani kupata urahisi wa kuwafikia. Kwa ujinga wao wa kutotii katika hali yao ya kutokuwa na hatia, wao walikuwa wamejianika kwenye majaribu; na sasa, katika hali hii ya hatia, wangekuwa na uwezo mdogo wa kudumisha uadilifu wao. [TA 61.3; UM Aya ya 69]

Kwa unyenyekevu na huzuni isiyo na kifani au kuelezeka, waliyaaga makazi mazuri, na wakaenda kukaa juu ya nchi, ambapo palikuwa na laana ya dhambi.— Patriachs and Prophets, 61.. [TA 62.1; UM Aya ya 70]

Malaika watakatifu walitumwa kufulikuza jozi la hao wasiotii kutoka bustani, huku malaika wengine wakiilinda njia ya mti wa uzima. Kila mmoja wa malaika hawa mwenye nguvu alikuwa na upanga unaong'aa katika mkono wake wa kulia.— Spiritual Gifts 3:45. [TA 62.2; UM Aya ya 71]

Malaika wenye nguvu, wenye miale ya nuru inayowakilisha na panga zinazowaka moto wakigeuka kila upande, wakawekwa kama walinzi wa kuilinda njia ya mti wa uzima kutokaribiwa na Shetani na wanandoa walioasi.—The Review and Herald, Februari 24, 1874. [TA 62.3; UM Aya ya 72]

Ulikuwa ni mpango makini na uliokusudiwa wa Shetani kwamba Adamu na Hawa waanguke kwa kutomtii Mungu, na kujipatia hasira Zake na kisha wale ule mti wa uzima, ili waweze kuendeleza maisha ya dhambi. Lakini malaika watakatifu walitumwa waharibu njia yao kuuendea mti wa uzima. Kuzunguka malaika hawa kuliangaza miale ya mwanga kila upande, ambayo ilikuwa na mwonekano wa panga lenye kumeta-meta.—The Spirit of Prophecy 1:44. [TA 62.4; UM Aya ya 73]

Baada ya anguko hilo, Shetani aliwaagiza malaika zake wafanye jitihada ya kipekee ili kukuza imani ya kutokufa kwa asili ya mwanadamu; na walipowashawishi watu kupokea kosa hili, waliwaongozawatu kuhitimisha kwamba mwenye dhambi angeishi katika taabu ya milele (dini ya umizimu uongo mwingine unahusika katika hili, watu huamini kwamba mtu wao aliyekufa anaishi mahali fulani na anaweza kuitwa, hili si kweli, wafu hawana fahamu kutokana na Maandiko Matakatifu).—The Spirit of Prophecy 4:354. [TA 62.5; UM Aya ya 74]

## SURA YA 6

## MALAIKA KABLA NA BAADA YA GHARIKA YA NUHU

### Mpango wa Wokovu Waelezwa Zaidi

Malaika walifanya mawasiliano na Adamu baada ya anguko lake, na kumjulisha juu ya mpango wa wokovu, na kwamba wanadamu hawakuwa katika hali isiyoweza kupata ukombozi.— Spiritual Gifts 3:52. [TA 63.1; UM Aya ya 1]

Malaika walimjulisha Adamu kwamba, kama uasi wake ulivyoleta kifo na huzuni, uzima na kutokufa vitaletwa katika nuru kupitia dhabihu ya Yesu

Kristo.— The Spirit of Prophecy 1:51. [TA 63.2; UM Aya ya 2]

Bustani ya Edeni iliendelea kuwepo duniani kwa muda mrefu baada ya mwanadamu kutengwa kutoka katika njia zake za njema na za kupendeza. Jamii ya wanadamu walioanguka dhambini kwa muda mrefu waliruhusiwa kuyatazama makazi yao walioishi hali wakiwa hawana hatia (nje yake), kuingia kwao humo kulizuiliwa tu na Malaika walinzi.- Patriachs and Prophets, 62. [TA 63.3; UM Aya ya 3]

### Ibada Iliyofanyika Kwenye Lango Lililolindwa na Makerubi

Katika lango la Paradiso linalolindwa na makerubi, utukufu wa Bwana ulidhihirishwa, na hapa walikuja waabudu wa kwanza ..Ni mahali hapa ndipo ambapo Kaini na Habili walileta dhabihu zao, na ndipo Mungu alipowashukia ili kuwasiliana nao. [TA 63.4; UM Aya ya 4]

Fikra za mashaka zisingeweza kukataa uwepo wa Edeni wakati ikionekana waziwazi, lango lake likizuiliwa kwa kulindwa na Malaika walinzi. Mpangilio wa uumbaji, kusudi la hii bustani, historia ya miti yake miwili iliyohusiana kwa karibu na hatima ya mwanadamu, zilikuwa Kweli zisizopingika. Na uwepo wa Mungu na mamlaka Yake makuu, wajibu wa sheria Yake, zilikuwa Kweli ambazo wanadamu hawakuthubutu kuhoji wakati Adamu akiwa miongoni mwao.— Patriachs and Prophets, 83, 84. [TA 64.1; UM Aya ya 5]

Kaini na Habili walikuwa wameelekezwa kuhusiana na majaliwa yaliyofanywa kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Walipaswa kutekeleza utaratibu wa utii wa unyenyekevu, unaoonyesha heshima yao kwa Mungu, na imani yao na utegemezi wao kwa Mkombozi aliyeahidiwa, kwa kuwachinja wazaliwa wa kwanza wa wanyama, na kuitoa kwa utakatifu ile damu, kama sadaka ya kuteketezwa kwa Mungu. [TA 64.2; UM Aya ya 6]

Kaini hakuwa tayari kabisa kufuata mpango wa utiifu, na kujipatia mwana-kondoo na kumtoa pamoja na mazao ya nchi. Yeye alitwaa tu matunda ya ardhi na kupuuza matakwa ya Mungu Habili alimshauri ndugu yake asije mbele ya Bwana pasipo damu ya dhabihu. Kaini akiwa mkubwa, hakumsikiliza ndugu yake. [TA 64.3; UM Aya ya 7]

Habili akaleta wazaliwa wa kwanza wa kundi lake walionona kama Mungu alivyoamuru; na kwa imani kamili ya Masihi atakayekuja, na kwa heshima ya unyenyekevu, aliitoa sadaka. Mungu akaitakabali sadaka yake. Nuru ikamulika kutoka mbinguni na kuteketeza sadaka ya Habili. Kaini hakuona udhihirisho wowote kwamba sadaka yake imekubaliwa. Akamkasikiria Mungu, pamoja na ndugu yake. Mungu akajinyenyekeza kumtuma malaika kwa Kaini ili kuzungumza naye. [TA 64.4; UM Aya ya 8]

Malaika akauliza sababu ya hasira yake, na kumjulisha kuwa kama akifanya

vyema, na kuyafuata maagizo Mungu aliyoyatoa, Atamkubali, na kuitakabali sadaka yake. Lakini kama akikataa kunyenyekea chini ya mipango ya Mungu, na kumwamini na kumtii, Hawezi kuikubali sadaka yake. [TA 64.5; UM Aya ya 9]

Malaika anamwambia Kaini kwamba Mungu hakumtendea yeye pasipo haki, au hakuna upendeleo ulioonyeshwa kwa Habili; bali hiyo ilikuwa ni kwa sababu ya dhambi yake mwenyewe, na kutotii kwa waziwazi amri za Mungu, ndio maana hakuikubali sadaka yake—na kama akifanya vyema, basi yeye angekubaliwa na Mungu. Lakini hata baada ya kuelekezwa hivyo kwa uaminifu, Kaini hakutubu. Katika wivu na chuki yake akashindana na Habili, na kumlaumu wakati Habili akiuthibitisha mpango wa Mungu, Kaini anakasirika, na hasira yake inaongezeka na kuwaka dhidi ya Habili, mpaka katika ghadhabu yake akamuua.— Spiritual Gifts 3:47-49. [TA 65.1; UM Aya ya 10]

### Adamu na Malaika Waliwafundisha Watu wa Kabla ya Gharika

Manufaa yaliyofurahiwa na wanadamu wa kipindi kile cha kabla ya gharika katika kujipatia ujuzi wa Mungu kupitia kazi Zake haujawahi kufikiwa tangu wakati huo. Na mbali na kuwa kipindi cha giza la kidini, hicho kilikuwa ndicho kipindi cha nuru kubwa. Ulimwengu wote ulikuwa na fursa ya kupokea mafundisho kutoka kwa Adamu, na wale waliomcha Mungu pia walikuwa na Kristo na malaika kama walimu wao.— Patriarchs and Prophets, 83. [TA 65.2; UM Aya ya 11]

Wanadamu waliishi karibia miaka elfu siku hizo za kabla ya gharika, na malaika waliwatembelea wakiwa na maelekezo moja kwa moja kutoka kwa Kristo.—Selected Messages 1:230. [TA 65.3; UM Aya ya 12]

### Henoko

Henoko alijifunza kutoka katika midomo ya Adamu hadithi chungu ya anguko, na hadithi ya thamani ya neema ya Mungu katika zawadi ya Mwanawe kama Mkombozi wa ulimwengu. Aliamini na kutegemea ahadi iliyotolewa. Henoko alikuwa mtu mtakatifu. Alimtumikia Mungu kwa moyo wote. Alitambua ufisadi wa jamii ya wanadamu, naye akajitenga na uzao wa Kaini, akawakemea kwa ajili ya uovu wao mkuu....Nafsi yake ilikuwa ikisumbuka kila siku alipowaona wakikanyaga mamlaka ya Mungu….Alichagua kujitenga nao na alitumia muda wake mwingi akiwa peke yake, akitoa muda kwa tafakari na maombi. Alimngoja Mungu, na kuomba kujua mapenzi yake kikamilifu zaidi, ili aweze kuyafanya. Mungu alizungumza na Henoko kupitia malaika Zake, na kumpa maelekezo ya Kimbingu. Alimjulisha kwamba hatamvumilia mwanadamu daima katika uasi wake—kwamba lilikuwa kusudi Lake kuwaangamiza wenye dhambi kwa kuleta gharika ya maji juu ya nchi. [TA 66.1; UM Aya ya 13]

Bwana alimfunulia Henoko mpango wa wokovu kikamilifu zaidi, na kwa Roho ya unabii akampeleka katika vizazi ambavyo vitaishi baada ya gharika, na kumwonyesha matukio makubwa yanayohusiana na ujio wa pili wa Kristo na mwisho wa dunia. [TA 66.2; UM Aya ya 14]

Henoko alihangaika kuhusu wafu (wale waliokufa). Ilionekana kwake kuwa wenye haki na waovu wangeenda mavumbini pamoja, na huo ungekuwa mwisho wao. Hakuweza kuona maisha ya wenye haki ngambo ya kaburi. Katika maono ya kinabii aliagizwa kuhusiana na Mwana wa Mungu, ambaye angekufa kama dhabihu ya mwanadamu, na akaonyeshwa kuja kwa Kristo katika mawingu ya mbinguni, akizungukwa na jeshi la malaika, kutoa uzima kwa wafu wema, na kuwakomboa kutoka katika makaburi yao….. [TA 66.3; UM Aya ya 15]

Henoko aliyarudia Maneno haya kwa watu kwa uaminifu yote ambayo alikuwa amefunuliwa kwake na Roho ya unabii. Wengine waliamini Maneno yake, na kuacha uovu wao kumcha na kumwabudu Mungu.— The Signs of The Times, Februari 20, 1879. [TA 67.1; UM Aya ya 16]

Henoko alichagua vipindi fulani vya kukaa peke yake, na wakati huo yeye hakuwaruhusu watu kumtafuta, kwa maana walikatiza tafakuri yake takatifu na ushirika wake na Mungu. Hakujitenga kila wakati kutoka kwa jamii ya wale waliompenda na kusikiliza maneno yake ya hekima; ila hakujitenga kabisa na waovu. Alikutana na wema na wabaya kwa nyakati tajwa, na akajitahidi kugeuza wasiomcha Mungu kutoka katika njia zao mbaya.— Spiritual Gifts 3:56. [TA 67.2; UM Aya ya 17]

Henoko aliendelea kukua kwa tabia za mbinguni zaidi wakati anapowasiliana na Bwana Mungu  akampenda Henoko, kwa sababu alimfuata Yeye kwa uthabiti, na kuuchukia uovu, akitafuta kwa bidii ujuzi kamili zaidi wa mapenzi Yake ili aweze kuyafanya. Alitamani kuungana kwa ukaribu zaidi na Mungu, ambaye alimcha, alimheshimu, na kumwabudu. Bwana hakuruhusu Henoko afe kama wanadamu wengine, bali alituma malaika Zake wamchukue mbinguni bila kuona kifo. Katika uwepo wa wenye haki na waovu, Henoko aliondolewa kwao. Wale waliompenda walifikiri kwamba huenda Mungu amempeleka katika baadhi ya maeneo yake ya mapumziko; lakini baada ya kumtafuta kwa bidii, na kutoweza kumpata, wakatoa taarifa kwamba hayupo, kwa maana Mungu alimtwaa kwenda mbinguni.— The Signs of the Times, February 20, 1879. [TA 67.3; UM Aya ya 18]

Magari ya moto ya Mungu yalitumwa kwa mtu huyu mtakatifu, naye alichukuliwa mbinguni.— The Review and Herald, Aprili19, 1870. [TA 68.1; UM Aya ya 19]

Bwana amenipa maono ya malimwengu mengine. Nilipewa mabawa, na

malaika akanihudumia kutoka mjini mpaka mahali angavu na patukufu. Kisha nikapelekwa kwenye ulimwengu uliokuwa na miezi saba. Huko nilimwona Enoko mzee mzuri, ambaye alikuwa amehamishwa. Kwa upande wake wa mkono wa kulia alikuwa na mtende mtukufu, na kwenye kila jani kuliandikwa "Ushindi." Kichwani mwake kulikuwa na shada la maua lenye kung'aa, na majani juu ya shada la maua, na katikati ya kila jani kuliandikwa "Safi," na kuzunguka shada hilo kulikuwa na mawe ya rangi mbalimbali, ambayo yaling'aa zaidi kuliko nyota, na kuakisi juu ya herufi na kuzikuza. Kwenye sehemu ya nyuma ya kichwa chake kulikuwa na upinde ambao umefungwa shada la maua, na juu ya upinde kulikuwa kumeandikwa "Utakatifu." Juu ya shada kulikuwa taji ya kupendeza iliyong'aa kuliko jua. Nilimuuliza kama hapa ndipo mahali alipochukuliwa kutoka duniani. Alisema, "Sivyo; jiji ni nyumbani kwangu, na nimekuja kutembelea mahali hapa."— Early Writings, 39, 40. [TA 68.2; UM Aya ya 20]

Henoko anawakilisha wale watakaobaki duniani na kuhamishwa kwenda mbinguni bila kuona kifo. Anawakilisha kundi ambalo litaishi katikati ya hatari za siku za mwisho, na kustahimili ufisadi wote, uovu, dhambi na makosa, na bado wasichafuliwe kabisa na uozo huo. Tunaweza kusimama kama Henoko. Kuna majaliwa kwa ajili yetu.....Malaika wa Mungu walio hodari, wanatumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu. Malaika hawa, wanapoona kwamba tunafanya yote tuwezayo kwa upande wetu kuwa washindi, watafanya, nao sehemu yao pasavyo, na nuru yao itatuangazia pande zote, na kurudisha nyuma ushawishi wa malaika waovu walio karibu nasi, na watafanya ngome kutuzunguka ambayo itakuwa kama ukuta wa moto.— The Review and Herald, Aprili 19, 1870. [TA 68.3; UM Aya ya 21]

**Nuhu**

Wale walioishi siku za Nuhu na Abrahamu walikuwa zaidi kama malaika kwa umbo, kwa uzuri na nguvu. Lakini kila kizazi kimekuwa kikizidi kuwa dhaifu.— Spiritual Gifts 1:69. [TA 69.1; UM Aya ya 22]

Zaidi ya miaka mia moja kabla ya gharika Bwana alimtuma malaika kwa Nuhu mwaminifu ili kumjulisha kuwa hangeendela tena kuwa na rehema juu ya jamii ya binadamu iliyoharibika. Lakini hangefanya bila kujua mpango Wake. Angemwagiza Nuhu, na kumfanya mhubiri mwaminifu kuuonya ulimwengu juu ya uharibifu wake unaokuja, ili wakazi wa dunia wasiwe na kisingizio.... [TA 69.2; UM Aya ya 23]

Malaika walitumwa kukusanya kutoka msituni na shambani Wanyama ambayo Mungu aliwaumba.— The Spirit of Prophecy 1:69, 72. [TA 69.3; UM Aya ya 24]

Malaika walikwenda mbele ya wanyama hawa ndipo nao wakafuata wawili

kwa wawili, dume na jike, na wanyama safi saba saba.— Spiritual Gifts 3:67. [TA 69.4; UM Aya ya 25]

Kila kitu kilikuwa tayari kwa ajili ya kufungwa kwa safina, ambako kusingewezekana kufanywa na Nuhu akiwa ndani. Malaika alionekana na watu wengi waliodhihaki akishuka kutoka mbinguni, amevikwa mwanga kama umeme. Akafunga mlango huo mkubwa wa nje, na kisha kuchukua safari yake ya kwenda mbinguni tena.—The Spirit of Prophecy 1:72. [TA 69.5; UM Aya ya 26]

### Gharika Yaja.

Licha ya maonesho yale mazito wale wa kabla ya gharika waliyoyashuhudia ya nguvu za Mungu—ya kutokea kwa njia isiyo ya asili ya wanyama wakiacha misitu na mashamba, na kuingia ndani ya safina, na ya malaika wa Mungu aliyevikwa mwanga, na utukufu wa kutisha; akishuka kutoka mbinguni na kuufunga mlango; bado walikuwa wagumu wa mioyo yao, na wakaendelea kufurahi na kucheza juu ya udhihirisho wa ishara za uweza wa Mungu. Lakini siku ya nane wingu jeusi lilikusanyika...Mvua ilishuka kutoka mawinguni juu yao. Hili lilikuwa jambo ambalo hawakuwahi kulishuhudia...Dhoruba iliongezeka kwa nguvu na uharibifu hadi maji yalionekana kutoka mbinguni kama maporomoko makuu ……Chemichemi za maji zilipasuka kutoka ardhini kwa nguvu isiyoelezeka, ikirusha mawe makubwa mamia ya futi katika anga, kisha yakadimimia ndani ya ardhi na kuzikwa..… [TA 70.1; UM Aya ya 27]

Ghasia uharibifu wa dhoruba ziliongezeka, na kulikuwa na mchanganyiko na vilio vya watu ambao walikuwa wameidharau mamlaka ya Mungu. Miti, majengo, mawe na ardhi vilitupwa kila pande. Hofu ya mwanadamu na mnyama ilikuwa juu ya maelezo. Na hata Shetani mwenyewe, ambaye alilazimika kuwa katikati ya mambo yanayotisha, aliofia uwepo wake mwenyewe. [TA 70.2; UM Aya ya 28]

Malaika hodari katika nguvu waliiongoza safina na kuihifadhi dhidi ya madhara. Kila wakati wa dhoruba hiyo ya kutisha ya siku arobaini usiku na mchana, uhifadhi wa safina ulikuwa muujiza wa nguvu kuu. — The Spirit of Prophecy 1:73, 75. [TA 70.2; UM Aya ya 29]

### Baada Ya Gharika

Kwa wasiwasi Nuhu na familia yake walitazama kupungua kwa maji. Alitamani kwenda tena juu ya nchi. Alimtuma kunguru ambaye aliruka na kurudi kutoka ndani ya safina. Naye hakupata habari aliyoitaka, na akamtuma hua, hakupata pa kutua, akarudi tena kwenye safina. Baada ya siku saba hua akatumwa tena, na jani la mzeituni likaonekana kinywani mwake, kulikuwa na furaha kubwa kwa familia hii ya watu wanane, ambayo ilikuwa na muda mrefu

imefungiwa ndani ya safina. Malaika akashuka tena na kuufungua mlango wa safina. Nuhu angeweza kuondoa kifuniko cha juu, lakini hakuweza kufuungua mlango ambao Mungu alikuwa ameufunga. Mungu alizungumza na Nuhu kupitia Malaika ambaye aliufungua mlango, akawaamuru watu wa familia/ukoo wa Nuhu watoke njeya safina, akatoka pamoja na kila kilicho hai…….[TA 71.1; UM Aya ya 30]

Baada ya Nuhu kutoka katika safina, alitazama huku na huku wanyama wenye nguvu na wakali aliowatoa katika safina; na kisha kwa familia yake yenye hesabu ya wanane, naye akaogopa sana kwamba wataangamizwa na wanyama. Lakini Bwana alimtuma malaika wake kumwambia Nuhu, "Kila mnyama wa katika nchi atawaogopa ninyi na kuwahofu, na kila ndege wa angani ,pamoja na vitu vyote vilivyojaa katika nchi, na samaki wote wa baharini; wametiwa mikononi mwenu. Kila kiendacho kilicho hai kitakuwa chakula chenu; kama nilivyowapa mboga za majani kadhalika nawepeni hivi vyote."— The Spirit of Prophecy 1:76, 78, 79. [TA 71.2; UM Aya ya 31]

**Wajenzi wa Babeli**

Baadhi ya wazao wa Nuhu upesi walianza kuasi...Wengine hawakuamini uwepo wa Mungu...Wengine waliamini Mungu Yupo...Wale waliokuwa maadui wa Mungu walihisi kuonywa kila siku kwa mwenendo wa haki na maisha ya utauwa ya wale waliopenda, waliotii, na kumwinua Mungu. Wasioamini wakashauriana wao kwa wao na wakakubaliana kujitenga na waaminio...Wakasafiri umbali kutoka kwao, na wakachagua uwanda mkubwa wa kukaa. Wakajijengea mji, kisha wakapata wazo la kujenga mnara mkubwa wa kufika mawingu, wapate....kutowatawanyika tena...Wangejenga mnara wao kwa urefu mkubwa zaidi kuliko maji yalivyozidi wakati wa Gharika.... na wangejifanya kuwa kama miungu na kuwatawala watu. [TA 72.1; UM Aya ya 32]

Walijiinua dhidi ya Mungu. Lakini Yeye hakuwaruhusu wakamilishe kazi yao. Walikuwa wameujenga mnara wao hadi urefu wa juu, wakati Bwana alipowatuma malaika wawili kuwafadhaisha katika kazi yao....Malaika walichanganya usemi wao...Baada ya haya, hakukuwa na maelewano katika kazi yao. Kukasirikiana na kutoweza kujibizana au kuwasiliana kwa kutokuelewana, na maneno mageni kati yao, wakaiacha kazi hiyo, wakatengana wao kwa wao, wakatawanyika katika nchi. Hadi wakati huu, watu walikuwa wakizungumza lugha moja. Umeme kutoka mbinguni, kama ishara ya ghadhabu ya Mungu, ulipasua kutoka juu mnara wao, na kuuangusha chini.—The Spirit of Prophecy 1:92, 93. [TA 72.2; UM Aya ya 33]

## SURA YA 7

## MALAIKA KATIKA NYAKATI ZA WAZEE WA IMANI

### Ibrahimu

Mungu alimpa Ibrahimu heshima kubwa. Malaika wa mbinguni walimtembea na kuzungumza naye kama rafiki na rafiki.— Patriachs and Prophets, 138. [TA 73.1; UM Aya ya 1]

Bwana aliwasilisha mapenzi Yake kwa Ibrahimu kupitia malaika. Kristo alimtokea, na kumpa maarifa dhahiri ya madai ya sheria ya maadili, na wokovu mkuu ambao ungetimizwa kupitia Yeye Mwenyewe.— The Review and Herald, April 29, 1875. [TA 73.2; UM Aya ya 2]

Baada ya kuzaliwa kwa Ishmaeli, Bwana alijidhihirisha tena kwa Ibrahimu, akamwambia, Agano Langu nitalifanya imara kati ya Mimi na wewe, na uzao wako baada yako, na vizazi vyao, kuwa agano la milele.” Tena Bwana alirudia kwa malaika Wake ahadi ya kumpa Sara mwana, na kwamba atakuwa mama wa mataifa mengi.—The Spirit of Prophecy 1:96. [TA 73.3; UM Aya ya 3]

Hukumu zilipokuwa karibu kushuka juu ya Sodoma, ukweli haukufichika kwake, naye akawa mwombezi kati ya Mungu na wenye dhambi. Mazungumzo

yake na malaika pia yanatoa mfano mzuri wa ukarimu. [TA 73.4; UM Aya ya 4]

Katika wakati wa joto na jua kali mzee huyu wa imani akiwa ameketi mlangoni pa hema yake, akatazama katika mazingira ya utulivu, naye akaona kwa mbali wasafiri watatu wakikaribia. Kabla ya kufika kwenye hema lake, wageni hawa walisimama, kana kwamba wanashauriana juu ya jambo la kufanya katika safari yao. Bila kusubiri wao waombe fadhila kwake, Ibrahimu alisimama upesi, na kama ilivyoonekana kwa uhakika, wao walikuwa wanaelekea kwenda upande mwingine, basi yeye akawafuata kwa haraka, na kwa uungwana mkubwa aliwasihi kibali chao cha kumngojea yeye awaletee kiburudisho cha maakuli. Kwa mikono yake mwenyewe alileta maji ili wapate kuosha mavumbi ya safari kutoka kwenye miguu yao. Yeye mwenyewe alichagua chakula chao, na walipokuwa wamepumzika chini ya kivuli tulivu, kiburudisho kikawa tayari, naye akasimama karibu nao kwa heshima wakati wao wakishiriki ukarimu wake…… [TA 74.1; UM Aya ya 5]

Ibrahimu mawazoni mwake alikuwa ameona tu wageni wake watatu ambao walikuwa wasafiri waliochoka, yeye hakudhania kuwa miongoni mwao hawa wasafiri watatu, Yupo Yule ambaye yeye anamwabudu, Yule ambaye hana dhambi. Lakini tabia ya halisi ya wajumbe wa mbinguni ilikuwa sasa imefunuliwa. Ingawa walikuwa njiani kama wahudumu wa ghadhabu, bado kwa Ibrahimu, mtu wa imani, walizinena kwanza baraka [TA 74.2; UM Aya ya 6]

Ibrahimu alikuwa amemheshimu Mungu, na Mungu akamheshimu, akimtwaa katika mashauri Yake, na kumfunulia makusudi Yake...Mungu alijua vyema kipimo cha hatia ya Sodoma; lakini alijieleza kwa jinsi ya wanadamu, ili kwamba haki ya matendo Yake iweze kueleweka. Kabla ya Yeye kwenda na kuleta hukumu juu ya waovu, basi angeenda Mwenyewe kuanzisha uchunguzi wa mwenendo wao; kama hawajapita mipaka ya rehema ya Mungu, bado angewajaalia. nafasi ya kutubu.—Patriarchs and Prophets, 138, 139. [TA 74.3; UM Aya ya 7]

### Kuangamizwa kwa Sodoma na Gomora

Wajumbe wawili wa mbinguni waliondoka, wakimwacha Ibrahimu peke yake na Yeye ambaye sasa alikuwa amemjua kuwa ni Mwana wa Mungu....Kwa heshima kubwa na unyenyekevu alihimiza ombi lake: “Nimeshika kusema na Bwana, nami ni mavumbi na majivu tu.” ....Akaja karibu na Yule mjumbe wa mbinguni, na akahimiza kwa bidii ombi lake. Ingawa Lutu alikuwa ameishi Sodoma, hakushiriki uovu wa wakazi wake. Ibrahimu alifikiri kwamba katika watu wengi walioko ndani ya jiji lazima kuwe na wengine walio waabudu wa Kweli wa Mungu. Na kwa mtazamo huu alisihi, “Hasha usifanye hivyo, ukamwue mwenye haki pamoja na mwovu, mwenye haki awe kama mwovu. Hasha; Mhukumu ulimwengu wote asitende haki?” Ibrahimu hakusihi mara

moja tu, bali mara nyingi. Ujasiri wake uliendelea kuongezeka wakati maombi yake yalipoendelea kukubaliwa, naye akaendelea mpaka akapata uhakika kwamba ikiwa hata kama wangepatikana kumi wenye haki ndani yake, jiji hilo lingeokolewa.— Partiachs and Prophets, 139, 140. [TA 75.1; UM Aya ya 8]

### Malaika Wawili Wamtembelea Lutu

Wakati wa jioni giza lilipokuwa linaingia, wageni wawili walikaribia lango la mji. Nao walionekana kama wasafiri wanaokuja kupumzika usiku huo. Hakuna hata mtu mmoja ambaye angeweza kutambua ishara kuu za hukumu zilizokuwa zimebebwa na wapita njia hao wanyenyekevu, kwa ajili ya umati huu wa watu waliokuwa wanastarehe kwa kujifurahisha (mashoga), watu hawa wasiojali hawakuwa na fununu hata kidogo katika namna ambayo wangewatendea uovu hawa wajumbe wa mbinguni, basi usiku ule ule wangefikia kilele cha mwisho cha maovu yao yaliyoleta maafa ya jiji lao lenye kiburi. Lakini alikuwapo mtu mmoja aliyeonyesha umakini na wema katika kuwajali wageni hawa, na kuwakaribisha nyumbani kwake. Lutu hakujua tabia yao halisi, lakini upole na ukarimu vilikuwa ni mazoea yake.— Partiachs and Prophets 158. [TA 75.2; UM Aya ya 9]

Malaika walimfunulia Lutu kusudi la ujio wao: "Tutapaharibu sisi mahali hapa, kwa kuwa kilio chao kimezidi mbele za BWANA; Naye Bwana ametutuma tupaharibu." Wageni ambao Lutu alijitahidi kuwalinda, sasa waliahidi kumlinda yeye, na kuwaokoa pia watu wote wa familia yake ambao wangekimbia pamoja naye kutoka katika mji ule mwovu…..Lutu akatoka kwenda kuwaonya watoto wake. Alirudia maneno ya malaika, "Ondokeni, mtoke mahali hapa; kwa sababu Bwana atauharibu mji huu." Lakini akawa kama achezaye machoni pao au kama mtu anayefanya mzaha tu…[TA 76.1; UM Aya ya 10]

Lutu akarudi nyumbani kwake kwa huzuni, na kusimulia kisa cha kushindwa kwake. Kisha malaika wakamwambia ainuke, amchukue mkewe na mabinti zake wawili waliokuwa wangali nyumbani mwake, na kuuacha mji huo
Akiwa ameduwazwa kwa huzuni, alikawiakawia, kwani hakupenda kuondoka. Kama zisingekuwa juhudi za malaika wa Mungu, wote wangeliangamia katika maangamizi ya Sodoma. Wajumbe wa mbinguni wakamshika mkono yeye na mkewe na binti zake, na kuwaongoza nje ya mji. [TA 76.2; UM Aya ya 11]

Hapa malaika waliwaacha, na kurudi Sodoma ili kukamilisha kazi yao ya maangamizi. Mwingine - Yule ambaye Ibrahimu alimsihi-alimkaribia Lutu. [TA 76.3; UM Aya ya 12]

Mkuu wa mbinguni alikuwa kando yake, hata hivyo alisihi juu ya maisha yake kana kwamba Mungu, ambaye amedhihirisha utunzaji na upendo huo kwake; asingemhifadhi. Alipaswa kumwamini kabisa Mjumbe wa Mungu, akitoa mapenzi yake na maisha yake katika mikono ya Bwana bila shaka au

swali. Lakini kama wengine wengi, yeye alijitahidi kujipangia kwa ajili yake mwenyewe….[TA 76.4; UM Aya ya 13]

Amri makini ilitolewa tena ili kuharakisha, maana tufani ya moto ingecheleweshwa kwa muda mfupi tu. Lakini mmojawapo wa wahanga hawa, yaani mke wa Lutu, alijaribu kugeuka nyuma mara moja ili kuangalia mji uliokuwa unaangamia, na mama huyu akawa mnara wa ukumbusho wa hukumu ya Mungu.— Partiachs and Prophets, 158-161. [TA 77.1; UM Aya ya 14]

### Ibrahimu Apimwa

Wakati Ibrahimu alipokuwa na umri wa karibu miaka mia moja, ile ahadi ya mwana ilirudiwa kwake, kwa uhakika kwamba mrithi wa baadaye anapaswa kuwa mtoto wa Sara…Kuzaliwa kwa Isaka, kukaleta furaha baada ya kungoja kwa muda mrefu, utimilifu wa matumaini yao ya thamani, ukaijaza hema ya Ibrahimu na Sara furaha. [TA 77.2; UM Aya ya 15]

Sara aliona tabia ya fujo ya Ishmaeli kuwa chanzo cha kudumu cha ugomvi, naye akamsihi Ibrahimu, akihimiza kwamba Hajiri na Ishmaeli watolewe nje ya boma lao. Mzee huyu wa imani aliingizwa kwenye fadhaa kubwa. Mzee akajifikiria moyoni kuwa "Je, angewezaje kumfukuza Ishmaeli mwanawe, akiwa bado anampenda?" Katika kuchanganyikiwa kwake alimsihi Bwana Mungu ampatie mwongozo. Bwana, kwa njia ya malaika mtakatifu, alimwagiza kukubali matakwa ya Sara   Na malaika alimpa ahadi ya kufariji kwamba ingawa atakuwa ametenganishwa nayo nyumba ya baba yake, Ishmaeli asingetengwa na Mungu; maisha yake yangehifadhiwa, naye atakuwa baba wa taifa kubwa. Ibrahimu alitii Neno la malaika, lakini haikuwa bila maumivu makali.— Patriarchs and Prophets, 146, 147. [TA 77.3; UM Aya ya 16]

Mungu alikuwa amemwita Ibrahimu kuwa baba wa waaminifu, na maisha yake yangesimama kama kielelezo cha imani kwa vizazi vilivyofuata. Lakini imani yake haikuwa kamilifu..…Ili aweze kufikia kiwango cha juu zaidi, Mungu alimpatia jaribio lingine, kuu kabisa ambalo mwanadamu amewahi kutakiwa kulistahimili. Katika maono ya usiku alielekezwa kwenda katika nchi ya Moria, na huko amtoe mwanawe kama kafara ya kuteketezwa sadaka juu ya mlima ambao angeonyeshwa. [TA 78.1; UM Aya ya 17]

Amri ilielezwa kwa maneno ambayo lazima yalisikika kwa uchungu sana moyoni mwa baba: "Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye,Isaka, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa." Isaka alikuwa ni nuru ya nyumba yake, faraja ya uzee wake, zaidi ya yote mrithi wa baraka iliyoahidiwa. [TA 78.2; UM Aya ya 18]

Shetani alikuwa hapo karibu kupendekeza kwamba lazima alikuwa amedanganyika, maana sheria ya Mungu inaamuru, "Usiue," na Mungu

asingeamuru kile ambacho kile hapo awali alikizuia. Akienda nje ya hema lake, Ibrahimu alitazama juu na kuona mng'ao tulivu wa mbingu iliyokuwa nyeupe bila mawingu, na akakumbuka ahadi aliyopewa karibu miaka hamsini iliyopita, kwamba uzao wake utakuwa mwingi sana usiohesabika kama nyota. Ikiwa ahadi hii ingetimizwa kupitia Isaka, ni kwa vipi auwawe basi? Ibrahimu alijaribiwa kuamini kwamba anaweza kuwa katika udanganyifu....Aliwakumbuka malaika waliotumwa kumfunulia kusudi la Mungu la kuiangamiza Sodoma, na ambao walimletea ahadi ya mwana huyu huyu, Isaka, naye alikwenda mahali ambapo mara kadhaa alikutana na wajumbe wa mbinguni, akitumaini kukutana nao tena, na kupokea maelekezo zaidi; lakini hakuna hata mmoja alikuja kumpatia msaada.— Patriarchs and Prophets, 147, 148. [TA 78.3; UM Aya ya 19]

Siku nzima alikuwa na matumaini ya kukutana na malaika atakayekuja kumbariki na kumfariji, au pengine kubatilisha amri ya Mungu, lakini hakuna mjumbe wa rehema aliyetoke…..Siku ndefu ya pili ikapita, usiku mwingine usio na usingizi wa kujidhili na maombi, na safari ya siku ya tatu ikaanza.— The Signs of the Times,Aprili 1, 1875. [TA 79.1; UM Aya ya 20]

Katika mahali palipoteuliwa walijenga madhabahu na kupanga kuni juu yake. Ndipo, kwa sauti ya kutetemeka, Ibrahimu akamfunulia mwanawe ujumbe wa Mungu. Ndipo kwa hofu kuu na mshangao Isaka alitambua hatima yake, lakini hakutoa upinzani wowote……Alikuwa mshiriki katika Imani alipoitwa atoe uhai wake kama dhabihu kwa Mungu….[TA 79.2; UM Aya ya 21]

Na sasa umefika wakati wa maneno ya mwisho ya upendo kunenwa, machozi ya mwisho kumwagwa, naye anamkumbatia kwa mara ya mwisho. Baba ananyanyua kisu ili amchinje mwanae, ndipo kwa ghafla mkono wake unashikiliwa. Malaika wa Mungu akamwaita mzee wa Imani kutoka mbinguni, "Ibrahimu, Ibrahimu!", naye anajibu kwa haraka, "Mimi hapa." Na tena sauti ikasikika, "Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa najua ya kuwa wewe unamcha Mungu, ikiwa hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee." …..[TA 79.3; UM Aya ya 22]

Mungu alimtoa Mwanawe afe kifo cha maumivu makali na aibu. Malaika walioshuhudia fedheha na uchungu wa roho ya Mwana wa Mungu hawakuruhusiwa kuingilia kati, kama ilivyokuwa kwa Isaka. Kulikuwa hakuna sauti ya kusema, "Imetosha." Ili kukomboa jamii wanadamu walioanguka, Mfalme wa utukufu alitoa uhai Wake. [TA 79.4; UM Aya ya 23]

Viumbe wa Mbinguni walikuwa mashahidi wa tukio hilo wakati imani ya Ibrahimu na utii wa Isaka vinajaribiwa…..Mbingu yote ilitazama kwa mshangao na kupendezwa kwa utiifu usioyumba wa Ibrahimu. Mbinguni yote ilishangilia uaminifu wake. Mashtaka ya Shetani yalionyeshwa kuwa ya uongo... [TA 80.1; UM Aya ya 24]

Ilikuwa vigumu hata kwa malaika kufahamu siri ya ukombozi—kufahamu kwamba Amiri Jeshi wa mbinguni, Mwana wa Mungu, lazima afe kwa ajili ya mkosaji. Wakati amri ilipotolewa kwa Ibrahimu kumtoa mwanawe, shauku ya wakazi wote wa mbinguni iliamshwa. Kwa shauku kubwa walifatilia kila hatua katika utimizwaji wa amri hii. Wakati ambapo kwa swali alilouliuza Isaka, “Yuko wapi mwana-kondoo wa sadaka ya kuteketezwa?” Ibrahimu alijibu, “Mungu atajipatia mwana-kondoo”: na wakati mkono wa baba ulipozuiwa alipokaribibia kumchinja mwanawe, na kondoo mume ambaye Mungu alijitwalia atolewe badala ya Isaka—ndipo nuru ilipoangazwa juu ya siri ya ukombozi, na hata malaika walielewa kwa uwazi zaidi majaliwa na mpango wa ajabu ambao Mungu alikuwa ameufanya kwa ajili ya wanadamu wokovu wa mwanadamu-Patriarchs and Prophets 153,154,155. [TA 80.2; UM Aya ya 25]

## Ndoa ya Isaka

Katika akili ya Ibrahimu, chaguo la mke kwa mwanawe lilikuwa jambo la umuhimu mkubwa; alikuwa na shauku ya kuona akioa mtu ambaye ambaye hatamuongoza kumwacha Mungu [TA 80.3; UM Aya ya 26]

Isaka, akitumaini hekima na mapenzi ya baba yake, aliridhika kumkabidhi jukumu hilo, akiamini pia kwamba Mungu Mwenyewe angeelekeza katika uchaguzi wa jambo hilo. Mawazo ya mzee wa Imani yaligeuka kwenda kwa jamaa za baba yake katika nchi ya Mesopotamia….Alikabidhi jambo hilo la maana kwa “mtumishi wake mzee,Eliezeri,” mtu mcha Mungu, mwenye uzoefu, na uamuzi makini, aliyekuwa amemtumikia kwa utumishi wa muda mrefu na huduma ya uaminifu……“Bwana Mungu wa mbinguni,” alisema, “aliyenitoa kutoka katika nyumba ya baba yangu, na katika nchi ya jamaa zangu, ... Yeye atampeleka malaika Wake mbele yako.” [TA 80.4; UM Aya ya 27]

Mjumbe akaondoka bila kukawia...Huko Harani, “mji wa Nahori,” akasimama nje ya kuta, karibu na kisima ambacho wanawake wa mahali pale walikuja wakati wa jioni kuteka maji....Huku akikumbuka maneno ya Ibrahimu, kwamba Mungu angemtuma malaika Wake pamoja naye, yeye aliomba kwa dhati ili kupata uongozi mzuri. Katika familia ya bwana wake alikuwa amezoea kuona matendo ya wema na ukarimu, na sasa aliomba kwamba tendo la wema liweze kumtambulisha kuonyesha msichana yule ambaye Mungu alikuwa amemchagua. [TA 81.1; UM Aya ya 28]

Muda mchache tu baada ya kutoa ombi, alipewa jibu. Miongoni mwa wanawake waliokuwa wamekusanyika pale kisimani, tabia ya adabu za mmoja, Rebeka,ilivuta usikivu wake. Alipokuwa akitoka kisimani, mgeni akaenda kumlaki, akiomba maji kutoka katika mtungi ulikokuwa begani mwake. Ombi hilo lilijibiwa kwa ukarimu, pamoja na kujitoa kuteka maji kwa ngamia pia, huduma ambayo ilikuwa desturi hata binti za wafalme kufanya kwa ajili ya

kondoo na ng'ombe wa baba zao. Kwa hivyo ishara iliyohitajika ikatolewa. [TA 81.2; UM Aya ya 29]

Ibrahimu alikuwa akiishi Beer-sheba, na Isaka, ambaye alikuwa akichunga mifugo katika nchi ya mipakani, alikuwa amerudi katika hema la baba yake ili kusubiri kuwasili kwa mjumbe kutoka Harani "Isaka akatoka ili kutafakari kondeni wakati wa jioni...Na yule mtumishi akamwambia Isaka mambo yote aliyoyafanya. Isaka akamwingiza katika ya hema ya Sara mama yake, akamtwaa Rebeka, akawa mke wake."— Patriarchs and Prophets, 171-173. [TA 81.3; UM Aya ya 30]

### Yakobo na Esau

Yakobo na Esau, wana mapacha wa Isaka, wanaonesha tofauti ya kustaajabisha; katika tabia na maisha. Tofauti hii ilitabiriwa na Malaika wa Mungu kabla ya kuzaliwa kwao. Wakati wa kujibu ombi la Rebeka kuhusu usumbufu wake alitangaza kwamba angepewa wana wawili, alimfungulia historia yao ya baadaye, kwamba kila mmoja angekuwa mkuu wa taifa lenye nguvu, lakini mmoja angekuwa mkuu kuliko mwingine, na kwamba mdogo angekuwa na ukuu. [TA 82.1; UM Aya ya 31]

Isaka..aliweka wazi kwamba Esau, kama mzaliwa wa kwanza, ndiye mwenye haki ya uzaliwa. Lakini Esau hakujali mambo ya ibada, hakuwa na mwelekeo wa kuwa na maisha ya kiroho...Rebeka alikumbuka maneno ya malaika, na...alikuwa ameshawishika kwamba urithi wa ahadi ya Mungu ulikusudiwa kwa Yakobo. Alirudia kumweleza Isaka maneno ya Malaika; lakini mapenzi ya baba yalikuwa juu ya mwana mkubwa, naye hakuyumbishwa katika kusudi lake.— Patriarchs and Prophets, 177, 178. [TA 82.2; UM Aya ya 32]

Yakobo alikuwa amejifunza kutoka kwa mama yake juu ya taarifa ya mbingu kwamba haki ya mzaliwa wa kwanza inapaswa kumwangukia, na alijawa na shauku isiyoweza kutamkwa ya faida ambayo angeipata. Haikuwa anatamani sana kumiliki mali ya baba yake; haki ya uzaliwa wa kiroho ndiyo aliyokuwa akiitamani sana. [TA 82.3; UM Aya ya 33]

Esau aliporudi nyumbani siku moja akiwa anazimia na kuchoka kwa sababu ya shughuli zake za uwindaji, mwisho ... alijitolea kutuliza njaa ya kaka yake kwa gharama ya haki ya uzaliwa wa kwanza. "Tazama, mimi ni karibu ya kufa," alipaza sauti mwindaji huyu asiyejali na, mwenye kujiendekeza na kuifurahisha nafsi yake, "itanifaa nini haki hii ya uzazi?" Na kwa mlo wa bakuli la dengu nyekundu alitupilia mbali haki yake ya mzaliwa wa kwanza……[TA 83.1; UM Aya ya 34]

Yakobo na Rebeka walifanikiwa katika kutimiza kusudi lao, lakini waliambulia tu shida na huzuni kwa udanganyifu wao. Mungu alikuwa

ametamka kuwa Yakobo angepokea haki ya mzaliwa wa kwanza, na Neno Lake lingetimizwa katika wakati Wake mwenyewe, kama wangemngoja kwa imani kufanya hivyo kwa ajili yao. [TA 83.2; UM Aya ya 35]

Alipotishiwa kifo na hasira za Esau, Yakobo akatoka nyumbani kwa baba yake akiwa mkimbizi  Usiku wa ya siku ya pili ulimkuta yuko mbali na mahema ya baba yake. Alijiona kuwa ni mtu wa kutengwa na jamii, na alijua kwamba taabu hii yote ililetwa juu yake kwa sababu ya njia yake mbaya. Giza la kukata tamaa liliusonga moyo wake, naye akashindwa kuomba. Lakini alikuwa mpweke sana kiasi kwamba alihisi hitaji la ulinzi kutoka kwa Mungu kuliko alivyowahi kuuhitaji hapo awali. Kwa kilio na majuto makuu alitubu dhambi yake, na kuomba uthibitisho fulani kwamba hajaachwa kabisa. [TA 83.3; UM Aya ya 36]

Mungu hakumwacha Yakobo...Bwana kwa huruma akafunua tu kile ambacho Yakobo alimhitaji—Mwokozi....Akiwa amechoshwa na safari yake, huyu mzururaji akajilaza chini, na jiwe likiwa kama mto wake. Alipokuwa amelala, aliona ngazi, yenye kung'aa na kumetameta, ambayo kitako chake kilisimama juu ya nchi na ncha yake ya juu ya ilifika mbinguni. Katika ngazi hii, malaika walikuwa wakipanda na kushuka; juu yake alikuwapo Bwana wa utukufu, na sauti Yake ikasikika kutoka mbinguni: “Mimi ni Bwana Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka.” [TA 83.4; UM Aya ya 37]

Katika njozi hii mpango wa ukombozi uliwasilishwa kwa Yakobo....Ngazi inamwakilisha Yesu, njia teule ya mawasiliano. Kama kwa haki yake mwenyewe asingeliziba shimo ambalo dhambi ilisababisha malaika wanaohudumia hawangeweza kuwasiliana na mwanadamu aliyeanguka. [TA 84.1; UM Aya ya 38]

Kwa imani mpya na ya kudumu katika ahadi za Mungu, na kuhakikishiwa juu ya uwepo na ulinzi wa malaika wa mbinguni, Yakobo aliendelea na safari yake hadi “nchi ya wana wa Mashariki.”— Patriachs and Prophets, 178-180, 183, 184, 188. [TA 84.2; UM Aya ya 39]

Ingawa Yakobo alikuwa ameondoka Padan-aramu kwa kulitii agizo la Mungu, alikuwa na masumbufu mengi alipokuwa akitembea tena njia ambayo alikuwa ameipita kama mkimbizi miaka ishirini kabla. Dhambi yake katika udanganyifu wa baba yake ilikuwa mbele yake daima…Kadiri alivyokaribia mwisho wa safari yake, wazo la Esau lilileta wasiwasi mwingi wa kutokea jambo baya....Kwa mara nyingine tena Bwana akampa Yakobo ishara ulinzi wa kimbingu.— Patriarchs and Prophets, 195. [TA 84.3; UM Aya ya 40]

Yakobo alipokuwa akienda zake, malaika wa Mungu walikutana naye. Na alipowaona alisema, Hili ni jeshi la Mungu. Aliwaona Malaika wa Mungu katika ndoto, wakipiga kambi kumzunguka.— Spiritual Gifts 3:127. [TA 84.4; UM Aya ya 41]

Moja kwa moja mbele yake....Yakobo, alipokuwa anaongoza njia, aliyaona majeshi mawili ya malaika wa mbinguni wakitembea kwa mtindo wa gwaride ili kumwongoza na kumlinda; na alipowaona alizungumza kwa lugha ya sifa, akisema na kushangilia, "Hili ni jeshi la Mungu." Akapaita mahali pale Mahanaimu, ambayo humaanisha majeshi mawili, au kambi mbili.— The Signs of the Times, November 20, 1879. [TA 84.5; UM Aya ya 42]

Hata hivyo Yakobo alihisi kwamba alikuwa na jambo la kufanya kwa ajili ya usalama wake binafsi. Kwa hiyo aliwatuma wajumbe na salamu za upatanisho kwa ndugu yake Lakini watumishi wakarudi na habari kwamba Esau alikuwa anakaribia na watu mia nne, na hakuna jibu lolote lililotolewa kwa ujumbe ule wa kirafiki "Ndipo Yakobo akaogopa sana na kufadhaika sana."....Kwa hiyo akawagawanya familia yake na watumishi katika makundi mawili, ili moja likishambuliwa, lingine liweze kupata nafasi ya kutoroka [TA 85.1; UM Aya ya 43]

Walikuwa wamefika sasa mto Yaboki, na usiku ulipoingia. Yakobo akaipeleka familia yake kuvuka mto, naye akabaki peke yake ng'ambo hii. Alikuwa ameamua kuutumia usiku huu katika maombi, na alitamani kuwa peke yake na Mungu. [TA 85.2; UM Aya ya 44]

Ghafla mkono wenye nguvu ukawekwa juu yake. Alidhani kwamba huyo alikuwa adui akitafuta uhai wake, naye akajitahidi kupambana kujinasua kutoka mikononi mwa mshambulizi wake. Katika giza wawili hawa walipambana ili kupata ushindi. Hakuna neno lililosemwa, lakini Yakobo aliweka nguvu zake zote, na wala hakulegeza juhudi zake hata kidogo. Alipokuwa akipigania maisha yake, wazo la hatia yake liliikandamiza roho yake; dhambi zake ziliinuka mbele yake, ili kumfungia nje mbali na Mungu. Lakini katika upeo wa taabu yake ya kutisha alizikumbuka ahadi za Mungu, na moyo ukamiminwa ili kusihi rehema Zake. Mapambano yaliendelea Hata karibu na mapambazuko, ambapo mgeni Huyu aligusa uvungu wa paja la Yakobo, nao ukalemaa pale pale. Mzee huyu wa imani sasa alitambua asili ya Mpinzani wake. Alijua kwamba alikuwa akipambana na mjumbe wa mbinguni, na hii ndiyo sababu nguvu zake zilizokaribia kupita juhudi za kibinadamu hazikupata ushindi kwake.—Patriachs and Prophets 196, 197. [TA 85.3; UM Aya ya 45]

Yule aliyeshindana mweleka na Yakobo anaitwa Mwanadamu; Hosea alimwita Yeye Malaika; wakati Yakobo akisema, "Nimemwona Mungu uso kwa uso". Inasemekana alikuwa na UWEZO pamoja na Mungu. Mkuu wa mbinguni, Ndiye ambaye alikuwa amekuja, Yule Malaika wa agano, aliyekuja kwa umbo na kuonekana kama Mwanadamu, kwa Yakobo.— The Signs of the Times, November 20, 1879. [TA 86.1; UM Aya ya 46]

Alikuwa ni Kristo, "Malaika wa agano," ambaye alikuwa amejifunua

Mwenyewe kwa Yakobo. Mzee huyu wa imani sasa alikuwa mlemavu, na mwenye maumivu mno, lakini bado hakulegeza kumshikilia kwake Bwana...Ni lazima awe na uhakika kwamba dhambi yake ilikuwa imesamehewa....Malaika alijaribu kujiachilia; Akamhimiza akisema, "Niache niende, kwa maana kunapambazuka": lakini Yakobo akajibu, Sikuachilii mpaka unibariki. Iwapo huu ungekuwa ujasiri wa majivuno na ufidhuli, Yakobo angeliangamizwa palepale mara moja; lakini ujasiri wake huu ulikuwa ni uthibitisho wa mtu ambaye anakiri kutostahili kwake, hata hivyo anatumaini katika uaminifu wa Mungu anayetunza maagano. Yakobo "alikuwa na uwezo juu ya Malaika, na akamshinda." ... [TA 86.2; UM Aya ya 47]

Wakati Yakobo alipokuwa akipigana mweleka na Malaika, mjumbe mwingine wa mbinguni alitumwa kwa Esau. Katika ndoto, Esau alimwona kaka yake akiwa uhamishoni kwa miaka ishirini mbali na nyumbani kwa baba yake; alishuhudia huzuni yake alipogundua kuwa mama yake amekufa; na alimwona amezungukwa na majeshi ya Mungu. Ndoto hii ilisimuliwa na Esau kwa askari wake, pamoja na agizo la kutomdhuru Yakobo, kwa vile Mungu wa baba yake alikuwa pamoja naye. [TA 86.3; UM Aya ya 48]

Uzoefu wa Yakobo katika usiku ule wa mieleka na uchungu inawakilisha majaribu ambayo watu wa Mungu wanapaswa kuyapitia mara tu kabla ya kuja kwa Kristo mara ya pili.—Patriarchs and Prophets, 197-201. [TA 87.1; UM Aya ya 49]

## SURA YA 8

## MALAIKA WAKATI WA KUTOKA

### Kuzaliwa Kwa Musa

Kadiri muda ulivyosonga mbele, yule mtu mkuu ambaye Misri ilikuwa inamtegemea kwa mafanikio... alikufa na kuzikwa kaburi. Basi “akainuka mfalme mpya juu ya Misri ambaye hakumjua Yusufu.” ... “Akawaambia watu wake, Angalieni, watu wa wana wa Israeli ni wengi tena wana nguvu zaidi kuliko sisi.” Amri zilitolewa ... kuwaangamiza watoto wa kiume wa Kiebrania wakati wa kuzaliwa kwao. Shetani ndiye aliyekuwa mhamasishaji wa jambo hili. Alijua kwamba mkombozi angeinuliwa miongoni mwa Waisraeli; na kwa kumwongoza mfalme kuwaangamiza watoto wao alitarajia kuharibu kusudi la kimbingu....[TA 88.1; UM Aya ya 1]

Wakati amri hii ilipokuwa ikitekelezwa kikamilifu, mtoto wa kiume alizaliwa kwa Amramu na Yokebedi....Mama alifaulu kumficha mtoto Musa, kwa miezi mitatu. Ndipo, alipogundua kwamba hangeweza tena kumweka kwa usalama, alitayarisha kisafina kidogo ya manyasi, kwa kukiziba kabisa kwa kutumia sifa na lami; na akiisha kumlaza mtoto ndani yake, alikiweka katika majani kwenye ukingo wa mto. Hakuthubutu kubaki pale kumlinda ili asipoteze uhai wa mtoto na wake mwenyewe; lakini dada yake, Miriam, alisubiri pembeni, ... akitazama kwa hamu kuona nini kingetokea kwa mdogo wake. Pia kulikuwa na watazamaji wengine. Maombi ya dhati ya mama yalikuwa yamemkabidhi mtoto wake katika uangalizi wa Mungu; na malaika wasioonekana, wakatanda juu ya mahali pale duni alikolazwa. Malaika wakamwelekeza binti Farao kwenda hapo. Udadisi wake ulichochewa na kikapu kidogo, na alipomtazama mtoto mzuri ndani yake, kwa haraka alisoma kisa husika. Machozi ya mtoto mchanga yaliamsha huruma yake, na...alidhamiria kwamba alipaswa kuokolewa; angemuasili/angemchukua kama mtoto kuwa wake mwenyewe.—Patriarchs and Prophets, 241-243. [TA 88.2; UM Aya ya 2]

Wazee wa Israeli walifundishwa na malaika kwamba wakati wao ukombozi ulikuwa karibu, na kwamba Musa ndiye mtu ambaye Mungu angemtumia ili kukamilisha kazi hii. Malaika walimwagiza Musa pia kwamba Yehova alikuwa amemchagua avunje utumwa wa watu Wake. Yeye, akidhani kwamba wangepata uhuru wao kwa nguvu ya silaha, alitarajia kuongoza jeshi la Waebrania dhidi ya majeshi ya Misri.— Patriarchs and Prophets, 245. [TA 89.1; UM Aya ya 3]

Musa alibaki ikulu hadi alipokuwa na umri wa miaka ipatayo arobaini...Siku

moja alipokuwa nje nya ikulu, akamwona Mmisri akimpiga Mwisraeli, akasogea, na kumwua yule Mmisri... na mara akauzika mwili mchangani...Musa alitoroka na kukimbia kuelekea Arabia...Baada ya muda, Musa alimwoa mmoja wa binti za Yethro; na hapa, akiwa katika utumishi wa baba mkwe wake, kama mchungaji wa mifugo yake; alidumu miaka arobaini.— Patriarchs and Prophets, 246, 247. [TA 89.2; UM Aya ya 4]

**Musa Akiwa Midiani**

Kama macho ya Musa yangefumbuliwa, angaliona wajumbe wa Mungu, malaika safi, watakatifu, wakiinama kwa upendo kwake, wakimwangazia nuru yao kando yake. — The Signs of the Times, February 19, 1880. [TA 90.1; UM Aya ya 5]

Akiwa katika shughuli zake aliona kichaka, matawi, majani na shina, vyote vikiwaka moto, lakini havikuteketea. Alikaribia ili kuona mandhari haya ya ajabu, ndipo sauti iliposema naye kutoka kwenye miale ya moto. Ilikuwa ni sauti ya Mungu. Alikuwa Yeye ambaye, kama Malaika wa Agano, alikuwa amejifunua Mwenyewe kwa wazee wa Imani katika nyakati zilizopita. Mwili wa Musa ulitetemeka, alifurahi sana kwamba Bwana alimwita kwa jina lake. Kwa midomo inayotetemeka akajibu, “Mimi hapa. Alionywa asimwendee Muumba wake pasipo kicho: “Vua viatu vyako miguuni mwako; kwa kuwa mahali uliposimama ni mahali patakatifu.” “Musa akauficha uso wake; kwa maana aliogopa kumtazama Mungu.”— The Signs of the Times, Februari 26, 1880. [TA 90.2; UM Aya ya 6]

Musa akashika njia pamoja na mkewe na watoto wake kwenda Misri...Wakiwa njiani kutoka Midiani, Musa alipata mshtuko na onyo la kutisha la ghadhabu ya Bwana. Malaika alimtokea kwa njia ya vitisho, kana kwamba angemharibu pale pale. Hakuna maelezo yaliyotolewa; lakini Musa akakumbuka kwamba alikuwa amepuuzia mojawapo ya matakwa ya Mungu; kwa kusikiliza ushawishi wa mke wake, alikuwa amepuuza kufanya kaida ya tohara kwa mtoto wao mdogo. Alikuwa ameshindwa kutimiza masharti ambayo mtoto wake angeweza kustahiki baraka za agano la Mungu pamoja na Israeli....Sipora, akiogopa kwamba mumewe atauawa. alifanya tohara hii mwenyewe, na kisha malaika akamruhusu Musa kuendelea na safari yake. Katika utume wake kwa Farao, Musa alipaswa kuwa katika nafasi ya hatari kubwa; maisha yake yangeweza kuhifadhiwa tu kupitia ulinzi wa malaika watakatifu. Lakini kama akiishi kwa kupuuzia wajibu unaojulikana, basi yeye asingekuwa salama; kwa maana malaika wa Mungu wasingemlinda.—Patriarchs and Prophets, 255, 256. [TA 90.3; UM Aya ya 7]

Haruni, akiongozwa na malaika, akatoka kwenda kumlaki ndugu yake; ambaye alikuwa ametengana naye kwa muda mrefu; nao walikutana katika

upweke wa nyikani, karibu na Horebu...Wakasafiri pamoja mpaka Misri; na walipofika nchi ya Gosheni, walianza kuwakusanya wazee wa Israeli.—Patriarchs and Prophets, 257. [TA 91.1; UM Aya ya 8]

### Mapigo ya Misri

Musa na Haruni walikuwa wawakilishi wa Mungu kwa mfalme mwenye jeuri, mkaidi, na makuhani wasiotubu, waliokuwa wamedumu katika uasi, walioshirikiana wenyewe na malaika waovu. Farao na watu wakuu wa Misri walikuwa si wajinga kuhusiana na serikali yenye hekima ya Mungu. Nuru angavu ilikuwa ikimulika katika nyakati zote, ikielekeza kwa Mungu, na kwa serikali Yake ya haki, na kwa madai ya sheria Yake. Yusufu na wana wa Israeli kule Misri walikuwa wameweka wazi maarifa ya Mungu. Hata baada ya watu wa Israeli kuwekwa utumwani kwa Wamisri, sio wote waliochukuliwa kuwa watumwa. Wengi waliwekwa katika vyeo vya maana, na hao walikuwa mashahidi wa Mungu.— The Youth's Instructor, Aprili 8, 1897. [TA 91.2; UM Aya ya 9]

Shetani ... hali akijua vizuri kwamba Musa alichaguliwa na Mungu kuvunja nira ya utumwa juu ya wana wa Israeli ……naye akashauriana na malaika zake jinsi ya kukamilisha kazi ambayo ilipaswa kujibu makusudi mawili: 1. Kuharibu ushawishi wa kazi utakaofanywa na Mungu kwa njia ya mtumishi wake Musa, kwa kufanya kazi kupitia mawakala wake, na hivyo kuikabili kazi ya Kweli ya Mungu; 2. Kuwa na ushawishi kwa kazi yake kupitia wachawi ambayo ingeendelea kupitia zama zote na kuharibu katika mawazo ya wengi imani ya Kweli katika miujiza mikuu na kazi zitakazofanywa na Kristo wakati atakapokuja katika ulimwengu huu.—Testimonies for The Church 1:291. [TA 92.1; UM Aya ya 10]

Musa na Haruni waliingia katika nyua za mfalme wa Misri...... mbele ya mfalme ambaye alikuwa na ufalme wenye nguvu zaidi uliowahi kuwepo enzi hizo, wakasimama kama wawakilishi wawili wa jamii ya watumwa, kuirudia amri kutoka kwa Mungu kwa ajili ya kuwekwa huru kwa Israeli. Mfalme alidai muujiza, katika ushahidi wa maagizo yao waliyopewa na mbingu……Haruni sasa akaitwaa ile fimbo, akaitupa chini mbele ya Farao. Nayo Ikawa nyoka. Mfalme alituma watu waitwe "wenye hekima na wachawi," ambao 'walitupa chini kila mtu fimbo yake, nazo pia zikawa nyoka; lakini fimbo ya Haruni ikameza fimbo zao." ... [TA 92.2; UM Aya ya 11]

Kiuhalisia waganga hao hawakufanya fimbo zao kuwa nyoka wa kiukweli; lakini kwa uchawi, wakisaidiwa na mdanganyifu mkuu, waliweza kutengeneza mwonekano wa macho kama huo. Ilikuwa nje ya uwezo wa Shetani kubadili fimbo kuwa nyoka walio hai (kuumba). Mkuu wa uovu, ingawa ana kila hekima na uwezo wa malaika aliyeanguka, yeye hana uwezo wa kuumba, au kutoa uhai;

hii ni haki ambayo ni Mungu pekee Ndiye anailimili (mmiliki Wake). Lakini yote yaliyokuwa ndani ya uwezo wa Shetani kufanya, aliyafanya; akiigiza kile kilichokuwepo. Kwa macho ya kibinadamu fimbo zilibadilishwa kuwa nyoka....Hapakuwa na muonekano wa kuwatofautisha na yule nyoka aliyetokana na Musa. Ingawa Bwana alimfanya nyoka wa kweli ameze wa uongo, lakini hata hili lilionwa na Farao, kuwa si kazi ya nguvu za Mungu, bali ni matokeo ya aina ya uchawi ulio bora kuliko ule wa watumishi wake. [TA 92.3; UM Aya ya 12]

Farao alitaka kuhalalisha ukaidi wake katika kuipinga amri ya Mungu, na kwa hivyo alikuwa akitafuta kisingizio cha kupuuza miujiza ambayo Mungu alikuwa ameifanya kupitia kwa Musa. Shetani alimpa kile alichokitaka. Kwa kazi aliyoifanya kupitia kwa waganga, akawafanya Wamisri waone kuwa Musa na Haruni walikuwa waganga na wachawi tu, na kwamba ujumbe wao ulioletwa haukuweza kudai heshima kama unaotoka kwa Mungu mkuu. Hivyo uwongo wa Shetani ulifanikisha kusudi lake, la kutia moyo Wamisri katika uasi wao, na kuufanya moyo wa Farao kuwa mgumu dhidi ya usadikidho. Shetani alikusudia pia kuitikisa imani ya Musa na Haruni kuhusu asili ya kimbingu ya utume wao.— Patriarchs and Prophets, 263, 264. [TA 93.1; UM Aya ya 13]

Wakati miujiza ilipofanywa mbele ya mfalme, Shetani alikuwa kando ili kukabiliana na ushawishi wake na kumzuia Farao kukiri ukuu wa Mungu na kutii agizo lake. Shetani alifanya kwa uwezo wake wote kuiga kazi ya Mungu na kuyapinga mapenzi Yake. Matokeo yalikuwa tu ni kuandaa njia ya udhihirisho mkubwa zaidi wa uwezo na utukufu wa Mungu, na kufanya dhahiri zaidi, kwa Waisraeli na kwa Misri yote, uwepo wa enzi kuu ya Mungu wa Kweli na aliye hai.— Patriarchs and Prophets, 334. [TA 93.2; UM Aya ya 14]

Dhoruba, pigo la saba, ikaja siku ya pili yake kama ilivyoamriwa, radi na mvua ya mawe, na moto ukachanganyikana nayo, na ukaangamiza kila kitu. mimea, ikavunjavunja miti, na kuwapiga wanadamu na wanyama. Hadi sasa hakuna maisha ya Wamisri yaliyokuwa yamechukuliwa, lakini sasa kifo na ukiwa vilifuata mkondo wa yule malaika mwenye kuharibu. Ardhi ya Gosheni pekee ndiyo iliyoachwa bila maafa/uharibifu.— The Signs of the Times, Machi 18, 1880. [TA 94.1; UM Aya ya 15]

Bwana kwa mkono wa Musa akawapa wana wa Israeli maagizo juu ya kuondoka kwao Misri, na hasa kwa ajili ya kuhifadhiwa kwao dhidi na hukumu inayokuja. Kila familia, peke yake au kushirikiana na nyingine, ilipaswa kumchinja mwana-kondoo au mwana-mbuzi “asiye na ila,” na kwa kutumia tawi la hisopo kunyunyiza damu yake katika “kizingiti cha juu na miimo miwili ya ya mlango” wa nyumba yao, ili malaika mwenye kuharibu akija usiku wa manane, asiingie katika makazi hayo. [TA 94.2; UM Aya ya 16]

Bwana alitangaza: “Maana Nitapita katika nchi ya Misri usiku huo, Nami nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazokuwamo; na Nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, lisiwapige pigo lolote likawaangamiza.”— Patriarchs and Prophets, 274. [TA 94.3; UM Aya ya 17]

Wana wa Israeli walikuwa wamefuata maelekezo waliyopewa na Mungu; na wakati malaika wa mauti alipokuwa akipita nyumba hadi nyumba kati ya Wamisri, wote walikuwa tayari kwa safari yao.— The Spirit of Prophcy 1:204. [TA 94.4; UM Aya ya 18]

Katika usiku wa manane kila nyumba ya Wamisri iliamshwa kutoka usingizini kwa kilio cha uchungu. Waliogopa kwamba wote watakufa. Walikumbuka kilio cha uchungu na maombolezo yaliyosikika kwa Waebrania kwa sababu ya amri isiyo ya kibinadamu ya mfalme katili ya kuua watoto wao wote wa kiume mara tu walipozaliwa. Wamisri hawakuweza kumwona yule malaika mwenye kulipiza kisasi, aliyeingia katika kila nyumba na kuleta pigo la kifo, bali walijua kwamba alikuwa ni Mungu wa Waebrania aliyesababishia mateso kama yale waliyowaletea Waisraeli.— The Youth’s Instructor, Mei 1, 1873. [TA 94.5; UM Aya ya 19]

**Kristo, Kiongozi Asiyeonekana wa Israeli**

Huko Misri taarifa ilienea kwamba wana wa Israeli ... walikuwa wakisonga mbele kuelekea Bahari ya Shamu ……..Farao akakusanya majeshi yake ... na akiwa na watu wakuu wa milki yake, aliongoza mashambulizi ya jeshi. [TA 95.1; UM Aya ya 20]

Waebrania walikuwa wamepiga kambi kando ya bahari …..Ghafla waliziona kwa mbali silaha zinazometammeta na magari ya farasi yanayotembea vikiashiria vikosi vya mbele vya jeshi kubwa ….Hofu ilijaa mioyoni mwa Israeli. Wengine walimlilia Bwana, lakini walio wengi waliharakisha kwa Musa pamoja na malalamiko yao...Jibu lake la utulivu na la uhakika kwa watu lilikuwa, “Msiogope, simameni tu, mkauone wokovu wa Bwana.” ... [TA 95.2; UM Aya ya 21]

Nguzo ya ajabu ya wingu, Ilifuatwa kama ishara ya Mungu kusonga mbele; lakini sasa wakaulizana wao kwa wao iwapo inaweza iashirie balaa fulani kubwa; kwa sababu, isingewaongoza kwenye upande mbaya wa mlima, kwa njia isiyopitika? Hivyo malaika wa Mungu alionekana kwa akili zao zilizodanganyika kama dalili ya maafa. [TA 95.3; UM Aya ya 22]

Lakini sasa, jeshi la Wamisri lilipowakaribia, wakitarajia kuwafanya kuwa mawindo rahisi, nguzo ya mawingu ilipanda kwa utukufu katika mbingu, ikapita juu ya Waisraeli, na kushuka kati yao na majeshi ya Misri. Ukuta wa giza

ukatenga kati ya wale wanaofuatwa na wafuatiliaji. Wamisri hawakuweza tena kuitambua kambi ya Waebrania, wakalazimika kusimama. Lakini kadiri giza la usiku lilivyozidi, ile nguzo ya wingu ikawa nuru kuu kwa Waebrania, ikiifunika kambi yote kwa mwangaza wa mchana. [TA 95.4; UM Aya ya 23]

Ndipo tumaini likarudi katika mioyo ya Israeli. Musa akainua sauti yake kwa Bwana. "Bwana akamwambia Musa, ...waambie na wana wa Israeli, waendelee mbele. Nawe inua fimbo yako, na ukanyoshe mkono wako juu ya bahari, na kuigawanya; nao wana wa Israeli watapita katikati ya bahari katika nchi kavu." ... [TA 96.1; UM Aya ya 24]

"Wamisri wakawafuatia, wakaingia nyuma yao hata katikati ya bahari, na farasi wote wa Farao, na magari yake, na wapanda farasi wake. Ikawa katika zamu ya alfajiri Bwana akalitazama jeshi la Wamisri katika nguzo ya moto na ya wingu; na akalifadhaisha jeshi la Wamisri."— Patriarchs and Prophets, 283-287. [TA 96.2; UM Aya ya 25]

Malaika wa Mungu walipita katikati ya jeshi lao na kuondoa magurudumu ya gari lao la vita.—The Spirit Of Prophecy 1:209. [TA 96.3; UM Aya ya 26]

Wamisri walishikwa na mkanganyiko na hofu ..., walijaribu kurudi nyuma, na kukimbilia ufukweni ambako walikuwa wametoka. Lakini Musa akanyosha fimbo yake juu, na maji yaliyorundikana, yakivuma na kuunguruma, yakiwa na hamu ya mawindo yake, yaliharakisha kwa pamoja na kulimeza Jeshi la Misri ndani ya vilindi vyake vya giza.— Patriarchs and Prophets, 287. [TA 96.4; UM Aya ya 27]

Kiongozi wa Waisraeli alikuwa jemadari mkuu wa majeshi. Malaika Wake, wanaotenda agizo Lake, walitembea pande zote mbili za lile jeshi kubwa la Israeli, na hakuna madhara yaliyoweza kuwapata. Israel ilikuwa salama....Ndipo ukaja wimbo mtakatifu wa ushindi, ukiongozwa na Miriamu.—The Review na Herald, June 1, 1897. [TA 97.1; UM Aya ya 28]

Yesu alikuwa malaika aliyefunikwa katika ya nguzo ya wingu mchana na nguzo ya moto wakati wa usiku.— The Review and Herald, June 17, 1890. [TA 97.2; UM Aya ya 29]

## SURA YA 9

## Malaika Katika Kuzunguka-zunguka kwa Israeli Jangwani

Kristo alikuwa Malaika aliyeteuliwa na Mungu kwenda mbele ya Musa jangwani, kuwaongoza Waisraeli katika safari yao hadi nchi ya Kanaani.— The Review and Herald, Mei 6, 1875. [TA 98.1; UM Aya ya 1]

Katika njia yote ya uongozi wa Mungu, Waisraeli walikuwa wakipata maji ya kuwaburudisha wenye kiu, mkate kutoka mbinguni ili kushibisha njaa yao; na amani na usalama chini ya wingu lenye kivuli mchana na nguzo ya moto usiku. Malaika walikuwa wakiwahudumia walipokuwa wakipanda juu ya njia zenye mawe, au kupitia njia zenye taabu jangwani.— The Signs of the Times, Oktoba 21, 1880. [TA 98.2; UM Aya ya 2]

Mungu alionyesha utunzaji Wake mkuu na upendo Wake mkuu kwa watu Wake kwa kuwapa mkate kutoka mbinguni. "Mwanadamu alikula chakula cha malaika": yaani, chakula walichopewa na malaika.—The Spirit of Prophecy 1:226. [TA 98.3; UM Aya ya 3]

## Israeli Huko Sinai

Na sasa mbele yao katika ukuu wenye taadhima mlima Sinai uliinuka kwa muonekano mkubwa. Nguzo ya wingu ilisimama juu ya kilele chake, na watu walitandaza hema zao kwenye uwanda wa chini. Hapa pakawa makazi yao kwa karibu mwaka mzima. Usiku nguzo ya moto iliwahakikishia ulinzi wa Mungu, na wakiwa wamegubikwa na usingizi, mkate wa mbinguni ukaanguka taratibu katika kambi [TA 98.4; UM Aya ya 4]

Muda mfupi tu baada ya kupiga kambi pale Sinai, Musa aliitwa apande mlimani ili kukutana na Mungu. Naye alipanda yake alipanda katika njia yenye mwinuko na miamba iliyochongoka, na kulikaribia lile wingu lililoashiria uwepo wa Yehova. Israeli ilikuwa sasa iwekwe katika mahusiano ya karibu na ya kipekee na Mwenyezi Mungu, yaani YEYE Aliye Juu. [TA 99.1; UM Aya ya 5]

Akiongea kutoka katika giza nene lililomfunika, alipokuwa amesimama juu ya mlima, akiwa amezungukwa na kundi la malaika, Bwana alitangaza sheria Yake …. Mipango ilipaswa kufanywa sasa ili kusimamishwa kikamilifu kwa taifa lililochaguliwa chini ya Yehova kuwa mfalme wao.— Patriachs and Prophets, 301, 303, 304, 312. [TA 99.2; UM Aya ya 6]

## “Na Wanifanye Patakatifu”

Wakati wa kukaa kwake mlimani, Musa alipokea maagizo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Patakatifu ambamo uwepo wa Mungu ungedhihirishwa kwa njia

maalumu. “Na wanifanyie Patakatifu, ili nipate kukaa kati yao,” ilikuwa agizo la Mungu.— Patriachs and Prophets, 313. [TA 99.3; UM Aya ya 7]

Jengo la hema liligawanywa katika vyumba viwili kwa kutumia pazia nzito na zuri, au utando mkubwa mnene, ulioning’inizwa kutoka katika nguzo zilizofunikwa kwa dhahabu; na pazia kama hilo lilifunga mlango wa chumba cha kwanza. Haya, kama mapazia ya ndani, yaliyotumika kutengeneza dari, yalikuwa yenye mapambo na rangi za kuvutia zaidi, samawi, zambarau, na nyekundu, zililipangwa kwa uzuri, kisha nyuzi za dhahabu na fedha zilitariziwa na picha za makerubi kuwakilisha jeshi la malaika ambao wanajihusisha na kazi ya Patakatifu pa mbinguni, na ambao ni roho zinazohudumu kwa watu wa Mungu duniani.— Patriachs and Prophets, 347. [TA 99.4; UM Aya ya 8]

Baada ya ujenzi wa maskani kukamilika, Musa aliichunguza kazi yote, naye akailinganisha na mfano na maagizo aliyokuwa ameyapokea kutoka kwa Mungu, na akaona kwamba kila sehemu yake ilipatana na mfano/kielelezo; naye akawabariki watu. Mungu alitoa mfano wa Sanduku la Agano kwa Musa, na maelekezo mahsusi jinsi ya kulitengeneza. Sanduku la Agano lilitengenezwa kuzihifadhi zile mbao za mawe, ambazo Mungu aliandika juu yake, kwa chanda Chake Mwenyewe, amri kumi. Ilikuwa katika umbo kama la kasha/kifua, nayo ilikuwa imefunikwa na kupambwa kwa dhahabu safi. Ilikuwa imepambwa kwa taji ya dhahabu juu kuizunguka. [TA 100.1; UM Aya ya 9]

Kifuniko cha Sanduku hili takatifu kilikuwa Kiti cha Rehema, kilichotengenezwa kwa dhahabu imara. Kwenye kila mwisho wa kiti cha rehema kuliwekwa kerubi safi, kwa dhahabu imara. Nyuso zao zilielekeana, kwa kutazamana kwa heshima kuelekea chini, kuelekea Kiti cha Rehema, ambapo huwakilisha malaika wote wa mbinguni wakitazama kwa kicho na heshima sheria ya Mungu iliyowekwa ndani ya Sanduku la Agano katika Patakatifu pa mbinguni. Makerubi hawa walikuwa na mabawa. Bawa moja la kila malaika lilinyooshwa juu, huku jingine la kila malaika likifunika maumbo yao. [TA 100.2; UM Aya ya 10]

Sanduku la Patakatifu pa duniani lilikuwa ni kielelezo cha Sanduku la Agano la Kweli la mbinguni. Hapo, kando ya Sanduku hilo la mbinguni, walisimama malaika walio hai, mwisho huu wa Sanduku la Agano, kila moja akiwa na bawa moja kukifunika Kiti cha Rehema, na kunyoosha juu, huku mabawa mengine yakiwa yamekunjwa juu ya maumbo yao kama ishara ya kicho na unyenyekevu.—The Spirit Of Prophecy 1:272. [TA 100.3; UM Aya ya 11]

Juu ya Kiti cha Rehema kulikuwa na Shekina, udhihirisho wa uwepo wa Mungu; na kutoka katikati ya makerubi, Mungu alifanya mapenzi Yake kujulikana. Ujumbe wa kimbingu wakati mwingine ulifikishwa kwa kuhani mkuu kwa sauti kutoka katika wingu.— Patriachs and Prophets 349. [TA 101.1; UM Aya ya 12]

Wakati Bwana hakujibuu kwa sauti, alitoa miale ya nuru takatifu na utukufu kukaa juu ya kerubi upande wa kuume wa Sanduku la Agano, kwa ishara ya kibali, au kukubaliwa. Ikiwa maombi yao yalikataliwa, wingu likakaa juu ya Kerubi upande wa kushoto.—The Spirit of Prophecy 1:399. [TA 101.2; UM Aya ya 13]

Kupitia Kristo, kusudi ambalo hema lilikuwa ishara yake lilipaswa kutimizwa—jengo hilo tukufu, kuta zake zenye dhahabu ya kumeta-meta inayoakisi rangi za upinde wa mvua, mapazia yaliyovutia na taswira za makerubi, harufu ya uvumba iliyopanda kila wakati na kuenea kila mahali, makuhani waliovikwa mavazi meupe yasiyo na mawaa, na katika siri ya ndani kabisa; juu ya Kiti cha Rehema, kati ya vielelezo vya malaika walioinama, wanaoabudu, utukufu wa Yule aliye Mtakatifu. Kwa ujumla, Mungu alitamani watu Wake walione na kulisoma kusudi Lake kwa nafsi za wanadamu. Lilikuwa kusudi lilelile kwa muda mrefu baada ya hayo lililosemwa na mtume Paulo, akisema kwa Roho Mtakatifu; [TA 101.3; UM Aya ya 14]

“Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa ni Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?”—Education, 36. [TA 101.4; UM Aya ya 15]

Chini ya mlima Sinai, Shetani alianza kutekeleza mipango yake kupindua sheria ya Mungu, na hivyo kuendeleza kazi ile ile aliyoianza mbinguni. Wakati wa siku arobaini Musa alipokuwa katika mlima pamoja na Mungu, Shetani alikuwa na shughuli nyingi, za kusisimua ndani yao mashaka, upotovu, na uasi. Wakati Mungu alipokuwa anaandika sheria Yake, ili itiiwe na watu Wake wa agano, Waisraeli, walikuwa wakikana uaminifu wao kwa Yehova, na kudai miungu ya dhahabu! ... [TA 101.5; UM Aya ya 16]

Ulimwengu wote ulikuwa umeshuhudia matukio hayo ya Sinai. Katika utendaji kazi wa tawala hizo mbili, kulionekana tofauti kati ya serikali ya Mungu na ile ya Shetani. Tena malimwengu mengine yasiyo na dhambi yaliona matokeo ya uasi wa Shetani, na aina ya serikali ambayo angeiweka mbinguni, kama angeruhusiwa kuchukua fimbo ya utawala.— Patriarchs and Prophets, 335,336. [TA 102.1; UM Aya ya 17]

Je, tunaweza kustaajabu kwamba “utukufu ulio bora sana” ulioakisiwa kutoka kwa Yeye aliye na uwezo wote, na Yule Asiye na kikomo uking’aa usoni mwa Musa kwa mng’ao mkubwa hivi kwamba watu hawakuweza kuuona? Nguvu na muhuri wa Mungu ilikuwa juu yake, Nayo ikamfanya kuonekana kama mmoja wa malaika wanaong'aa kutoka kwenye kiti cha enzi.—Testimonies for the Church 4:533. [TA 102.2; UM Aya ya 18]

Katika safari zao zote, Waisraeli walipolalamika juu ya matatizo ya njia, na kunung'unika dhidi ya viongozi wao, Musa aliwaambia, “Manung’uniko yenu ni dhidi ya Mungu. Sio mimi, bali Mungu aliyeleta ukombozi wenu.” Lakini maneno

yake ya harara mbele ya mwamba huo, “Je, tuwatokezee maji?” yalikuwa yamekaribia kuwa ukubali wa shutuma yao…..Bwana angeondoa wazo hii milele kutoka katika akili zao, kwa kumzuia Musa kuingia katika Nchi ya Ahadi. Hapa palikuwa na ushahidi usio na shaka kwamba kiongozi wao hakuwa Musa, bali ni Malaika mkuu ambaye Bwana alikuwa amesema juu yake, “Tazama, namtuma Malaika aende mbele yako, ili kukulinda njiani, na kukupeleka mahali pale ambapo nimekutengenezea. Jitunzeni mbele Yake, na kuitii sauti Yake; ... kwa kuwa Jina langu limo ndani Yake.”— Patriarchs and Prophets, 419. [TA 102.3; UM Aya ya 19]

### Kufa na Kufufuka kwa Musa

Musa akageuka kutoka katika mkutano, na katika ukimya na upweke aliipanda njia yake juu ya mlima ... Juu ya kile kilele cha upweke alisimama, na kutazama kwa macho yasiyofifia madhari iliyotandazwa mbele yake.—Patriachs and Prophets, 471. [TA 103.1; UM Aya ya 20]

Hayakuwa mapenzi ya Mungu kwamba mtu ye yote apande pamoja na Musa mpaka kilele cha Pisga. Hapo alisimama, juu ya kile kilele maarufu cha juu ya Pisga, mbele ya Mungu na malaika wa mbinguni.—Spiritual Gifst 4a:57. [TA 103.2; UM Aya ya 21]

Malaika pia walimfunulia Musa kwamba ingawa aliomboleza kwa sababu alikuwa amefanya dhambi na hakuweza kuingia katika Nchi ya Ahadi, na ingawa alihisi kwamba amewakosesha wana wa Israeli, bado ilikuwa ni dhambi yao wenyewe, roho yao ya manung'uniko na kulalamika, ambayo ilimpelekea kukengeuka kutoka katika haki na kutenda dhambi iliyomzuia kuingia Nchi ya Ahadi. Malaika walimwambia kwamba yeye siyo yule ambaye ameteseka sana kupita wote, kwani yeye hakuhisi moyoni mwake kina kamili cha dhambi yao, ila Kristo Mwenyewe, ambaye Ndiye kiongozi wao asiyeonekana, Yeye Huyu Ndiye ambaye walikuwa wamemwasi....Wajumbe wa mbinguni pia walirejelea matoleo ya dhabihu zilizoashiria kusulubishwa kwa Kristo, na kufungua mbele ya akili ya Musa matukio ambayo yatatokea katika siku zijazo .... [TA 103.3; UM Aya ya 22]

Wakati maono ya kusulubishwa yalipowasilishwa mbele ya Musa, ni tukio la ajabu kiasi gani lilikuwa juu ya kilele cha Pisga! ... Alitazama mandhari mbele yake ya siku za mbeleni mpaka kuja kwa Yesu (Panoramic view) ambapo aliona mateso ya Malaika Yule ambaye alikuwa amewaongoza Waisraeli katika jangwa, akiwaongoza katika safari yao ya kutangatanga kutoka Misri hadi Kanaani….Alipoona kupaa kwa Mwokozi na kuona kwamba yeye mwenyewe atakuwa mmoja wao wale ambao watakuwepo katika kumhudumia Mwokozi kufungua ile milango ya umilele, ni badiliko la jinsi gani lililotokea katika uso wake Musa! .... [TA 103.4; UM Aya ya 23]

Aliiona nchi ikisafishwa kwa moto na kusafishwa kutoka katika kila aina ya dhambi, kila alama ya laana, na kufanywa upya na kupewa watakatifu kuimiliki milele na milele Musa alipoona tukio hili, furaha na ushindi vilionyeshwa katika uso wake. Aliweza kuelewa majeshi ya malaika wote waliofunuliwa kwake. Aliyatafakari maono haya kwa jumla kama yalivyooneshwa kwake.—Manuscript Releases la 10:151, 152, 154, 155, 159. [TA 104.1; UM Aya ya 24]

Baada ya kuiona Kanaani na kuridhika, alijilaza kama shujaa aliyechoka, na kupumzika. Usingizi ukamjia, lakini ulikuwa ni usingizi wa kifo. Malaika waliuchukua mwili wake na kuuzika bondeni. Waisraeli hawakuweza kupata mahali alipozikwa. [TA 104.2; UM Aya ya 25]

Shetani alifurahi kwamba alikuwa amefaulu kumfanya Musa atende dhambi dhidi ya Mungu. Kwa kosa hili, Musa alikuja chini ya mamlaka ya kifo. Kama angeendelea kuwa mwaminifu, na maisha yake hayangeribiwa na kosa moja, la kushindwa kutoa kwa Mungu utukufu wa kutoa maji kutoka kwenye mwamba, angeliingia Nchi ya Ahadi, na angehamishwa mbinguni bila kuonja mauti. Mikaeli, au Kristo, pamoja na malaika waliomzika Musa, walishuka kutoka mbinguni, baada ya kukaa kaburini kwa muda mfupi, na kumfufua Musa.—Spiritual Gifts 4a:57, 58. [TA 104.3; UM Aya ya 26]

Nguvu ya kaburi ilikuwa kamwe haijawahi kuvunjwa, na wote waliokuwa kaburini Shetani alidai kuwa ni mateka wake, ambao kamwe wasingefunguliwa kutoka katika gereza lake la giza. [TA 105.1; UM Aya ya 27]

Kwa mara ya kwanza, Kristo alikuwa anakaribia kutoa uhai kwa marehemu. Pale Mfalme wa uzima na wale wanaong'aa walipolikaribia kaburi, Shetani alipatwa na mshangao wa hofu kwa ukuu Wake. Pamoja na malaika wake waovu alisimama kupinga uvamizi wa eneo ambalo alidai kuwa ni lake.—Patriachs and Prophets, 478. [TA 105.2; UM Aya ya 28]

Kristo na malaika walipokaribia kaburi, Shetani na malaika zake wakatokea kaburini, walikuwa wakilinda mwili wa Musa ili usije ukaondolewa. Kristo na malaika Zake walipokaribia, Shetani alipinga njia yao, lakini aliondolewa, na utukufu na nguvu ya Kristo na malaika Zake na kuanguka kando. Shetani alidai mwili wa Musa, kwa sababu ya kosa lake moja; lakini Kristo kwa upole alimrejelea Baba Yake na kumwambia Shetani, "Bwana na akukemee." Kristo alimwambia Shetani kwamba alijua kwamba Musa alikuwa ametubu kosa hili kwa unyenyekevu, na wala sasa hapakuwa na waa juu ya tabia yake, na jina lake lilisimama katika kitabu cha kumbukumbu mbinguni bila shida yoyote. Ndipo Kristo aliufufua mwili ya Musa.— Spiritual Gifts 4a:58. [TA 105.3; UM Aya ya 29]

**Balaamu, Nabii Aliyekosea**

Mungu akamjia Balaamu usiku kwa njia ya mmoja wa malaika Zake na kumwuliza, Ni watu gani hawa walio pamoja nawe? Na Balaamu akamwambia Mungu, Balaki "mwana wa Sipori, mfalme wa Moabu, amewatuma akaniambia, tazama, kuna watu wametoka Misri... Njoo, sasa, unilaanie watu hawa....Ndipo Mungu akamwambia Balaamu, Wewe usiende pamoja nao. Usiwalaani watu hawa; maana wamebarikiwa." Malaika akamwambia Balaamu kwamba wana wa Israeli walikuwa chini ya uongozi wa bendera ya Mungu wa mbinguni; na hakuna laana kutoka mwanadamu ingeweza kurudisha nyuma kuendelea kwao. [TA 105.4; UM Aya ya 30]

Asubuhi Balaamu aliamka, na kwa kusita akawaambia wale watu ili kumrudia Balaki, kwa maana Bwana hakumruhusu kwenda pamoja nao. Kisha Balaki akawatuma wakuu wengine, ... wenye hadhi za juu zaidi kuliko wajumbe wa kwanza; na wakati huu wito wa Balaki ukawa wa haraka zaidi. "Usiruhusu chochote, nakuomba, kikuzuie kuja kwangu kwako, kwa maana nitakupa heshima kuu sana Na Balaamu akajibu, akasema, ... Laiti Balaki angenipa nyumba yake imejaa fedha na dhahabu, siwezi kwenda zaidi ya Neno la Bwana Mungu wangu, kufanya kidogo au zaidi."— Spiritual Gifts 4a:44. [TA 106.1; UM Aya ya 31]

Kwa mara ya pili Balaamu alijaribiwa....Alitamani sana kutii ombi la mfalme; na ingawa mapenzi ya Mungu yalikuwa tayari Kwa hakika yamefunuliwa kwake waziwazi, aliwahimiza wajumbe kusubiri, ili apate kuuliza zaidi kwa Mungu; kana kwamba Yule Asiye na mwisho ni mwanadamu, hata ashawishike.—Patriarchs and Prophets, 440. [TA 106.2; UM Aya ya 32]

Malaika alitumwa kwa Balaamu kumwambia, "Ikiwa watu hao wanakuja ili kukuita, ondoka, uende pamoja nao; lakini Neno lile nitakalokuambia, ndilo utakalotenda."— Spiritual Gifts 1:321. [TA 106.3; UM Aya ya 33]

Balaamu alikuwa amepokea ruhusa ya kwenda pamoja na wajumbe kutoka Moabu, ikiwa wangekuja asubuhi kumwita. Lakini wakakasirishwa na kuchelewa kwake, na wakitarajia kukataliwa tena, walianza safari yao ya kurudi nyumbani bila mashauriano zaidi naye. Kila udhuru wa kutii ombi la Balaki sasa ulikuwa umeondolewa. Lakini Balaamu aliazimia kupata zawadi ile; na akamchukua yule mnyama ambaye alizoea kumpanda, aliondoka na kuanza safari yake. Aliogopa kwamba hata sasa ruhusa ya Mungu inaweza kuondolewa, na akaharakisha kwenda mbele kwa bidii, akikazana ili kwa namna fulani asije akaikosa ile zawadi aliyoahidiwa.— Patriarchs and Prophets, 441. [TA 107.1; UM Aya ya 34]

Hasira ya Mungu ikawaka juu ya Balaamu kwa ajili ya uthubutu wake wa kipumbavu dhidi ya Mbingu, na "malaika wa Bwana akasimama njiani kwa ajili ya kumpinga." Mnyama alipomwona mjumbe wa Mungu, ambaye alikuwa, hata hivyo, asiyeonekana kwa bwana wake, akageuka kando na barabara kuu

kuelekea shambani. Kwa mapigo makali, Balaamu alimrudisha mnyama huyo katika njia; lakini tena, mahali pembamba palipozingirwa na kuta, na malaika akatokea, na mnyama, akijaribu kukwepa sura ya kutisha, aliubamiza mguu wa mpanda farasi kwenye ukuta.—The Signs of the Times, Novemba 25, 1880. [TA 107.2; UM Aya ya 35]

Ghadhabu ya Balaamu ilikuwa haijathibitiwa, na kwa fimbo yake akampiga mnyama kwa ukatili zaidi kuliko hapo kabla. Mungu sasa akafungua kinywa Chake, na kwa hivyo "punda asiyeweza kusema akanena kwa sauti ya kibinanadamu," naye aliuzuia "wazimu wa nabii yule.” 2 Petro 2:16. “Nimekutenda nini,” alisema, "hata ukanipiga mara tatu hizi?" [TA 107.3; UM Aya ya 36]

Akiwa na hasira kwa kuzuiwa kwa jinsi hiyo katika safari yake, Balaamu akamjibu mnyama kama ambavyo angezungumza na kiumbe mwenye akili—“Kwa sababu umenidhihaki; laiti ningalikuwa na upanga mkononi mwangu, ningekuua sasa hivi.” ... [TA 107.4; UM Aya ya 37]

Macho ya Balaamu sasa yakafumbuliwa, akamwona yule Malaika wa Mungu akiwa amesimama na upanga umefutwa tayari kumwua. Kwa hofu "akainamisha kichwa, akaanguka kifudifudi." Malaika akamwambia, Mbona umempiga punda wako mara tatu hizi? Tazama, nilitoka ili kukupinga, kwa maana njia yako ni potofu mbele yangu; punda akaniona, naye akageuka upande mbele zangu mara tatu hizi: kama asingeniacha, bila shaka ningalikuua wewe na kumwacha yeye hai.” ... [TA 108.1; UM Aya ya 38]

Alipomwona mjumbe wa Mungu, Balaamu akapiga kelele na kulia kwa hofu, “Nimefanya dhambi; kwa maana sikujua ya kuwa umesimama njiani kinyume chngu; basi sasa, kama umechukizwa, nitarudi tena.”— Patriarchs and Prophets, 442, 443. [TA 108.2; UM Aya ya 39]

Baada ya malaika kumwonya Balaamu kwa mkazo kwamba asiwafurahishe na kuwaridhisha Wamoabu, alimpa ruhusa tena ya kuendelea na safari yake. [TA 108.3; UM Aya ya 40]

Balaki alikutana na Balaamu, na akamwuliza kwa nini alichelewa hivyo wakati alipomuita; ... Balaamu akajibu, Tazama, Lo! Nimekuja kwako. Kisha akamwambia kwamba hakuwa na uwezo wa kusema chochote. Lile Neno ambalo Mungu angempa, ndilo angeweza kunena, na asingeweza kufanya kinyume au zaidi. Balaamu aliamuru dhabihu kulingana na kawaida za dini. Mungu alimtuma malaika Wake kukutana na Balaamu, kumpa maneno ya kusema, kama alivyokuwa amefanya katika nyakati ambapo Balaamu alikuwa amejitoa wakfu kwa ajili ya utumishi wa Mungu. “BWANA akatia Neno katika kinywa chaa Balaamu akatunga mithali yake, akasema, Balaki, mfalme wa Moabu amenileta kutoka Aramu, akisema, Njoo, unilaanie Yakobo, na uje, uwatukane Israeli. Nimlaanije, ambaye Mungu hajamlaani? Au nimshutumuje

yeye ambaye Bwana hakumshutumu?..... [TA 108.4; UM Aya ya 41]

Balaki alikatishwa tamaa na kukasirika. Akapiga kelele, “Umenitenda nini? Nilikuchukua ili uwalaani adui zangu, na tazama, wewe umewabariki.” Balaki akafikiri kwamba mwonekano mkuu wa Waisraeli katika hema zao ... ndiyo uliomzuia asiwalaani. Akafikiri kama atampeleka....ambako Israeli hawataonekana kwa ukuu wao, basi wanaweza kupewa laana kutoka kwa Balaamu. Tena, huko Sofimu ... Balaamu alitoa sadaka za kuteketezwa, kisha akaenda peke yake kwenda kuzungumza na malaika wa Mungu. Malaika akamwambia Balaamu nini cha kusema.—The Spirit of Prophecy 1:322-324. [TA 109.1; UM Aya ya 42]

**Yoshua Awaongoza Israeli Kwenda Kanaani**

Wana wa Israeli wakamwombolezea Musa kiongozi wao aliyeondoka, na siku thelathini zilitolewa kwa huduma maalum kwa heshima ya kumbukumbu yake... Yoshua sasa alikuwa kiongozi aliyetambulika kwa Israeli. [TA 109.2; UM Aya ya 43]

Sasa maagizo yalitolewa ili kujitayarisha mapema …..Nao wakaondoa kambi yao ... jeshi likashuka hadi mpaka wa Yordani. Patriachs and Prophets, 481, 483. [TA 109.3; UM Aya ya 44]

Malaika wanne wa mbinguni daima waliambatana na Sanduku la Agano la Mungu katika safari zake zote, ili kulilinda na hatari zote, na kutimiza utume wowote uliohitajika kuhusiana na Sanduku hilo la Agano. Yesu Mwana wa Mungu, alisindikizwa na malaika wa mbinguni, alitangulia mbele ya Sanduku la Agano lilipokuja hadi Yordani; na maji yakasimama mbele za uwepo Wake. Kristo na malaika wakasimama karibu na sanduku na makuhani katika ufuo wa mto mpaka Israeli wote walipovuka Yordani.—The Spirit of Prophecy 1:399. [TA 109.4; UM Aya ya 45]

Kama macho ya Yoshua yangefumbuliwa ... na angaliweza kustahimili yale aliyoona (mwanga na utukufu), basi angaliwaona malaika wa Bwana wakipiga kambi na wana wa Israeli; kwa maana jeshi la mbinguni lililofundishwa lilikuwa limekuja kuwapigania watu wa Mungu, na Jemadari wa jeshi la Bwana alikuwako akiamuru.— The Review and Herald, Julai 19, 1892. [TA 110.1; UM Aya ya 46]

Yoshua alipojitenga na majeshi ya Israeli, ili kutafakari na kuomba kwa ajili ya uwepo pekee wa Mungu kuwa naye, aliona Mtu mrefu wa kimo, akiwa amevaa mavazi ya vita, na upanga Wake mkononi Mwake....Huyu hakuwa malaika wa kawaida. Bali alikuwa ni Bwana Yesu Kristo, Yeye aliyewaongoza Waebrania jangwani, Akiwa amefunikwa na nguzo ya moto wakati wa usiku, na nguzo ya wingu mchana. Mahali alipokuwa palifanywa kuwa Patakatifu kwa

uwepo Wake, kwa hiyo Yoshua aliagizwa kuvua viatu vyake.— Spiritual Gifts 4a:61. [TA 110.2; UM Aya ya 47]

Kwa hofu, Yoshua akaanguka kifudifudi, akasujudu na kusikia uhakikisho, “Nimeutia Yeriko, na mfalme wake mkononi mwako, na watu hodari wa vita,” naye akapokea maelekezo kwa ajili ya kutekwa kwa mji huo.— Patriachs and Prophets, 488. [TA 110.3; UM Aya ya 48]

Jemedari wa jeshi la Bwana hakujidhihirisha kwa kutano lote. Bali Aliwasiliana na Yoshua pekee, ambaye alisimulia habari ya mazungumzo haya kwa Waebrania. Ilikuwa ni juu yao kuamini au kutilia shaka maneno ya Yoshua, aau kufuata maagizo yaliyotolewa kwa Jina la Jemedari wa Jeshi la Bwana, au kuasi dhidi maelekezo yake na kukana mamlaka yake. Hawakuweza kuona jeshi la malaika, likiongozwa na Mwana wa Mungu.—Testimonies for the Church 4:162, 163. [TA 110.4; UM Aya ya 49]

### Kutekwa Kwa Yeriko

Jemedari wa jeshi la Bwana Mwenyewe, alikuja kutoka mbinguni kuongoza majeshi ya mbinguni katika mashambulizi juu ya mji. Malaika wa Mungu walizishika kuta kubwa na kuziangusha chini.—. Testimonies for the Church 3:264. [TA 111.1; UM Aya ya 50]

Kristo na malaika walihudhuria wakati wa kuzunguka ukuta na Sanduku la Agano Yeriko, na hatimaye kuziangusha kuta kubwa za jiji, na kuiweka Yeriko mikononi mwa Israeli.—The Spirit of Prophecy 1:399. [TA 111.2; UM Aya ya 51]

Yeriko ulipoanguka, hakuna mkono wa mwanadamu uliogusa kuta za mji; kwa maana malaika wa Bwana walipindua ngome, nao wakaiingia ngome ya adui. Haikuwa Israeli, bali Jemedari wa Jeshi la Bwana Ndiye aliiteka Yeriko. Lakini Israeli walikuwa na sehemu yao ya kufanya, kuonesha imani yao kwa Jemedari wa wokovu wao.— The Review and Herald, Julai 19, 1892. [TA 111.3; UM Aya ya 52]

Ikiwa shujaa mmoja angeweka nguvu zake dhidi ya kuta, utukufu wa Mungu ungepungua na mapenzi Yake yangekatishwa tamaa (yangehafifishwa). Lakini kazi iliachiwa kwa Mwenye Enzi (Mwenyezi); na kama msingi wa ile minara ungewekwa katikati ya dunia na vilele vyake kufikia upeo wa mbinguni, matokeo yangekuwa yaleyale, wakati Jemedari wa jeshi la Bwana alipoongoza majeshi Yake ya malaika kwenye shambulio hilo.— The Signs of the Times, Aprili 14, 1881. [TA 111.4; UM Aya ya 53]

## SURA YA 10

## MALAIKA KUTOKA KIPINDI CHA WAAMUZI HADI UFALME WA AWALI

### Kristo Kama “Malaika Wa Bwana”

Mungu alipotuma malaika zake zamani kuhudumu au kuwasiliana na watu binafsi, walipogundua kwamba alikuwa ni malaika waliokuwa wamemwona na kuzungumza naye, waliingiwa na hofu, wakaogopa kwamba watakufa. Walikuwa na maoni hayo ya kuogofya juu ya ukuu na uweza wa Mungu, wakafikiri kuwa kwenye uhusiano wa karibu sana na wa moja kwa moja na uwepo Wake Mtakatifu, kungewaangaiza wao…… Waamuzi 6:22, 23; 13:21, 22; Yoshua 5:13-15.— Spiritual Gifts 4b:152. [TA 112.1; UM Aya ya 1]

Baada ya kifo cha kiongozi wao Yoshua na wazee ambao walihusiana naye, watu walianza hatua kwa hatua kuurudia tena ibada ya sanamu. [TA 112.2; UM Aya ya 2]

Bwana hakuruhusu dhambi za watu Wake kupita bila onyo. Kulikuwa bado na waabuduo waaminifu katika Israeli; na wengi wengine, kutokana na mazoea na ushirika wa awali, walihudhuria ibada ya Mungu kwenye hema. Kundi kubwa lilikusanyika huko katika tukio la sikukuu ya kidini, wakati Malaika wa Mungu, akitokea kwa mara ya kwanza huko Gilgali, Naye akajidhihirisha kwa mkutano huko Shilo... [TA 112.3; UM Aya ya 3]

Malaika huyu, yaani Yule Yule aliyemtokea Yoshua wakati wa kutwaliwa kwa Yeriko, hakuwa na mwonekano wa tofuti na wa Mwana wa Mungu....Aliwaonyesha kwamba hakuwa amevunja ahadi Zake kwao, bali wao wenyewe walikuwa wamevunja agano lao takatifu. [TA 113.1; UM Aya ya 4]

"Ikawa, Malaika wa Bwana aliponena haya maneno kwa wana wa Israeli wote, ndipo watu waliiinua sauti na kulia." "Nao wakamtolea Bwana dhabihu huko." Lakini toba yao haikuleta matokeo ya kudumu.— The Signs of the Times, Juni 2, 1881. [TA 113.2; UM Aya ya 5]

### Gideoni

Gideoni alikuwa mwana wa Yoashi, wa kabila ya Manase. Ukoo ambao familia hii ilitoka haukuwa na nafasi ya uongozi, lakini nyumba ya Yoashi ilijulikana kwa wema na uadilifu    Kwa Gideoni ulikuja wito wa kimbingu wa kuwakomboa watu wake. Alikuwa amehusihwa wakati wa kupura ngano....Gideoni alipokuwa akifanya kazi , kwa siri na ukimya, alitafakari kwa huzuni juu ya hali ya Israeli, na alifikiria jinsi nira ya mdhalimu itakavyoweza kuvunjwa kutoka kwa watu wake. [TA 113.3; UM Aya ya 6]

Mara "Malaika wa Bwana" akamtokea na kumwambia kwa Maneno, "Yehova Yu pamoja nawe, Eee shujaa."— Patriachs and Prophets 546. [TA 113.4; UM Aya ya 7]

Malaika Huyu alikuwa amefunika utukufu wa Uungu kwa uwepo Wake, lakini hakuwa mwingine ila Kristo, Mwana wa Mungu. Nabii au Malaika alipotoa ujumbe mtakatifu, Maneno yake yalikuwa, "Bwana asema, Nitafanya hivi," lakini imesemwa kuhusu Mtu aliyezungumza na Gideoni, "Bwana akamwambia, nitakuwa pamoja nawe." [TA 132.5; UM Aya ya 8]

Akitaka kuonyesha heshima ya pekee kwa mgeni Wake mashuhuri, na baada ya kupata uhakikisho kwamba Malaika angekawia, Gideoni akaenda kwa haraka hemani mwake, na kutoka katika zizi lake akamtayarisha mwana-mbuzi na mikate isiyotiwa chachu, aliyoileta ili kumpatia…..[TA 114.1; UM Aya ya 9]

Zawadi ilipotolewa, Malaika alisema, "Chukua nyama na mikate isiyotiwa chachu, na kuiweka juu ya mwamba huu, na kuumwaga mchuzi. Gideoni akafanya hivyo, na ndipo Bwana akampa ishara ambayo aliitamani. Akiwa na

ile fimbo mkononi mwake, Malaika aliigusa nyama na mikate isiyotiwa chachu, na moto ukatoka mwambani na kuteketeza yote kama dhabihu, na si kama chakula cha kumkaribisha wageni; maana alikuwa Mungu, na sio mwanadamu. Baada ya ishara hii ya tabia Yake ya Kiungu, malaika akatoweka. [TA 114.2; UM Aya ya 10]

Aliposhawishika kwamba alikuwa amemwona Mwana wa Mungu, Gideoni akajawa na hofu, akasema, “Ole wangu, Ee Bwana Mungu! kwa kuwa nimemwona Bwana uso kwa uso.” [TA 114.3; UM Aya ya 11]

Kisha Mungu akamtokea Gideoni mara ya pili akasema, Amani iwe nawe, usiogope, hautakufa. Haya maneno ya neema yalinenwa na Mwokozi Yule Yule Mwenye huruma ambaye aliwaambia wanafunzi waliojaribiwa katika bahari yenye dhoruba, “Ni Mimi; msiogope”—Yeye aliyewatokea wale wenye huzuni huko juu ghorofani, akamwambia Gideoni Maneno yale yale, Amani iwe kwako.”— The Signs of the Times, Juni 23, 1881. [TA 114.4; UM Aya ya 12]

### Samsoni

Katikati ya uasi ulioenea, waabudu halisi wa Mungu waliendelea kumsihi kwa ajili ya ukombozi wa Israeli   Juu ya mpaka wa nchi ya vilima unaoelekea nchi tambarare ya Wafilisti, kulikuwa na mji mdogo wa Sora. Hapa ilikaa familia ya Manoa, wa kabila ya Dani, mojawapo ya familia chache ambazo huku kukiwa na uasi mkuu ilikuwa imebaki na uaminifu kwa Yehova. Kwa mke asiye na mtoto wa Manoa, “ [TA 114.5; UM Aya ya 13]

Malaika wa Yehova” alimtokea akiwa na ujumbe kwamba alipaswa kuwa na mtoto wa kiume, ambaye kupitia kwake Mungu angeanza kuwakomboa Israeli. Kuhusiana na hili, Malaika alimpa maagizo kuhusu tabia zake mwenyewe, na pia malezi ya mtoto wake.... [TA 115.1; UM Aya ya

Mwanamke akamtafuta mume wake, na, baada ya kumwelezea Malaika, alirudia ujumbe Wake. Kisha, kwa hofu kwamba wataweza kufanya kosa fulani katika kazi muhimu waliyokabidhiwa, kisha mume akaomba, hebu “Yule mtu wa Mungu uliyemtuma na arudi tena kwetu na atufundishe tutakachomtenda mtoto atakayezaliwa.” [TA 115.2; UM Aya ya 14]

Malaika alipotokea tena, swali la Manoa la wasiwasi lilikuwa, "Tutafuata nini kwa ajili ya mtoto, na tufanye nini kwake?" (je! Huyo mtoto atakuwa wa namna gani, na kazi yake itakuwa ni nini?) (tumleeje mtoto) Maagizo yaliyotangulia yalirudiwa—“Katika yote niliyowaambia mwanamke na ajihadhari. Asile kitu chochote kinachotokana na mzabibu, asinywe divai wala kileo, wala asile kitu chochote kichafu. Yote niliyomwamuru na ayatunze.”— Patrichs and Prophets, 560, 561. [TA 115.3; UM Aya ya 15]

Manoa na mke wake hawakujua kwamba Yule anayezungumza nao alikuwa

Yesu Kristo. Walimtazama kama mjumbe wa Bwana, lakini kwamba alikuwa nabii au malaika, wao hawakuweza kujua. Wakitaka kudhihirisha ukarimu kwa mgeni wao, walimsihi asubiri huku wakimuandalia mwanambuzi. Lakini katika kuitojua tabia Yake, wao walishindwa kujua kama wangemtolea sadaka ya kuteketezwa au kuiweka mbele Yake kama chakula. [TA 115.4; UM Aya ya 16]

Malaika akajibu, "Ijapokuwa unanizuia, sitakula mkate wako; na ukitaka kutoa sadaka ya kuteketezwa, itakupasa kuitoa kwa Bwana." Akihisi kuhakikishiwa, sasa, ya kwamba mgeni wake alikuwa nabii,Manoa akasema, Jina lako ni nani, hata maneno yako yatakapotimia tukupe heshima yako?" [TA 116.1; UM Aya ya 17]

Jibu lilikuwa, "Mbona unaniuliza Jina Langu, kwani Jina hilo ni la ajabu?" Akitambua tabia ya Kiungu ya mgeni wake, Manoa "alichukua mwana-mbuzi, pamoja na sadaka ya unga, akamtolea Bwana sadaka juu ya mwamba; Malaika akafanya muujiza; naye Manoa na mkewe wakatazama... Moto ukitoka mwambani, nao ukaiteketeza dhabihu, na kadiri mwali wa dhabihu ulivyopanda kuelekea mbinguni, "Malaika wa Bwana akapanda na mwali wa moto wa madhabahu. Manoa na mkewe wakakitazama, na wakaanguka chini kifudifudi." Hakukuwa na swali zaidi kuhusu tabia ya mgeni wao. Walijua kwamba walikuwa wamemwona Mtakatifu, ambaye, alikuwa ameufunika utukufu Wake katika nguzo ya mawingu jangwani, na kuongoza Israeli kama Msaidizi wake jangwani. [TA 116.2; UM Aya ya 18]

Hofu, woga, na wasiwasi ulijaza moyo wa Manoa, naye aliweza tu kusema, "Hakika tutakufa, kwa sababu tumemwona Mungu!" Lakini mwenzake katika saa ile adhimu alikuwa na imani zaidi kuliko yeye. Naye akamkumbusha kwamba Bwana alikuwa ameikubali sadaka yao, na alikuwa amewaahidi mwana ambaye angeikomboa Israeli. Huu ulikuwa uthibitisho wa neema badala ya ghadhabu. (yaani kama watakufa watapataje mtoto!)— The Signs la Times, Septemba 15, 1881. [TA 116.3; UM Aya ya 19]

Ahadi ya Mungu kwa Manoa ilitimizwa kwa wakati wake, basi kukazaliwa mwana, ambaye alipewa jina la Samsoni. Kwa agizo la Malaika hakuna wembe ungepita juu ya kichwa cha mtoto, akiwa amewekwa wakfu kwa Mungu kama Mnadhiri, tangu kuzaliwa kwake.— The Signs la Times, Oktoba 6, 1881. [TA 117.1; UM Aya ya 20]

### Samweli na Eli

Samweli alikuwa mtoto aliyezungukwa na ushawishi/mvutano mbaya zaidi. Aliona na kusikia mambo ambayo yalihuzunisha nafsi yake. Wana wa Eli, ambao walihudumu katika ofisi takatifu, walitawaliwa na Shetani. Watu hawa walichafua anga yote iliyowazunguka. Wanaume na wanawake kila siku walivutiwa na dhambi na makosa, lakini Samweli alienenda bila waa. Mavazi

yake ya tabia hayakuwa na doa. Hakuwa na ushirika, au kujifurahisha hata kidogo, na dhambi zilizojaa Israeli yote na taarifa za kutisha. Samweli alimpenda Mungu; aliiweka nafsi yake katika uhusiano wa karibu na mbingu kiasi kwamba malaika alitumwa kuzungumza naye kwa ajili ya dhambi za wana wa Eli, ambazo zilikuwa zikiipotosha Israeli.— Testimonies for the Church 3:472, 473. [TA 117.2; UM Aya ya 21]

Makosa ya wana wa Eli yalikuwa ya makusudi sana, ... hata hakukuwa ana dhabihu ambayo ingeweza kulipia makosa ya makusudi kama haya….Hawa wadhambi wakalipeleka sanduku kwenye kambi ya Israeli. [TA 117.3; UM Aya ya 22]

Mungu aliruhusu Sanduku Lake la Agano kuchukuliwa na adui zao ili kuwaonyesha Israeli jinsi ilivyokuwa bure kulitumainia Sanduku hilo, ambalo ni ishara tu ya uwepo Wake, wakati walikuwa wananajisi amri zilizokuwa ndani ya Sanduku hilo la Agano. [TA 117.4; UM Aya ya 23]

Wafilisti walikuwa na ushindi, kwa sababu walikuwa, kama walivyodhani, Mungu maarufu wa Waisraeli, ambaye alikuwa ametenda maajabu hayo kwao, na kuwafanya hofu kwa adui zao. Wakalichukua sanduku la Mungu mpaka Ashdodi, wakaliweka katika hekalu la kifahari liliyofanywa kwa heshima ya mungu wao maarufu na aliyependwa zaidi, Dagoni, na kuliweka karibu na upande wa mungu wao. Asubuhi makuhani wa miungu hii waliingia hekaluni, wakaogopa sana kumwona Dagoni ameanguka kifudifudi mpaka ardhini mbele ya sanduku la Bwana...Malaika wa Mungu, ambao daima waliongozana na Sanduku la Agano, waliangusha mungu wa sanamu asiye na akili, na baadaye kuikatakata, ili kuonyesha kwamba Mungu, Mungu aliye hai, alikuwa juu ya miungu yote, na mbele Zake kila mungu wa kipagani alikuwa si kitu.—Spiritual Gifts 4a:106, 107. [TA 118.1; UM Aya ya 24]

Watu wa Beth-shemeshi wakaeneza upesi habari ya kwamba lile sanduku lilikuwa katika milki yao, na watu wa nchi Jirani walikusanyika kukaribisha kurudi kwake. Sanduku liliwekwa juu ya jiwe ambalo lilitumika kwanza kwa ajili ya madhabahu, na mbele yake dhabihu za ziada zilitolewa kwa Bwana…..Badala ya kuandaa mahali panapofaa kwa ajili ya kulipokea, waliliruhusu libaki katika shamba la mavuno. Walipokuwa wakiendelea kulitazama Sanduku la Agano takatifu na kuzungumza juu yake, na namna ya ajabu ambayo lilikuwa limerejeshwa, walianza kudhani kwamba ndani yake kulikuwa na nguvu za kipekee. Hatimaye, kwa kutekewa na udadisi, waliondoa vifuniko na kujitosa kulifungua… [TA 118.2; UM Aya ya 25]

Hata Wafilisti wapagani hawakuthubutu kuondoa kifuniko chake. Malaika wa mbinguni, wasioonekana, muda wote waliliangalia katika safari zake zote. Shauku isiyo na heshima/kicho ya watu wa Beth-shemeshi iliadhibiwa kwa haraka. Wengi walipigwa na kifo cha ghafula.— Patriachs and Prophets, 589.

[TA 118.3; UM Aya ya 26]

## Sauli na Yonathani

Mungu alikuwa amemwinua Samweli kuwa mwamuzi wa Israeli. Aliheshimiwa na watu wote. Mungu alipaswa kutambuliwa kama Mkuu wao, hata hivyo Akawaweka watawala wao, na akawajaza Roho yake, na aliwasilisha mapenzi Yake kwao kupitia malaika zake.— Spiritual Gifts 4a:67. [TA 119.1; UM Aya ya 27]

Kwa sababu ya dhambi ya Sauli katika sadaka yake ya kiburi, Bwana hakumpa heshima ya kuwashinda Wafilisti. Yonathani, mwana wa mfalme, mtu aliyemcha Bwana, alichaguliwa kuwa chombo cha kuwakomboa Israeli. [TA 119.2; UM Aya ya 28]

Malaika wa mbinguni walimlinda Yonathani na mtumishi wake, Malaika wakapigana kando yao, na Wafilisti wakaanguka mbele yao.— Patriachs and Prophets, 623. [TA 119.3; UM Aya ya 29]

Malaika wa Mungu walipigana upande wa Yonathani, na Wafilisti akaanguka pande zote. Hofu kubwa ikalishika jeshi la Wafilisti shambani na ngomeni....Nchi ikatetemeka mbele yao,kana kwamba kuna kundi kubwa la wapanda farasi na magari ya vita yaliyoandaliwa kwa vita. Yonathani na mchukua silaha wake, na hata jeshi la Wafilisti walijua ya kuwa Bwana alikuwa anafanya kazi kwa ajili ya ukombozi wa Waebrania.— Spiritual Gifts 4a:70. [TA 119.4; UM Aya ya 30]

## Miaka Ya Awali Ya Daudi

Samweli hakuja tena kwa Sauli na maagizo kutoka kwa Mungu. Bwana hangeweza kumtumia kutekeleza makusudi yake. Lakini alimtuma Samweli mpaka nyumba ya Yese, ili kumtia mafuta Daudi, ambaye amemchagua kuwa mtawala badala ya Sauli, ambaye Yeye alikuwa amemkataa. [TA 119.5; UM Aya ya 31]

Wana wa Yese walipokuwa wakipita mbele ya Samweli, angemchagua Eliabu, ambaye alikuwa wa kimo kirefu, mwenye sura ya heshima; malaika wa Mungu alisimama karibu naye ili kumwongoza katika uamuzi muhimu, na akamwagiza kwamba asihukumu kwa sura. Eliabu hakumcha Bwana. Moyo wake haukumwelekea Mungu. Angekuwa mtawala mwenye kiburi, anayejitukuza. Hakuna aliyepatikana kati ya wana wa Yese ila Daudi, mdogo kabisa, ambaye kazi yake ilikuwa duni ile ya kuchunga kondoo.— Spiritual Gifts 4a:77, 78. [TA 120.1; UM Aya ya 32]

Daudi hakuwa wa kimo kilichoinuka; lakini uso wake ulikuwa mzuri, unaoonesha unyenyekevu, uaminifu, na ujasiri wa kweli. Malaika wa Mungu

aliashiria kwa Samweli kwamba Daudi ndiye ampake mafuta, kwani alikuwa mteule wa Mungu. Tangu wakati huo Bwana alimpa Daudi akili na moyo wenye ufahamu.—The Spirit of Prophecy 1:368. [TA 120.2; UM Aya ya 33]

Kaka mkubwa wa Daudi, Eliabu, ... alikuwa na wivu juu ya Daudi, kwa sababu aliheshimiwa mbele yake. Alimdharau Daudi, akamtazama yeye kama duni kwake. Alimshutumu mbele ya wengine kwa kutoroka bila kujulikana kwa baba yake kuona vita Daudi aliyajibu mashtaka yasiyo ya haki, na kusema, "Nimefanya nini sasa? Je, hakunsi neno kuwa hilo?" Daudi hakumweleza kaka yake kuwa alikuja kuwasaidia Israeli; kwamba Mungu alimtuma kumuua Goliathi. Mungu alikuwa amemchagua kuwa mtawala wa Israeli; na kama majeshi ya Mungu aliye hai yalikuwa katika hatari hiyo, alikuwa ameelekezwa na Malaika kuiokoa Israeli.— The Spirit of Prophecy 1:371. [TA 120.3; UM Aya ya 34]

## Sauli Apingana Na Malaika

Sauli aliruhusu misukumo yake itawale uamuzi wake, mpaka akambukia kwenye ghadhabu ya nia yake. Alikuwa na hisia ya hasira na wazimu, alikuwa tayari kuchukua uhai wa yeyote aliyethubutu kupinga mapenzi yake....Ilikuwa ni tabia ya Daudi isiyo na lawama na uaminifu uliotukuka iliyokuwa imeamsha hasira ya mfalme; na aliona maisha na uwepo wa Daudi unamletea aibu. [TA 121.1; UM Aya ya 35]

Akafika Rama, akasimama kwenye kisima kikubwa huko Seku. Watu walikuwa wanakusanyika kuteka maji, naye akauliza ni wapi Samweli na Daudi walikuwa wakikaa. Alipoambiwa kwamba walikuwa huko Nayothi, akafanya haraka kufika mahali pale. Lakini malaika wa Mungu alikutana naye njiani na kumdhibiti. Roho wa Mungu alimshika kwa uwezo wake, akaendelea na safari huku akimwomba Mungu na utabiri na nyimbo takatifu. Alitabiri juu ya kuja kwa Masihi kama Mkombozi wa ulimwengu. Alipofika mpaka Nayothi huko Rama, akaweka kando mavazi yake yaliyokuwa ishara kituo chake, na mchana kutwa, na usiku kucha, akalala mbele ya Samweli na wanafunzi wake, chini ya ushawishi wa Roho wa Mungu.— The Signs of the Times, Agosti 24, 1888. [TA 121.2; UM Aya ya 36]

## Ibada Ya Umizimu Ya Sauli Huko Endori Na Kifo Chake

Vita vikatangazwa tena kati ya Israeli na Wafilisti...Sauli alikuwa amejua kwamba Daudi na jeshi lake walikuwa pamoja na Wafilisti, naye alitazamia kwamba mwana wa Yese angechukua nafasi hii kulipiza kisasi kwa mabaya yaliyompata. Mfalme alikuwa katika huzuni kubwa  Kesho yake, Sauli lazima apigane na Wafilisti. Vivuli vya majanga yanayouata vilikuwa vikikusanya giza juu yake kumzunguka; alitamani sana msaada na mwongozo. Lakini alitafuta

ushauri kutoka kwake Mungu bila mafanikio. “BWANA hakumjibu, wala kwa ndoto, wala kwa Urimu;wala kwa manabii.” ..... [TA 121.3; UM Aya ya 37]

Ndipo Sauli akawaambia watumishi wake, Nitafutieni mwanamke aliye na pepo wa utambuzi, nipate kumwendea na kuuliza kwake.” ... Aliambiwa, mfalme kwamba mwanamke aliyekuwa na pepo wa utambuzi alikuwa akiishi katika kujificha huko Endori. Mwanamke huyu alikuwa ameingia katika agano na Shetani alijisalimisha chini ya udhibiti wake, kutimiza makusudi yake; na katika majibu kwake, mkuu wa uovu alimfanyia maajabu, na kufunua mambo ya siri kwake. [TA 122.1; UM Aya ya 38]

Sauli akajibadilisha, akatoka usiku akiwa na watumishi wawili tu, ili kumtafuta yule mwanamke mchawi. Gizani, Sauli na watumishi wake wakavuka nchi tambarare, nao wakapita salama jeshi la Wafilisti, wakavuka kilele chamlima, wakafika nyumba ya upweke ya mchawi wa Endori.... [TA 122.2; UM Aya ya 39]

Baada ya kufanya huduma yake ya kuongea na wafu, alisema, “Naona miungu anatoka katika nchi  Mzee anazuka, naye amefunikwa vazi. Naye Sauli akatambua ya kuwa ni Samweli.”.... [TA 122.3; UM Aya ya 40]

Hakuwa nabii mtakatifu wa Mungu aliyezuka katika huduma ya uchawi wa kuongea na wafu. Samweli hakuwepo katika eneo hilo la roho wauovu. Muonekano huo usio wa kawaida ulitengenezwa na nguvu za Shetani.—Patriachs and Prophets, 675, 676, 679... [TA 122.4; UM Aya ya 41]

Maneno ya kwanza ya mwanamke chini ya mvuto wa uchawi wake wa kuongea na wafu yalielekezwa kwa mfalme, “nini umenidanganya? Kwa kuwa wewe ni Sauli. Hivyo tendo la kwanza la pepo mchafu lililomtengeneza nabii, lilikuwa kuwasiliana kwa siri na mwanamke huyu mwovu, kumwonya kuhusu udanganyifu uliokuwa umefanywa juu yake. Ujumbe kwa Sauli kutoka kwa yule nabii aliyejifanya ulikuwa, “Kwa nini umenitaabisha, hata kunipandisha? Sauli akajibu, mimi nina huzuni sana; kwa maana Wafilisti wananifanyia vita, na Mungu ameniacha, wala hanijibu tena, wala kwa manabii; wala kwa ndoto; kwa hiyo nimekuita upate kuniambia nifanyeje.” [TA 122.5; UM Aya ya 42]

Samweli alipokuwa hai, Sauli alikuwa amedharau shauri lake, na alikuwa amechukizwa na maonyo yake. Lakini sasa, katika saa ya dhiki yake na msiba, alihisi kwamba mwongozo wa nabii ndio ulikuwa tumaini lake pekee, na ili kuwasiliana na balozi wa Mbinguni, alikimbilia kwa mjumbe wa kuzimu! Sauli alikuwa amejiweka kabisa chini ya nguvu za Shetani; na sasa yeye ambaye furaha yake pekee ni kusababisha taabu na uharibifu, alitumia vyema nafasi yake, kumharibu mfalme asiye na furaha. Kwa kujibu ombi la Sauli la uchungu ulikuja ujumbe wa kutisha, ukidhaniwa unatoka katika midomo ya Samweli: [TA 123.1; UM Aya ya 43]

“Kwa nini kuniuliza mimi, akiwa Bwana amekuacha, na amekuwa adui yako? ... Kwa sababu hukuitii si sauti ya Bwana, ... kwa hiyo ... tena Bwana atawatia Israeli pamoja nawe katika mikono ya Wafilisti.”— Patriachs and Prophets, 680. [TA 123.2; UM Aya ya 44]

Sauli alipomhitaji Samweli, Bwana hakumfanya Samweli kumtokea Sauli. Hakuona chochote. Shetani hakuruhusiwa kumsumbua Samweli aliyesalia kaburini, na kumleta katika hali halisi kwa mchawi wa Endori. Mungu hampi Shetani uwezo wa kuwafufua wafu. Lakini malaika wa Shetani wanajifanya kuwa kama marafiki waliokufa, na kusema na kufanya kama wao, ili kupitia marafiki wanaodai kuwa walikufa apate kutimiza vizuri zaidi kazi yake ya udanganyifu. Shetani alimjua Samweli vizuri, naye alijua jinsi ya kumwakilisha mbele ya mchawi wa Endori, na kutamka kwa usahihi hatima ya Sauli na wanawe.— The Spirit of Prophecy 1:376. [TA 123.3; UM Aya ya 45]

Maelezo ya Maandiko ya ziara ya Sauli kwa mwanamke wa Endori yamekuwa chanzo cha mkanganyiko kwa wanafunzi wengi wa Biblia. Kuna baadhi ya wanaochukua msimamo kwamba Samweli alikuwepo katika mazungumzo na Sauli, lakini Biblia yenyewe inatoa msingi wa kutosha kinyume na hitimisho hilo. Ikiwa, kama inavyodaiwa na wengine, Samweli alikuwa mbinguni, lazima awe ameitwa kutoka huko, ama kwa uwezo wa Mungu au na Shetani. Hakuna anayeweza kuamini hata kidogo kwamba Shetani alikuwa na uwezo wa kumwita nabii mtakatifu wa Mungu kutoka mbinguni ili kuipa heshima huduma ya kuongea na wafu ya mwanamke aliyetelekezwa. Wala hatuwezi kuhitimisha kwamba Mungu alimwita kwenye pango la mchawi; kwa kuwa Bwana alikuwa amekataa tayari kuwasiliana na Sauli kwa ndoto, kwa Urimu, au kwa manabii. Hizi zilikuwa njia za mawasiliano zilizowekwa na Mungu mwenyewe, na hakuziacha ili kufikisha ujumbe kupitia kwa wakala wa Shetani. [TA 124.1; UM Aya ya 46]

Ujumbe wenyewe ni ushahidi tosha wa asili yake. Lengo lake halikuwa kumwongoza Sauli kwenye toba, bali kumhimiza katika uangamivu; na hii si kazi ya Mungu, bali ya Shetani. Zaidi ya hayo, kitendo cha Sauli katika kutafuta ushauri kwa mwanamke mchawi kinatajwa katika Maandiko kuwa sababu moja kwa nini alikataliwa na Mungu na kuachwa hata kufikia maangamizo. “Basi Sauli alikufa kwa ajili kosa lake alilomkosa Bwana, kwa sababu ya Neno la Bwana, asilolishika, na tena kwa kutaka shauri kwa mwenye pepo wa utambuzi, aulize kwake; asiulize kwa Mungu; kwa hiyo akamwua, na ufalme akamgeuzia Daudi mwana wa Yese.” 1 Mambo ya Nyakati 10:13, 14.— Patriachs and Prophets.683. [TA 124.2; UM Aya ya 47]

## SURA YA 11

## MALAIKA TANGU ENZI ZA DAUDI HADI KUTEKWA NA BABELI

### Utawala Wa Daudi

Sanduku la Agano lilibaki katika nyumba ya Abinadabu mpaka Daudi alipotawazwa kuwa mfalme. Ndipo akawakusanya wateule wote wa Israeli, watu thelathini elfu, nao wakaenda kulileta Sanduku la Agano la Mungu. Nao wakaliweka Sanduku hilo juu ya gari jipya, kisha akalileta kutoka katika nyumba ya Abinadabu. Uza na Ahio, wana wa Abinadabu, wakaliendesha gari. Daudi na nyumba yote ya Israeli walicheza mbele za Bwana kwa vinanda vya namna nyingi. "Na walipofika kwenye uga wa Nakoni, Uza akalinyooshea mkono Sanduku la Agano la Mungu, na akalishika, kwa maana wale ng'ombe walikunguwaa. Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Uza, na Mungu akampiga huko kwa kosa lake; naye akafa hapo karibu na sanduku la Mungu. Uza aliwakasirikia wale ng'ombe, kwa sababu walijikwaa. Akaonyesha kutomwamini Mungu kwa dhahiri, kana kwamba Yeye aliyelileta sanduku kutoka katika nchi ya Wafilisti, hangeweza kuliangalia. Malaika waliolihudumia Sanduku la Agano walimpiga Uza kwa sababu ya kukosa subira na kuweka mkono wake juu ya Sanduku la Agano la Mungu.— Spiritual Gifts 4a:111. [TA 126.1; UM Aya ya 1]

Kwa nia ya kupanua ushindi wake kati ya mataifa ya kigeni, Daudi aliamua kuongeza jeshi lake kwa kuhitaji utumishi wa kijeshi kutoka kwa wote waliokuwa na umri ufaao. Ili kutekeleza hili, ikawa muhimu kufanya sensa ya watu. Ilikuwa ni kiburi na tamaa ya ukuu vilivyochochea kitendo hiki cha mfalme…..[TA 127.1; UM Aya ya 2]

Kusudi la kitendo hiki lilikuwa kinyume kabisa na kanuni za kanuni za serikali inayoongozwa na Mungu. Hata Yoabu alilipinga hili, japo yeye

mwenyewe alihusika na mipango ya ufidhuli hapo awali. “Lakini neno la mfalme likashinda dhidi ya Yoabu.” ... [TA 127.2; UM Aya ya 3]

Asubuhi iliyofuata ujumbe ulileTwa kwa Daudi na nabii Gadi: “BWANA asema hivi, Jichagulie njaa ya miaka mitatu; au miezi mitatu ya kuangamizwa mbele ya adui zako, ukipatwa na upanga wa adui zako; ama siku tatu upanga wa Bwana, yaani, tauni katika nchi, na malaika wa Bwana akiharibu katika mipaka yote ya Israeli. Kwa hiyo sasa,” alisema nabii, “basi ufikiri ni jawabu gani nimrudishie Yeye aliyenituma..” [TA 127.3; UM Aya ya 4]

Jibu la mfalme lilikuwa, ... “Na tuanguke sasa mkononi mwa Bwana; kwa maana rehema Zake ni nyingi; wala nisianguke katika mkono wa mwanadamu.”—Patriarchs and Prophets, 747, 748. [TA 127.4; UM Aya ya 5]

Uharibifu wa haraka ulifuata. Elfu sabini waliangamizwa kwa tauni. Daudi na wazee wa Israeli walikuwa katika aibu na maumivu, wakiomboleza mbele za Bwana. Malaika wa Bwana alipokuwa njiani kuiangamiza Yerusalemu, Mungu alimwambia Malaika aache kazi yake ya mauti, Malaika huyu, aliyekuwa amevaa mavazi ya vita, na upanga uliofutwa mkononi mwake na huku akiunyosha juu ya Yerusalemu, akafunuliwa na kuonekana machoni mwa Daudi, na kwa wale walio pamoja naye. Daudi akaogopa sana, lakini akalia kwa uchung dhiki yake na huruma yake kuhusiana na Israeli. Akaomba kwa Mungu kuwaokoa kondoo hao. Kwa uchungu yeye akakiri, “Nimefanya dhambi, na nimefanya kwa uovu; lakini kondoo hawa wamefanya nini? Mkono wako, nakuomba, uwe juu yangu, na juu ya nyumba ya baba yangu.”— The Spirit of Prophecy 1:385, 386. [TA 127.1; UM Aya ya 6]

Malaika mwenye kuharibu aliacha mpango wake nje ya Yerusalemu. Akasimama juu ya Mlima Moria, “katika kiwanja cha kupuria cha Arauna Myebusi.” Kwa kuongozwa na nabii, Daudi akaenda mlimani, na huko akamjengea Bwana madhabahu, “na kutoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani, wakamwita Bwana; Naye akamjibu kutoka mbinguni kwa moto juu ya madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa.” “Basi Bwana aliiridhia nchi, na tauni ikazuiliwa katika Israeli.” [TA 128.1; UM Aya ya 7]

Mahali ambapo madhabahu ilijengwa, tangu wakati huo na kuendelea palitambulika kuwa ardhi takatifu, palikabidhiwa kwa mfalme na Ornani kama zawadi. Lakini mfalme akakataa kuipokea “Daudi akampa Ornan kwa ajili ya mahali hapo shekeli mia sita za dhahabu kwa uzani. Hapo ndipo pahali ambapo Abrahamu alijenga madhabahu akinuia kumtoa mwanawe kafara, na kisha pakawekwa wakfu kwa ukombozi huu mkuu (wa malaika wa kuleta tauni alipozuia uharibifu), hapo baadaye palichaguliwa kama mahali pa hekalu lililojengwa na Sulemani…[TA 128.2; UM Aya ya 8]

Tangu mwanzoni kabisa wa utawala wa Daudi, mojawapo ya mipango yake

bora zaidi ilikuwa ni ule wa kumjengea Bwana hekalu. Ingawa hakuwa ameruhusiwa kutekeleza mpango huu, hata hivyo alikuwa amedhihirisha ari na moyo kwa ajili ya huo mkakati.— Patriachs and Prophets, 748, 750.

Bwana, kwa njia ya malaika Wake, alimwagiza Daudi, na kumpa kielelezo cha nyumba ambayo Sulemani angemjengea. Malaika aliagizwa kusimama kando ya Daudi alipokuwa akiandika, kwa manufaa ya Sulemani, maelekezo muhimu kuhusiana na mipango ya nyumba.— Spiritual Gifts 4a:94. [TA 129.1; UM Aya ya 9]

**Sulemani**

Mioyo ya watu ikamgeukia Sulemani kama ilivyokuwa kwa Daudi, nao wakawa wakimtii katika mambo yote. Bwana akamtuma Malaika Wake amwelekeze Sulemani kwa ndoto, wakati wa usiku. Aliota kuwa Mungu anazungumza naye. "Mungu akasema, Omba utakalo nikupe. Sulemani akasema, Umemfanyia mtumishi wako Daudi, Fadhili kuu, baba yangu, kadiri alivyoenenda mbele zako katika Kweli, na katika haki, na katika unyofu wa moyo pamoja Nawe; Nawe umemwekea fadhili hii kuu maana umempatia mwana wa kuketi katika kiti chake cha enzi, kama hivi leo, nipe mtumishi wako mwenye moyo wa adili niwahukumu watu wako, nipate kupambanua kati ya jema na baya; kwa maana ni nani awezaye kukuhukumu hawa watu Wako walio wengi?"— Spiritual Gifts 4a:96, 97. [TA 128.1; UM Aya ya 10]

Mbali na makerubi juu ya sanduku, Sulemani alifanya malaika wengine wawili wa ukubwa zaidi, wamesimama kila mwisho wa Sanduku la Agano, wakiwakilisha malaika wa mbinguni ambao daima huilinda sheria ya Mungu. Haiwezekaniki kuelezea uzuri na fahari ya maskani hii. Humo, kama katika hema jangwani, Sanduku hilo takatifu lilikuwa likibebwa kwa utaratibu mtukufu, wa heshima, na kuwekwa mahali pake chini ya mabawa ya wale makerubi wawili wa kifahari waliosimama juu ya sakafu.—The Spirit of Prophecy 1:413. [TA 129.1; UM Aya ya 11]

**Eliya**

Baada ya kuonekana kwake kwa mara ya kwanza kwa Ahabu, akimwonesha hukumu za Mungu kwa sababu ya uasi wake na wa Israeli, Mungu alielekeza kutoka katika nguvu za Yezebeli mpaka mahali pa usalama milimani, karibu na kijito cha Kerithi. Hapo alimheshimu Eliya kwa kumpelekea chakula asubuhi na jioni kwa malaika wa mbinguni. Kisha, kijito kilipokauka, akampeleka kwa mjane wa Sarepta, na kufanya muujiza wa kila siku wa kuitunza familia ya

mjane na Eliya kwa chakula. Testimonies for the Church 3:288. [TA 130.1; UM Aya ya 12]

Akikabiliana na Mfalme Ahabu na manabii wa uongo na kuzungukwa na majeshi ya Israeli yaliyokusanyika, Eliya akasimama, pekee yake na akaonekana kuitetea heshima ya Yehova. Yeye ambaye ufalme wote ulimshutumu kwa uzito wa ole zake, sasa yuko mbele yao, akiwa hana ulinzi mbele ya mfalme wa Israeli, mbele ya manabii wa Baali, watu wa vita, na maelfu ya watu waliokuwepo. Lakini Eliya hayuko peke yake. Juu na karibu naye kuna ulinzi wa majeshi ya mbinguni—malaika walio na nguvu nyingi zaidi.— Prophets and Kings,147. [TA 130.2; UM Aya ya 13]

Katika mwanga kamili wa jua, akiwa amezungukwa na maelfu -watu wa vita, manabii wa Baali, na mfalme wa Israeli— anasimama bila ulinzi, Eliya, anaonekana peke yake, ila si peke yake. Jeshi lenye nguvu zaidi la mbinguni lilimzunguka. Malaika walio na nguvu nyingi wamekuja kutoka mbinguni kumlinda nabii mwaminifu na mwenye haki. Kwa ukali na sauti ya kuamuru Eliya analia: "Mtasitasita katikati ya mawazo wawili hata lini? ikiwa Bwana Ndiye Mungu, mfuateni Yeye; bali ikiwa ni Baali, haya mfuateni yeye. Na watu hawakumjibu neno lolote."— Testimonies for the Church 3:280. [TA 130.3; UM Aya ya 14]

Wakati Israeli juu ya Karmeli wana shaka na kusitasita, sauti ya Eliya tena inavunja ukimya: "Mimi, mimi peke yangu, nimesalia kuwa nabii wa Bwana Mungu; lakini manabii wa Baali ni watu mia nne na hamsini. Kwa hiyo basi na watutolee ng'ombe wawili; nao wachague ng'ombe mmoja kwa ajili yao wenyewe, na kumkata vipande vipande, na kuiweka juu ya kuni, wala wasitie moto chini: nami nitamtengeza huyo ng'ombe wa pili, na kumweka juu ya kuni, wala sitatia moto chini; nanyi liitieni jina la miungu yenu, nami nitaomba kwa Jina la Bwana; na Mungu atakayejibu kwa moto, na awe Ndiye Mungu."—Prophets and Kings, 148, 149. [TA 131.1; UM Aya ya 15]

Jinsi gani Shetani, ambaye alianguka kama umeme kutoka mbinguni, angependelea kuja ili kuwasaidia wale aliowadanganya, na ambao akili zao alikuwa amezidhibiti, na ambao walikuwa wamejitoa kikamilifu kwa utumishi wake. Kwa furaha angelituma moto na kuwasha dhabihu zao; lakini Yehova alikuwa amemwekea mipaka Shetani. Alikuwa amezuia uwezo wake, na mbinu zake zote hazingeweza kufua dafu katika kutoa cheche hata moja kwenye madhabahu za Baali.—The Review and Herald, Septemba 30, 1873. 16]

Je, Mungu alimwacha Eliya katika saa yake ya kujaribiwa? Oh!, hapana! Alimpenda Mtumishi Wake hata hapo Eliya alipohisi ameachwa na Mungu na mwanadamu, kuliko wakati, alipoyajibu maombi yake, kwa moto kutoka mbinguni na kuangaza kilele cha mlima. Na sasa, Eliya alipolala, sauti laini na yenye mguso wa kupendeza ikamwamsha. Aliamka kwa hofu, kana kwamba

akitaka kukimbia, akiogopa kwamba adui amempata. Lakini sura ya huruma iliyomwinamia haikuwa ya uso wa adui, bali ya rafiki. Mungu alikuwa ametuma malaika kutoka mbinguni na chakula kwa ajili ya mtumishi Wake. “Amka ule,” malaika akasema. “Akatazama, na tazama, palikuwa na mkate uliookwa juu ya makaa, na gudulia la maji kichwani pake. [TA 131.3; UM Aya ya 17]

Baada ya Eliya kushiriki katika kiburudisho kilichotayarishwa kwa ajili yake, akalala tena. Mara ya pili malaika akaja. Akamgusa mtu huyu ayechoka, akasema kwa huruma, “Ondoka, ule; Kwa sababu ya safari hii ni kubwa mno kwako.” "Akainuka, akala na kunywa" na kwa nguvu ya chakula hicho aliweza kusafiri “siku arobaini usiku na mchana mpaka Horebu, mlima wa Mungu,” ambapo alipata kimbilio katika pango.—Prophets and Kings, 166. [TA 132.1; UM Aya ya 18]

Jangwani, katika upweke na kuvunjika moyo baada ya uzoefu wake wa kilelel cha Mlima Karmeli, Eliya alikuwa amesema kwamba ilikuwa imetosha kuishi na alikuwa ameomba kwamba afe. Lakini Bwana katika huruma Zake hakufanya kulingana na neno lake. Bado kulikuwa na kazi kubwa ya Eliya kufanya.—Prophets and Kings, 228. [TA 132.2; UM Aya ya 19]

Kwa njia ya Malaika mwenye nguvu Neno la Bwana lilimjia,“Unafanya nini hapa, Eliya?” Kwa uchungu wa roho, Eliya aliomboleza akieleza malalamiko yake: “Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya Bwana, Mungu wa Mjeshi wa kwa maana wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga; nimesalia mimi peke yangu; nao wananitafuta roho yangu, wapate kuiondoa.” [TA 132.3; UM Aya ya 20]

Akimwita nabii huyo atoke kwenye pango alimokuwa amejificha, malaika akamwambia asimame mbele za Bwana juu ya mlima, na asikilize Neno Lake. Eliya alipotii, “Na tazama, Bwana akapita; upepo mwingi wenye nguvu ukapasua milima, ukaivunja vipande vipande miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule: na baada ya upepo tetemeko la ardhi; lakini Bwana hakuwamo katika tetemeko hilo; na baada ya tetemeko la ardhi moto; lakini Bwana hakuwamo motoni na baada ya moto sauti ndogo tulivu. Na ikawa, Eliya alipoisikia, alijifunika uso wake katika vazi lake, akatoka, na akasimama kwenye mlango wa pango.” Chuki yake ilinyamazishwa, roho yake ikalainika na kutiishwa. Sasa alijua kwamba imani tulivu, ya kumtegemea Mungu kwa uthabiti, daima ingempatia msaada wakati wa uhitaji.— The Review and Herald, Oktoba 23, 1913. [TA 132.4; UM Aya ya 21]

Eliya alipokuwa karibu kumwacha Elisha, akamwambia, “Omba lolote utakalo kwangu nikutendee kabla sijaondolewa kwako. Na Elisha akasema, nakuomba, sehemu mara dufu ya roho yako na iwe juu yangu.” 2Wafalme 2:9—GW (1915) 116. [TA 133.1; UM Aya ya 22]

“Naye Eliya akasema, Umeomba neno gumu; lakini ukiniona nitakapoondolewa kwako, utalipata; ...Ikawa walipokuwa wakiendelea mbele na kuzungumza, tazama! kukatokea gari la moto na farasi wa moto, likawatenga wote wawili; naye Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli. [TA 133.2; UM Aya ya 23]

“Elisha akaona, akapaza sauti, Baba yangu, baba yangu, gari la wa Israeli, na wapanda farasi wake!”—Education, 60. [TA 133.3; UM Aya ya 24]

### Elisha

Katika Wafalme wa Pili tunasoma jinsi malaika watakatifu walivyokuja kwa katika utume wa kuwalinda wateule wa Bwana. Nabii Elisha alikuwa huko Dothani, na huko mfalme wa ... Syria akatuma farasi na magari na watu wengi kumchukua. “Na mtumishi wa mtu wa Mungu alipoinuka asubuhi na mapema, na kutoka nje, tazama, jeshi limeuzunguka mji pamoja na farasi na magari. Mtumishi wake akamwambia, Ole wetu! tufanyeje?”—Australian Union Gleaner. Agosti 20, 1902. [TA 134.1; UM Aya ya 25]

“Usiogope,” lilikuwa jibu la nabii; “maana wale walio pamoja nasi ni wengi kuliko wale walio pamoja nao.” Na kisha, ili kwamba mtumishi apate kujua hili mwenyewe, “Elisha akaomba, akasema, Bwana, nakuomba, mfumbue macho yake, apate kuona.” “Bwana alifungua macho ya kijana; naye akaona: na tazama, mlima ulikuwa umejaa farasi na magari ya moto kumzunguka Elisha pande zote.” Kati ya mtumishi wa Mungu na majeshi ya maadui wenye silaha palikuwa na kikosi cha malaika wa mbinguni wanazunguka. Walikuwa wameshuka kwa nguvu kuu, si kuharibu, si kwa ajili ya kushurutisha ibada au heshima, bali kupiga kambi pande zote na kuwahudumia wale wa Bwana walio dhaifu na wasiojiweza.—Prophets and Kings,256, 257. [TA 134.2; UM Aya ya 26]

Elisha hakuruhusiwa kumfuata bwana wake katika gari la moto. Juu yake Bwana aliruhusu uje ugonjwa wa muda mrefu. Wakati saa nyingi za udhaifu na mateso ya kibinadamu, imani yake ilizishikilia imara ahadi za Mungu, na aliona daima juu yake wajumbe wa faraja na amani wa mbinguni wakimzunguka. Kama ilivyokuwa katika Dothani wakati ameona majeshi ya mbinguni yamemzunguka, magari ya moto ya Israeli na wapanda farasi wake, hivyo sasa alikuwa na ufahamu wa uwepo wa malaika wenye huruma; naye alitegemezwa.—Prophets and Kings,263, 264. [TA 134.3; UM Aya ya 27]

### Isaya

Katika siku ya Isaya ibada ya sanamu haikusababisha mshangao. Mazoea mabaya yalikuwa yameenea sana miongoni mwa matabaka yote, kiasi kwamba

wachache waliobaki kuwa waaminifu kwa Mungu mara nyingi walijaribiwa kuvunjika moyo na kuruhusu kufa moyo na huzuni kuingia kwenye fikra. [TA 135.1; UM Aya ya 28]

Mawazo kama haya yalikuwa yakiijaza akili ya Isaya alipokuwa amesimama katika nyua/varanda ya ukumbi wa hekalu. Ghafla lango la pazia la ndani la hekalu lilionekana kuinuliwa au kuondolewa, na yeye aliruhusiwa kutazama ndani, juu ya Patakatifu pa Patakatifu, ambapo hata miguu ya nabii huyu haikuweza kuingia. Maono yaliinuka mbele Yake Bwana, aketiye juu ya kiti cha enzi kilicho juu sana, na kuinuliwa sana, na mfululizo wa Utukufu Wake ukiijaza hekalu. Katika kila upande wa kiti cha enzi walingojea maserafi, nyuso zao zimefunikwa kwa kicho, walipokuwa wakihudumu mbele ya Muumba wao, na kuungana katika ibada sifa za dhati, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu Wake."— Prophets and Kings 306, 307. [TA 135.2; UM Aya ya 29]

Utukufu usioelezeka ulitoka kwa Yule aliyekuwa kwenye kiti cha enzi, na pindo Lake likalijaza hekalu Makerubi walikuwa upande huu wa kiti cha rehema, kama walinzi kumzunguka Mfalme mkuu, wakang'aa kwa utukufu ambao uliwafunika kutoka katika uwepo wa Mungu. Kadiri nyimbo zao za sifa ziliposikika kwa kina, na maelezo ya dhati ya kuabudu, nguzo za lango zikatetemeka kana kwamba zinatikiswa na tetemeko la ardhi. Viumbe hawa watakatifu waliimba sifa na utukufu wa Mungu kwa midomo yao isiyochafuliwa na dhambi. Tofauti kati ya sifa hafifu ambazo yeye Isaya alikuwa amezoea kumtolea Muumba na sifa thabiti za maserafi, zikamstajaabisha na zikamfanya nabii huyo apwaye. Alikuwa kwa wakati fulani na upendeleo wa hali ya juu wa kuthaminiwa kuwa na usafi usio na doa la tabia iliyotukuka ya Yehova. [TA 135.3; UM Aya ya 30]

Wakati alipokuwa akisikiliza wimbo wa malaika, walipokuwa wakipiga kelele, "Mtakatifu! Mtakatifu, mM akatifu, ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake," utukufu, uweza, na adhama ni vyake isiyo na kifani Bwana alipita mbele ya maono yake, na akavutiwa moyoni mwake. Katika nuru wa mng'ao huu usio na kifani, uliodhihirisha yote aliyoyapaswa kufanya aweze kustahimili katika ufunuo wa tabia ya kimbingu, hali yake ya ndani ya uchafu ilijitokeza mbele yake kwa uwazi wa kushangaza. Kila maneno yake yalionekana kuwa machafu kwake mwenyewe.— The Review and Herald, Oktoba 16, 1888. [TA 136.1; UM Aya ya 31]

Maserafi walikaa katika uwepo wa Yesu, lakini walijifunika mabawa yao nyuso zao na miguu yao. Walimtazama Mfalme katika Uzuri Wake, na kusujudu huku wakijifunika. Isaya alipouona utukufu wa Mungu, nafsi yake ilisujudu katika udongo. Kwa yale maono mengi yasiyooneka, machache aliyoruhusiwa kwa neema kuyatazama, hayo yalitosha kumjaza aibu na unyenyekevu. Haya

ndiyo matokeo kwenye akili ya mwanadamu wakati miale ya Jua la Haki inapomulika kwa utukufu ndani ya nafsi….Kadiri utukufu unaoongezeka wa Kristo unavyofunuliwa, mwanadamu hataona utukufu ndani yake; kwani ulemavu wake wa nafsi uliofichika huanikwa wazi, na kujitegema, kujiweka katika wadhifa wa juu na kujitukuza huzimwa kama moto. Nafsi inakufa, na Kristo anaishi.—The Signs of the Times, Desember 3, 1894. [TA 136.2; UM Aya ya 32]

Hilo ndiyo mandhari iliyompokea Isaya alipoitwa katika utume wa kinabii; lakini bado hakukata tamaa, kwa sababu masikioni mwake ilivuma sauti ya wimbo wa ushindi wa malaika wanaozunguka kiti cha enzi cha Mungu, "Dunia yote imejaa utukufu Wake." Isaya 6:3. Kisha imani yake iliimarishwa kwa maono ya ushindi mtukufu wa kanisa la Mungu, wakati "dunia itajawa na kumjua Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari." Isaya 11:9.— Prophets and Kings, 371. [TA 137.1; UM Aya ya 33]

### Ezekieli

Juu ya ukingo wa mto Kebari, Ezekieli aliona tufani inayoonekana kuja kutoka kaskazini, "wingu kubwa, na moto ukifanya duara ya nuru, na mwangaza pande zote, na katikati yake kitu kama rangi ya kaharabu katikati ya moto huo." Idadi ya magurudumu yakipishana yalisogezwa na viumbe hai wanne. Juu yake haya yote "kulikuwa na mfano wa kiti cha enzi, kuonekana kwake kama yakuti samawi; na juu ya kiti cha enzi mfano wa muonekano wa Mtu juu yake." "Kukaonekana katika makerubi mfano wa mkono wa mwanadamu chini ya mbawa zao." Ezekieli 1:4, 26; 10:8. [TA 137.2; UM Aya ya 34]

Mpangilio wa magurudumu ulikuwa mgumu kiasi kwamba kwa mtazamo ulionekana kuwepo mkanganyiko, hata hivyo yalisonga mbele kwa upatanifu kamili. Viumbe wa Mbinguni, waliendelea kusogea kwa kuongozwa kwa mkono ulio chini ya mabawa ya makerubi ambao ulikuwa ukitoa nishati ya kuyasukuma magurudumu hayo; juu yao, kwenye kile kiti cha enzi cha yakuti, alikuwepo Yule wa Milele; na kuzunguka kiti cha enzi kulikuwa na upinde wa mvua, ambayo ni nembo ya rehema ya Mungu...Kama ilivyokuwa katika mtanziko wa magurudumu yaliyokuwa chini ya uongozi wa Ule Mkono chini ya mbawa za makerubi, ndivyo mambo tata ya wanadamu yalivyo chini ya udhibiti wa Mungu. Katikati ya magomvi na ghasia za mataifa, Yeye aketiye juu ya makerubi angali anaongoza mambo ya dunia hii.— Prophets and Kings, 535, 536. [TA 137.3; UM Aya ya 35]

## SURA YA 12

## MALAIKA TANGU UHAMISHONI KAMA MATEKA HADI KWA YOHANA MBATIZAJI

### Danieli na Wenzake Watatu

Upendo na ucha Mungu ulikuwa kwa Danieli, naye alielimisha na kuzoeza uwezo wake wote kuitikia upendo unaojali wa Mwalimu Mkuu kwa kadiri inavyowezekana, akiiweka nia katika kukubali kutenda matakwa Yake. Vijana wanne wa Kiebrania hawakuruhusu nia za ubinafsi na upendo wa maburudisho na starehe kuchukua nyakati za thamani za maisha haya. Walifanya kazi kwa moyo wa na akili za utayari. Hiki sio kiwango cha juu kuliko kila Mkristo awezacho kukifikia. Mungu Anataka kutoka kwa kila Mkristo anayejifunza, zaidi ya kile Alichompatia.. Ninyi ni "tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na wanadamu."—Fundamentals of Christian Education, 230. [TA 139.1; UM Aya ya 1]

Wale wanaofanya kama vile Danieli na wenzake walivyofanya watakuwa na ushirikiano wa Mungu na malaika.— Manuscript Releases 4:125. [TA 139.2; UM Aya ya 2]

### Tanuru La Moto La Nebukadneza

Kama ilivyokuwa katika siku za Shadraka, Meshaki, na Abednego, ndivyo itakavyokuwa katika siku za kipindi cha mwisho cha historia ya dunia, Bwana atafanya kazi kwa uwezo mkuu kwa ajili ya wanaosimama imara katika haki, yaani jambo lililo sahihi. Yeye Aliyetembea na Waebrania waliostahili katika tanuru ya moto atakuwa pamoja na wafuasi Wake popote walipo. Uwepo Wake wa kudumu uwatafariji na kuwastahilisha. Katika wakati wa taabu—taabu ambayo haijawahi kutokea tangu kuwepo kwa taifa—wateule Wake watasimama bila kuondoshwa. Shetani pamoja na majeshi yote ya uovu hayawezi kuwaharibu watakatifu wa Mungu walio dhaifu zaidi. Malaika walio na uwezo mkubwa zaidi watawalinda, na kwa niaba yao Yehova atajidhihirisha kuwa "Mungu wa miungu," awezaye kuokoa wale ambao wameweka tumaini lao Kwake.— Prophets and Kings, 513. [TA 139.3; UM Aya ya 3]

### Karamu ya Belshaza

Walipokuwa katikati ya furaha ya kuabudu sanamu usiku ule, uso wa mfalme ukambadilika ghafla, na akaonekana kulegea kwa hofu; kwa maana Tazama! mkono usio na damu unaweka alama za ajabu kwenye ukuta dhidi

yake. Wafanyao karamu wakapata udadisi, na kwao, maandishi yasiyoeleweka. Makelele ya karamu yakakoma, na ukimya wenye uchungu ukaupata umati. Mawazo ya mfalme yalisumbuliwa, "viungo vya viuno vyake vikalegea, na magoti yake yakangongana moja dhidi ya mwingine." (yakapiga makofi) Akitetemeka kwa hofu, naye "alilia kwa sauti kubwa waletwe wachawi, na Wakaldayo, na wanajimu. Na mfalme akanena, akawaambia wenye hekima wa Babeli, Kila asomaye Maandiko haya, na kunionyesha tafsiri yake, atavikwa mavazi ya zambarau na kuwa na mkufu wa dhahabu shingoni mwake, na atakuwa mtu wa tatu katika ufalme." Lakini watu hawa hawakuweza kutafsiri herufi za ajabu zilizoandikwa kwa mkono wa malaika wa Mungu kama ilivyokuwa wakati wa kutafsiri ndoto ya Nebukadneza.—Review and Herald, Februari 8, 1881. [TA 140.1; UM Aya ya 4]

Kulikuwa na shahidi katika jumba la mfalme Belshaza kwenye karamu hiyo….Malaika katika tukio hilo aliandika maandishi ya ajabu katika kuta za ikulu.— The Ellen G. White 1888 Materials, 517. [TA 141.1; UM Aya ya 5]

**Danieli Kwenye Tundu La Simba**

Danieli alimwomba Mungu wake mara tatu kwa siku. Shetani hukasirishwa kwa maombi ya dhati, na bidii, kwa maana anajua kwamba atapata hasara. Danieli alipendwa kuliko maliwali na wakuu, kwa sababu ya roho ya ubora iliyokuwa ndani yake. Malaika waovu waliogopa ushawishi wake ungedhoofisha udhibiti wao juu ya watawala wa ufalme …….Washitaki wa jeshi la malaika waovu liliwachochea maliwali na wakuu kuwa na wivu na kijicho, nao wakamtazama Danieli kwa makini ili kupata neno fulani dhidi yake ili wapate kumshitaki kwa mfalme, lakini hawakufanikiwa. Kisha hawa mawakala wa Shetani wakatafuta kuufanya uaminifu wake kwa Mungu iwe sababu ya uangamivu wake. Malaika waovu waliweka mpango kwa ajili yao, na mawakala hawa waliutekeleza kwa uthabiti. Mfalme alikuwa hajui juu ya uharibifu wa hila uliokusudiwa dhidi ya Danieli. [TA 141.2; UM Aya ya 6]

Pamoja na kujua kikamilifu juu ya amri ya mfalme Danieli bado aliinama mbele za Mungu wake, "madirisha yake yakiwa wazi." Akazingatia maombi kwa Mungu kuwa yenye umuhimu wa kutosha hata kama ni kuyatoa maisha yake dhabihu badala ya kuacha kusali. Kwa sababu ya kusali kwake kwa Mungu, yeye alitupwa katika tundu la simba. Malaika waovu walitimiza kusudi lao. Lakini Danieli aliendelea kuomba, hata katika tundu la simba….Je! Mungu alimsahau? Hapana!; Yesu, Mkuu wa majeshi ya mbinguni, alimtuma malaika Wake kuvifunga vinywa vya wale simba wenye njaa ili wasimdhuru mtu wa Mungu anayesali na kote kulikuwa na amani katika shimo hilo la kutisha. Mfalme alishuhudia kuhifadhiwa kwake alikokupata, naye akamtoa nje kwa heshima. Shetani na malaika zake walishindwa na kukasirika. Mawakala ambao Shetani alikuwa amewatumia walihukumiwa kuangamia kwa njia ya

kutisha ambayo walikuwa wamepanga kumwangamiza Danieli.— Spiritual Gifts 4b:85, 86. [TA 141.3; UM Aya ya 7]

### Gabrieli Atumwa kufafanua Maono ya Danieli 8

Muda mfupi kabla ya kuanguka kwa Babeli, Danieli alipokuwa akitafakari juu ya unabii wa Isaya na Yeremia na kumtafuta Mungu kuzielewa hizo nyakati, alipewa mfululizo wa maono kuhusu kuinuka na kuanguka kwa falme. Kwa maono ya kwanza, kama yalivyoandikwa katika sura ya saba ya kitabu cha Danieli, tafsiri ilitolewa; lakini si yote yaliyowekwa wazi kwa nabii. "Fikra zangu zilinifadhaisha sana," aliandika juu ya uzoefu wake katika wakati huo, "na uso wangu ukanibadilika: lakini nikaliweka jambo hilo moyoni mwangu." Danieli 7:28. [TA 142.1; UM Aya ya 8]

Kupitia maono mengine nuru zaidi ilitolewa juu ya matukio hayo ya siku zijazo; na ilikuwa mwisho wa maono haya ndipo Danieli aliposikia "mtakatifu mmoja akinena, na mtakatifu mwingine akamwuliza huyo aliyenena, Maono hayo yatakuwa hata lini? Jibu hilo lililotolewa lilikuwa, "Hata saa za nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa," alifadhaika. Kwa dhati alitafuta maana ya maono hayo. Hakuweza kuelewa uhusiano kati ya miaka sabini ya utumwa, kama ilivyotabiriwa na Yeremia, na ile miaka elfu mbili na mia tatu (2300) ambayo alisikia katika maono mgeni wa mbinguni akitangaza kwamba siku hizi zingepita kabla ya Patakatifu pa Mungu kutakaswa. Malaika Gabrieli alimpa sehemu ya tafsiri; hata hivyo nabii aliposikia Maneno haya, "Maono hayo ... yatakuwa ya siku nyingi," alizimia. [TA 142.2; UM Aya ya 9]

Akiwa bado amelemewa na mzigo kwa ajili ya Israeli, Danieli alijifunza upya unabii wa Yeremia. Kulikuwa na mambo yaliyokuwa wazi sana…..[TA 143.1; UM Aya ya 10]

Akiwa na imani yenye msingi wa Neno hakika la unabii, Danieli alimsihi Bwana ili ahadi hiyo itimizwe upesi.— Prophets and Kings, 553, 554. [TA 143.2; UM Aya ya 11]

Kadiri maombi ya Danieli yalivyoendelea, malaika Gabrieli akaja kwa upesi, kutoka katika nyua za mbinguni, na kumwambia kwamba maombi yake yamesikiwa na kujibiwa. Malaika huyu mwenye nguvu alitumwa kumpa maarifa na ufahamu—kufungua mbele yake siri za nyakati zinazokuja. Hivyo, huku akitafuta kwa bidii kujua na kuelewa ukweli, Danieli alisogezwa katika ushirika na mjumbe aliyeteuliwa na Mbingu.— The Review and Herald, Februari 8, 1881. [TA 143.3; UM Aya ya 12]

Hata kabla Danieli hajamaliza kumsihi Mungu, Gabrieli akamtokea tena na kuelekeza usikivu wake kwenye maono aliyokuwa ameyaona hapo kabla ya

kuanguka kwa Babeli wakati wa kifo cha Belshaza. Ndipo malaika akaeleza kwa undani kipindi cha yale majuma sabini.— The Review and Herald, Machi 21, 1907. [TA 143.4; UM Aya ya 13]

## Pambano Katika Kuwaongoa Wafalme Wa Uajemi

Mawakala wa Mbinguni wanapaswa kushindana na vikwazo kabla ya kusudi la Mungu kutimiwa kwa wakati wake. Mfalme wa Uajemi alikuwa anatawaliwa na malaika wa juu zaidi wa waovu wote. Alikataa, kama alivyofanya Farao, kulitii Neno la Bwana. Gabrieli alisema,Shetani alinipinga siku ishirini na moja kwa mambo yake dhidi ya Wayahudi. Lakini Mikaeli alikuja kunisaidia wake, nami nikamwacha huko pamoja na wafalme wa Uajemi, akidhibiti mamlaka, akitoa maelekezo yanaofaa dhidi ya mabaya.— The S.D.A. Bible Commentary 4:1173. [TA 144.1; UM Aya ya 14]

Koreshi, mfalme wa Uajemi alikuwa amepinga maoni ya Roho wa Mungu wakati wa majuma matatu Danieli alipokuwa amefunga na kuomba, lakini Mkuu wa Mbinguni, <alaika mkuu, Mikaeli, alitumwa kugeuza moyo wa mfalme mkaidi kuchukua hatua iliyoamuliwa kujibu maombi ya Danieli.— The Review and Herald, Februari 8, 1881. [TA 144.2; UM Aya ya 15]

Mtu ambaye alikuwa Ndiye Mwana wa Mungu alimtokea Danieli. Maelezo haya ya Danieli yanafanana na yale yaliyotolewa kwa Yohana wakati Kristo alipofunuliwa kwake kwenye Kisiwa cha Patmo. [TA 144.3; UM Aya ya 16]

Bwana wetu sasa anakuja na mjumbe mwingine wa mbinguni kumfundisha Danieli kile ambacho kingetukia katika siku za mwisho.— The Review and Herald, Februari 8, 1881. [TA 144.4; UM Aya ya 17]

Danieli ... hakuweza kuutazama uso wa malaika, na hakuwa na nguvu; nguvu zote zilimwishia. Kwa hiyo malaika akaja kwake na kumweka katika magoti. Hakuweza tena kumtazama. Na kisha Malaika akamjia kwa sura ya mtu. Ndipo aliweza kustahimili kumtazama machoni (kumwona).— Manuscript Releases 2:348. [TA 144.5; UM Aya ya 18]

Ushindi ulipatikana hatimaye, na nguvu za adui zikadhibitiwa siku zote za Koreshi, aliyetawala miaka saba; na siku zote za mwanawe Cambyses, aliyetawala kama miaka saba na nusu.— The Review and Herald, Desember 5, 1907. [TA 145.1; UM Aya ya 19]

### Hekalu la Pili

Hekalu la pili halikuwa sawa na la kwanza kwa fahari, wala halikupewa heshima ya kuwa na zile ishara zinazoonesha uwepo wa Mungu ambazo zilikuwemo kwenye hekalu la kwanza. Hakukuwa na udhihirisho wa nguvu za

Mungu za kuashiria kuwekwa wakfu kwake. Hakuna wingu la utukufu lililoonekana kujaza Patakatifu palipojengwa upya. Hakuna moto kutoka mbinguni ulioshuka kuteketeza dhabihu juu ya madhabahu yake. Shekina haikukaa tena kati ya makerubi katika Patakatifu pa Patakatifu; Sanduku la Agano, Kiti cha Rehema, na Meza za ushuhuda hazikupatikana humo. Hakuna ishara kutoka mbinguni iliyomjulisha kuhani aliyeomba mapenzi ya Yehova.—Prophets and Kings, 596, 597. [TA 145.2; UM Aya ya 20]

### Ezra

Wana wa utumwa waliokuwa wamerudi pamoja na Ezra "wakatoa sadaka sadaka za kuteketezwa kwa Mungu wa Israeli" kwa ajili ya sadaka ya dhambi na kama ishara ya ukarimu na shukrani kwa ajili ya ulinzi wa malaika watakatifu wakati wa safari.—Prophets and Kings, 619. [TA 145.3; UM Aya ya 21]

### Nehemia

Miezi minne Nehemia alisubiri nafasi nzuri ya kuwasilisha ombi lake kwa mfalme. Wakati huu, ingawa moyo wake ulikuwa umelemewa na huzuni, alijitahidi kujistahi kwa uchangamfu mbele ya kifalme. Katika kumbi hizo za anasa na fahari, wote lazima waonekane wachangamfu na wenye furaha. Dhiki haipaswi kutupa kivuli chake juu ya uso wa mtumishi yeyote wa mfalme. Lakini katika wakati wa utumishi Nehemia, mambo yakiwa yamefichwa machoni pa wanadamu, maombi yalikuwa mengi, maungamo, na machozi, yalisikiwa na kushuhudiwa na Mungu na malaika.—Prophets and Kings, 630. [TA 146.1; UM Aya ya 22]

### Maono ya Zekaria

"Kisha nikainua macho yangu," asema Zekaria, "nikaona, na tazama mtu mwenye kamba ya kupimia mkononi mwake. Ndipo nikasema, unakwenda wapi? Naye akaniambia, ninakwenda kuupima Yerusalemu, nione upana wake ulivyo, na urefu wake ulivyo. Na tazama, malaika aliyesema nami akatoka, na malaika mwingine akaenda akatoka kwenda kuonana naye, akamwambia, piga mbio, ukaseme na kijana huyu; na kusema, Yerusalemu utakaliwa na watu kama vijiji visivyo na kuta kwa ajili wingi wa watu na mifugo iliyomo ndani yake; kwa maana Mimi, asema Bwana, nitakuwa kwake ukuta wa moto kuuzunguka, na nitakuwa huo utukufu ndani yake."— The Review and Herald, Desemba 26, 1907. [TA 146.2; UM Aya ya 23]

### Maono ya Yoshua na Malaika

Tukio la mashtaka ya Shetani liliwasilishwa mbele ya nabii. Anasema,

“Akanionyesha Yoshua, kuhani mkuu, amesimama mbele ya malaika wa Bwana, na Shetani amesimama mkono wake wa kuume. Kushindana naye.”—The Review and Herald, Agosti 22, 1893. [TA 146.3; UM Aya ya 24]

Kielelezo cha nguvu na cha kuvutia zaidi cha kazi ya Shetani na kazi ya Kristo, na uwezo wa Mpatanishi wetu kumshinda mshitaki wa watu wake ,kimetolewa katika unabii wa Zekaria. Katika maono matakatifu nabii anamtazama Yoshua kuhani mkuu, “amevaa mavazi machafu,” akisimama mbele ya Malaika wa Bwana, akisihi rehema za Mungu kwa niaba ya watu Wake walio katika dhiki kuu. Shetani anasimama mkono wake wa kuume ili kumpinga. [TA 147.1; UM Aya ya 25]

Kwa sababu Israeli walikuwa wamechaguliwa kuhifadhi maarifa ya Mungu duniani, walikuwa, tangu kuwepo kwao kwanza kama taifa, walengwa mahsusi wa uadui wa Shetani, na alikuwa amekusudia kusababisha uangamivu wao. Hakuweza kuwadhuru wakati walipokuwa watiifu kwa Mungu; kwa hiyo alikuwa ametumia uwezo wake wote na hila ili kuwashawishi katika dhambi. Wakiwa wamenaswa na majaribu yake waliasi sheria ya Mungu na hivyo kutengwa na Chanzo cha nguvu zao, na kuachwa kuwa mawindo ya adui zao wa kipagani. Nao walichukuliwa utumwani Babeli, na huko wakabaki kwa miaka mingi. [TA 147.2; UM Aya ya 26]

Lakini hawakuachwa na Bwana. Manabii wake walitumwa kwao kwa makaripio na maonyo. Watu waliamka kuona hatia yao, wakajinyenyekeza mbele za Mungu, na kurudi Kwake kwa toba ya Kweli. Kisha Bwana akawatumia ujumbe wa kuwatia moyo, akitangaza kuwa atawaokoa kutoka katika utumwa wao na kuwarudisha katika fadhila Zake. Jambo hili ndilo Shetani alikusudia kulizuia. Masalio ya Israeli walikuwa tayari wamerudi katika nchi yao wenyewe, na Shetani alikuwa akitafuta kuwatumia mataifa ya kikafiri, waliokuwa wajumbe wake, ili kuwaangamiza kabisa. [TA 147.3; UM Aya ya 27]

Kuhani mkuu, Yoshua hakuweza kujitetea mwenyewe au watu wake dhidi ya mashtaka ya Shetani. Hakudai kwamba Israeli wako huru dhidi ya kosa. Katika mavazi yake machafu, yanayoashiria dhambi za watu ,ambazo amezibeba kama mwakilishi wao, anasimama mbele ya Malaika, akiungama hatia yao, huku akielekeza kwenye toba na unyonge wao, wakitegemea rehema ya Mkombozi Mwenye kusamehe dhambi na katika imani inayodai ahadi za Mungu. [TA 148.1; UM Aya ya 28]

Kisha Malaika, ambaye ni Kristo Mwenyewe, Mwokozi wa wenye dhambi, akamnyamazisha mshitaki wa watu wake, akisema: “Bwana na akukemee, Ee Shetani; Bwana aliyechagua Yerusalemu na akukeme: Je! Hiki si kijinga kilichotolewa motoni?”Israeli walikuwa kwa muda mrefu wakikaa katika tanuru ya mateso. Kwa sababu ya dhambi zao walikuwa wamekaribia kuteketezwa na moto uliowashwa na Shetani na mawakala wake ili kuwaangamiza, lakini

Mungu alikuwa sasa ameweka mkono Wake kuwaokoa. Katika toba na unyenyekevu wao Mwokozi Mwenye huruma hatawaacha watu Wake katika nguvu za katili za makafiri. [TA 148.2; UM Aya ya 29]

Maombezi ya Yoshua yanapokubaliwa, amri inatolewa, “Mvueni hizi nguo zenye uchafu,” kutoka kwake na kwa Yoshua Malaika asema, “Tazama, nimekuondolea uovu wako; Nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi.” "Hivyo wakamvika kilemba kichwani, na kumvika mavazi.” Dhambi zake na za watu wake zikasamehewa. Israeli walivikwa “mavazi ya thamani”—haki ya Kristo ilihesabiwa kwao. Kile kilemba kilichowekwa juu ya kichwa cha Yoshua kilikuwa kama kile kilichokuwa kikivaliwa na makuhani na kiliandikwa maandishi, “Mtakatifu kwa Bwana,” ikimaanisha kwamba, licha ya makosa yake ya awali, sasa alikuwa amestahili kuhudumu mbele za Mungu katika Patakatifu Pake. [TA 148.3; UM Aya ya 30]

Baada ya kumkabidhi hadhi ya ukuhani Malaika alitangaza hivi: “Bwana wa majeshi asema hivi; kama ukienda katika njia Zangu, na kuyashika maagizo Yangu, ndipo utakapoihukumu nyumba Yangu, na kuzilinda nyua Zangu, Nami nitakupa nafasi ya kunikaribia kati yao wasimamao karibu.” Angeheshimiwa kama mwamuzi au mtawala juu ya hekalu na huduma zake zote; angetembea kati ya malaika wanaohudumu, hata katika maisha haya, na hatimaye kujiunga na umati wenye utukufu unaozunguka kiti cha enzi cha Mungu.—Testimonies for Church 5:467-469. [TA 149.1; UM Aya ya 31]

Neno hili la uhakikisho limetolewa kwa wote walio na imani katika Mungu. Pokea ahadi hii ya ajabu. Sio mwanadamu anayesema. “Bwana wa majeshi asema hivi; kama ukienda katika njia Zangu, na kuyashika maagizo Yangu, ndipo utakapoihukumu nyumba Yangu, na kuzilinda nyua Zangu, Nami nitakupa nafasi ya kunikaribia kati yao wasimamao karibu.” [TA 149.2; UM Aya ya 32]

"Kati yao wasimamao karibu." Majeshi ya adui, ambayo hujaribu kuwatia watu wa Mungu katika mabaya, na majeshi ya mbinguni, malaika elfu kumi mara elfu kumi, wanaowalinda na kuwahifadhi watu wa Mungu wanaojaribiwa, wakiwainua na kuwatia nguvu, hawa ndio wasimamao karibu. Na Mungu anawaambia Waumini Wake: mtatembea kati yao. Hamtatekewaa na nguvu za giza. Nanyi mtasimama mbele Yangu, mbele ya malaika watakatifu, ambao wametumwa kuwahudumia wale watakaorithi wokovu.— The Review and Herald, Aprili 30, 1901. [TA 149.3; UM Aya ya 33]

### Maono ya Taa Saba na Mizeituni Miwili

Mara baada ya maono ya Zekaria ya Yoshua na malaika, yaliyotolewa kwa kuhani mkuu kama ushuhuda binafsi kwa ajili ya kutiwa moyo kwake mwenyewe na faraja ya watu wote wa Mungu, nabii alipokea ushuhuda wa binafsi kuhusu kazi ya Zerubabeli. “Na yule malaika aliyesema nami,” Zekaria

anasema, “akanijia mara ya pili; akaniamsha, kama mtu aamshwapo katika usingizi wake, akaniluza, unaona nini? Nikasema, Nimetazama, na tazama, kinara cha taa cha dhahabu tupu, nacho kina bakuli juu yake, na taa zake saba juu yake; na tena iko mirija saba ya kuleta mafuta, kwa taa zote zilizo juu yake; na mizeituni miwili karibu yake, mmoja upande wa kuume wa lile bakuli, na mmoja upande wake wa kushoto.”— The Review and Herald, Januari 16, 1908. [TA 150.1; UM Aya ya 34]

“Ndipo nikajibu, nikamwambia, ni nini mizeituni hii miwili iliyo upande wa kuume wa kinara cha taa kile na upande wake wa kushoto? Nami nikajibu mara ya pili, nikamwuliza, ni nini haya matawi matawi ya mizeituni ambayo kwa njia ya ile mifereji miwili ya dhahabu hutoa mafuta yao? Akanijibu na akisema, “Hivi ni hao wana wawili wa mafuta, wasimamao karibu na Bwana wa dunia yote.” [TA 150.2; UM Aya ya 35]

Watiwa-mafuta wanaosimama karibu na Bwana wa dunia yote wana nafasi aliyokuwa amepewa Shetani kama kerubi afunikaye. Kupitia kwa viumbe watakatifu wanaokizunguka kiti Chake cha enzi, Bwana huendeleza mawasiliano ya kudumu na wakazi wa dunia.— The Review and Herald, July 20, 1897. [TA 150.3; UM Aya ya 36]

### Malaika Wakati wa Esta

Uamuzi wa mfalme Ahasuero dhidi ya Wayahudi ulitokana na madai ya uongo kwa njia ya upotoshaji wa watu wa kipekee. Shetani alianzisha njama hiyo ili kuwaondoa duniia wale waliohifadhi ujuzi wa Mungu wa Kweli. Lakini njama zake zilishindwa na nguvu ya kupinga ambayo inatawala kati ya wana wa wanadamu. Malaika walio na nguvu nyingi zaidi walipewa kazi ya kulinda watu wa Mungu, na njama za watesi wao ziliwarejea vichwani mwao wenyewe.—Testimonies for the Church 5:450. [TA 151.1; UM Aya ya 37]

Siku iliyopangwa kwa ajili ya uangamivu wao, “Wayahudi wakakusanyika mijini kwao katika majimbo yote ya mfalme Ahasuero, ili kutia mikono yao kwa wale waliowatakia hasara (kuwadhuru); wala asiweze mtu wa kuwazuia; kwa kuwa hofu yao imewaangukia watu wote.” Malaika walio na nguvu nyingi walikuwa wametumwa na Mungu kuwalinda watu Wake waliokuwa “wakishindania maisha yao.” Esta 9:2, 16 .— Prophets and Kings, 602. [TA 151.2; UM Aya ya 38]

### Baba wa Yohana Mbatizaji

Zakaria aliishi katika “nchi ya vilima vya Yudea,” lakini alikuwa ameenda mpaka Yerusalemu kuhudumu kwa muda wa juma moja katika hekalu, huduma ilihitajika mara mbili kwa mwaka kutoka kwa makuhani wa kila aina. [TA 151.3; UM Aya ya 39]

Alikuwa amesimama mbele ya madhabahu ya dhahabu katika mahali [atakatifu pa hekalu...Ghafla akawa katika uwepo wa Mungu. Malaika wa Bwana alikuwa "amesimama upande wa kuume wa madhabahu ya kufukizia." Nafasi ya malaika ilikuwa dalili ya fadhili, lakini Zakaria hakulijua hili. Kwa miaka mingi alikuwa ameomba kwa ajili ya kuja wa Mkombozi; sasa mbingu zilikuwa zimemtuma mjumbe wake kutangaza kwamba maombi haya yalikuwa karibu kujibiwa; lakini rehema za Mungu zilionekana kuwa kubwa sana kwake kwa kuziamini. Alijawa na hofu na kufadhaika. [TA 151.4; UM Aya ya 40]

Lakini alisalimiwa kwa uhakikisho wa shangwe: "Usiogope, Zakaria; kwa maana dua yako imesikiwa; na mkeo Elisabeti atakuzalia mtoto mwanaume, nawe utamwita jina lake Yohana  Zakaria akamwambia malaika, Nitajuaje Neno hilo, maana mimi ni mzee, na mke wangu ni mkongwe wa siku nyingi." [TA 152.1; UM Aya ya 41]

Kwa swali la Zakaria, malaika akamwambia, "Mimi ni Gabrieli, nisimamaye mbele za Mungu; nami nimetumwa niseme nawe, na kukupasha habari hizi njema." Miaka mia tano nyuma, Gabriel alikuwa amemjulisha Danieli kipindi cha unabii ambacho kingeendelea hadi kuja kwake Kristo. Maarifa yanayosema kwamba mwisho wa kipindi hiki ulikuwa karibu ulimsukuma Zakaria kuomba kwa ajili ya majilio Masihi. Sasa yule mjumbe ambaye kwake unabii ulitolewa naye alikuja kutangaza utimilifu wake. [TA 152.2; UM Aya ya 42]

Maneno ya yule malaika, "Mimi ni Gabrieli, nisimamaye mbele ya uso wa Mungu," yanaonesha kwamba ana cheo cha juu sana katika nyua za mbinguni. Alipokuja na ujumbe kwa Danieli, alisema, "wala hapana anisaidiaje juu ya hao , ila huyo Mikaeli, mkuu wenu." Danieli 10:21. Kuhusu Gabrieli Mwokozi anazungumza katika Ufunuo, akisema kwamba "naye akatuma kwa mkono wa malaika Wake akamwonesha mtumishi Wake Yohana." Ufunuo 1:1. Na kwa Yohana malaika alisema, "Mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii." Ufunuo 22:9. Ni wazo la kupendeza na ajabu, kwamba malaika anayesimama karibu kwa heshima baada ya Mwana wa Mungu ndiye yule anachaguliwa kufunua makusudi ya Mungu kwa wanadamu wenye dhambi.— The Desire of Ages, 97-99. [TA 152.3; UM Aya ya 43]

Kazi ya Yohana Mbatizaji ilitabiriwa na malaika ambaye alimtokea Zakaria hekaluni. "Usiogope, Zakaria" alisema "kwa maana dua yako imesikiwa; na mkeo Elisabeti atakuzalia mtoto mwanaume, nawe utamwita jina lake Yohana. Naye ... atajazwa na Roho mtakatifu, ... na wengi katika wana wa Israeli atawarejeza kwa Bwana Mungu wao. Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya na nguvu zake."— The Review and Herald, Februari 20, 1900. [TA 153.1; UM Aya ya 44]

Malaika Gabrieli alitoa maagizo ya pekee kwa wazazi wa Yohana kuhusu

kuitawala nafsi (kiasi). Somo lilitolewa kuhusu matengenezo ya afya na mmoja wa malaika aliyetukuka kutoka kwenye kiti cha ufalme cha mbinguni.—The Spirit of Prophecy 2:43. [TA 153.2; UM Aya ya 45]

Ndani ya Yohana Mbatizaji, Mungu alimwinua mjumbe kuandaa njia ya Bwana. Huyu alipaswa kutoa kwa ulimwengu ushuhuda usiotikisika, kukemea na kuonya dhambi. Katika kuutangaza utume na kazi ya Yohana, malaika alisema: "Atatangulia mbele Zake (Kristo) katika roho ya Eliya na nguvu zake, ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto; na kuwatilia waasi akili za wenye haki; na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa."— The Review and Herald, August 2, 1898. [TA 153.3; UM Aya ya 46]

## SURA YA 13

## KUFANYIKA MWILI NA MAISHA YA AWALI YA KRISTO

### Kufanyika Mwili ni Fumbo lenye Kina

Katika kutafakari juu ya Kristo kufanyika mwili katika ubinadamu, tunakanganyika mbele ya fumbo lisilofumbulika ambalo akili ya mwanadamu haiwezi kulielewa. Kadiri tunavyolitafakari, ndivyo linavyoonekana kuwa la kushangaza zaidi. Ni utofauti mpana jinsi gani kati ya uungu wa Kristo na

mtoto mchanga asiyejiweza katika hori la Bethlehemu! Je, tunawezaje kupima umbali kati ya Mungu Mweza na mtoto asiyejiweza? Na angali ni Muumba wa ulimwengu, ambaye ndani yake ulikuwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili, alidhihirika katika mtoto mchanga asiyejiweza ndani ya hori. Akiwa tofauti mbali mno kuliko malaika yeyote, akiwa sawa na Baba katika heshima na utukufu, na bado akiwa amevaa vazi la ubinadamu! Uungu na ubinadamu viliunganika kwa njia ya ajabu, na mwanadamu na Mungu wakawa kitu kimoja. Ni katika muungano huu ambapo tunapata tumaini letu jamii iliyoanguka. E. G. White, The Signs of the Times, Julai 30, 1896. [TA 154.1; UM Aya ya 1]

**Malimwengu Yote Yalitazama Tukio Hili.**

Kuja kwa Kristo katika ulimwengu wetu lilikuwa tukio kuu, si kwa ulimwengu huu tu, bali kwa malimwengu yote ya milki ya Mungu. Mbele ya wakuu wa mbinguni alipaswa kujivika asili yetu, ili ajaribiwe katika mambo yote kama sisi. E. G. White, The Signs of the Times, Februari 20, 1893. [TA 154.2; UM Aya ya 2]

Kwa kule kuja kuishi kati yetu, Yesu alikuwa amfunue Mungu kwa wanadamu na kwa malaika....Lakini ufunuo huu haukutolewa kwa ajili ya watoto wake waliozaliwa katika dunia hii tu. Ulimwengu wetu mdogo ni kitabu cha malimwengu mengine kujifunzia. Kusudi la Mungu la kushangaza la neema, siri ya pendo lenye kukomboa, ni mada ambayo kwayo “malaika hutamani kuichungulia,” na itakuwa mada ya wao kujifunza katika vizazi visivyokoma. E. G. White, The Desire of Ages, 19, 20. [TA 155.1; UM Aya ya 3]

**Kwa Nini Kristo Alichukua Asili ya Mwanadamu**

[Shetani] alikuwa amejigamba kwa malaika wa mbinguni kwamba endapo Kristo angetokea, akichukua asili ya mwanadamu, Angekuwa dhaifu kuliko yeye mwenyewe [Shetani], na angemshinda kwa uwezo wake [Shetani]. Alishangilia kwamba Adamu na Hawa pale Edeni hawakuweza kupinga hila yake alipoweka mvuto wa tamaa yao. E. G. White, The Review and Herald, Julai 28, 1874. [TA 155.2; UM Aya ya 4]

Mwana pekee wa Mungu alikuja katika ulimwengu wetu kama mwanadamu, ili kuufunulia ulimwengu kwamba wanadamu wanaweza kuitunza sheria ya Mungu. Shetani, yule malaika aliyeanguka, alikuwa ametangaza kwamba hakuna mwanadamu ambaye angeweza kuitunza sheria ya Mungu baada ya anguko la Adamu. E. G. White, Manuscript Releases 6:334. [TA 155.3; UM Aya ya 5]

Shetani alidai kwamba haiwezekani kwa wanadamu kuishika sheria ya Mungu. Ili kuthibitisha uongo wa dai hili, Kristo aliacha amri Yake kuu, akajitwika asili ya mwanadamu, na akaja duniani kusimama juu ya jamii

iliyoanguka, ili kuonyesha kwamba ubinadamu ungeweza kustahimili vishawishi vya Shetani. E. G. White, The Upward Look, 172. [TA 155.4; UM Aya ya 6]

### Asili ya Kibinadamu ya Kristo

Asili yake [Kristo] ya kibinadamu iliumbwa; hata haikuwa na uwezo wa kimalaika. Ilikuwa ya kibinadamu, ifananayo na yetu. E. G. White, Selected Messages 3:129. [TA 156.1; UM Aya ya 7]

Kristo katika udhaifu wa ubinadamu ilikuwa akabiliane na majaribu ya yeye ambaye ana uwezo wa hali ya juu zaidi ambayo Mungu alikuwa ameiweka kwa familia ya malaika. E. G. White, The Review and Herald, Januari 28, 1909. [TA 156.2; UM Aya ya 8]

Kisa cha Bethlehemu ni mada isiyoweza kuelezwa ikaisha yote. Ndani yake kumefichwa "utajiri wa hekima na maarifa ya Mungu!" Warumi 11:33. Tunashangazwa na kafara ya Mwokozi ya kufanya mbadilishano kwa kuchukua hori la ng'ombe badala ya kiti cha enzi cha mbinguni, na badala ya wingi wa malaika wamzungukao akawa na wanyama katika zizi. Kiburi cha mwanadamu na kutaka kujitosheleza vinakemewa na uwepo wa Mwokozi. Lakini huu ulikuwa ni mwanzo tu wa Yeye kujidhili. Ingekuwa ni hatua ya kujishusha kwa hali ya juu sana kwa Mwana wa Mungu kuchukua ubinadamu, hata pale Adamu alipokuwa katika hali ya kutokuwa na hatia pale Edeni. Lakini Yesu alikubali ubinadamu pale jamii ya wanadamu ilipokuwa imedhoofishwa kwa miaka elfu nne ya kuwepo kwa dhambi. Kama ilivyo kwa kila mtoto wa Adamu Yeye pia alikubali matokeo ya utendaji wa sheria kuu ya kurithisha nasaba. Matokeo haya yalivyokuwa ni kama inavyoonekana katika historia ya wazazi wake wa kidunia. Alikuja akiwa na nasaba hizo ili ashiriki huzuni na majaribu, na kutupatia kielelezo cha maisha yasiyo ya dhambi. E. G. White, The Desire of Ages, 48, 49. [TA 156.3; UM Aya ya 9]

Kama Mungu, Kristo hangeweza kwa vyo vyote vile kujaribiwa kutoka kwenye uaminifu wake mbinguni. Lakini Kristo alivyojinyenyekeza kwa asili ya mwanadamu, angeweza kujaribiwa. Hakuwa hata amejivika asili ya malaika, bali ubinadamu, sawa kabisa na asili yetu wenyewe, isipokuwa tu hakuwa na doa la dhambi. Mwili wa mwanadamu, akili ya mwanadamu, yenye sifa zote za kipekee, Alikuwa mfupa, ubongo, na misuli. Mtu wa mwili wa nyama kama wetu, alizingirwa na udhaifu wa ubinadamu. Hali ya mambo katika maisha Yake ilikuwa ya jinsi ile alivyoanikwa na masumbufu yote yanayowakumba wanadamu, si katika utajiri wa mali, si katika urahisi wa maisha, bali katika umaskini na uhitaji na unyonge. Alipumua hewa ile ile anayopumua mwanadamu. Aliikanyaga dunia yetu kama mwanadamu. Alikuwa na utambuzi, dhamiri, kumbukumbu, radhi, na shauku vya nafsi ya kibinadamu ambavyo viliunganishwa na asili Yake ya kiungu. E. G. White, Manuscript Releases

16:181, 182. [TA 157.1; UM Aya ya 10]

Ndani ya Mtoto wa Bethlehemu kulikuwa kumefichwa utukufu ambao mbele ya huo malaika husujudu. Mtoto huyu mchanga asiyejitambua alikuwa mzao aliyeahidiwa, ambaye madhabahu ya kwanza kwenye lango la Edeni ilielekeza kwake. E. G. White, The Desire of Ages, 52. [TA 157.2; UM Aya ya 11]

### Gabrieli Ampasha Habari Bikira Mariamu

Kabla ya kuzaliwa kwake [Kristo], malaika alikuwa amemwambia Mariamu, “Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele." Luka 1:32,33. Maneno haya Mariamu alikuwa ameyatafakari moyoni mwake; lakini ingawa aliamini kwamba mtoto wake angekuwa Masihi wa Israeli, hakuelewa utume Wake. E. G. White, The Desire of Ages, 81, 82. [TA 157.3; UM Aya ya 12]

Malaika wanawatazama wasafiri waliochoka, Yusufu na Mariamu, wakielekea mji wa Daudi, ili kuhesabiwa, kulingana na agizo la Kaisari Augusto. Katika amri ya Mungu, Yusufu na Mariamu walikuwa wameletwa hapa; kwa maana hapa ndipo unabii ulikuwa umetabiri kwamba Kristo atazaliwa. Wanatafuta mahali pa kupumzika katika nyumba ya wageni, lakini wanarudishwa kwa kuwa hakuna nafasi. Matajiri na wenye kuheshimika wamekaribishwa, na kupata kiburudisho na nafasi, huku wasafiri hawa waliochoka wakilazimika kutafuta mahali katika jengo duni ambalo huhifadhi wanyama. E. G. White, The Review and Herald, Desemba 17, 1872. [TA 158.1; UM Aya ya 13]

### Kabla ya Kuzaliwa kwa Kristo

Mbinguni ilieleweka kwamba wakati ulikuwa umefika wa kuja kwa Kristo ulimwenguni, na malaika wanaacha utukufu ili kushuhudia kupokelewa kwake na wale aliokuja kuwabariki na kuwaokoa. Walikuwa wameshuhudia utukufu wake mbinguni, na wanatazamia kwamba atapokelewa kwa heshima kulingana na tabia yake na adhama ya utume Wake. Malaika wanapoikaribia dunia, wanakuja kwanza kwa watu ambao Mungu alikuwa amewatenga na mataifa ya ulimwengu kama hazina Yake ya pekee. Hawaoni mvuto wa kipekee miongoni mwa Wayahudi, hawangojei na kutazama kwa hamu ili wapate kuwa wa kwanza kumpokea Mkombozi, na kukiri kuja Kwake.E. G. White, The Review and Herald, Desemba 17, 1872. [TA 158.2; UM Aya ya 14]

Malaika anazuru dunia ili kuona ni akina nani walio tayari kumkaribisha Yesu. Lakini haoni dalili zozote za matarajio. Hasikii sauti ya kusifu na ya ushindi kwamba kipindi cha kuja kwa Masihi kimewadia. Malaika anazunguka zunguka

kwa muda juu ya jiji lililochaguliwa na hekalu ambapo uwepo wa kiungu umedhihirishwa kwa kipindi kirefu; lakini hata hapa ni kutojali kulekule. [TA 158.3; UM Aya ya 15]

Kwa mshangao mjumbe wa kimbingu yu karibu kurudi mbinguni akiwa na habari za kufedhehesha, anapogundua kundi la wachungaji wanaochunga mifugo yao usiku, na, wanavyotazama anga lenye nyota, wanatafakari juu ya unabii wa Masihi ajaye duniani, na wakitamani ujio wa Mkombozi wa ulimwengu. Hapa kuna kundi lililotayarishwa kumpokea mjumbe wa mbinguni. Na mara malaika wa Bwana anatokea, akitangaza habari njema ya furaha kuu. E. G. White, The Great Controversy, 314. [TA 159.1; UM Aya ya 16]

Malaika walipita karibu na shule ya manabii, majumba ya wafalme, na kuwatokea wachungaji wanyenyekevu, wakilinda mifugo yao usiku, kwenye tambarare za Bethlehemu. Malaika mmoja alionekana mara ya kwanza, amevikwa mavazi ya mbinguni; na wachungaji walishangaa na kuogopa sana kiasi kwamba wangeweza tu kutazama utukufu wa ajabu wa yule mgeni wa mbinguni kwa mshangao usioneneka. Malaika wa Bwana akaja kwao, akasema, “Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. Na hii ndiyo ishara kwenu; mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe” (Luka 2:10-12). [TA 159.2; UM Aya ya 17]

Mara tu macho yao yalipozoea uwepo wa utukufu wa malaika mmoja, basi, tazama! tambarare nzima iliangazwa na utukufu wa ajabu wa umati wa malaika waliojaa katika tambarare za Bethlehemu. Malaika alituliza hofu za wachungaji kabla ya kufungua macho yao kutazama umati wa jeshi la mbinguni, lote likimsifu Mungu, na kusema, “Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia” (Luka 2:14). E. G. White, The Review and Herald, Desemba 9, 1884. [TA 159.3; UM Aya ya 18]

Wachungaji wanajawa na furaha, na, vile utukufu angavu unapotoweka, na malaika kurudi mbinguni, wote wanawakwa na habari njema, na wanaharakisha kumtafuta Mwokozi. Wanampata Mkombozi mchanga, kwa jinsi ile wajumbe wa kimbingu walivyoshuhudia, akiwa amevikwa nguo za kitoto, na amelala katika sehemu ndogo ya hori iliyowekewa mipaka. E. G. White, The Review and Herald, Desemba 17, 1872. [TA 160.1; UM Aya ya 19]

Shetani aliona nyanda za Bethlehemu zikiangazwa na utukufu mwingi wa umati wa malaika wa mbinguni. Alisikia wimbo wao, “Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.” Mkuu wa giza aliwaona wachungaji waliostaajabu wakijawa na hofu walipozitazama tambarare zilizoangazwa. Walitetemeka mbele ya mwonekano wa utukufu wa kukanganyisha ambao ulionekana kuziingia fahamu zao. Mwasi mkuu

mwenyewe alitetemeka kwa tangazo la malaika kwa wachungaji, “Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana.” [TA 160.2; UM Aya ya 20]

Wimbo wa wajumbe wa mbinguni wakitangaza ujio wa Mwokozi kwa ulimwengu ulioanguka, na furaha iliyoonyeshwa katika tukio hili kuu, Shetani alijua haikuwa na faida kwake. Matazamio maovu yaliamshwa katika akili yake juu ya mvuto huu wa ujio wa Yesu kwa ulimwengu vile matokeo yangekuwa katika ufalme wake [Shetani]. E. G. White, The Review and Herald, Machi 3, 1874. [TA 160.3; UM Aya ya 21]

**Mamajusi**

Haikuwa pale juu ya vilima tu vya Yudea, haikuwa tu pale penye wachungaji duni, ambapo malaika walipata watazamaji wa kuja kwa Masihi. Katika nchi ya mataifa walikuwako wale waliomtazamia; walikuwa watu wenye hekima, matajiri na wakuu, wanafalsafa wa Mashariki. Wanafunzi wa asili, Mamajusi walikuwa wamemwona Mungu katika kazi ya mikono yake. Toka katika Maandiko ya Kiebrania walikuwa wamejifunza juu ya ile Nyota kutokea katika Yakobo, na kwa hamu kubwa wakangojea kuja Kwake, ambaye hakupaswa kuwa tu “Faraja ya Israeli,” bali “Nuru ya kuwaangazia Mataifa,” na “kwa wokovu hata miisho ya dunia.” Luka 2:25, 32; Matendo 13:47. E. G. White, The Great Controversy, 315. [TA 161.1; UM Aya ya 22]

Wale mamajusi ... walikuwa wamesoma unabii, na walijua wakati ulikuwa umekaribia ambapo Kristo angekuja, na walikuwa wakingojea kwa hamu ishara fulani ya tukio hili kuu, ili wapate kuwa miongoni mwa watu wa kwanza kumkaribisha yule Mfalme mchanga wa mbinguni, na kumwabudu. Wenye hekima hao walikuwa wameona mbingu zikiangazwa na nuru, ambayo iliwafunika wajumbe wa mbinguni waliotangaza ujio wa Kristo kwa wachungaji wa Israeli, na baada ya yule malaika mjumbe kurudi mbinguni, nyota yenye kung’aa ilionekana, na kungoja angani. Mwonekano usio wa kawaida wa ile nyota kubwa, yenye kung’aa ambayo hawakuwa wamewahi kuiona hapo awali, ikining’inia kama ishara katika mbingu, ulivuta usikivu wao, na Roho wa Mungu akawasukuma kumtafuta Mgeni huyo wa mbinguni kwenye ulimwengu ulioanguka. E. G. White, Redemption or the First Advent of Christ With His Life and Ministry, 16. [TA 161.2; UM Aya ya 23]

Pindi nuru [ya malaika kule Bethlehemu] ilipotoweka, nyota yenye kung’aa ilitokea, na ikaendelea kuwepo angani. Haikuwa nyota iliyosimama wala haikuwa sayari, hali ile iliibua udadisi wa mtu aliye makini. Nyota ile ilikuwa ni kundi la malaika waliokuwa mbali, lakini wale wenye hekima walikuwa hawajui nyota ya namna hii. Hata hivyo walishawishika kuamini kwamba nyota ile

ilikuwa na umuhimu kwao. Waliwauliza makuhani na wanafalsafa, na walitafuta katika maandishi yaliyo katika magombo ya kale. Unabii wa Balaamu ulikuwa umesema, "Nyota itatokea katika Yakobo Na fimbo ya enzi itainuka katika Israeli." Hesabu 24:17. Je, hii nyota ngeni haiwezi kuwa imetumwa kama kiashiria cha Yeye Aliyeahidiwa? Mamajusi walikuwa wamekaribisha nuru ya ukweli uliotumwa na mbingu; sasa ilimwagwa juu yao kwa miale inayoangaza zaidi. Katika ndoto waliagizwa kwenda kutafuta habari za Mfalme aliyezaliwa. E. G. White, The Desire of Ages, 60. [TA 162.1; UM Aya ya 24]

Malaika wa Mungu, katika mwonekano wa nyota, waliwaongoza mamajusi katika misheni yao ya kumtafuta Yesu. Walikuja na zawadi na matoleo ya thamani ya uvumba na manemane, ili kutoa matoleo yao kwa Mfalme mchanga aliyetabiriwa katika unabii. Waliwafuata wale wajumbe wanaong’aa wakiwa na uhakika na shangwe kuu. E. G. White, The Review and Herald, Desemba 9, 1884. [TA 162.2; UM Aya ya 25]

Wale mamajusi waliongoza njia yao ambapo nyota ilionekana kuwaongoza. Walipokuwa wakiukaribia mji wa Yerusalemu, ile nyota ilifunikwa na giza, na haikuwaongoza tena. Walifikiri kwamba Wayahudi katika Yerusalemu hawangeweza kutojua tukio kubwa la kuja kwa Masihi, na walifanya uchunguzi katika ujirani wa Yerusalemu. Walisema wazi kusudi la safari yao. Walikuwa wakimtafuta Yesu, mfalme wa Wayahudi, kwa maana walikuwa wameona nyota yake mashariki, na walikuja kumwabudu. E. G. White, Redemption or the First Advent of Christ With His Life and Ministry 16. [TA 162.3; UM Aya ya 26]

Kuwasili kwa mamajusi kulisikika upesi Yerusalemu kote. Safari yao ngeni ilizua msisimko miongoni mwa watu, ambao ulipenya hadi kwenye jumba la Mfalme Herode. Yule Mwedomi mwenye hila alishtuka kwa kuarifiwa uwezekano wa mpinzani kuinuka. [TA 163.1; UM Aya ya 27]

Herode aliwashuku makuhani kwa kupanga njama na wageni ili kuchochea ghasia kwa umma na kumwondoa kwenye kiti cha utawala. Hata hivyo, alificha madhanio yake, akaazimia kuzuia njama zao kwa werevu wa hali ya juu. Akiwaita wakuu wa makuhani na waandishi, akawauliza kuhusu mafundisho ya vitabu vyao vitakatifu kuhusu mahali pa kuzaliwa kwa Masihi. [TA 163.2; UM Aya ya 28]

Uchunguzi huu toka kwa mnyang'anyi wa madaraka, pamoja na ombi la wageni [mamajusi], ulichoma kiburi cha walimu wa Kiyahudi. Ile kutojali vitabu vya unabii ambako kulionyeshwa na wayahudi hawa kulimkasirisha yule jeuri hasidi. Aliwafikiria kana kwamba wanajaribu kuficha utambuzi wao wa jambo hilo. Kwa mamlaka ambayo hawakuwahi kuthubutu kuipuuza, aliwaamuru wachunguze kwa karibu, na kutangaza mahali pa kuzaliwa kwa Mfalme wao mtarajiwa. “Wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi; maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii. [TA 163.3; UM Aya ya 29]

Makuhani na wazee wa Yerusalemu hawakuwa wajinga kuhusu kuzaliwa kwa Kristo kama walivyojifanya. Taarifa ya ujio wa malaika kwa wachungaji ilikuwa imeletwa Yerusalemu, lakini marabi waliiona kuwa isiyostahili kutambuliwa. Wao wenyewe wanaweza kuwa wamempata Yesu, na wanaweza kuwa tayari kuwaongoza mamajusi hadi mahali alipozaliwa; lakini badala ya hili, mamajusi walikuja kuamsha usikivu wao [wayahudi] katika kuzaliwa kwa Masihi. "Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" walisema; "Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumwabudu." [TA 163.4; UM Aya ya 30]

Sasa kiburi na wivu vilifunga mlango wa nuru. Laiti kama ripoti zilizoletwa na wachungaji na mamajusi zingetambuliwa, zingewaweka makuhani na marabi katika nafasi isiyowastahili kabisa, zikikanusha madai yao ya kuwa watetezi wa kweli ya Mungu. Walimu hawa wasomi wasingejishusha kufundishwa na wale waliowaita wapagani. Walisema, haingewezekana kwamba Mungu alikuwa amewapita ili kuwasiliana na wachungaji wasiojua au mataifa wasiotahiriwa. Waliazimia kuonyesha dharau yao kwa habari zilizokuwa zenye kumsisimua Mfalme Herode na Yerusalemu yote. Hawakutaka hata kwenda Bethlehemu kuona kama mambo hayo ndivyo yalivyo. [TA 164.1; UM Aya ya 31]

Wale mamajusi waliondoka Yerusalemu peke yao. Vivuli vya usiku vilikuwa vikianguka walipokuwa wakitoka nje ya malango, lakini kwa furaha yao kubwa waliiona tena ile nyota, na kuelekezwa Bethlehemu. Hawakuwa wamepokea habari kama hiyo ya hali duni ya Yesu kama ilivyotolewa kwa wachungaji... Huko Bethlehemu hawakuona walinzi wa kifalme waliowekwa kumlinda Mfalme aliyezaliwa. Hakuna hata mmoja wa watu walioheshimiwa duniani aliyehudhuria. Yesu alikuwa amelazwa kwenye hori. Wazazi wake, wakulima wasio na elimu, walikuwa ndio walezi Wake pekee. E. G. White,, [TA 164.2; UM Aya ya 32]

"Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia." Waligundua kwamba ule mwonekano wa nje na wa hali ya chini wa Yesu ulikuwa umefunika ndani yake uwepo wa Uungu. E. G. White, The Desire of Ages, 63. [TA 164.3; UM Aya ya 33]

Baada ya misheni ya mamajusi kukamilishwa, walikuwa wakikusudia kurudi, na kupeleka habari za furaha kwa Herode juu ya mafanikio ya safari yao. Lakini Mungu alituma malaika wake wakati wa usiku ili kugeuza njia ya wenye hekima. Katika maono ya usiku waliambiwa waziwazi wasirudi kwa Herode. Waliwatii wajumbe wa mbinguni, na kurudi nyumbani kwao kwa njia nyingine. E. G. White, Redemption or the First Advent of Christ With His Life and Ministry 19. [TA 165.1; UM Aya ya 34]

Kwa namna iyo hiyo Yusufu alipokea onyo la kukimbilia Misri pamoja na Mariamu na mtoto. Malaika akasema, "Ukae huko hata nikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amwangamize." Yusufu alitii bila kukawia, akafunga safari usiku kwa usalama zaidi. [TA 165.2; UM Aya ya 35]

Kule Yerusalemu Herode alingoja bila subira kurudi kwa wenye hekima. Na muda ulipopita, nao hawakuonekana, shuku zake zikachochewa....Askari wakatumwa mara moja kwenda Bethlehemu, wakiwa na amri ya kuwaua watoto wote wa chini ya miaka miwili. E. G. White, The Desire of Ages, 64-66. [TA 165.3; UM Aya ya 36]

Lakini mamlaka kuu ilikuwa ikifanya kazi dhidi ya mipango ya mkuu wa giza. Malaika wa Mungu walivuruga mipango yake, na kulinda uhai wa Mkombozi mchanga. E. G. White, The Signs of the Times, Agosti 4, 1887. [TA 165.4; UM Aya ya 37]

Yusufu, ambaye bado alikuwa Misri, sasa aliamriwa na malaika wa Mungu kurudi katika nchi ya Israeli; ... lakini akiwa anatambua kwamba Arkelao alikuwa akitawala katika Uyahudi mahali pa baba yake, aliogopa kwamba njama za baba dhidi ya Kristo zingeweza kutekelezwa na mwana. [TA 165.5; UM Aya ya 37]

Tena Yusufu alielekezwa mahali pa usalama. Alirudi Nazareti, makao yake ya awali, na hapa kwa karibu miaka thelathini Yesu aliishi.... Mungu ... aliwaagiza malaika kumhudumia Yesu na kumlinda mpaka atakapokamilisha utume wake duniani, na kufa kwa mikono ya wale ambao Alikuja kuwaokoa. E. G. White, The Desire of Ages, 66, 67. [TA 166.1; UM Aya ya 38]

### Miaka ya Ukimya

Tangu miaka Yake ya awali, [Kristo] aliishi maisha ya taabu. Sehemu kubwa ya maisha Yake duniani ilitumika katika kazi ya subira katika karakana ya seremala huko Nazareti. Akiwa amevalia mavazi ya mfanyakazi wa kawaida Bwana wa uzima alikanyaga barabara za mji mdogo alimoishi, akienda na kurudi toka katika taabu yake ya unyonge; na malaika wahudumu walimhudumia Alipotembea pamoja na wakulima na wafanyakazi, akiwa hatambuliwi wala kuheshimiwa. E. G. White, The Review and Herald, Oktoba 3, 1912. [TA 166.2; UM Aya ya 39]

Katika kipindi chote cha utoto na ujana Wake [Kristo], Alidhihirisha ukamilifu wa tabia ambayo iliashiria maisha Yake baada ya maisha ya duniani. Alikua katika hekima na maarifa. Alipokuwa akishuhudia matoleo ya dhabihu, Roho Mtakatifu alimfundisha kwamba maisha yake yangetolewa kwa ajili ya maisha ya ulimwengu. Alikua kama mmea mwororo, sio katika jiji kubwa na lenye kelele, ambalo limejaa machafuko na ugomvi, lakini katika mabonde yaliyotulia kati ya vilima. Alilindwa kutoka miaka Yake ya kwanza kabisa na malaika wa

mbinguni, lakini maisha Yake yalikuwa mapambano ya muda mrefu dhidi ya nguvu za giza. Mawakala wa kishetani waliungana na wale wa kibinadamu kufanya maisha Yake kuwa ya vishawishi na majaribu. Kwa njia ya mawakala wasio wa kawaida, maneno Yake, ambayo yalikuwa uzima na wokovu kwa wote wanaoyapokea na kuyatenda, yalipotoshwa na kufasiriwa vibaya. E. G. White, The Signs of the Times, Agosti 6, 1896. [TA 166.3; UM Aya ya 40]

Yesu alizifanya njia duni za maisha ya mwanadamu kuwa takatifu kwa kielelezo Chake. Kwa miaka thelathini alikuwa mkazi wa Nazareti. Maisha yake yalikuwa ya kujishughulisha kwa bidii. Yeye, Mkuu wa enzi ya mbinguni, alitembea mitaani, akiwa amevaa vazi rahisi la mfanyakazi wa kawaida. Alijitaabisha juu na chini ya miinuko ya mlima, akienda na kutoka katika kazi Yake ya chini. Malaika hawakutumwa kumchukua juu ya mbawa zao ili kumpandisha kwenye miinuko yenye kuchosha, au kutoa nguvu zao katika kufanya kazi yake duni. Hata hivyo, Alipotoka kwenda kuchangia katika kuitegemeza familia kwa kazi Yake ya kila siku, Alikuwa na uweza uleule kama vile alipofanya muujiza wa kulisha watu elfu tano wenye njaa kwenye ufukwe wa Galilaya. E. G. White, The Health Reformer, Oktoba 1, 1876. [TA 167.1; UM Aya ya 41]

## SURA YA 14

## MALAIKA KWENYE UBATIZO WA KRISTO NA JANGWANI

### Kubatizwa Kwa Kristo

Pale Yesu alipokuja kubatizwa, Yohana aliona ndani yake usafi wa tabia ambao hajapata kuona kamwe ndani ya mtu yeyote...Yesu alipoomba kubatizwa, Yohana alisita, akahamaki, "Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?" Kwa mamlaka imara lakini kwa upole, Yesu alijibu, "Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote." Na Yohana, akikubaliana, alimpeleka Yesu ndani ya Yordani, na kumtosa ndani ya maji. "Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake. E. G. White, The Desire of Ages, 110, 111. [TA 168.1; UM Aya ya 1]

Malaika wa mbinguni walikuwa wakitazama kwa hamu kuu tukio la ubatizo wa Mwokozi, na laiti kama macho ya wale waliokuwa wakitazama yangefumbuliwa, wangaliona jeshi la mbinguni likimzunguka Mwana wa Mungu alipokuwa akiinama kwenye kingo za Yordani. E. G. White, The Youth's Instructor, June 23, 1892. [TA 168.2; UM Aya ya 2]

Jicho la Mwokozi linaonekana kupenya mbinguni anapoimimina nafsi yake katika maombi. Anajua vyema jinsi dhambi ilivyofanya mioyo ya watu kuwa

migumu, na jinsi itakavyokuwa vigumu kwao kutambua utume Wake, na kukubali kipawa cha wokovu. Anamwomba Baba kwa ajili ya uwezo wa kushinda kutokuamini kwao, kuvunja minyororo ambayo Shetani amewatia moyoni, na kwa niaba yao kumshinda yule mharibifu. Anaomba ushahidi wa Mungu kumkubali mwanadamu katika nafsi ya Mwanawe. [TA 169.1; UM Aya ya 3]

Malaika hawajapata kamwe kusikia sala kama hiyo. Wana shauku ya kupeleka kwa Kamanda wao mpendwa ujumbe wa hakikisho na faraja. Lakini hapana; Baba mwenyewe atajibu ombi la Mwanawe. Moja kwa moja toka kwenye kiti cha enzi inaachiwa miale ya utukufu Wake. Mbingu zinafunguka, na juu ya kichwa cha Mwokozi nuru angavu yenye umbo mithili ya hua—ishara inayomfaa Yeye, aliye mpole na mnyenyekevu. [TA 169.2; UM Aya ya 4]

Watu walisimama kimya wakitazama kwa Kristo. Umbo lake lilifunikwa katika nuru ambayo daima hukizunguka kiti cha enzi cha Mungu. Uso wake ulioinuliwa ulitukuzwa kiasi ambacho hawakuwahi kuona uso wa mwanadamu vile. Kutoka katika mbingu zilizofunguka ilisikika sauti ikisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.” E. G. White, The Desire of Ages, p. 111, 112. [TA 169.3; UM Aya ya 5]

Bwana alikuwa ameahidi kumpa Yohana ishara ambayo kwayo angeweza kujua ni nani aliyekuwa Masihi, na sasa Yesu alipopanda toka majini, ishara iliyoahidiwa ilitolewa; kwa maana aliona mbingu zimefunguka, na Roho wa Mungu, kama hua aliyeng’arishwa kwa dhahabu, alitua juu ya kichwa cha Kristo, na sauti ikatoka mbinguni, ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.” E. G. White, The Youth's Instructor, Juni 23, 1892. [TA 169.4; UM Aya ya 6]

Kati ya umati mkubwa pale Yordani, ni wachache tu pamoja na Yohana waliotambua maono ya mbinguni. E. G. White, The Desire of Ages, 112. [TA 170.1; UM Aya ya 7]

Wakati wa ubatizo wa Mwokozi, Shetani alikuwa miongoni mwa walioshuhudia. Aliuona utukufu wa Baba ukimfunika Mwanawe. Alisikia sauti ya Yehova ikishuhudia uungu wa Yesu. Tangu dhambi ya Adamu, jamii ya wanadamu ilikuwa imetengwa mbali na ushirika wa moja kwa moja na Mungu; mahusiano kati ya mbingu na dunia yalikuwa yamefanyika kupitia Kristo; lakini sasa Baba mwenyewe alisema kwamba Yesu alikuwa amekuja “katika mfano wa mwili ulio wa dhambi” (Warumi 8:3). Hapo awali alikuwa amewasiliana na wanadamu kwa njia ya Kristo; sasa Aliwasiliana na wanadamu katika Kristo. Shetani alitumaini kwamba kuchukia kwa Mungu uovu kungeleta utengano wa milele kati ya mbingu na dunia. Lakini sasa ilionekana wazi kwamba uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu ulikuwa umerejeshwa. E. G. White, The Desire of Ages, 116. [TA 170.2; UM Aya ya 8]

Shetani angeweza kuona kupitia ubinadamu Wake [Kristo] utukufu na usafi wa Yule ambaye alikuwa ameshirikiana naye katika nyua za mbinguni. Mbele ya mjaribu kuliinuka taswira ya kile ambacho yeye mwenyewe alikuwa katika wakati huo, kerubi afunikaye, mwenye uzuri na utakatifu. E. G. White, The Bible Echo, Julai 23, 1900. [TA 170.3; UM Aya ya 9]

**Kujaribiwa kwa Kristo Mara tatu Jangwani**

Shetani alikuwa ametangaza kwa malaika wenzake kwamba angemshinda Kristo kwa tamaa ya chakula. Alitumaini kupata ushindi juu Yake katika udhaifu Wake. E. G. White, The Signs of the Times, Aprili 4, 1900. [TA 170.4; UM Aya ya 10]

Shetani aliona kwamba ni sharti ama ashinde au ashindwe. Masuala ya pambano yalikuwa mazito mno kiasi kwamba ilikuwa vigumu kuwaachia malaika wake [Shetani]. Ni lazima yeye binafsi apigane vita. E. G. White, The Desire of Ages, 116. [TA 171.1; UM Aya ya 11]

Akiwa nyikani, Kristo alifunga, lakini hakuwa na hisia za njaa.... Alitumia muda huo katika maombi ya bidii, akiwa amejifungia ndani na Mungu. Ilikuwa ni kana kwamba alikuwa katika uwepo wa Baba Yake.... Mawazo ya vita vilivyokuwa mbele Yake yalimfanya asahau hata mambo mengine yote, na nafsi yake ililishwa mkate wa uzima.... Aliona kuvunjika kwa mamlaka ya Shetani kwa walioanguka na waliojaribiwa. Alijiona akiwaponya wagonjwa, akiwafariji wasio na tumaini, akiwachangamsha waliokata tamaa, na akiwahubiri maskini injili—akifanya kazi ambayo Mungu alikuwa amemkabidhi; wala hakutambua njaa mpaka pale siku arobaini za saumu yake zilipotimia. [TA 171.2; UM Aya ya 12]

Maono hayo yalipita, na kisha, kwa hitaji kubwa, asili ya kibinadamu ya Kristo ilihitaji chakula. Sasa ilikuwa nafasi ya Shetani kufanya shambulio lake. Aliazimia kuonekana kama mmoja wa malaika wa nuru waliomtokea Kristo katika maono Yake. E. G. White, Manuscript Releases 21:8, 9. [TA 171.3; UM Aya ya 13]

Mara malaika anatokea mbele Yake [Kristo], inaonekana ni mmoja wa malaika ambaye Yeye aliwaona muda si mrefu tangu wakati huo.... Maneno kutoka mbinguni, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye,” bado yalikuwa yakidunda katika masikio ya Shetani. Lakini aliazimia kumfanya Kristo asiamini ushuhuda huo. E. G. White, Manuscript Releases 21:9. [TA 171.4; UM Aya ya 14]

Shetani alimtokea [Kristo] ... kama malaika mzuri toka mbinguni, akidai kwamba alikuwa na agizo toka kwa Mungu ili kutangaza mfungo wa Mwokozi mwishoni. E. G. White, The Review and Herald, Januari 14, 1909. [TA 171.5; UM

Aya ya 15]

[Shetani] alimwambia Mkombozi kwamba Hahitaji kufunga tena, kwamba kujiepusha Kwake kwa muda mrefu kulikubaliwa na Baba, kwamba Alikuwa ameenda mbali vya kutosha, na kwamba Alikuwa huru kufanya muujiza kwa niaba Yake mwenyewe. E. G. White, The Signs of the Times, July 29, 1889. [TA 172.1; UM Aya ya 16]

Kwa kuwa aliamini kwamba malaika ambaye alikuwa amejidhania kuwa hangeweza kutambuliwa, sasa alijifanya kutilia shaka uungu wa Kristo. E. G. White, The Spirit of Prophecy 2:91. [TA 172.2; UM Aya ya 17]

### Jaribu la Kwanza

Shetani alijadiliana na Kristo hivi: Ikiwa maneno yaliyonenwa baada ya ubatizo wake kwa hakika yalikuwa ni maneno ya Mungu, kwamba alikuwa Mwana wa Mungu, hahitaji kupitia hisia za njaa; Angeweza kumpa uthibitisho wa uungu Wake kwa kuonyesha uweza Wake katika kubadili mawe ya nyika hiyo kuwa mkate. E. G. White, Redemption or the First Advent of Christ With His Life and Ministry, 48. [TA 172.3; UM Aya ya 18]

Shetani alimwambia Kristo kwamba [Kristo] alipaswa kuitua tu miguu yake katika njia iliyotiwa doa la damu lakini sio kuipitia, kwamba ni kama vile Ibrahimu alipimwa ili kuonyesha utii wake kikamilifu. Pia alisema kwamba yeye ndiye malaika aliyezuia mkono wa Ibrahimu pale kisu kilipoinuliwa ili kumchinja Isaka, na sasa alikuwa amekuja kuokoa maisha Yake (Kristo); kwamba haikuwa sharti kwake kuvumilia njaa hii yenye uchungu na mauti kutokana na kukosa chakula; na kwamba (shetani) angemsaidia kubeba kazi katika mpango wa wokovu. E. G. White, The Review and Herald, Agosti 4, 1874. [TA 172.4; UM Aya ya 19]

Kisha [Shetani] akavuta usikivu wa Kristo kuuelekea mwonekano wake mwenyewe wa kuvutia, uliovikwa nuru na nguvu katika uwezo. Alidai kuwa mjumbe moja kwa moja toka kwenye kiti cha ufalme cha Mbinguni, na kudai kwamba alikuwa na haki ya kudai kwa Kristo uthibitisho wa kuwa Kwake Mwana wa Mungu. E. G. White, The Review and Herald, Agosti 4, 1874. [TA 173.1; UM Aya ya 20]

Ilikuwa kwa ... maneno [ya Shetani], si kwa sura yake, ambapo Mwokozi alimtambua adui. E. G. White, The Review and Herald, Julai 22, 1909. [TA 173.2; UM Aya ya 21]

Katika kuchukua asili ya mwanadamu, Kristo hakuwa sawa kwa sura na malaika wa mbinguni, lakini asili hii ya ubinadamu ilikuwa mojawapo ya fedheha iliyohitajika ambayo Yeye alikubali kwa hiari alipokuwa Mkombozi wa mwanadamu. Shetani alihimiza kwamba ikiwa kweli alikuwa Mwana wa Mungu

angempa ushahidi fulani wa tabia Yake iliyotukuka. Alidokeza kwamba Mungu hatamwacha Mwanawe katika hali ya kuhuzunisha hivyo. Alitangaza kwamba mmoja wa malaika wa mbinguni alikuwa amehamishiwa duniani, na kuonekana Kwake kulionyesha kwamba badala ya kuwa Mfalme wa Mbinguni, alikuwa malaika aliyeanguka. Alielekeza mvuto kwenye mwonekano wake mwenyewe mzuri, uliovikwa nuru na nguvu, na kwa matukano akalinganisha unyonge wa Kristo na utukufu wake mwenyewe. E. G. White, The Spirit of Prophecy 2:91. [TA 173.3; UM Aya ya 22]

**Jaribu la Pili**

“Kisha mwovu alimchukua Yesu na kumpeleka katika mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, na akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini: maana imeandikwa: "Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.” E. G. White, The Desire of Ages, 124. [TA 173.4; UM Aya ya 23]

Shetani, ili kuonyesha nguvu zake, alimchukua Yesu mpaka Yerusalemu, na kumweka juu ya kinara cha hekalu. E. G. White, Spiritual Gifts 1:32. [TA 174.1; UM Aya ya 24]

[Shetani] alihitaji tena kwa Kristo, kama kweli alikuwa Mwana wa Mungu, ampe ushahidi kwa kujitupa kutoka kwenye kimo kirefu chenye kusulikisha alipokuwa amemweka. Alimsihi Kristo aonyeshe imani yake katika uangalizi wa Baba yake kwa kujitupa chini kutoka hekaluni. Katika jaribu la kwanza la Shetani juu ya hamu ya chakula, alijaribu kuzua mashaka juu ya pendo la Mungu na uangalizi kwa ajili ya Kristo kama Mwana Wake, kwa kuonyesha hali iliyokuwa imemzunguka na njaa Yake kama uthibitisho kwamba hakuwa katika kibali cha Mungu. Katika hili hakufanikiwa. Kisha alijaribu kujipatia faida ya imani na tumaini kamilifu ambalo Kristo alikuwa ameonyesha kwa Baba Yake wa mbinguni ili kumsihi ajifanye. “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini: maana imeandikwa: "Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.” E. G. White, The Review and Herald, August 18, 1874. [TA 174.2; UM Aya ya 25]

Adui mwerevu anawasilisha maneno yaliyotoka katika kinywa cha Mungu. Bado anaonekana kama malaika wa nuru, na anaonyesha wazi kwamba anayafahamu Maandiko, na anaelewa maana ya kile kilichoandikwa. Vile Yesu alivyotumia neno la Mungu hapo awali ili kutegemeza imani Yake, mjaribu sasa analitumia kuonyesha udanganyifu wake. Anadai kwamba alikuwa akijaribu tu uaminifu wa Yesu, na sasa anapongeza uthabiti Wake. Vile Mwokozi alivyodhihirisha imani kwa Mungu, Shetani anamsihi atoe ushahidi mwingine wa imani Yake. [TA 174.3; UM Aya ya 26]

Lakini kwa mara nyingine jaribu hili linatanguliwa na kiashiria cha kutilia

shaka, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu." Kristo alikuwa anajaribiwa kujibu hiyo "ukiwa;" lakini alikwepa hata jambo dogo tu la kukubali mashaka. Asingehatarisha maisha yake kwa kumpa Shetani uthibitisho. E. G. White, The Desire of Ages, 124. [TA 175.1; UM Aya ya 27]

Shetani aliponukuu ahadi, “Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua,” aliondoa maneno, “Wakulinde katika njia zako zote”: yaani, katika njia zote za uchaguzi wa Mungu. Yesu alikataa kwenda nje ya njia ya utii. Huku akidhihirisha tumaini kamili kwa Baba Yake, Asingejiweka Mwenyewe bila kuamriwa katika nafasi ambayo ingelazimu Baba Yake kuingilia kati ili kumwokoa na kifo. Asingelazimisha Ulinzi wa Mungu uje kumwokoa, na hivyo kushindwa kumpa mwanadamu kielelezo cha uaminifu na utii. E. G. White, The Signs of the Times, Desemba 10, 1902. [TA 175.2; UM Aya ya 28]

Laiti kama Yesu angejitupa kutoka kileleni, hangalimtukuza Baba yake; kwani hakuna ambaye angeshuhudia kitendo hicho ila Shetani na Malaika wa Mwenyezi Mungu. Na ingekuwa kumjaribu Bwana kuonyesha uweza wake kwa adui mwenye chuki. Ingekuwa kujishusha mbele ya yule ambaye Yesu alikuja kumshinda. E. G. White, Spiritual Gifts 1:33. [TA 175.3; UM Aya ya 29]

### Jaribu la Tatu

Yesu alikuwa mshindi katika jaribu la pili, na sasa Shetani anajidhihirisha katika tabia yake halisi. Lakini hajioneshi kama jitu la kutisha sana, mwenye miguu iliyogawanyika na mbawa za popo. Yeye ni malaika mwenye nguvu, ingawa ameanguka. Anajinadi kuwa kiongozi wa uasi na mungu wa ulimwengu huu. [TA 175.4; UM Aya ya 30]

Akiwa amemweka Yesu juu ya mlima mrefu, Shetani alizifanya falme za ulimwengu, katika utukufu wazo wote, zipite mbele Yake zikionyesha mandhari yote ya kipekee. E. G. White, The Desire of Ages, 129. [TA 176.1; UM Aya ya 31]

Katika majaribu yake mawili ya kwanza, [Shetani] alikuwaameficha tabia na kusudi lake hasa, akijidai kuwa mjumbe aliyetukuka kutoka katika nyua za mbinguni. Lakini sasa anauvua mwonekano wake wote wa awali, akijidhihirisha kuwa ndiye Mkuu wa Giza, na kudai dunia i chini ya utawala wake. E. G. White, The Spirit of Prophecy 2:95. [TA 176.2; UM Aya ya 32]

Yule mdanganyifu mkuu alitafuta kupofusha macho ya Kristo kwa mng’ao na kumetameta kwa ulimwengu, na kumwonesha mbele Yake falme za ulimwengu huu na utukufu wazo. Yule ambaye alikuwa ameanguka kutoka mbinguni, aliupamba ulimwengu kama vile umenakshiwa kwa dhahabu mithili ya ule ulimwengu wa juu, ili aweze kumshawishi Kristo akubali rushwa, na kuanguka chini na kumwabudu. E. G. White, The Signs of the Times, Machi 28, 1895. [TA 176.3; UM Aya ya 33]

Mwangaza wa jua ulitanda kwenye majiji yenye mahekalu, majumba ya marumaru, mashamba yenye rutuba, na mashamba ya mizabibu yenye matunda. Alama za uovu zilifichwa. Macho ya Yesu, ambayo muda si mrefu yalishuhudia utusitusi na ukiwa, sasa yalitazama mandhari ya uzuri na ukuu usio na kifani. Ndipo sauti ya mjaribu ikasikika: “Nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako." [TA 176.4; UM Aya ya 34]

Sasa mjaribu akaanika mamlaka yote aliyokuwa amenyang’anya. Kristo angejiokoa na hali yake ya kutisha ya siku za mbele kwa kukiri ukuu wa Shetani. Lakini kufanya hivyo, ilikuwa ni kusalimisha ushindi katika pambano kuu. E. G. White, The Desire of Ages, 129. [TA 177.1; UM Aya ya 35]

Akimwita [Shetani] kwa jina lake halisi, Yesu anamkemea yule mdanganyifu. Uungu ulitoa mwako katika ubinadamu unaoteseka, na alidhihirisha kupitia neno Lake mamlaka ya mbinguni. Anamfunulia yule mdanganyifu kwamba, ingawa alikuwa amejivika tena vazi la malaika wa nuru, tabia yake halisi haikufichwa kwa Mwokozi wa ulimwengu. Alimwita Shetani, malaika wa giza, ambaye alikuwa ameacha makazi yake ya awali, na alikuwa amekataa uaminifu kwa Mungu. E. G. White, The Signs of the Times, Machi 28, 1895. [TA 177.2; UM Aya ya 36]

Shetani alitoka eneo hilo akiwa adui aliyeshindwa, akifukuzwa kwa amri kali. Kwa neno la Kristo, “Ondoka, Shetani,” malaika aliyeanguka mwenye nguvu hakuwa na chaguo ila kutii. Malaika walio na nguvu nyingi walikuwako katika uwanja wa vita, wakilinda makusudi ya nafsi iliyojaribiwa, na walikuwa tayari kumpinga adui. E. G. White, The Review and Herald, Aprili 24, 1894. [TA 177.3; UM Aya ya 37]

### Malaika wa Mbinguni Walimtazama Kristo Akijaribiwa

Inaonekana Kristo alikuwa peke yake pamoja naye [Shetani] katika jangwa la majaribu. Hata hivyo, hakuwa peke yake, kwa kuwa malaika walikuwa wamemzunguka kama vile malaika wa Mungu wanavyoagizwa kuwahudumia wale walio chini ya mashambulizi ya kutisha ya adui. E. G. White, Manuscript Releases 16:180. [TA 177.4; UM Aya ya 38]

Mbingu zote zilitazama pambano kati ya Mkuu wa nuru na mkuu wa giza. Malaika walisimama tayari kuingilia kati kwa niaba ya Kristo ikiwa Shetani angevuka mpaka uliowekwa. E. G. White, The Bible Echo, Septemba 3, 1900. [TA 177.5; UM Aya ya 39]

Haya yalikuwa majaribu halisi, siyo maigizo. Kristo "aliteswa alipojaribiwa" (Waebrania 2:18). Malaika wa mbinguni walikuwapo kwenye jambo hilo, na

walihakikisha sheria inainuliwa, ili Shetani asizidi mipaka yake na kuishinda asili ya kibinadamu ya Kristo. E. G. White, Selected Messages 1:94. [TA 178.1; UM Aya ya 40]

Uchovu ulikuwa umemwacha [Kristo] kama mfu. "Na tazama, wakaja malaika wakamtumikia." Mikono yao ilimzunguka. Kifuani mwa malaika mkuu zaidi mbinguni Kichwa chake kilitulia.... Adui alishindwa. E. G. White, The Bible Echo, Septemba 3, 1900. [TA 178.2; UM Aya ya 41]

Baada ya Shetani kumaliza majaribu yake, alimwacha Yesu kwa muda fulani, na malaika walimtayarishia chakula nyikani. E. G. White, Early Writings, 158. [TA 178.3; UM Aya ya 42]

**Baada ya Jaribu la Tatu**

Baada ya Shetani kushindwa kumshinda Kristo nyikani, aliunganisha majeshi yake ili kumpinga katika huduma Yake, na ikiwezekana kuikwamisha kabisa kazi Yake. Yale ambayo hangeweza kutimiza kwa juhudi za moja kwa moja, za yeye kabisa kuhusika, aliazimia kutekeleza kwa mkakati. Mara tu alipojiondoa katika pambano la nyikani, alienda na malaika walio upande wake katika baraza kuimarisha mipango yake kwa kupofusha akili za Wayahudi, ili kwamba wasimtambue Mkombozi wao. Alipanga kufanya kazi kwa kutumia mawakala wake walio wanadamu katika ulimwengu wa kidini, kwa njia ya kuwajaza na wao ule uadui alio nao dhidi ya mkuu wa ile kweli. Alipanga kuwafanya wamkatae Kristo na kufanya maisha Yake kuwa machungu kadiri iwezekanavyo, akitumaini kumkatisha tamaa katika utume Wake. E. G. White, The Desire of Ages, 205, 206. [TA 178.4; UM Aya ya 43]

## SURA YA 15

## MALAIKA WEMA NA WAOVU WAKATI WA HUDUMA YA KRISTO

### Kupagawa na Mapepo katika Siku za Yesu.

Kipindi cha huduma ya Kristo miongoni mwa watu kilikuwa cha kushughulika sana na majeshi ya ufalme wa giza. Kwa zama na zama Shetani na malaika zake waovu walikuwa wametafuta kutawala miili na roho za watu, kuwaletea dhambi na maumivu. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 257. [TA 180.1; UM Aya ya 1]

Udanganyifu wa dhambi ulikuwa umefikia kilele chake (katika kipindi cha Yesu alipoanza huduma Yake). Mbinu zote za kupotosha roho za watu zilikuwa zimewekwa katika utendaji... Mbinu za Shetani ziliwekwa ndani ya watu, miili ya watu, iliyofanywa iwe makao ya Mungu, ilikuwa imekuwa makao ya pepo waovu. Fahamu, utambuzi, huruma, viungo vya wanadamu, vilitumiwa na nguvu ovu zisizo za kawaida katika kuendekeza tamaa zenye kuchukiza. Muhuri wenyewe wa mapepo ulionekana katika nyuso za watu. Sura za wanadamu zilionyesha mwonekano wa pepo waovu waliowapagaa...[180.2; UM Aya ya 2]

Shetani alikuwa anajigamba kwamba amefanikiwa kuharibu sura ya Mungu ndani ya mwanadamu. Ndipo Yesu akaja kurejesha ndani ya mtu sura ya Muumba wake... Alikuja kufukuza mapepo ambayo yanatawala dhamiri. Alikuja kutuinua juu toka mavumbini, kuumba upya tabia iliyopotoshwa ili ifanane na ile ya kimbingu, na kuifanya kuwa njema kwa utukufu wake. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 36-38. [TA 180.3; UM Aya ya 3]

Ukweli kwamba watu wamepagawa na mapepo u wazi katika Agano Jipya. Watu walioteswa hivyo hawakutaabishwa na magonjwa kutokana tu na sababu za kawaida za asili. Kristo alikuwa anaelewa fika juu ya kile alichokuwa anashughulika nacho, na alitambua uwepo na utendakazi dhahiri wa roho wachafu. E. G. White, The Roho ya Unabii, juzuu ya 4, uk. 332 [TA 181.1; UM Aya ya 4]

Shetani na malaika zake walikuwa wakishughulika hasa wakati wa huduma ya Kristo, wakiwavutia watu kutokuamini, wawe na chuki, na dhihaka. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk.1:36. [TA 181.2; UM Aya ya 5]

## Kukataliwa kule Nazareti

Katika siku zake za utoto na ujana, Yesu alikuwa ameabudu miongoni mwa ndugu zake katika sinagogi la Nazareti. Tangu kuanza kwa kazi yake hakuwa pamoja nao, lakini si kwamba hawakujua kilichompata. Alipojitokeza tena miongoni mwao, hamu na matarajio yao yalisisimka hata upeo....[181.3; UM Aya ya 6]

Rabi alipokuwa mahali pa sinagogi, alitarajiwa kuhubiri, na Mwisraeli yeyote angesoma aya kutoka katika manabii. Katika Sabato hii Yesu aliombwa kushika nafasi hiyo katika ibada. "Akasimama ili asome. Akapewa chuo cha nabii Isaya." Luka 4:16, 17...[181.4; UM Aya ya 7]

Yesu alisimama mbele ya watu kama mfafanuzi wa unabii uliomhusu Yeye mwenyewe. Akiwa anaelezea maneno yale aliyokuwa amesoma, alimwongelea Masihi kama mtoa uhuru kwa waliokandamizwa, mwokoaji wa waliofungwa, mponyaji wa wagonjwa, anayewarejeshea vipofu kuona, na anayeufunulia ulimwengu nuru ya ukweli... Kadiri mioyo yao ilivyosukumwa na Roho Mtakatifu, waliitikia kwa hamasa wakisema amen na kumsifu Bwana. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 236, 237. [TA 182.1; UM Aya ya 8]

Roho alishuhudia kwa uweza hivyo kwenye madai Yake Kristo kiasi kwamba mioyo ya wote waliokuwa kwenye sinagogi waliitikia maneno mazuri yaliyotiririka toka kinywani Mwake. Hapa kilikuwa kipindi muhimu mno pamoja na kundi hilo. Vile uungu wa Kristo ulipomulika katika ubinadamu, utambuzi wao wa kiroho ulihuishwa. Uweza mpya wa utambuzi na uthamini uliwaijia, na kusadiki kulikuwa karibu hakuzuiliki kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Lakini shetani alikuwa karibu kuinua mashaka, kutokuamini, na kiburi. E. G. White, Alama za Nyakati, Septemba 14, 1882. [TA 182.2; UM Aya ya 9]

Pale Yesu alipotangaza kwamba, "Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu," ghafla walirudi kujifikiria wao, na madai yake Yeye aliyekuwa anawahutubia. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 237. [TA 182.3; UM Aya ya 10]

Huyu Yesu ni nani? Waliuliza. Yeye aliyedai kuwa utukufu wa Masihi ni wake alikuwa mwana wa seremala, na alikuwa ameshughulika katika sehemu Yake ya kazi ya ufundi pamoja na baba yake Yusufu... Ingawa maisha Yake hayakuwa na mawaa, hawakuamini kwamba alikuwa Yeye Aliyeahidiwa. [TA 182.4; UM Aya ya 11]

Kadiri walivyofungua mlango wa mashaka, mioyo yao ilikuwa migumu sana isiyoweza kulainishwa. Shetani alikuwa ameazimia kwamba macho yaliyo na upofu yasifunguke siku ile, wala roho zilizofungwa utumwani zisiwekwe huru...[TA 183.1; UM Aya ya 12]

Maneno ya Yesu kwa wasikilizaji wake katika sinagogi yalipiga kwenye mzizi wa hali yao ya kujihesabia haki, yakilenga kwao kwenye mioyo yao ukweli mchungu kwamba walikuwa wamemwacha Mungu na kunyang'anywa haki yao ya kuwa watu wake... Sasa wakabeza imani ile ambayo Yesu alikuwa amewavuvia mwanzoni. Hawakuweza kukiri kwamba Yeye aliyekulia katika umaskini na hali ya chini alikuwa zaidi ya mwanadamu wa kawaida. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 237-239. [TA 183.2; UM Aya ya 13]

Malaika wa nuru walikuwapo pale, wakitazama kwa hamu kubwa uamuzi wa wakati. Malaika wa shetani pia walikuwapo hapo kuinua mashaka na chuki...[TA 183.3; UM Aya ya 14]

Kutoka katika kutokuamini kuliinuka kusudio ovu la kudhuru. Kwamba mtu aliyetoka katika ufukara na kuzaliwa kinyonge athubutu kuwakemea, mioyoni mwa Wanazareti kulijaa chuki inayofikia wazimu. Kutaniko likavunjika kwa kukanganyikiwa. Watu walimwinulia mikono, wakimtoa katika sinagogi na kumtupa nje ya mji. E. G. White, Alama za Nyakati, Juni 16, 1887. [TA 183.4; UM Aya ya 15]

Wote walionekana na nia ya kumwangamiza Yeye. Walimharakisha kwenye ukingo wenye mteremko mkali, wakikusudia kumtupa kwa kutanguliza kichwa. Kelele na maapizo vililijaza anga. Wengine walikuwa wakitupa mawe na uchafu Kwake; lakini ghafla alitoweka katikati yao, wasijue ni kwa jinsi gani na wakati gani. Malaika wa Mungu walimhudumia Yesu katikati ya kundi lenye ghasia lililoghadhabika, na kuhifadhi maisha Yake. Wajumbe wa Mungu walikuwa upande Wake ndani ya sinagogi, akiwa ananena; na walimwandama pale aliposogelewa na kutamaniwa na wayahudi wasioamini waliokuwa na ghadhabu. Malaika hawa walipofusha macho ya umati huo wenye wazimu, na kumwongoza Yesu mahali salama. E. G. White, Roho ya Unabii, juzuu ya 2 uk. 114, 115. [TA 183.5; UM Aya ya 16]

### Mtu Aliyepagawa Katika Sinagogi Kule Kapernaumu

Katika hekalu Yesu alizungumzia ufalme ule aliokuja kuanzisha, na utume Wake wa kuwaweka huru mateka wa Shetani. Alikatizwa na kelele ya kushtua. Mtu aliyepagawa alikimbia mbele akitoka katikati ya watu, huku akilia, "Acha! Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Umekuja kutuangamiza? Nakujua u nani, Mtakatifu wa Mungu." [TA 184.1; UM Aya ya 17]

Sasa kukatawala mkanganyiko na hofu. Usikivu wa watu ulihama kutoka kwa Kristo, na maneno yake hayakutiliwa maanani. Hili lilikuwa kusudi la Shetani kumpeleka yule mhanga katika sinagogi. Lakini Yesu alimkemea yule pepo, akisema, "Fumba kinywa, mtoke. Ndipo yule pepo akamwangusha katikati, akamtoka asimdhuru neno." [TA 184.2; UM Aya ya 18]

Akili ya mhanga huyu mnyonge ilikuwa imetiwa giza na Shetani, lakini katika uwepo wa Mwokozi mwale wa nuru ulikuwa umepenya giza hilo. Aliamshwa kutamani kuwa huru kutoka katika utawala wa Shetani; lakini pepo alishindana na uwezo wa Kristo. Pale yule mtu alipojaribu kuomba msaada kwa Yesu, roho mchafu aliweka maneno mdomoni mwake, na akalia kwa masumbuko ya hofu. Yule aliyepagawa alitambua japo kidogo kwamba alikuwa mbele yake Yeye ambaye angeweza kumweka huru; lakini wakati alipojaribu kuujia mkono ule wenye uweza, dhamiri nyingine ilimzuia, maneno ya huyo pepo yalitamkwa kupitia kinywa cha mtu yule. Pambano kati ya nguvu za Shetani na hamu ya mtu yule kutaka kuwa huru likikuwa la kutisha. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 255. [TA 184.3; UM Aya ya 19]

Yeye aliyemshinda adui mkuu jangwani, alishindana na mateka huyu aliyetapatapa toka mikononi mwa shetani. Yesu alitambua fika kuwa ingawa akiwa amejivika umbo jingine, pepo huyu alikuwa roho yule yule mwovu aliyekuwa amemjaribu kule jangwani. E. G. White, Roho ya Unabii, juzuu ya 2, uk. 180. [TA 185.1; UM Aya ya 20]

Pepo alikita nguvu zake zote ili kuendelea kumtawala mhanga yule. Kusalimu amri hapa ingekuwa ni kumpa Yesu ushindi. Ilionekana kama vile ni lazima adui yule aliyemtesa mtu yule asababishe maisha yake kupotea katika pambano lile dhidi ya adui aliyeharibu utu wake. Lakini Mwokozi alitamka kwa mamlaka, na kumweka huru yule mateka. Yule mtu aliyekuwa amepagawa na pepo alisimama mbele ya watu waliokuwa katika mshangao akiwa na furaha ya kuwekwa huru... Jicho lake lile lililokuwa likitazama likiwa na moto wa wazimu, sasa liling'aa likiwa na utambuzi, likifurika machozi ya shukrani. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 256. [TA 185.2; UM Aya ya 21]

### Kuponywa kwa Mtumishi wa Akida

Akida kwa jicho la imani aliona kuwa malaika wa Mungu walikuwa wamemzunguka Yesu, na kwamba neno Lake lingemwamuru malaika kwenda kwa mtumishi wake mgonjwa. Alitambua kuwa neno Lake lingeenda katika chumba kile, na ya kwamba mtumishi wake angeponywa. E. G. White, The Review and Herald, Machi 11, 1890. [TA 185.3; UM Aya ya 22]

### Watu wa Gadara Waliopagawa na Mapepo

Asubuhi na mapema Mwokozi na wale waliokuwa naye waliifikilia pwani...Watu wawili waliopagawa na pepo, wakitoka makaburini, waliwajia kwa haraka kama vile kuja kuwararua na kuwavunja vunja. Vipande vya minyororo waliyokuwa wamefungwa ili kudhibitiwa wakaikatakata vilikuwa vinaning'inia. Walikuwa wakitokwa na damu kwa sababu ya kujikatakata kwa mawe makali. Walikuwa na macho makali ya hasira yaliyokazwa kupitia katikati ya nywele

zao nyingi na ndefu, mwonekano wa mwanadamu ukiwa umeondolewa na mapepo yale yaliyowapagaa, nao wakaonekana kama wanyama wa mwitu zaidi kuliko mwonekano wa wanadamu. [TA 186.1; UM Aya ya 23]

Wanafunzi na wenzao wengine walikimbia mbali kwa hofu; lakini wakati huo wakagundua kwamba Yesu hakuwa pamoja nao, nao wakarudi kumtafuta. Alikuwa amesimama pale pale walipomwacha. Yeye aliyekuwa ametuliza dhoruba, ambaye kabla alikuwa amekutana na Shetani na akamshinda, hakukimbia mapepo haya. Pale watu wale, waliokuwa wakisaga meno, wakitokwa na mapovu mdomoni, walipomkaribia, Yesu alinyosha mkono ule uliokuwa umetumika kuyapa mawimbi ishara ya kutulia, na watu wale wakaweza kusogea karibu. Mapepo yale yakasimama yakipiga kelele mbele yake pasipo msaada. [TA 186.2; UM Aya ya 24]

Kwa mamlaka aliwaamuru wale pepo wachafu kuwatoka watu wale. Maneno yake yalipenya hadi katika fahamu za waathirika wale zilizokuwa zimetiwa giza. Kwa kiasi kidogo walitambua kwamba pale karibu alikuwepo Yeye ambaye angeweza kuwaokoa kutoka katika kuteswa na pepo wale. Walianguka miguuni pa Yesu ili kumwabudu; lakini pindi vinywa vyao vilipofunguka kuomba rehema Yake, pepo wale waliongea kupitia vinywa hivyo, kila mmoja akilia kwa nguvu kwamba, "Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu? Nakuapisha kwa Mungu usinitese”... [TA 186.3; UM Aya ya 25]

Kwenye ubavu wa mlima mahali ambapo si mbali sana kulikuwa na kundi kubwa la nguruwe wakilisha. Pepo wale wakaomba waruhusiwe kuingia kwa nguruwe hawa, naye Yesu akawaruhusu. Mara taharuki ikawajaa. Wakiwa wamepagawa wakatelemka haraka kuelekea penye ukuta wa ukingo wa bahari, na pasipo kuchunguza huko chini, wakaporomoka na kutumbukia ziwani, wakaangamia. [TA 187.1; UM Aya ya 26]

Hayo yakiendelea badiliko zuri la kushangaza lilikuwa limekuja kwa wale waliokuwa wamepagawa. Nuru ilikuwa imeangaza katika mawazo yao. Macho yao yaliangaziwa na mwale wa utambuzi. Mwonekano wao, ambao ulikuwa umebadilishwa na kuwa katika sura ya Shetani, uligeuka ghafla na kuwa sura nzuri ya mwanadamu, mikono ile iliyokuwa na makovu ilitulia, na kwa sauti ya kupendeza watu wale walimsifu Mungu kwa wokovu waliopata. Sasa watu hawa walikuwa wamevishwa nguo na wakiwa katika hali nzuri, wakiwa wamekaa miguuni pa Yesu, wakisikiliza maneno yake, na kulitukuza jina lake Yeye aliyekuwa amewaponya. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 337, 338. [TA 187.2; UM Aya ya 27]

**Kuponywa kwa Mwana Aliyepagawa**

Yule mvulana aliletwa, na mara macho ya Yesu yalipomwona, pepo yule akamwangusha chini na kumtia kifafa. Aligaagaa na kutoa povu, akitoa sauti zisizo za kawaida. [TA 187.3; UM Aya ya 28]

Kwa mara nyingine tena mkuu wa uzima na mkuu wa nguvu za giza walikuwa wamekutana katika uwanja wa mapambano. Malaika wa nuru na majeshi ya malaika waovu, pasipo kuonekana, walikuwa wanasogea karibu ili kuliona lile pambano. Kwa muda kitambo, Yesu alimruhusu roho mchafu kudhihirisha nguvu zake, ili kwamba watazamaji waelewe uponyaji ambao ungefanyika muda si mrefu. [TA 187.4; UM Aya ya 29]

Yesu akamgeukia yule mgonjwa na kusema, "Ewe pepo bubu na kiziwi, mimi nakuamuru, mtoke huyu, wala usimwingie tena." Kukawa na kilio, mapambano yenye uchungu. Katika kutoka, pepo yule anaonekana kama vile anararua uhai wa mhanga yule. Yule mvulana akalala pasipo kutikisika, akiwa kama asiye na uhai. Makutano wananong’ona wakisema, "Amekufa." Lakini Yesu anamshika mkono, na kumwinua, anampeleka kwa babaye, akiwa amekamilika mwili na akili. Baba na mwanae wanalisifu jina la Mponyaji wao. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 428, 429. [TA 187.5; UM Aya ya 30]

**Yesu Anashutumiwa Kuwa Ana Pepo**

Yesu alijitangaza kuwa Mchungaji Mwema, kwa sababu aliyatoa maisha Yake kwa ajili ya kondoo...Yesu alinena maneno hayo yakisikiwa na umati mkubwa wa watu, na mvuto wa kina ulifanywa mioyoni mwa wengi waliosikiliza. Waandishi na Mafarisayo walijawa na wivu kwa sababu alipendwa na wengi... Alipokuwa akijishuhudia mwenyewe kama Mchungaji wa Kweli, Mafarisayo walisema, “Ana pepo huyu, tena ana wazimu; mbona mnamsikiliza?” Lakini wengine waliibainisha sauti ya Mchungaji wa Kweli, na walisema:... [TA 188.1; UM Aya ya 31]

“Maneno hayo siyo ya mtu mwenye pepo. Je! Pepo aweza kuwafumbua macho vipofu? Basi huko Yerusalemu ilikuwa Sikukuu ya Kutabaruku; ni wakati wa baridi. Naye Yesu alikuwa akitembea hekaluni, katika ukumbi wa Sulemani. Basi Wayahudi walimzunguka, wakamwambia, Hata lini utatuhangaisha nafsi zetu? Kama wewe ndiwe Kristo, utuambie waziwazi. Yesu akawajibu, Naliwaambia, lakini ninyi hamsadiki. Kazi hizi ninazozifanya kwa jina la Baba yangu ndizo zinazonishuhudia... Mimi na Baba tu umoja.”... [TA 188.2; UM Aya ya 32]

Wayahudi walielewa maana Yake... na wakaokota mawe ili wampige. Yesu akawatazama kwa upole na pasipo haya, na kusema, “Kazi njema nyingi nimewaonyesha, zitokazo kwa Baba; kwa ajili ya kazi ipi katika hizo mnanipiga kwa mawe?” [TA 189.1; UM Aya ya 33]

Mfalme wa mbingu alisimama, kwa utulivu akiwahakikisha kama Mungu mbele ya maadui zake. Nyuso zao zilizokunjamana, mikono yao iliyojawa na mawe, havikumtisha. Alitambua kuwa majeshi yasiyoonekana, vikosi vya malaika, vilimzunguka, na katika neno moja toka kinywani Mwake [malaika] wangeutia umati hofu endapo umati ungethubutu kumpiga [Yesu] jiwe hata moja. E. G. White, Alama za Nyakati, Novemba 27, 1893. [TA 189.2; UM Aya ya 34]

Ijapokuwa Yesu alitoa ushuhuda wa uweza Wake wa kiungu, hata hivyo hakuruhusiwa kufundisha masomo Yake pasipo kuingiliwa. Watawala walitafuta kumwanika mbele ya watu ili adhihakiwe. Wasingemruhusu kutangaza mawazo na mafundisho Yake kwa njia nyoofu, lakini, japokuwa aliingiliwa, nuru ilitia mweko akilini mwa mamia, na pale watawala waliposikia maneno ya Yesu, yale yaliyovikwa uweza na kuteka usikivu wa watu, walikasirika, na kusema, "U Msamaria, nawe una pepo" Yesu alikabiliana na tuhuma hizi kwa heshima tulivu, bila hofu na bila kusita akidai kuwa haki za agano zilimlenga, na hazikupokelewa kupitia Ibrahimu. Alitangaza, "Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko." Ghadhabu ya wayahudi haikujua mipaka, na walijitayarisha kumpiga mawe, lakini malaika wa Mungu, wasioonekana na wanadamu, walimharakisha kumtoa mkutanoni. E. G. White, Alama za Nyakati, Mei 26,1890. [TA 189.3; UM Aya ya 35]

### Malaika Waovu Katika Umbo La Mwanadamu Walikuwa Miongoni Mwa Wasikilizaji Wa Kristo.

Wakijifungamanisha na wasikilizaji wa Kristo walikuwa ni malaika katika umbo la wanadamu, wakifanya ushawishi wao, wakipinga, wakitumia vibaya na kuyapotoa maneno ya Mwokozi. E. G. White, The Review and Herald, Agosti 11, 1903. [TA 190.1; UM Aya ya 36]

Kristo alikuwa mwalimu katika makutano ya malaika hawa kabla hawajaanguka toka katika makazi yao ya juu. E. G. White, Selected Messages, juzuu ya 3, uk. 410. [TA 190.2; UM Aya ya 37]

### Ufufuo wa Lazaro

Kristo angeweza kuliamuru jiwe litoke, nalo lingeitii sauti yake. Angeweza kuwaagiza malaika ambao walikuwa karibu naye pale kando ili wafanye kazi hiyo. Kwa kuagiza kwake kule, hata mkono usioonekana ungeliondoa lile jiwe. Lakini lilitakiwa liondolewe na mikono ya mwanadamu. Kwa njia hiyo Kristo alitaka kuonyesha kwamba uanadamu unatakiwa kushirikiana na uungu. Nguvu ya uungu haiagizwi kutenda kile ambacho nguvu ya kibinadamu inaweza kukifanya. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 535. [TA 190.3; UM Aya ya 38]

### Yesu Aliwindwa toka Mji na Mji Wakati wa Huduma Yake.

Yesu aliwindwa toka mahali na mahali wakati wa kazi Yake. Makuhani na watawala walifuata nyayo Zake. Waliutafsiri vibaya utume na kazi Yake. Alikuja kwa watu Wake nao hawakumpokea. Malaika walitazama pambano katika kila hatua. Waliona roho na utendaji wa adui. Walitazama kwa mshangao mbinu za shetani dhidi ya Mwana mtukufu wa Mungu. Waliona kuwa yeye aliyekuwa katika nafasi ya pili toka kwa Yesu kwa uweza na utukufu ameanguka chini zaidi kiasi kwamba anawashawishi wanadamu kufuatilia nyayo za Kristo toka mji na mji. E. G. White, Alama za Nyakati, Novemba 25, 1889. [TA 190.4; UM Aya ya 39]

Tena na tena Angeuawa ikiwa malaika wa mbinguni wasingemtumikia na kuyalinda maisha Yake mpaka wakati ambapo suala la wayahudi kama taifa limeamuliwa. E. G. White, The Review and Herald, Oktoba 12,1897. [TA 191.1; UM Aya ya 40]

## SURA YA 16

## MALAIKA TOKA KATIKA MATESO YA KRISTO HADI KIFO CHAKE

### Yesu Na Wanafunzi Wake Waenda Gethsemane

Akiwa pamoja na wanafunzi Wake, Mwokozi alipita taratibu kuelekea katika bustani ya Gethsemane. Mbalamwezi ya msimu wa Pasaka, mbalamwezi kubwa na iliyojaa, ilimlika kupitia katika anga lisilo na mawingu... Walipokaribia bustanini, wanafunzi wake walikuwa wamegundua badiliko lililomjia Bwana wao. Kamwe hawakuwahi kumwona akiwa na huzuni na ukimya kiasi kile. Kadiri alivyoendelea, hali hii ya huzuni ilizidi kuwa kubwa... [TA 192.1; UM Aya ya 1]

Karibu na mahali pa kuingilia bustanini, Yesu aliwaacha wanafunzi pale isipokuwa watatu, akiwataka wajiombee na kumwombea na Yeye. Aliingia katika faragha za bustani ile akiwa pamoja na Petro, Yakobo na Yohana... [TA 192.2; UM Aya ya 2]

"Kaeni hapa, mkeshe pamoja nami," aliwaambia. [TA 192.3; UM Aya ya 3]

Alienda mbele kidogo kutoka mahali walipokuwa... na kuanguka kifudifudi chini. Alihisi kwamba dhambi ilikuwa imemtenganisha na Baba yake. Pengo lililokuwa katikati lilikuwa pana sana, baya sana, lenye kina kirefu sana, kiasi kwamba roho yake ilitetemeshwa nalo... [TA 192.4; UM Aya ya 4]

Yesu alipohisi kuvunjika kwa mwungano wake na Baba, aliogopa kwamba katika hali ya ubinadamu asingeweza kustahimili pambano lililokuwa linakuja dhidi ya nguvu za giza. Katika jangwa la majaribu hatima ya jamii ya wanadamu ilikuwa hatarini. Kristo alikuwa mshindi. Sasa mjaribu alikuwa amekuja kwa ajili ya pambano lake la mwisho la kuogofya. Alikuwa amejiandaa kwa pambano hili kwa miaka mitatu ya huduma ya Kristo. Kila kitu kwake mwovu kilikuwa kama kiko hatarini. Ikiwa angeshindwa hapa, tumaini lake la ukuu lingepotea; hatimaye falme za ulimwengu zingekuwa za Kristo; yeye angepinduliwa na kutupwa nje. Lakini ikiwa Kristo angeshindwa, dunia ingekuwa ufalme wa Shetani, na jamii ya wanadamu ingekuwa chini ya mamlaka yake milele. Akiwa na masuala hayo ya pambano mbele yake, nafsi ya Kristo ilijawa na utisho wa kutengwa na Mungu. Shetani alimwambia kwamba kama alikuwa amekuwa mdhamini wa ulimwengu wenye dhambi, ile hali ya kutenganishwa ingekuwa ya milele. [TA 192.5; UM Aya ya 5]

Shetani alileta mbele ya Mkombozi hali iliyo katika namna zilizo ngumu sana kwamba: Watu wanaodai kuwa walio juu ya wengine wote kwa mafanikio ya mali na hali njema ya kiroho wamekukataa... Mmoja wa wanafunzi wako mwenyewe...atakusaliti. Mmojawapo wa wafuasi wako shupavu atakukana. Wote watakuacha... [TA 193.1; UM Aya ya 6]

Katika masumbuko yake anaishikilia ardhi yenye baridi, kama vile kuzuia asisukumiwe mbali zaidi na Mungu... Sauti inatoka katika midomo yake iliyochoka ikisema, "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke." Lakini hata sasa anaongeza, "Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo

wewe." E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 685-687. [TA 193.2; UM Aya ya 7]

### Malaika Katika Gethsemane

Ulimwengu wa mbinguni ulikuwa umetazama kwa hamu kuu maisha yote ya Kristo—kila hatua tangu kuzaliwa horini hata sasa kwenye mandhari ya kutisha. Ni mandhari iliyoje hii kwa malaika elfu kumi mara elfu kumi, kwa makerubi na maserafi, kuitazama. E. G. White, Alama za Nyakati, Disemba 9, 1897. [TA 193.3; UM Aya ya 8]

Malaika walikuwa wakingojea juu angani wakitazama mahali pale [Gethsemane], wakishuhudia tukio. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 47. [TA 194.1; UM Aya ya 9]

Walimwona Mwana wa Mungu, Kamanda wao mpendwa, akiwa katika masumbuko yapitayo uwezo wa kibinadamu akifa katika uwanja wa pambano kuuokoa ulimwengu uliopotea na unaoangamia. Mbingu yote ilisikia ombi lile la Kristo. [TA 194.2; UM Aya ya 10]

Masumbuko makali ya roho Yake ambayo, toka katika udhaifu Wake na midomo inayotetemeka kwa mara tatu yalisukuma kilio, "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke. Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe." Yalitikisa mbingu yote. Walimwona Bwana wao amezingirwa na majeshi ya vikosi vya shetani, ubinadamu Wake ulilemewa na hofu isiyoelezeka. E. G. White, Alama za Nyakati, Disemba 9,1897. [TA 194.3; UM Aya ya 11]

Malaika wale waliokuwa wamefanya mapenzi ya Kristo mbinguni walikuwa na hamu ya kumfariji; lakini ilikuwa nje na uweza wao kupunguza ukali wa maumivu Yake. Walikuwa hawajatambua dhambi za ulimwengu ulioharibika, na walitazama kwa mshangao kusudi lao la kuabudu kwa huzuni isiyoelezeka. Ingawa wanafunzi walishindwa kusikitikia pamoja na Bwana wao katika saa ya usumbufu wa pambano Lake, mbingu yote ilikuwa imefurikwa na huruma na ikingojea matokeo kwa hamu yenye maumivu. E. G. White, The Present Truth, Disemba 3, 1885 aya 9. [TA 194.4; UM Aya ya 12]

Mara tatu ombi la kuepushwa na kikombe hicho lilikuwa limelazimisha toka midomoni Mwake. Mbingu ilikuwa haiwezi kuvumilia zaidi mandhari ile, na ilikuwa imemtuma mjumbe wa faraja kwa Mwana wa Mungu aliyenyong'onyea, akiwa amechoka na anakufa chini ya malimbikizo ya hatia ya ulimwengu. Ibid. Februari 18, 1886. [TA 194.5; UM Aya ya 13]

Katika upeo mkuu wa hatari, pale moyo na roho vinapolemewa na mzigo wa dhambi, Gabrieli anatumwa kumtia nguvu Mtesekaji wa kimbingu, na kumchangamsha ili aikanyage njia iliyochafuliwa na damu." E. G. White, Alama

za Nyakati, Disemba 9, 1897. [TA 195.1; UM Aya ya 14]

Katika kilele hiki cha kutisha, wakati ambapo kila kitu kilikuwa hatarini, wakati kikombe cha kutisha kilipokuwa kinatetema mkononi mwa mwenye kuteseka, mbingu zilifunguka, nuru ilimlika katika giza la dhoruba katika saa ile ya zahama, na malaika mwenye nguvu asimamaye katika uwepo wa Mungu, anayekalia nafasi iliyoachwa na Shetani alipoanguka, alikuja karibu na Kristo. Malaika hakuja kuchukua kikombe kile kutoka mkononi mwa Kristo, bali kumtia nguvu ili akinywee, pamoja na hakikisho la upendo wa Baba... [TA 195.2; UM Aya ya 15]

Wale wanafunzi waliokuwa wamelala walikuwa wameamshwa ghafla na nuru iliyokuwa imemzunguka Mwokozi. Walimwona malaika akiinama kwa Bwana wao aliyechoka. Walimwona akiinua kifuani pake kichwa cha Mwokozi, na kumwonyesha mbinguni. Waliisikia sauti yake, kama sauti ya muziki mtamu, akinena maneno ya faraja na tumaini... Kwa mara nyingine tena wanafunzi wakiwa katika uchovu wao wanatingwa na usingizi wa ajabu uliokuwa umewazinga. Kwa mara nyingine tena Yesu anawakuta wamelala usingizi. [TA 195.3; UM Aya ya 16]

Akiwatazama kwa huzuni anawaambia, “Laleni sasa, mpumzike; tazama, saa imekaribia, na Mwana wa Adamu anatiwa katika mikono ya wenye dhambi.” [TA 195.4; UM Aya ya 17]

Hata aliponena maneno haya, alisikia vishindo vya miguu ya kundi la watu wenye fujo wakimtafuta, na akasema, “Ondokeni, twendeni zetu; tazama, yule anayenisaliti amekaribia.” [TA 195.5; UM Aya ya 18]

Hazikuonekana dalili za masumbuko aliyokuwa amepata Yesu wakati huu alipotembea ili kukutana na mwenye kumsaliti. Akiwa amesimama mbele zaidi ya wanafunzi wake alisema, “Ni nani mnayemtafuta?” Wakajibu, “Ni Yesu Mnazareti.” Yesu akajibu, “Ni mimi.” E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 693, 694. [TA 196.1; UM Aya ya 19]

Ilikuwa ndani ya uweza Wake kujiokoa. Pale aliposema maneno, “Ni mimi,” papo japo malaika walimzunguka, na umati ule ulikuwa na ushahidi wote walioweza kuwa nao kwamba Kristo alikuwa ni Uweza wa Mungu. E. G. White, This Day With God, uk. 267. [TA 196.2; UM Aya ya 20]

Ilikuwa vigumu kwa malaika kuvumilia tukio lile. Wangemwokoa Yesu...lakini malaika mwenye amri aliwazuia...Yesu alitambua kuwa malaika walikuwa wakishuhudia tukio la kufedheheshwa Kwake...Malaika mwepesi wa huruma angeufanya umati huo uanguke chini, na kumwokoa Yesu. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 50, 51. [TA 196.3; UM Aya ya 21]

Yule malaika ambaye kabla alikuwa amemhudumia alikuja katikati ya Yesu

na lile kundi. Nuru ya kimbingu iliangaza usoni pa Yesu, na umbo kama la hua lilimtia kivuli pande zote. Katika uwepo wa utukufu huu wa kimbingu, lile kundi la wauaji halikustahimili wakati huu kusimama. Waliweweseka kurudi nyuma. Makuhani, wazee, askari, na hata Yuda mwenyewe, walianguka chini kama watu waliokufa... Lakini mambo yalibadilika haraka. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 694, 695. [TA 196.4; UM Aya ya 22]

Malaika alitoweka na kumwacha Yesu akiwa amesimama mtulivu na akiwa huru, kukiwa na miali angavu ya mbalamwezi usoni pake dhaifu, na bado amezungukwa ma wale watu waliodhoofishwa na uweza wa kiungu, huku wanafunzi walikuwa katika mshangao mkubwa hata kushindwa kusema neno. Vile malaika alipoondoka, askari shupavu wa Kirumi wananyanyuka kwanza, na, pamoja na kuhani na Yuda, wanamzunguka Kristo kana kwamba wameona haya juu ya udhaifu wao, na wakiwa na hofu kuwa angewakwepa. E. G. White, Alama za Nyakati, Agosti 21, 1879. [TA 196.5; UM Aya ya 23]

Wanafunzi walikuwa wamedhani kwamba Bwana wao hawezi kuruhusu achukuliwe...Walifadhaika na kuumia walipoona kamba zikiletwa ili kuifunga mikono yake Yeye waliyempenda. Kwa hasira Petro alichomoa upanga wake na...kukata sikio la mtumishi wa kuhani mkuu. Yesu alipoona hicho kilichofanyika, alijifungua mikono yake,...akasema, “Mwe radhi kwa hili,” akaligusa sikio lililojeruhiwa, nalo likapona wakati huo huo. Halafu akamwambia Petro, “Rudisha upanga wako mahali pake:... Ama wadhani ya kuwa mimi siwezi kumsihi Baba yangu, naye ataniletea sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?” E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 696. [TA 197.1; UM Aya ya 24]

Maneno haya yaliponenwa, mionekano ya malaika ilichangamshwa. Toka wakati ule na sasa walitamani kumzunguka Kamanda wao na kulitawanya kundi hilo lenye hasira. Lakini tena huzuni ilitanda kwa malaika pale Yesu alipoongeza, lakini ni kwa vipi sasa ili maandiko yatimizwe, kwamba ndivyo inavyotakiwa kuwa? Mioyo ya wanafunzi ilizama tena kwenye kufa moyo na kuvunjwa matumaini, pale Yesu alipokubali kundi lile kumteka. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 48. [TA 197.2; UM Aya ya 25]

### Mbele ya behewa la Anasi na Kayafa

Kristo alikuwa ahojiwe kwa kufuata utaratibu mbele ya Sanhedrin; lakini kwanza kwa Anasi alihojiwa kwa mahojiano ya awali... [TA 197.3; UM Aya ya 26]

Baraza lilipokwisha kukusanyika katika ukumbi wa hukumu, Kayafa alikalia kiti chake kama mwenyekiti...Lakini kadiri sasa Kayafa alivyomwangalia mshtakiwa huyu, alipigwa na mshangao mkubwa kwa mwonekano Wake

mtukufu na wenye hadhi kuu. Usadikisho ulimjia kwamba mtu huyu alitoka kwa Mungu. Kilichofuata aliondosha kwa dharau wazo hilo. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 698, 703, 704. [TA 198.1; UM Aya ya 27]

Mbingu yote waliona jinsi Kristo anavyotendewa kikatili. Katika matukio ya kuogofya yaliyokuwa yakiendeshwa ukumbini pa hukumu, Mungu aliuonyesha ulimwengu wa mbinguni roho ambayo ingedhihirishwa na wale wasio tayari kutii sheria Yake. E. G. White, Manuscript Releases, juzuu ya 12, uk. 412. [TA 198.2; UM Aya ya 28]

Ilikuwa vigumu kwa malaika kuvumilia kuona tukio hilo. Wangemwokoa na mikono ya wachunguza makosa Wake; lakini malaika wenye amri kuu waliwazuia...Yesu alitambua kuwa malaika walikuwa wakishuhudia tukio la kuteswa kwake. [TA 198.3; UM Aya ya 29]

Pale alisimama Yesu, mpole na mnyenyekevu mbele ya kundi lenye hasira, likimtuhumu makosa mabaya. Walimtemea mate usoni—uso ule ambao siku moja watatamani kujificha toka kwa huo, ambao utaangazia mji wa Mungu, uking'ara kwa uangavu zaidi kuliko jua—lakini Yeye hakuwaangalia kwa hasira hao washtaki wake. Kwa upole aliinua mkono Wake, na kujipangusa. Walimvika kichwa Chake kwa vazi kuukuu; na kumfunika uso, kisha wakampiga usoni, na kusema, bashiri ni nani aliyekupiga. Kulikuwa na rabsha miongoni mwa malaika. Wangemwokoa papo hapo, lakini malaika mwenye amri aliwazuia. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 50, 51. [TA 198.4; UM Aya ya 30]

### Mbele ya Pilato

Wanadamu walikuwa wametiwa roho ya kishetani katika wakati ambapo waliamua kumchagua Baraba, mwizi na mwuaji, badala ya Mwana wa Mungu. Nguvu ya kipepo ilitawala ubinadamu; vikosi vya malaika waovu walidhibiti uwezo wa kibinadamu wa watu, na katika kujibu swali la Pilato juu ya mtu ambaye anapaswa afunguliwe, walitamka kwa hasira, "Mwondoe huyu, utufungulie Baraba." Pale Pilato aliponena tena kwao kuhusiana na Yesu, kilio cha sauti iliyopwelea kiliinuka, "Msulibishe! Msulibishe." Kupitia kujiachia kwenye nguvu za kipepo, watu waliongozwa kusimamia upande wa mwasi mkuu. [TA 199.1; UM Aya ya 31]

Malimwengu yasiyoanguka walitazama tukio kwa mshangao, wakiwa hawawezi kutambua matokeo mabaya ambayo dhambi ilikuwa imeyafanya. Vikosi vya malaika waovu viliwadhibiti makuhani na watawala, nao ndio waliopaza sauti za mapendekezo ya shetani katika kuwashawishi na kuwajaribu watu kwa madanganyo na njama kumkataa Mwana wa Mungu, na badala yake kumchagua mnyang'anyi na mwuaji....ni tukio lililoje kwa Mungu kulitazama, kwa maserafi na makerubi kuliangalia! Mwana pekee wa Mungu, Mkuu wa mbinguni, Mfalme wa utukufu, alidhihakiwa, alitukanwa, alisutwa,

alikataliwa, na kusulibishwa na wale ambao alikuja kuwaokoa, ambao walijiachia kutumiwa na shetani. E. G. White, The Review and Herald, Aprili 14, 1896. [TA 199.2; UM Aya ya 32]

Malaika waliokuwa wakishuhudia tukio zima walitia alama usadikisho wa Pilato, na walitambua huruma yake kwa Yesu... [TA 199.3; UM Aya ya 33]

Shetani na malaika zake walikuwa wakimjaribu Pilato, na kutaka kumwongoza kuelekea upotevuni. Kwake walipendekeza kwamba ikiwa asingeshiriki katika kumhukumu Yesu, wengine wangeshiriki. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 54, 56. [TA 200.1; UM Aya ya 34]

Hata sasa Pilato hakuachwa atende pasipo utambuzi. Ujumbe toka kwa Mungu ulimwonya kitendo alichokuwa karibu kukiamuru. Katika kujibu ombi la Kristo, mke wa Pilato alikuwa ametembelewa na malaika toka mbinguni, na katika ndoto (mwanamke) alikuwa amemwona Mwokozi na kuzungumza naye... Alimwona akishtakiwa katika shauri lile lililofanyika katika ukumbi wa hukumu. Aliiona mikono ikiwa imefungwa kama mikono ya mhalifu. Alimwona Herode na askari wake wakifanya kazi ya kutisha. Aliwasikia makuhani na wakuu, wakiwa wamejawa na husuda na ubaya, kwa hasira wakimshtaki. Alisikia maneno, "Sisi tunayo sheria, na kwa sheria hiyo amestahili kufa." [TA 200.2; UM Aya ya 35]

Alimwona Pilato akimtoa Yesu ili apigwe, baada ya kuwa ametangaza, "Mimi sioni hatia yoyote kwake." Aliisikia hukumu iliyotamkwa na Pilato, na kumwona akimtoa Yesu kwa wauaji wake. Aliuona msalaba ukiinuliwa kule Kalwari. Aliiona dunia ikifunikwa na giza, na kukisikia kilio kisicho cha kawaida kwamba, "Imekwisha." Bado tukio jingine lilionekana kwa mwanamke huyu. Alimwona Kristo akiwa ameketi kwenye wingu jeupe, huku dunia ikipepesuka angani, na wauaji wake wale wakikimbia kutoka mbele ya utukufu wake. Kwa kilio cha hofu yule mama aliamka, na mara moja alimwandikia Pilato maneno ya onyo. [TA 200.3; UM Aya ya 36]

Wakati Pilato alipokuwa akisitasita kwamba afanye nini, mjumbe alipenya katika umati, na kumpatia Pilato barua kutoka kwa mke wake, iliyosomeka hivi: [TA 200.4; UM Aya ya 37]

"Usiwe na neno na yule mwenye haki; kwa maana nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake." [TA 201.1; UM Aya ya 38]

Uso wa Pilato ulibadilika. Alichanganyikiwa na hisia zake mwenyewe. Lakini wakati alipokuwa akiendelea kukawia kutenda, makuhani na wakuu walikuwa wakiendelea kuhamasisha zaidi mawazo ya watu... [TA 201.2; UM Aya ya 39]

Pilato alitamani kumwokoa Yesu. Lakini aliona kwamba hawezi kufanya hilo, na bado akabaki na cheo chake na heshima yake. Kuliko apoteze mamlaka

yake ya duniani, alichagua kuutoa kafara uhai usio na hatia... [TA 201.3; UM Aya ya 40]

Pilato alijisalimisha chini ya matakwa ya kundi la wenye hasira. Badala ya kuhatarisha kupoteza cheo chake, alimtoa Yesu ili asulibiwe. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 732, 733, 738. [TA 201.4; UM Aya ya 41]

**Kusulibiwa kwa Kristo**

Mwana wa Mungu alitolewa kwa watu kusulibiwa...walimtwisha msalaba mzito...lakini Yesu alizimia asiweze kuendelea. Kisha wakamteka...ambaye alikuwa bado hajaikiri waziwazi imani katika Kristo, lakini alimwamini. Waliutwika msalaba kwake na akaubeba mpaka eneo la kifo. Makundi ya malaika waliongoza angani juu ya eneo lote. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 57. [TA 201.5; UM Aya ya 42]

Ni nani walioshuhudia matukio haya? Ulimwengu wa kimbingu, Mungu Baba, shetani na malaika zake. The Bible Echo, May 29, 1899. [TA 201.6; UM Aya ya 43]

Malaika wa kimbingu... walisikia masuto ya dhihaka na hasira. Kwa furaha wangeachia nafasi zao na kumwendea Mwana wa Mungu katika kuteseka Kwake na maumivu ya mwili, lakini hili hawakuruhusiwa kutenda. E. G. White, Manuscript Releases juzuu ya 18, uk. 71. [TA 201.7; UM Aya ya 44]

"Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe," lilikuwa ni suto la dhihaka alilotupiwa Kristo wakati wa maumivu ya kifo Chake msalabani. Wakati wo wote angeliweza kujiokoa Mwenyewe, na kushuka toka msalabani; lakini angefanya hivyo, dunia ingekabidhiwa kuwa chini ya utawala wa mwasi mkuu. Ilikuwa ni mastaajabu kwa malaika kwamba Kristo hakuwapiga kwa mauti wadhihaki Wake. [TA 202.1; UM Aya ya 45]

Kwa wale waliomdhihaki Kristo alivyotundikwa msalabani, shetani na malaika zake waliwakilishwa. Aliwajaza maneno mabaya na yenye chuki. Alitia msukumo masuto yao. Ibid. Uk. 72. [TA 202.2; UM Aya ya 46]

Falme na mamlaka za giza zilikusanyika kuuzunguka msalaba. Mwasi mkuu, bakiwa bado analo umbo lake la kifahari, aliongoza jeshi la waasi, walioungana na wanadamu katika vita dhidi ya Mungu. E. G. White, Alama za Nyakati, Aprili 14, 1898. [TA 202.3; UM Aya ya 47]

Kristo alikuwa akipambana na mamlaka ya shetani, ambaye alikuwa akijinadi kwamba Kristo yuko mikononi mwake, kwamba alikuwa na nguvu zaidi ya Mwana wa Mungu, kwamba Mungu amemkana Mwana Wake, na kwamba Kristo hakuwa tena katika mkono wa Mungu. E. G. White, Shuhuda kwa Kanisa, juzuu ya 2, uk. 2:214. [TA 202.4; UM Aya ya 48]

Kristo hakujisalimisha kwa adui, hata katika maumivu Yake machungu. Vikosi vya malaika waovu walimzunguka; hata hivyo malaika watakatifu waliamriwa ktokuacha nafasi zao, na kuingilia pambano na adui mwenye masuto na ukosoaji, wala hawakuruhusiwa kuihudumia roho iumiayo ya Yule atesekaye. Ilikuwa ni katika saa hii ya kutisha ya giza, uso wa Baba Yake umejificha, vikosi vya malaika waovu vikimzunguka, dhambi za ulimwengu zi juu Yake, ambapo katika midomo yake iliyodhoofu yalitoka maneno ya uchungu, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" Bible Echo and Signs of the Times, January 1, 1887. [TA 202.5; UM Aya ya 49]

Giza lililofunika dunia katika kusulibiwa Kwake lilificha kundi la mawakala wa mbinguni wenye nguvu, lakini dunia ilitikisika katika kupitapita kwa umati wa malaika wa kimbingu. Miamba ilipasuka; kwa masaa matatu dunia ilifunikwa na giza lisilopenyeka; asili ikiwa na tabia yake ya kuifunika dunia ilificha mateso ya Mwana wa Mungu. E. G. White, Manuscript Releases, juzuu ya 5, uk. 353. [TA 203.1; UM Aya ya 50]

Baba, akiwa na malaika Zake wa kimbingu, alifunikwa katika giza hilo nene. Mungu alikuwa karibu na Mwana Wake, ingawa hakujidhihirisha Kwake au kwa mwanadamu ye yote. Kama mwale mmoja wa utukufu uweza na Wake ungepenya wingu zito lililomfunika, kila aliyekuwapo pale angefutiliwa mbali. Ibid. Juzuu ya 12, uk. 385. [TA 203.2; UM Aya ya 51]

Mbingu ingewezaje kunyamaza kimya? Je, twaweza kustaajabu juu ya giza la kuogofya lisilo la kawaida lililoning'inia juu ya msalaba? Je, twaweza kustaajabu pale miamba ilipopasuka, ngurumo ilipolia, radi ilipomulika, tikisiko la dunia kwa kishindo cha jeshi la mbinguni walipomtazama Kamanda wao mpendwa akiteseka katika ufidhuli ule? E. G. White, The Review and Herald, Septemba 1, 1891. [TA 203.3; UM Aya ya 52]

Pale Kristo aliposema, "Imekwisha," malimwengu yasiyoanguka nao walihifadhiwa. Kwao pambano lilipiganwa na ushindi ukapatikana. Tangu hapo shetani hakuwa tena na sehemu katika kuuvuruga upendo unaotamalaki katika malimwengu. Ibid. Machi 12, 1901. [TA 204.1; UM Aya ya 53]

Malaika watakatifu walipigwa na hofu kwamba mmoja wao angeangukia mbali kiasi cha kuweza kutenda ukatili wa namna ile kama ilivyodhihirishwa kwa Mwana wa Mungu pale Kalwari. Kila wazo la huruma walilowahi kujisikia mioyoni mwao kwa ajili ya shetani uhamishoni pake lilizimika mioyoni mwao. E. G. White, Alama za Nyakati, Septemba 23, 1889. [TA 204.2; UM Aya ya 54]

Ilikuwa si mkono wa kuhani uliorarua toka juu hadi chini pazia la kupendeza lililotenganisha patakatifu na patakatifu mno. Ulikuwa ni mkono wa Mungu. Pale Kristo aliposema, "Imekwisha," Mwangalizi mtakatifu aliyekuwa mgeni asiyeonekana katika karamu ya Belshaza alilitamkia taifa la kiyahudi kuwa taifa

lililovuliwa sifa kama taifa la Mungu. Mkono ule ule ulioandika ukutani maneno yaliyotamka uangamivu wa Belshaza na mwisho wa ufalme wa Babeli, mkono huo huo ulirarua pazia la hekalu toka juu hata chini. E. G. White, S.D.A. Ufafanuzi wa Biblia, juzuu ya 5, uk. 1109. [TA 204.3; UM Aya ya 55]

Viongozi wa kiyahudi waliushusha mwili Wake, na kuulaza katika kaburi jipya la Yusufu, wakalizungushia jiwe kubwa mlangoni, kwakifanya hivyo kwa kudhani kwamba wanafunzi Wake wangelikuja na kumwiba katika majira ya usiku. Malaika waovu walishangilia kulizunguka kaburi, kwa kuwa walidhani kwamba Kristo ameshindwa. Kundi la maaskari wa Kirumi waliamriwa kulilinda kaburi, na tahadhari kuu ziliwekwa na wayahudi kuufanya ushindi wao uwe kamili. Lakini malaika wa kimbingu walikuwa wakipalinda pahali pale alipokuwa amelala Kamanda wao mpendwa. E. G. White, The Review and Herald, Oktoba 9, 1888. [TA 204.4; UM Aya ya 56]

Ilikuwa mpaka kifo cha Kristo ambapo tabia ya shetani ilifunuliwa waziwazi kwa malaika au kwa malimwengu yasiyoanguka. Ndipo madanganyo na shutuma zake ambaye hapo mwanzo alikuwa malaika aliyeinuliwa vilionekana katika nuru dhahiri. E. G. White, Alama za Nyakati, Agosti 27, 1902. [TA 205.1; UM Aya ya 57]

Kifo cha Kristo msalabani kilihakikisha maangamizo ya yeye aliye na nguvu za mauti, mwanzilishi wa dhambi. Shetani anapoangamizwa, hakutakuwepo na ye yote wa kujaribiwa kutenda uovu; hakutakuwa na haja ya kurudia upatanisho; na hakutakuwa na hatari ya uasi mwingine katika ulimwengu wa Mungu. Kile ambacho peke yake chaweza kufaa kuzuia dhambi katika ulimwengu huu wa giza, kitazuia dhambi mbinguni. [TA 205.2; UM Aya ya 58]

Manufaa ya kifo cha Kristo yataonekana kwa watakatifu na malaika. Wanadamu walioanguka hawatakuwa na makazi katika paradiso ya Mungu pasipo Mwanakondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa kwa misingi ya dunia...Malaika humpatia heshima na utukufu Kristo, kwani hata wao hawako salama isipokuwa kwa kutazama mateso ya Mwana wa Mungu. Ni kwa njia ya ufanisi wa msalaba ambapo malaika wa mbinguni wanalindwa dhidi ya uasi. Pasipo msalaba hawawezi kamwe kuwa salama dhidi ya uovu kama ilivyokuwa kwa malaika kabla ya anguko la shetani. Ukamilifu wa malaika ulishindwa mbinguni. Ukamilifu wa mwanadamu ulishindwa Edeni...Mpango wa wokovu, ukifunua haki na pendo la Mungu, hutoa ulinzi daima dhidi ya uasi katika malimwengu yasiyoanguka...Kifo cha Kristo katika msalaba wa kalwari ndio tumaini pekee katika ulimwengu huu, na litakuwa mada yetu katika ulimwengu ujao. Ibid. Disemba 30, 1889. [TA 203.3; UM Aya ya 59]

Kristo, katika maisha Yake na kifo Chake, daima amesimika swali pana kama kuna kujikana nafsi pamoja na Mungu, na kama Mungu ni nuru na upendo. Hili lilikuwa swali lililotia uchochezi huko mbinguni juu, ambalo lilikuwa

ndio mwanzo wa ukengeufu wa shetani toka kwa Mungu. Badiliko au ukomeshaji wa sheria za serikali Yake katika mahakama za mbinguni ulidaiwa kuwa uwe ushahidi wa upendo wa Mungu. E. G. White, The Review and Herald, Oktoba 21,1902. [TA 206.1; UM Aya ya 60]

## SURA YA 17

## MALAIKA TOKA KUFUFUKA KWA YESU MPAKA KUPAA KWAKE

### Asubuhi ya Kufufuka Kwake

Wanafunzi walipumzika sabato, wakihuzunikia kifo cha Bwana wao, wakati Yesu, Mfalme wa utukufu, akiwa amelala kaburini. Usiku ulipokaribia, askari walikusanyika kulinda mahali alipopumzika Mwokozi, wakati malaika, wasioonekana walikuwa wakipazunguka mahali hapo patakatifu angani. E. G. White, Maandiko ya Awali, uk. 181. [TA 207.1; UM Aya ya 1]

Usiku wa siku ya kwanza ya juma ulikuwa unapita taratibu. Saa ya giza kuu, kabla tu ya kupambazuka, ilikuwa imefika. Kristo alikuwa bado ni mfungwa mle katika kaburi lake. Jiwe kubwa lilikuwa bado liko mahali pake pale; lakiri ya Kirumi ilikuwa haijavunjwa; walinzi wa Kirumi walikuwa wanalinda lindo lao. Na walikuwepo walinzi wengine wasioonekana. Majeshi ya malaika waovu yalikuwa yamekusanyika pale. Ikiwa ingewezekana, mfalme wa giza pamoja na

jeshi lake lililoasi wangeendelea kulifanya kaburi lililokuwa na Mwana wa Mungu lifungwe kwa lakiri milele. Lakini jeshi la mbinguni lililizunguka kaburi. Malaika wale wenye nguvu zaidi walikuwa wanalilinda kaburi, na wakisubiri kumkaribisha Mfalme wa uzima. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 779. [TA 207.2; UM Aya ya 2]

Kukiwa bado kungali usiku, malaika waangalizi walitambua kuwa saa ya kuachiwa kwa Mwana mpendwa wa Mungu, Kamanda wao mpendwa, ilikuwa karibu kufika. Wakiwa wanasubiri kwa shauku kuu saa ya ushindi Wake, malaika mwenye nguvu alikuja akipaa kwa kasi toka mbinguni. E. G. White, Maandiko ya Awali, uk. 181. [TA 208.1; UM Aya ya 3]

Malaika mwenye nguvu zaidi toka mbinguni, aliyeshikilia nafasi ambayo shetani aliiacha, alipewa kazi na Baba, na akiwa amevikwa deraya ya mbinguni, alitawanya giza akiwa katika njia yake. Uso wake ulikuwa kama radi, na mavazi yake meupe kama theluji. E. G. White, S.D.A. Ufafanuzi wa Biblia, juzuu ya 5, uk. 1110. [TA 208.2; UM Aya ya 4]

Mmoja miongoni mwa jeshi la malaika aliyekuwa ameshuhudia mateso ya Yesu, na alikuwa akilinda mahali patakatifu alipopumzika Yesu, aliungana na malaika atokeaye mbinguni, na kwa pamoja walishuka kaburini. Nchi ikatikisika na kutetemeka walipokaribia, na kulikuwapo na tetemeko kuu. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 66. [TA 208.3; UM Aya ya 5]

Uso wanaouona [askari wa kirumi] si uso wa mpiganaji mwenye mwili wa kufa; ni uso wa mwenye uwezo mkuu kuliko wote miongoni mwa jeshi la Bwana. Mjumbe huyu ndiye anayekalia nafasi iliyoachwa na Shetani wakati alipoanguka. Huyu ndiye yule aliyetangaza katika vilima vya Bethlehemu kuhusu kuzaliwa kwa Kristo. Dunia inatetemeka wakati anapokaribia, majeshi ya giza yanakimbia. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 779, 780. [TA 208.4; UM Aya ya 6]

Malaika alilikaribia kaburi, akaliviringisha jiwe kana kwamba ni jiwe changarawe, na akalikalia. Nuru ya mbinguni ililizunguka kaburi, na mbingu yote ilimulikwa kwa utukufu wa malaika. E. G. White, S.D.A. Ufafanuzi wa Biblia, juzuu ya 5, uk. 1110. [TA 208.5; UM Aya ya 7]

Kamanda malaika aliliweza lile jiwe kuu ambalo lilihitaji wanaume wengi wenye nguvu kuliweka pale, aliliviringisha, na kulikalia, huku mwenzake akiingia ndani na kufungua yote aliyokuwa amefungwa usoni na kichwani. [209.1; UM Aya ya 8]

Ndipo malaika mkuu, kwa sauti iliyofanya nchi itikisike, alisikika: Yesu, wewe Mwana wa Mungu, Baba yako akuita! Ndipo Yeye aliyetwaa uweza wa kuishinda mauti na kaburi, kwa kishindo cha mshindi, alitokea kaburini, katikati ya nchi inayopepesuka, katikati ya mwako wa radi na ngurumo. E. G. White,

Roho ya Unabii, juzuu ya 3, uk. 192. [TA 209.2; UM Aya ya 9]

Yeye aliyesema, “Nautoa uhai wangu ili niutwae tena,” alitoka kaburini hata uzimani uliokuwa ndani Yake Mwenyewe. Ubinadamu ulikufa; uungu haukufa. Katika uungu Wake, Kristo alikuwa nao uweza wa luvunja minyororo ya mauti. E. G. White, The Youth’s Instructor, Agosti 4, 1898. [TA 209.3; UM Aya ya 10]

Kristo katika Uungu Wake aling’aa akiwa anatoka kaburini, na akatoka akiwa mshindi juu ya mauti na kaburi. E. G. White, Alama za Nyakati, Mei 30, 1895. [TA 209.4; UM Aya ya 11]

Walinzi wa kirumi...waliwezeshwa kutazama tukio hilo, kwani walikuwa na ujumbe kuubeba kama mashahidi wa kufufuka kwa Kristo. E. G. White, S.D.A. Ufafanuzi wa Biblia, juzuu ya 5, uk. 1110. [TA 209.5; UM Aya ya 12]

Hofu ya kutisha iliwashika walinzi. Ulikuwa wapi sasa uwezo wao kuulinda mwili wa Yesu? Hawakufikiri juu ya wajibu wao, au wa wanafunzi wakimwiba Yesu. Walishangazwa na kushtushwa, vile nuru angavu ipitayo kiwango ya malaika ilivyokuwa inang’ara mahali hapo kote kwa uangavu zaidi ya jua. Walinzi wa kirumi waliwaona malaika, na kuanguka ardhini kama wafu. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 66. [TA 209.6; UM Aya ya 13]

Kwa kicho cha juu keshi la malaika walitazama tukio. Na vile Yesu alipokuwa akitembea toka kaburini katika uadhama, wale malaika wang’aao walisujudu na kumwabudu; kisha wakamwimbia nyimbo za shangwe na ushindi. Ibid. Uk. 66, 67. [TA 210.1; UM Aya ya 14]

Askari...waliwasikia wakazi wa mbinguni wakiimba kwa furaha kuu na shangwe: Umemshinda shetani na nguvu za giza! Umeitowesha mauti kwa ushindi! “Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku” (Ufunuo 12:10). E. G. White, Roho ya Unabii, juzuu ya 3, uk. 194. [TA 210.2; UM Aya ya 15]

Jeshi la malaika likiwa linarejea mbinguni, na nuru na utukufu kutoweka, walinzi wa kirumi waliamka kuona ikiwa ilikuwa salama kwao kustahimili kupatazama. Walijawa na mshangao walipoona kwamba jiwe kubwa lilikuwa limeviringishwa toka mlangoni pa kaburi, na Yesu amefufuka. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 68. [TA 210.3; UM Aya ya 16]

Shetani sasa hakushinda. Malaika zake walikuwa wamekimbia mbele ya nuru angavu ipenyayo ya malaika wa mbinguni. Kwa uchungu walimlalamikia mkuu wao, kwamba mawindo yao wamepokonywa kwa nguvu toka mikononi mwao, na kwamba Yeye waliyemchukia sana amefufuka toka katika wafu. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 67. [TA 210.4; UM Aya ya 17]

## Baada Tu Ya Kufufuka Kwa Yesu

Kwa muda kitambo shetani alionekana kuhuzunika na alionyesha kusikitika. Aliitisha shauri na malaika zake kujadili kile wanachotakiwa baadaye kutenda kinyume na serikali ya Mungu. Shetani alisema, mwapaswa kuharakisha kwa makuhani wakuu na wazee. Tulifanikiwa katika kuwalaghai na kuwapofusha macho yao, na kuishupaza mioyo yao dhidi ya Yesu. Tuliwaaminisha kuwa Yeye ni laghai. Wale walinzi wa kirumi watapeleka habari za kuchukiza kwamba Kristo amefufuka. Tuliwaongoza makuhani na wazee kumchukia Yesu, na kumwua. Wafahamisheni kuwa, kwa kuwa walikuwa wauaji Wake, pale itakapojulikana kwamba Yesu amefufuka, watapigwa mawe hadi kufa kwa kuwa walimwua mtu asiye na hatia. ibid uk. 67, 68. [TA 211.1; UM Aya ya 18]

Walinzi wa kirumi walitoka kaburini, wakiwa wamegharikishwa na kile walichokiona na kukisikia, na kushika njia yao haraka mjini, wakiwapasha habari wale waliokutana nao kuhusiana na matukio ya kustaajabisha waliyoshuhudia...Wakati huo huo mjumbe aliwaendea makuhani na watawala, akiwatangazia: Kristo yule mliyemsulibisha amefufuka toka katika wafu! [TA 211.2; UM Aya ya 19]

Papo hapo mtumishi alitumwa akiwa na ujumbe wa siri kuwaitisha walinzi wa kirumi kwenye behewa la kuhani mkuu. Walihojiwa kwa ukaribu zaidi; walifunua kikamilifu kile walichokishuhudia kaburini: kwamba mjumbe wa kutisha alikuja tokea mbinguni mwenye sura mithili ya uangavu wa radi, na mwenye mavazi meupe kama theluji; kwamba nchi ilitikisika na kutetemeka, na walipigwa na kukosa nguvu; kwamba malaika alilishika jiwe lile kubwa mlangoni mwa kaburi na kuliviringisha kana kwamba limekuwa jiwe changarawe; kwamba mwonekano wa utukufu mkuu ulitokea kaburini; kwamba viitikio vya sauti vilizifanya mbingu na nchi vitoe sauti za nyimbo za ushindi na shangwe; kwamba pale nuru ilipofifia, na muziki kukoma, walirejea katika nguvu zao, wakiliona kaburi liko tupu, na mwili wa Yesu hauonekani po pote. Redemption: Or the Resurrection of Christ; and His Ascension, section 6, 14, 15. [TA 211.3; UM Aya ya 20]

Walinzi wa kirumi waliharakisha kwa makuhani wakuu na wazee wakiwa na simulizi ya kushangaza ya kile walichokiona; na wale wauaji waliposikia habari ya kustaajabisha, udhaifu ulimshika kila mmoja. Hofu iliwaingia juu ya kile walichokitenda. Ndipo wakatambua kwamba ikiwa habari ilikuwa ya kweli, wameangamia. Kwa muda kidogo walichanganyikiwa, na kutazamana kwa ukimya, wasijue la kutenda ama kusema. Waliwekwa katika nafasi ambayo wasingeiamini isipokuwa iwe kushutumu kuwe mikononi mwao. [TA 212.1; UM Aya ya 21]

Walikwenda faragha kushauriana kile kinachotakiwa kufanyika. Waliazimu

kuwa endapo itaenea mbali kwamba Yesu amefufuka, na habari ya utukufu wa kushangaza kiasi hicho, uliowafanya walinzi waanguke kama wafu ikiweza kuwafikia watu, kwa hakika watu wataghadhabika, na wanaweza kuwachinja. Waliazimu kuwakodisha askari ili kulificha suala lenyewe. Waliwapa pesa nyingi, wakisema, Semeni, wanafunzi Wake walikuja usiku na kumwiba wakati tukiwa usingizini. Na walinzi walipouliza kile kinachopaswa kufanyika kwa ajili yao kwa kosa la kulala katika lindo lao, kuhani na wazee walisema kwamba wangemshawishi mkuu na kuwaokoa. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 1, uk. 68. [TA 212.2; UM Aya ya 22]

### Wanawake Waja Kaburini

Wanawake waliokuwa wamesimama karibu na msalaba wa Kristo walitazama na kusubiri saa za Sabato zipite. Mnamo siku ya kwanza ya juma, asubuhi na mapema, walishika njia kwenda kaburini, wakiyachukua manukato ya thamani ili kuupaka mwili wa Mwokozi... [TA 213.1; UM Aya ya 23]

Wakiwa hawajui hata kilichokuwa kinatokea, walifika karibu na bustani, wakisema kadiri walivyoendelea kwenda, “Ni nani atakayetuvingirishia lile jiwe mlangoni pa kaburi?” Walijua kwamba wasingeweza kuliondoa lile jiwe, lakini bado waliendelea kwenda. Na tazama, mbingu ziliangaza ghafla kwa utukufu ambao haukuletwa na jua lililokuwa linapambazuka. Nchi ilitetemeka. Waliona kwamba lile jiwe lilikuwa limevingirishiwa pembeni. Kaburi lilikuwa tupu. [TA 213.2; UM Aya ya 24]

Wale wanawake hawakuwa wamekuja kaburini wakitoka wote katika uelekeo mmoja. Mariamu Magdalena alikuwa wa kwanza kufika pale; na kwa kuona kwamba jiwe lilikuwa limeondolewa, aliharakisha kwenda kuwaambia wanafunzi. Wakati hayo yanatokea wale wanawake wengine walifika pale. Nuru ilikuwa inaangaza mahali pale pa kaburi, lakini mwili wa Yesu haukuwemo mle. Kadiri walivyokawia-kawia pale, ghafla waliona kwamba hawakuwa peke yao. Kijana mmoja wa kiume aliyekuwa amevikwa mavazi yang’aayo alikuwa amekaa kando ya kaburi. Huyu alikuwa yule malaika aliyekuwa amelivingirisha jiwe. Alikuwa amechukua mwonekano wa mwanadamu ili kwamba asiwashitue hawa rafiki za Yesu. Lakini nuru ya mbinguni ilikuwa bado inaangaza kumzunguka. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 788, 789. [TA 213.3; UM Aya ya 25]

Wanawake walishtushwa mno, na wakasujudu nyuso zao hata nchi; kwa maana mwonekano wa kiumbe wa mbinguni ulikuwa mkubwa wasioweza kuustahimili. Malaika aliamriwa kuendelea kuuficha utukufu wake kabla hajazungumza nao. E. G. White, The Youth’s Instructor, July 21, 1898. [TA 214.1; UM Aya ya 26]

“Msiogope ninyi” alisema, “kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu

aliyesulibiwa. Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa. Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu. Tazama, awatangulia kwenda Galilaya; ndiko mtakakomwona. Haya, nimekwisha waambia." [TA 214.2; UM Aya ya 27]

Kwa mara nyingine wanaangalia ndani ya kaburi, na wanasikia tena habari zile za kushangaza. Malaika mwingine ambaye yuko katika umbo la mwanadamu yupo pale, na anasema, "Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka. Kumbukeni alivyosema nanyi alipokuwa akaliko Galilaya, akisema, Imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa wenye dhambi, na kusulibiwa, na kufufuka siku ya tatu." [TA 214.3; UM Aya ya 28]

Amefufuka, amefufuka! Wanawake wale wanayarudia maneno hayo tena na tena. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 789. [TA 214.4; UM Aya ya 29]

### Kupaa kwa Yesu kwa Baba Yake

Malaika walikuwa wamesema kwamba, "Enendeni zenu, mkawaambie wanafunzi wake, na Petro, ya kwamba awatangulia kwenda Galilaya; huko mtamwona, kama alivyowaambia." Malaika hawa walikuwa wamekuwa na Kristo kama malaika walinzi katika maisha yake yote ya duniani. Walikuwa wameshuhudia kushtakiwa na kusulibiwa kwake. Walikuwa wamesikia maneno yake kwa wanafunzi wake. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 793. [TA 214.5; UM Aya ya 30]

Wanawake wale waliondoka haraka pale kaburini "kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi wake habari." [TA 214.6; UM Aya ya 31]

Mariamu hakuwa amesikia hizo habari njema. Alienda kwa Petro na Yohana akiwa na ujumbe wa huzuni kwamba, "Wamemwondoa Bwana kaburini, wala hatujui walikomweka." [TA 215.1; UM Aya ya 32]

Wale wanafunzi waliharakisha kwenda kaburini, na kukuta hali iko vile Mariamu alivyosema. Waliona sanda na kitambaa, lakini hawakumwona Bwana wao... [TA 215.2; UM Aya ya 33]

Mariamu alikuwa amefuatana na Yohana na Petro kwenda kaburini; waliporudi Yerusalemu, yeye alibaki. Alipoangalia ndani ya kaburi lililo wazi, majonzi yaliujaza moyo wake. Alipochungulia ndani, aliwaona wale malaika wawili, mmoja akiwa sehemu ya kichwani na mwingine sehemu ya miguuni mahali hapo ulipokuwa umelazwa mwili wa Yesu. Wakamwuliza, "Mama, unalilia nini?" Akajibu kwamba, "Kwa sababu wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka. [TA 215.3; UM Aya ya 34]

Halafu aligeuka, kwenda mbali na wale malaika, akidhani kwamba angeweza kupata mtu wa kumwambia kitu kilichokuwa kimefanyika kuhusu

mwili wa Yesu. Sauti nyingine ikamwambia, “Mama, unalilia nini? Unamtafuta nani?” Kwa macho yale yaliyofurikwa na machozi, Mariamu aliona umbo la mwandamu, naye akidhani kwamba ni mtunzaji wa bustani ile, alimwambia, “Bwana, ikiwa umemchukua wewe, uniambie ulipomweka, nami nitamwondoa... [TA 215.4; UM Aya ya 35]

Lakini sasa kwa sauti yake halisi iliyokuwa inajulikana Yesu alisema, “Mariamu.” Sasa alijua kwamba yule aliyekuwa anazungumza naye si mtu mgeni kwake, na alipogeuka alimwona Kristo aliye hai akiwa mbele yake. Kwa furaha alisahau kwamba Kristo alikuwa amesulibiwa. Alipomkimbilia kwa shangwe, kama anayetaka kukumbatia miguu yake, alisema, “Raboni.” Lakini Kristo alinyosha mkono wake, akisema, “Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba.”... [TA 215.5; UM Aya ya 36]

Yesu alikataa kupokea heshima ya watu wake mpaka alipokuwa na uhakika kwamba dhabihu yake ilikuwa imepokelewa na Baba. Alipaa kwenda mbinguni, na alilisikia hakikisho kutoka kwa Mungu mwenyewe kwamba upatanisho wake kwa ajili ya dhambi za wanadamu ulikuwa umetosha na kuzidi, kwamba kwa damu yake wote wangepata uzima wa milele... [TA 216.1; UM Aya ya 37]

Baada ya kuwa amepaa kwenda kwa Baba, Yesu alijitokeza kwa wale wanawake wengine, akisema, “Salamu! Wakakaribia wakamshika miguu, wakamsujudia. Kisha Yesu akawaambia, Msiogope; enendeni, mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakakoniona.” E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 789, 790, 793. [TA 216.2; UM Aya ya 38]

### Kuonekana Kwingine Baada Ya Kufufuka Kwake

Baadaye jioni sana mnamo siku ile ya kufufuka, wawili miongoni mwa wanafunzi walikuwa njiani wakienda Emau, mji mdogo ulio umbali wa maili nane kutoka Yerusalemu...Walikuwa wamesikia habari za asubuhi kuhusu kuondolewa kwa mwili wa Kristo kutoka katika kaburi, na taarifa ya wanawake waliokuwa wameona malaika na kukutana na Yesu. Sasa walikuwa wanarejea majumbani mwao... [TA 216.3; UM Aya ya 39]

Wakiwa hawajafika mbali katika safari yao mtu mgeni kwao aliungana nao, lakini walikuwa wamesongwa na mfadhaiko wao na kuvunjwa matumaini kiasi kwamba hawakumtazama kwa ukaribu. Waliendelea na mazungumzo yao, wakieleza mawazo ya mioyo yao... Kadiri walivyoongea habari zilizokuwa zimetokea, Yesu alitamani kuwafariji... Lakini lazima kwanza awape mafundisho ambayo wasingeyasahau kamwe... [TA 216.4; UM Aya ya 40]

Akianzia kwa Musa... Kristo alifafanua katika Maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe...Akitoa hoja kutoka katika unabii, Kristo aliwapatia wanafunzi wake wazo sahihi la vile ambavyo angekuwa katika

ubinadamu... [TA 217.1; UM Aya ya 41]

Wakati wa safari yao jua lilikuwa limezama... Na pindi wale wanafunzi walipotaka kuingia nyumbani kwao, yule mtu mgeni alionekana kama alikuwa aendelee na safari yake. Lakini wanafunzi walihisi kuvutwa naye sana...“Wakasema, “Kaa pamoja nasi.” Hakuonekana kukubali mwaliko ule, lakini walimsisitiza, wakisema, “Kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha.” Kristo alikubaliana na kule kusihi kwao. “Akaingia ndani kukaa nao.” ... [TA 217.2; UM Aya ya 42]

Mara chakula chepesi cha jioni kinaandaliwa. Kinawekwa mbele ya mgeni, ambaye amekaa kwenye kiti kikubwa cha mezani. Ananyosha mikono yake kukibariki chakula kile. Wale wanafunzi wanaanza kushangaa tena. Rafiki yao yule anainyosha mikono yake sawasawa kabisa na vile Bwana wao alivyofanya mara kwa mara. Wanatazama tena, na tazama, wanaona alama za misumari mikononi mwake. Wote wawili wanasema kwa msahangao kwamba, Ni Bwana Yesu! Amefufuka kutoka katika wafu! [TA 217.3; UM Aya ya 43]

Wanainuka ili kujitupa miguuni pake na kumsujudia, lakini anatoweka kutoka machoni pao... Lakini hawawezi kukaa na kuongea wakiwa na habari hizi za kuwaambia watu...Wanaacha mlo wao bila hata kuuonja, na mara wanashika njia tena kwa furaha wakirudi kwa njia ile ile waliyokuwa wamepita, wakiharakisha kwenda kuwapasha habari wanafunzi walioko mjini. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 795-801. [TA 217.4; UM Aya ya 44]

Walipofika Yerusalemu wale wanafunzi wawili waliingilia katika lango la mashariki, ambalo linakuwa wazi usiku nyakati za sikukuu...Wanaenda katika kile chumba cha ghorofani mahali Yesu alipokuwa kwa saa za jioni ile ya mwisho kabla ya kifo Chake...Wanakuta mlango wa chumba kile ukiwa umefungwa barabara. Wanabisha hodi, lakini hakuna anayeitika. Kote ni ukimya. Wanajitaja majina yao. Mlango unafunguliwa kwa uangalifu, wanaingia, na Mwingine, bila kuonekana, anaingia pamoja nao. Halafu mlango unafungwa tena na kukazwa, kuzuia wapelelezi wasiingie. [TA 217.5; UM Aya ya 45]

Wale wasafiri wanawakuta hawa katika mshangao. Sauti za wale waliomo katika chumba zinapaa kwa shukrani na nyimbo za sifa, zikisema, “Bwana amefufuka kweli kweli, naye amemtokea Simoni.” Ndipo wale wasafiri wawili...wanasimualia kisa cha ajabu cha jinsi Yesu alivyowatokea. Ndipo wakiwa wamemaliza tu...ndipo, tazama, Nafsi nyingine inasimama mbele yao... Ndipo wanasikia sauti ambayo si nyingine bali ni ya Bwana wao... [TA 218.1; UM Aya ya 46]

“Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho. Akawaambia, Mbona mnafadhaika? Na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama

mnavyoniona mimi kuwa nayo. Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake." E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 802, 803. [TA 218.2; UM Aya ya 47]

Idadi kadhaa ya wanafunzi walikifanya kile chumba cha juu kuwa nyumbani pao kwa muda, na wakati wa jioni wote isipokuwa Tomaso walikusanyika mahali hapa. Jioni moja Tomaso aliazimu kukutana na wengine... Wakati wanafunzi walipokuwa wakila chakula cha jioni, waliongea kuhusu ushahidi ambao Kristo alikuwa amewapatia katika unabii. "Akaja Yesu, na milango imefungwa, akasimama katikati, akasema, Amani iwe kwenu." [TA 218.3; UM Aya ya 48]

Akimgeukia Tomaso alimwambia, "Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu, wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye." ... [Tomaso] Hakuwa na hamu ya uthibitisho zaidi. Moyo wake uliruka kwa shangwe, na alijitupa miguuni pa Yesu akilia, "Bwana wangu na Mungu wangu." E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 807. [TA 219.1; UM Aya ya 49]

Yesu alikuwa ameahidi kukutana na wanafunzi wake kule Galilaya; na mara tu baada ya Pasaka kuhitimishwa walielekea katika eneo hilo... Miongoni mwa wanafunzi wale, saba walikuwa kundi moja. Walikuwa wamevaa nguo za hali duni za kivuvi...Walisumbuka na kazi ya usiku mzima, pasipo na mafanikio... Wakati wote mwangalizi aliye peke yake aliyekuwa pwani aliwafuata kwa jicho lake, wakati Yeye mwenyewe alikuwa haonekani. Baada ya muda mrefu kulipambazuka... na wanafunzi wale wakaona mtu mgeni akiwa amesimama ufukweni... Yohana alimtambua yule mgeni, na akasema kwa mshangao, "Ndiye Bwana." E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 809, 810. [TA 219.2; UM Aya ya 50]

Katika mkutano ule wa mlimani kule Galilaya, waamini wote ambao waliwezekana kuitwa kuja pamoja walikuwa wamekusanyika... Katika wakati uliomuliwa, kadiri ya watu mia tano walikuwa wamekusanywa kama kundi pale kando kando ya mlima, wakiwa na hamu ya kujifunza mambo yote ambayo yangewezekana kujifunzwa kutoka kwa wale waliokuwa wamemwona Kristo tangu kufufuka kwake... Ghafla Yesu alisimama katikati yao. Hakuna yeyote aliyeweza kueleza kwamba alikuwa ametoka wapi na amekujaje... Alitangaza kwamba alikuwa amepewa "mamlaka yote." Maneno yake yalichukua mawazo ya wasikilizaji wake na kuyapandisha juu kutoka katika vitu vya kidunia na vya muda kwenda kwa vitu vya mbinguni vya kudumu. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 818, 819. [TA 219;3; UM Aya ya 51]

Kwa siku arobaini Kristo alidumu kuwa duniani, akiwaandaa wanafunzi kwa ajili ya kazi iliyokuwa mbele yao na kueleza kile ambacho hapo kabla hawakuweza kukielewa. Alinena juu ya unabii kuhusiana na ujio Wake wa

kwanza, kukataliwa na wayahudi, na kifo Chake, akionyesha kuwa kila bayana ya unabii huu ilikuwa imetimizwa. Aliwaambia kwamba walipaswa kuuchukulia utimizo huu kama hakikisho la uweza ambao ungefuatana nao katika kazi zao za siku za usoni. E. G. White, Matendo ya Mitume, uk. 26. [TA 219.4; UM Aya ya 52]

**Kuonekana Kwa Kristo Mara Ya Mwisho Katika Kupaa Kwake.**

Wakati ulikuwa umewadia wa Kristo kupaa kwenda kwenye kiti cha enzi cha Baba Yake...Kama mahali pa kupaa Kwake, Yesu alichagua sehemu ambayo mara kwa mara ilitukuzwa kwa uwepo Wake... Mlima wa Mizeituni... [TA 220.1; UM Aya ya 53]

Sasa akiwa pamoja na wale wanafunzi wake kumi na mmoja Yesu alishika njia kwenda kwenye mlima huo. Walipopita katika lango la Yerusalemu, macho mengi ya watu wanaoshangaa yalikiangalia kile kikundi kidogo, kilichokuwa kinaongozwa na Yeye ambaye majuma machache tu yaliyokuwa yamepita alikuwa amehukumiwa na wakuu na kusulibishwa... Walipofika kwenye Mlima wa Mizeituni, Yesu aliongoza njia na kukipita kilele cha mlima ule, mpaka maeneo jirani na Bethania. Hapo alisimama kidogo, na wanafunzi wakakusanyika kwake. Miale ya nuru ilionekana kuangaza kutoka kwake kadiri alivyowatazama kwa upendo... Kwa mikono iliyokunjuliwa kuwabariki, na kama vile ni namna ya kuwahakikishia utunzaji na ulinzi wake, aliinuliwa taratibu kutoka miongoni mwao, akivutwa kwenda mbinguni kwa nguvu kubwa zaidi kuliko kani yoyote ya mvutano ya duniani. Kadiri alivyoondoka kwenda juu, wale wanafunzi waliopigwa butwaa walitazama kwa macho yaliyokazwa ili kuona hatua ya mwisho ya Bwana wao anayepaa. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 829-831. [TA 220.2; UM Aya ya 54]

Yesu alipopaa toka Mlima wa Mizeituni, si wanafunzi tu wachache waliomwona, bali wengi walikuwa wakitazama. Kulikuwa na wingi wa malaika, maelfu kwa maelfu waliomtazama Mwana wa Mungu akiwa anapaa kuelekea juu. The Ellen G. White 1888 Materials, 127.2. [TA 220.3; UM Aya ya 55]

Wanafunzi wakiwa bado wamekaza macho juu, zilisikika sauti kama wimbo mtamu zilizungumza nao. Waligeuka, wakaona malaika wawili wakiwa katika mwonekano wa wanadamu, ambao walizungumza nao, wakisema, “Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni.” [TA 221.1; UM Aya ya 56]

Malaika hawa walikuwa wa kundi lile lililokuwa linasubiri katika wingu ling’aalo ili kumsindikiza Yesu kwenda nyumbani kule mbinguni. Ni malaika walioinuliwa zaidi kuliko jeshi lote la malaika, na ni wale wawili waliokuwa wamekuja mahali pa kaburi wakati wa kufufuka kwa Kristo, na walikuwa

pamoja naye katika maisha yake yote ya duniani. E. G. White, Tumaini la Vizazi Vyote, uk. 831, 832. [TA 221.2; UM Aya ya 57]

Kristo alichukuliwa juu mbinguni katika wingu lenye malaika walio hai. E. G. White, Manuscript Releases 17:2. [TA 221.3; UM Aya ya 58]

Gari la malaika lilipokuwa limempokea, maneno Yake yaliwajia wanafunzi, "Tazama, niko pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." E. G. White, Matendo ya Mitume, uk. 65. [TA 221.4; UM Aya ya 59]

Maelfu na maelfu ya malaika walimsindikiza Kristo kwa heshima kuelekea katika mji wa Mungu, wakiimba, "Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Inukeni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia." Kwa furaha walinzi wa malango wanaitikia, wakisema, "Ni nani Mfalme wa utukufu?" E. G. White, The Review and Herald, July 29, 1890. [TA 221.5; UM Aya ya 60]

Kristo akiwa anakaribia kwenye Mji wa Mungu...sauti za maelfu ya malaika ziliinuliwa juu na malaika wakuu wakaimba, "Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Inukeni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia." [TA 222.1; UM Aya ya 61]

Halafu kunaibuka mwitikio, "Ni nani Mfalme wa utukufu?" na malaika wasindikizi wanajibu, "Bwana wa majeshi, Yeye ndiye Mfalme wa utukufu," (Zaburi 24:7-10) na gari la kimbingu linapita malangoni. E. G. White, The Review and Herald, July 29, 1890. [TA 222.2; UM Aya ya 62]

Kristo alipopaa juu, na akiwa na malimbuko wengi, akiwa anasindikizwa na jeshi la mbinguni, na kupokelewa malangoni pa mji...alikuwa na umbo lile lile tukufu alilokuwa nalo kabla ya kuja duniani kumfia mwanadamu. E. G. White, Karama za Roho, juzuu ya 4a, uk. 119. [TA 222.3; UM Aya ya 63]

**Kristo Anasindikizwa Mahali Alipo Baba.**

Mna kiti cha enzi, na kukizunguka ni upinde wa mvua wa ahadi. Mna maserafi na makerubi. Malaika wakimzunguka, na sasa Kristo anawapungia mkono akiwaacha. Anaingia kwenye uwepo wa Baba Yake. Anawaonyesha wale aliowashindia mauti—wale waliofufuka pamoja Naye, wawakilishi wa mateka wa mauti ambao watatoka makaburini mwao pale parapanda itakapolia. Anamkaribia Baba, na...anasema: Baba, imekwisha. Nimeyafanya mapenzi Yako, Ee Mungu wangu. Nimeikamilisha kazi ya ukombozi. Ikiwa haki yako imeridhika, "Baba, hao ulionipa nataka wawe pamoja nami po pote nilipo." E. G. White, The Youth's Instructor, August 11, 1898. [TA 222.4; UM Aya ya 64]

Mikono ya Baba inamkumbatia Mwana, na sauti Yake inasikika, ikisema, "Na wamsujudu malaika wote wa Mungu." E. G. White, Selected Messages, juzuu ya 1, uk. 306. [TA 223.1; UM Aya ya 65]

Umati wa malaika...wanasujudu kwa heshima mbele Yake, wakisema, “Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, na aishi tena, na kushinda zaidi ya kushinda.” E. G. White, The Signs of the Times, June 17, 1889. [TA 223.2; UM Aya ya 66]

Kristo alipopita katika malango ya mbinguni, alitukuzwa katikati ya kuabudiwa na malaika. Mara tu karamu ilipokwisha, Roho Mtakatifu alishuka kwa wanafunzi katika uvumi mwingi, na Kristo alitukuzwa kweli kweli, kwa utukufu ule ule ambao alikuwa nao alipokuwa pamoja na Baba tangu milele. Mmiminiko wa Kipentekoste ilikuwa ni habari ya mbingu kwamba kutawazwa kwa Mkombozi kulikuwa kumekamilika. Kwa mujibu wa ahadi Yake alimtuma Roho Mtakatifu toka mbinguni kwenda kwa wafuasi Wake, kama ishara kwamba kama Kuhani na Mfalme, amepokea mamlaka mbinguni na duniani, na alikuwa Mtiwa mafuta juu ya watu Wake. E. G. White, Matendo ya Mitume, uk. 38. [TA 223.3; UM Aya ya 67]

## SURA YA 18

## MALAIKA TANGU PENTEKOSTE HADI SIKU ZA MWISHO

### Malaika Hulinda Kweli za Thamani za Biblia

Niliona malaika wa Mungu wakiagizwa kulinda kwa uangalizi/umakini wa kipekee zile Kweli takatifu, Kweli muhimu ambazo zingetumika kama nanga kwa wanafunzi wa Kristo katika kila kizazi. Roho Mtakatifu aliweka juu ya mitume waliokuwa mashahidi wa Kusulubishwa kwa Bwana wetu, ufufuo, na kupaa Kwake—Kweli zile muhimu ambayo zingekuwa tumaini la Israeli. Wote walipaswa kumwangalia Mwokozi wa ulimwengu kama tumaini lao la pekee, na kutembea katika njia aliyokuwa ameifungua kwa dhabihu ya maisha Yake Mwenyewe, na kuishika sheria ya Mungu na wapate kuishi. Niliona hekima na wema wa Yesu katika kuwapa nguvu wanafunzi kuendelea na kazi ile ile ambayo Yeye alikuwa amechukiwa kwayo na kuuawa na Wayahudi. Kwa Jina Lake walikuwa na uwezo juu ya kazi za Shetani. Mwangaza wa nuru na utukufu mahsusi ulikita na kuzungia matukio ya wakati wa kifo na ufufuo Yesu, na kuufanya Ukweli huo mtakatifu kusisitizwa, yaani YEYE Ndiye Mwokozi wa ulimwengu.— Early Writings, 196, 197. [TA 224.1; UM Aya ya 1]

### Petro na Yohana Watolewa Gerezani

Muda mfupi baada ya kushuka kwa Roho Mtakatifu, na mara tu baada ya muda wa kuomba kwa bidii, Petro na Yohana walikuwa wakipanda kwenda hekaluni la kuabudu, wakamwona mlemavu masikini mwenye huzuni, nao wakamwonea huruma. “Na Petro, akimkazia macho yake kumtazama pamoja na Yohana, akasema, Tutazame. “Mimi sina fedha wala dhahabu; lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama, utembee.”— The Spirit of Prophecy 3:275, 276. [TA 225.1; UM Aya ya 2]

Masadukayo, ambao hawakuamini ufufuo, waliposikia mitume wakitangaza kwamba Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, walikasirika, wakitambua kwamba ikiwa mitume wangeruhusiwa kuhubiri ufufuo wa Mwokozi, na kutenda miujiza katika Jina Lake, basi fundisho lao la kuwa hakutakuwa na ufufuo litakataliwa na wote, na madhehebu ya hawa Masadukayo yangetoweka punde.— Acts of Apostles, 78. [TA 225.2; UM Aya ya 3]

Baadhi ya viongozi wa Hekalu na akida wa Hekalu walikuweko Masadukayo. Akida, kwa msaada wa idadi ya Masadukayo, wakawakamata wale mitume wawili, na kuwaweka gerezani kwani walikuwa wamechelewa sana kesi zao kusikilizwa usiku huo.—The Spirit of Prophecy 3:278. [TA 225.3; UM Aya ya 4]

Shetani alishinda, na malaika waovu wakashangilia; bali malaika wa Mungu walitumwa na kufungua milango ya gereza, na, kinyume na amri ya kuhani mkuu na wazee, akawaamuru waingie ndani ya hekalu; na kunena Maneno yote ya uzima huu.— Spiritual Gifts 1:83, 84. [TA 225.4; UM Aya ya 5]

Wakati huohuo kuhani mkuu na wale waliokuwa pamoja naye "wakaita baraza pamoja, na baraza lote la wana wa Israeli." Makuhani na wakuu walikuwa wameamua kuweka juu ya wanafunzi shtaka la uasi, kuwashtaki kwa kuwaua Anania na Safira; na kupanga njama ya kuwanyima makuhani mamlaka yao. [TA 226.1; UM Aya ya 6]

Walipotuma wafungwa waletwe mbele yao, walistaajabishwa sana na neno lililorudishwa, kwamba milango ya gereza ambayo ilikuwa imefungwa na makomeo vyema kwa ajili ya kuhakikisha usalama na ulinzi, na kisha walinzi wakasimama mbele ya mlango, sasa wafungwa hawakuwa ndani. [TA 226.2; UM Aya ya 7]

Punde taarifa ya kustaajabisha ikaja, "Tazameni, watu wale mliowaweka gerezani wako ndani ya hekalu, wamesimama na kuwafundisha watu. Ndipo yule jemedari akaenda pamoja na watumishi, wakawaleta si kwa nguvu; kwa maana waliwaogopa watu, wasije wakawapiga kwa mawe." [TA 226.3; UM Aya ya 8]

Petro na Yohana walipokuwa wamesimama kwa mara ya pili mbele ya Baraza watu ambao walionekana kuwakandamizwa kwa sababu ya mateso kutoka kwao, sasa walikuwa hawana hofu wala kusitasita hakukutambuliwa katika maneno wala mtazamo wao. Na kuhani mkuu akasema, "Je, hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu msifundishe kwa Jina hili? Nanyi tazameni, mmeijaza Yerusalemu mafundisho yenu, na mnataka kuileta damu ya mtu yule juu yetu," Petro akajibu, "Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu." Alikuwa ni Malaika kutoka mbinguni ambaye aliwatoa gerezani na kuwaamuru wafundishe hekaluni.— Acts of Apostles, 78-82. [TA 226.4; UM Aya ya 9]

Kisha wale wauaji walikasirika. Walitamani kuijaza mikono yao kwa damu tena kwa kuwaua mitume. Walikuwa wanapanga jinsi ya kufanya hivyo, wakati malaika kutoka kwa Mungu alipotumwa kwa Gamalieli kumsukuma moyonu mwake kuwashauri wakuu wa makuhani na wakuu. Gamalieli akasema, Jiepusheni na watu hawa, waacheni; kwa kuwa shauri hili au kazi hii iliwa imetoka kwa wanadamu, itavunjwa; lakini ikiwa imetoka kwa Mungu hamwezi kuivunja; msije mkaonekana mnapigana na Mungu. [TA 226.4; UM Aya ya 10]

Malaika wabaya walikuwa wanatembea juu ya makuhani na wazee kuwasukuma ili wawaue wale mitume; lakini Mungu alimtuma malaika Wake naye akalizuia hilo, kwa kuinua sauti kuwafadhili wanafunzi katika nyadhifa zao wenyewe (wakuu).— Spiritual Gifts 1:85. [TA 227.1; UM Aya ya 11]

### Filipo na Towashi Mkushi

Malaika wa mbinguni huwatazama wale wanaotafuta kupata nuru. Wanashirikiana na wale wanaojaribu kuleta roho kwa Kristo. Malaika kuwahudumia wale ambao watakuwa warithi wa wokovu. Hili linaoneshwa katika maisha ya Filipo na Mkushi.— The Bible Echo, December 10, 1900. [TA 227.2; UM Aya ya 12]

Mkushi/Methiopia huyu alikuwa mtu mwenye msimamo mzuri, cheo kizuri na ushawishi mkubwa. Mungu aliona kuwa akiongoka atawapa wengine nuru aliyokuwa aliyoipokea na kutoa ushawishi mkubwa kwa faida ya injili. Malaika wa Mungu walikuwa wakimtembelea kwa mtafutaji huyu wa nuru, naye alikuwa akivutwa kwa Mwokozi. Kwa huduma ya Roho Mtakatifu Bwana alimleta kukutana na mtu ambaye angemwongoza hadi kwenye nuru.—Conflict and Courage, 332. [TA 227.2; UM Aya ya 13]

Mungu alipomwonyesha Filipo kazi yake, ... alijifunza kuwa kila nafsi ina thamani mbele za Mungu, na Malaika watawapeleka mawakala walioteuliwa nuru kwa wale wanaoitafuta. Malaika wa mbinguni hawaibebi kazi ya kuhubiri injili*. Ni kwa kupitia huduma ya malaika ndiyo Mungu hutuma nuru kwa watu Wake, na kupitia watu Wake nuru hii itatolewa kwa ulimwengu.— The Bible Echo, December 10, 1900. (Ni kweli malaika ni wajumbe. Lakini, wao hutumwa kuleta nuru kwangu au kwako, wao ni mawakala, hawaendi kuinjilisha au kufanya uinjilisti....Malaika wanapeleka nuru kwa wakala, kisha wakala(mwanadamu) hupeleka nuru hiyo kwa ulimwengu. Hebu nuru hii ikufanye eh Mwanadamu kuwajibika, nami pia, Bwana atusaidie). [TA 227.4; UM Aya ya 14]

### Wongofu wa Paulo

Sauli alipokuwa akisafiri kwenda Dameski, akiwa na barua za kumruhusu kuwachukua wanaume au wanawake waliokuwa wakimhubiri Yesu na kuwaleta wakiwa amefungwa mpaka Yerusalemu, malaika waovu walifurahi kumzunguka. Lakini ghafla nuru kutoka mbinguni ikamwangazia pande zote, iliyofanya malaika uovu kukimbia.— Early Writings, 200. [TA 228.1; UM Aya ya 15]

Katika kumbukumbu ya wongofu wa Sauli, tumepewa kanuni muhimu ni, ambazo tunapaswa kuzikumbuka kila wakati. Sauli aliletwa moja kwa moja

katika uwepo wa Kristo....Alimkamata katika safari yake na kumsadikisha juu ya dhambi; lakini Sauli alipouliza, “Unataka nifanye nini?” Mwokozi alimweka Myahudi huyu aliyekuwa akiuliza katika muunganiko na Kanisa Lake, ili kupata ujuzi wa mapenzi ya Mungu kumhusu yeye. [TA 228.2; UM Aya ya 16]

Wakati Sauli akiwa peke yake katika nyumba ya Yuda aliendelea katika maombi na dua, Bwana akatokea katika maono kwa “mwanafunzi fulani huko Dameski, jina lake Anania,” akimwambia kwamba Sauli wa Tarso alikuwa akiomba, na kuhitaji msaada. “Simama, uende kwenye njia iitwayo Nyofu,” mjumbe wa mbinguni alisema, “na ukaulize katika nyumba ya Yuda mtu aitwaye Sauli, wa Tarso; kwa maana analia akiomba. [TA 228.3; UM Aya ya 17]

Anania hakuweza kuamini Maneno ya malaika; kwani taarifa za mateso makali ya Sauli kwa watakatifu huko Yerusalemu zilikuwa zimeenea sana na mbali. [TA 228.4; UM Aya ya 18]

Kwa kutii maagizo ya malaika, Anania akamtafuta mtu ambaye hivi karibuni alitoa vitisho dhidi ya wote ambao waliliamini Jina la Yesu; na kuweka mikono yake juu ya kichwa cha yeye aliyetubu, akisema, “Ndugu Sauli, Bwana, Yesu, aliyekutokea katika njia uliyoijia, amenituma, upate kuona tena, ukajazwe Roho Mtakatifu. [TA 229.1; UM Aya ya 19]

“Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama, akabatizwa.”— The Acts of Apostles, 120-122. [TA 229.2; UM Aya ya 20]

### Paulo Aondoka Dameski

Paulo alipokuwa akimhubiri Kristo huko Dameski, wote waliomsikia walikuwa wakishangaa....Upinzani ulikua mkali sana hata Paulo hakuruhusiwa kuendelea na kazi yake huko Dameski. Mjumbe kutoka mbinguni akasema aondoke kwa muda; naye “akaingia Arabuni” (Wagalatia 1:17). ambapo alitoka kwenye nyanja ya adui na kupata mahali patulivu kutafakari na kupata matengenezo (miaka mitatu). [TA 229.3; UM Aya ya 21]

Hapa, katika upweke wa jangwa, Paulo alikuwa na nafasi ya kutosha ya kusoma kwa utulivu na kutafakari Yesu alizungumza naye, na akamtia nguvu katika imani, akimpa kiasi kikubwa cha hekima na neema.— Acts of Apotles, 124-126. [TA 229.4; UM Aya ya 22]

Kazi ya Paulo huko Antiokia, akishirikiana na Barnaba, ilimtia nguvu katika kusadiki kwamba Bwana alikuwa amemwita afanye kazi maalum kwenye ulimwengu wa watu wa mataifa. Wakati wa kuongoka kwa Paulo, Bwana alikuwa ametangaza kwamba angefanywa kuwa mhudumu wa Mataifa, “kuyafumbua macho yao, na kuwageuza kutoka gizani na kuilekea nuru; waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu, kisha wapate msamaha

wa dhambi, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo Kwangu Mimi.” Matendo 26:18. Malaika aliyemtokea Anania, alikuwa amesema juu ya Paulo, “Yeye ni chombo kiteule Kwangu alichukue Jina Langu mbele ya mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli.” Matendo 9:15. Na Paulo mwenyewe, baadaye katika uzoefu wake wa Kikristo, wakati akisali katika hekalu la Yerusalemu, alikuwa ametembelewa na Malaika kutoka mbinguni, aliyemwambia, “Enenda zako, kwa maana Mimi nitakutuma uende mbali kwa watu wa Mataifa.” Matendo 22:21.— Acts of Apostles, 159. [TA 229.5; UM Aya ya 23]

### Kornelio na Petro

Mlinzi Mtakatifu Yule Yule aliyesema juu ya Ibrahimu, “Namjua yeye” alimjua Kornelio pia, na akatuma ujumbe moja kwa moja kutoka mbinguni kwenda kwake.— Acts of Apostles, 133. [TA 230.1; UM Aya ya 24]

Malaika alimtokea Kornelio alipokuwa kwenye maombi. Akida aliposikia akiitwa kwa jina lake, aliogopa, lakini yeye alijua kwamba mjumbe huyo ametoka kwa Mungu, naye akasema, “kuna nini, Bwana?”— The Acts of the Apostles, 133. [TA 230.2; UM Aya ya 25]

“Tuma watu wamwite mtu mmoja aitwaye Simoni, jina jingine Petro pamoja na Simoni mtengeneza ngozi. Naye akamwambia mahali pale pale Simoni mtengenezaji wa Ngozi alipoishi. Kisha malaika wa Bwana akamwendea Petro, na akiitayarisha akili yake kwa ajili ya kuwapokea watu hao.— The Ellen G. White 1888 Materials, 1746. [TA 230.3; UM Aya ya 26]

Kornelio alitii kwa furaha maono hayo. Wakati Malaika alipoondoka aliwaita “watumishi wake wawili wa nyumbani, na askari mmoja ,mtu mtauwa katika wale waliomhudumia daima; na alipokwisha kuwaeleza yote, akawatuma kwenda Yafa.”…..Malaika hakuagizwa kumwambia Kornelio kisa cha msalaba. Mwanadamu kama akida mwenyewe, mwenye udhaifu wa kibinadamu na majaribu ndiye alikuwa wa kumwambia juu ya Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. Kwake hekima Bwana huwaleta wale wanaoutafuta ukweli kuwasiliana pamoja na viumbe wenzao wanaojua Ukweli.— The Review and Herald,April 6, 1911. [TA 231.1; UM Aya ya 27]

Mara tu baada ya mahojiano na Kornelio, malaika akaenda kwa Petro, ambaye wakati huo alikuwa akisali juu ya dari ya nyumba yake aliyokuwa akikaa katika Yopa.— The Review and Herald, April 13, 1911. [TA 231.2; UM Aya ya 28]

Ilikuwa ni kwa kusitasita kwa kila hatua Petro alilichukua jukumu hilo lililowekwa juu yake kwa amri ya Bwana. Akisimulia uzoefu wake huo, yeye haitetei hatua yake kwa kanuni za jumla, lakini kama utofauti, lilifanyika kwa sababu ya ufunuo wa kimbingu. Na matokeo yake yalikuwa ya kumshangaza.

Kornelio alipomsimulia uzoefu wake, na Maneno ya malaika aliyemtokea katika maono, Petro alisema, “Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo; bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki; hukubaliwa Naye.”— Manuscript Releases 6:328, 329. [TA 231.3; UM Aya ya 29]

### Petro Atolewa Gerezani

Siku ya kuuawa kwa Petro hatimaye iliwekwa; lakini bado maombi ya waumini yalipaa Mbinguni. Na wakati nguvu zao zote na huruma zikiwa ni kusihi kwa bidii, Malaika wa Mungu walikuwa wakimlinda mtume aliyekuwa gerezani….Petro aliwekwa kati ya askari wawili, na kufungwa kwa minyororo miwili, kila minyororo ukiwa umefungwa kwenye kifundo cha kiganja cha mkono wa mmoja wa walinzi wake. Kwa hiyo walikuwa hawawezi kusogea bila wao kujua. Milango ya gereza ilikuwa imefungwa vizuri, na ulinzi mkali ukawekwa mbele yake. Nafasi zote za kujiokoa au kuponyoka, kwa njia za kibinadamu, zilizuiwa.— Redemption;au the Ministry of Peter and the Conversion of Saul, 70. [TA 231.4; UM Aya ya 30]

Petro alikuwa gerezani, akitarajia kutolewa nje siku ya pili auwawe; alikuwa amelala usiku “kati ya askari wawili, amefungwa minyororo miwili; na walinzi mbele ya mlango wakilinda gereza. Mara, malaika wa Bwana akasimama karibu naye, nuru ikamulika mule chumbani, akampiga Petro ubavuni, akamwamsha; akisema, Ondoka upesi,na minyororo yake ikamwanguka mikononi.” [TA 232.1; UM Aya ya 31]

Petro, ghafla aliamka, naye akashangazwa na mwangaza huo uliofurika shimo lake la kifungo, na uzuri wa mbinguni na mjumbe wa mbinguni. Hakuelewa tukio hilo, lakini alijua kuwa alikuwa huru, na katika fadhaa yake, kuchanganyikwa na furaha, yeye angetoka nje ya gereza bila kulindwa na hali ya hewa na baridi ya usiku. Malaika wa Mungu, akibainisha hali zote, alisema, kwa huruma juu ya hitaji la mtume: “Jifunge, kavae viatu vyako.” [TA 232.2; UM Aya ya 32]

Petro alitii bila kuyaweka mawazo yake kwenye hilo sana; kwani alifurahishwa sana na njozi za mafunuo ya utukufu toka mbinguni hivyo kwamba hakufikiria kuchukua koti lake. Kisha malaika akamwambia: “Jivike nguo yako, ukanifuate. Akatoka nje, akamfuata; na hakujua kuwa ni kweli yaliyofanywa na malaika; bali alidhani kwamba anaona maono. Walipopita lindo la kwanza na la pili, wakafika lango la chuma la kuingilia mjini; likawafungukia lenyewe.”— Testimonies for the Church 5:748. [TA 232.3; UM Aya ya 33]

Hakuna neno linalosemwa kati yao; hakuna sauti za nyayo. Malaika yuko mbele yake, akizungukwa na mwanga unaong’aa, na Petro, akiwa amechanganyikiwa, na bado akiamini kuwa yuko katika ndoto, anamfuata

mkombozi wake. Na ndivyo walivyopita katika njia moja, na kisha, utume wa malaika ulikamilika, naye anatoweka ghafla. [TA 233.1; UM Aya ya 34]

Nuru ya mbinguni ikafifia, na Petro akajihisi kuwa katika giza kuu; lakini macho yake yalipoanza kulizoea giza lile, taratibu likaonekana kupungua, naye akajikuta yuko peke yake ndani ya lile giza. Kulikuwa na ukimya mitaani, na hewa ya ubaridi wa usiku ukavuma juu ya paji la uso wake. Sasa alitambua kwamba alikuwa huru, katika sehemu ya mji anayoijua; alitambua mahali alipopazoea mara nyingi, na alitarajia apite hapo keshoye kwa mara ya mwisho….[TA 233.2; UM Aya ya 35]

Mtume alishika njia mara moja hadi kwenye nyumba ambayo ndugu zake walikusanyika, nao wakati huo walikuwa wakishiriki maombi ya bidii kwa ajili yake. "Petro alipobisha kilango kwenye lango (geti), kijakazi, jina lake Roda, alikuja kusikiliza. Na alipotambua ni sauti ya Petro, hakufungua lango kwa ajili ya furaha, bali alipiga mbio, akaingia ndani akawaambia kwamba Petro anasimama mbele ya lango. Wakamwambia, Una wazimu. Lakini yeye akakaza sana, akasema ya kwamba ndivyo hivyo. Wakasema, ni malaika wake."— The Acts of the Apostles, 147, 148. [TA 233.3; UM Aya ya 36]

Malaika yule yule ambaye alikuwa ametoka katika nyua za kifalme za mbinguni ili kumwokoa Petro kutoka katika nguvu za mtesaji wake, alikuwa mjumbe wa ghadhabu na hukumu kwa Herode. Malaika alimpiga Petro ili aamke kutoka usingizini; lakini ni kwa kipigo tofauti yeye alimpiga yule mfalme mwovu Herode, akileta ugonjwa wa kufa juu yake.—The Spirit of Prophecy 3:344. [TA 234.1; UM Aya ya 37]

### Kupigwa Mawe kwa Stefano

Stefano alipokuwa akitazama juu mbinguni, akapewa maono ya utukufu wa Mungu, na malaika wakamzunguka. Naye akapaza sauti, Tazama!, Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu.— Spiritual Gifts 1:89. [TA 234.2; UM Aya ya 38]

### Malaika Wakati wa Huduma ya Paulo

Biashara kubwa na yenye faida ilikuwa imekuzwa huko Efeso kutoka na utengenezaji na uuzaji wa vihekalu vidogo na picha, zilizowekwa mfano wa hekalu na sanamu ya Diana (mungu wa waatermi). Wale waliopenda hii biashara waliona faida zao zikipungua, na wote wakaungana mkono katika katika kuona kwamba mabadiliko yametokana na kazi ya Paulo. [TA 234.3; UM Aya ya 39]

"Mji wote ukajaa ghasia." Wakamtafuta Paulo, lakini mtume hakupatikana. Ndugu zake, wakipokea taarifa ya hatari, wakaharakisha kumtoa mahali pale. Malaika ya Mungu walikuwa wametumwa kumlinda mtume; wakati wake wa

kufa kifo cha shahidi ulikuwa bado haujafika.— The Acts of the Apostles, 292, 293. [TA 234.4; UM Aya ya 40]

Siku baada ya siku, Paulo na Sila walipokuwa wakienda kwenye ibada zao huko Filipi, mwanamke mmoja mwenye pepo wa uaguzi akawafuata, akilia, "Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kuwahubiria njia ya wokovu." Mwanamke huyu alikuwa wakala mahsusi wa Shetani; na kama vile pepo walivyotaabishwa na kuwapo kwake Kristo, ndivyo pepo mchafu aliyekuwa amemshika alikuwa hana raha mbele yao mitume. Shetani alijua kwamba ufalme wake ulikuwa umevamiwa, na akatumia njia hii ya kupinga kazi ya watumishi wa Mungu. Maneno ya sifa na ya kuwatambulisha yaliyotamkwa na mwanamke huyu yalisababisha maumivu katika kazi ya Mungu, na hata kuvuruga akili za watu kutoka kwenye zile Kweli zinazowasilishwa kwao, na kutupa sifa mbaya juu ya kazi hiyo kwa kusababisha watu kuamini kwamba watu walionena kwa Roho na nguvu za Mungu walichochewa na roho ile ile kama ya yule mwananamke aliyekuwa mjumbe wa Shetani. [TA 235.1; UM Aya ya 41]

Mitume walivumilia upinzani huu kwa siku kadhaa; kisha Paulo, chini ya uvuvio wa Roho wa Mungu, aliamuru pepo mchafu amtoke huyu mwanamke. Hivyo Shetani akapatikana na kukemewa. Ukimya wa haraka na kuendelea kukaa kimya kwa mwanamke huyo kulishuhudia kwamba mitume walikuwa watumishi wa Mungu, na kwamba pepo amewakiri kuwa hivyo, na alikuwa ametii amri yao. Mwanamke alipoondolewa roho ya ibilisi, na kurejeshwa katika hali yake, mabwana zake walikuwa na wasiwasi ya biashara yao. Waliona kwamba matumaini yote ya kupokea fedha kutoka kwa uaguzi na uganga wake yalikuwa katika mwisho, na kutambua kwamba, kama mitume wangeruhusiwa kuendelea na kazi zao, chanzo chao cha mapato kingetokomea/kingeondolewa mbali.—Sketches From the Life of Paul, 74, 75. [TA 235.2; UM Aya ya 42]

Baada ya yule mwanamke kuachiliwa kutoka kwa pepo mchafu, akawa mfuasi wa Kristo. Mabwana zake waliona kwamba tumaini lao la kupata faida lilikuwa limetoweka, wakawakamata Paulo na Sila, wakawapeleka mbele ya wakuu; kuwashtaki kwa kuuchafua mji. Hii ilizua taharuki. Umati ukawashambulia wanafunzi, na makadhi wakaamuru kwamba wafungwa wanapaswa kupigwa kwa bakora.— The Review and Herald, June 29, 1905. [TA 236.1; UM Aya ya 43]

Makadhi walipokwisha kuwapiga mapigo mengi Paulo na Sila, wakawatupa gerezani, wakimwamuru mlinzi wa gereza awalinde sana salama, naye akiisha kupokea amri hiyo akawatupa katika chumba cha ndani,akawafunga miguu yao kwa mkatale. Lakini malaika wa Mungu waliandamana nao hadi ndani ya kuta za gereza.— Spiritual Gifts 1:95, 96. [TA 236.2; UM Aya ya 44]

Mitume waliteswa sana kwa sababu ya maumivu nafasi ambayo waliwekwa, lakini hawakunung'unika. Badala yake, katika giza tupu na ukiwa wa shimo, walitiana moyo kila mmoja kwa mwenzake kwa maneno ya sala, na kumwimbia Mungu sifa kwa sababu wao walistahili kuaibishwa kwa ajili Yake Kwa mshangao wafungwa wengine walisikia sauti ya maombi na kuimba kutoka gereza la ndani.— Acts of Apostles, 213, 214. [TA 236.3; UM Aya ya 45]

Wakati watu waliokuwa wakatili na wenye kulipiza kisasi, au wakosaji wazembe wa majukumu mazito yanayowahusu, Mungu hakuwa amesahau kuwahurumia watumishi wake wanaoteseka. Malaika alitumwa kutoka mbinguni ili kuwafungua mitume. Alipokaribia gereza la Kirumi, nchi ikatetemeka chini ya miguu yake, mji wote ukatikisika kwa tetemeko la nchi, na kuta za gereza ziliyumba-yumba kama mwanzi katika upepo. Milango iliyofungwa sana ilifunguka; minyororo na pingu zilianguka kutoka mikononi na miguuni pa kila mfungwa.—The Spirit of Prophecy 3:382;383. [TA 236.4; UM Aya ya 46]

Mtume Paulo, katika kazi yake huko Efeso, alipewa ishara maalum za neema ya Mungu. Nguvu za Mungu ziliambatana na juhudi zake, na wengi waliponywa magonjwa ya kimwili. “Mungu akafanya kwa mikono ya Paulo miujiza ya kupita kawaida, hata wagonjwa wakaletewa leso na nguo zilizotoka mwilini mwake, magonjwa yao yakawaondokea, na pepo wachafu wakawatoka.” [TA 237.1; UM Aya ya 47]

Udhihirisho huu wa nguvu zisizo za kawaida ukawa na nguvu zaidi kuliko ilivyowahi kushuhudiwa huko Efeso, na ulikuwa wa namna ile ambayo haikuweza kuigwa na ujuzi wa mazingaombwe au uchawi ule watu walioutumia kuroga watu. Miujiza hii ilipofanyika kwa Jina la Yesu wa Nazareti, watu walipata nafasi ya kuona kwamba Mungu wa mbinguni alikuwa na nguvu zaidi kuliko wachawi ambao waliokuwa waabudu wa mungu wa kike Diana. Ndivyo Bwana alivyomtukuza mtumishi Wake, hata mbele ya waabudu masanamu wenyewe, juu isivyo na kipimo ya wenye nguvu zaidi na kati ya wachawi waliopendwa zaidi. ” [TA 237.2; UM Aya ya 48]

Lakini Yule ambaye pepo wote wabaya wanamtii na ambaye alikuwa amewapa watumishi Wake mamlaka juu yao, alikuwa karibu kuleta aibu kubwa zaidi na kushindwa kwa wale waliodharau na kulikufuru Jina Lake takatifu. Uchawi ulikuwa umekatazwa na sheria ya Musa, kwa kupigwa hadi kifo, lakini mara kwa mara ulikuwa ukifanywa kwa siri na Wayahudi walioasi. Wakati wa ziara ya Paulo huko Efeso, palikuweko katika jiji hilo “baadhi ya Wayahudi wenye kutanga-tanga, nao ni wapunga pepo,” ambao, waliona maajabu aliyoyafanya Paulo, “wakajaribu kutaja Jina la Bwana Yesu juu yao waliopagawa na pepo wachafu.” Jaribio lilifanywa na “wana saba wa mtu mmoja aitwaye Skewa, Myahudi, kuhani mkuu.” Walipompata mtu aliyepagawa

na pepo, wakamwambia, “Tunakuapisha kwa Yesu Yule anayehubiriwa na Paulo.” Lakini "yule pepo mchafu akawajibu, akawaambia, Yesu namjua, na Paulo namfahamu; lakini ninyi ni nani? Yule mtu aliyekuwa na pepo mchafu akawarukia akawaweza, akawashinda, hata wakatoka mbio katika nyumba ile wa uchi na kujeruhiwa.”…… [TA 237.3; UM Aya ya 49]

Mambo ambayo hapo awali yalikuwa yamefichwa sasa yaliletwa nuruni. Katika kuukubali Ukristo baadhi ya waumini hawakuwa wameachana kikamilifu na ushirikina wao. Kwa kiasi fulani bado waliendelea kufanya uchawi. Sasa, wakiwa wamesadikishwa na kosa lao, “wengi wa wale walioamini wakaja, wakaungama, wakidhihirisha matendo yao.” Hata kwa baadhi ya wachawi wenyewe kazi nzuri iliendelezwa; na “wengi katika wale waliotumia mambo ya uganga wakakusanya vitabu vyao, na wakavichoma moto mbele ya watu wote.” …… [TA 238.1; UM Aya ya 50]

Maandishi haya ya uaguzi yalikuwa na kanuni na namna za kuwasiliana na pepo wabaya. Zilikuwa kanuni za sheria- za ibada ya Shetani—maelekezo ya kuomba msaada wake na kupata habari kutoka kwake.— Acts of Apostles, 286 -289. [TA 238.2; UM Aya ya 51]

Taarifa ya hotuba ya Demetrio ilisambazwa haraka. Ghasia ilikuwa kali. Mji mzima wa Efeso ulionekana kuwa katika ghasia. Umati mkubwa ulikusanyika haraka, na wakafanya haraka kwenda katika karakana ya Akila, katika maeneo ya Wayahudi, kwa lengo la kumtafuta Paulo. Kwa hasira zao za wendawazimu/kichaa walikuwa tayari kumrarua vipande vipande. Lakini mtume hakupatikana. Ndugu zake, wakipokea taarifa ya hatari, walifanya haraka kumwondoa. Malaika ya Mungu alitumwa kumlinda mtume huyo mwaminifu.— Sketches from the Life of Paul, 143. [TA 238.3; UM Aya ya 52]

Makuhani wakuu na watawala waliposhuhudia matokeo kuhusiana na huo uzoefu wa Paulo, walichochewa na chuki dhidi yake. Waliona kwamba alimhubiri Yesu kwa ujasiri na kufanya miujiza kwa Jina Lake, kwamba watu wengi walimsikiliza na kuziacha mila zao na waliwatazama viongozi wa Kiyahudi kama wauaji wa Mwana wa Mungu. Hasira zao zikawaka, nao wakakusanyika ili kushauriana ni nini kilikuwa bora kufanywa ili kupunguza taharuki. Walikubalina kuwa njia pekee iliyo salama ilikuwa ni kumuua Paulo. Lakini Mungu aliijua nia yao, na Malaika walipewa kazi ya kumlinda, ili aweze kuishi nakutimiza utume Wake.— Early Writings, 202. [TA 239.1; UM Aya ya 53]

Sehemu hii ya historia imeandikwa kwa ajili ya maonyo yetu ambao miisho ya dunia imetujilia. Waefeso walidai kufanya mawasiliano na viumbe wasioonekana, ambao kwao walipata ujuzi wao wa yale yatakayotokea mbeleni. Katika siku zetu huu ushirika na wale roho za mapepo au zile zilizokufa huitwa Umizimu, na sanaa zinazotendwa kwa waaguzi si zote ni ujanja, na kujifanya. Ulimwengu unaoonekana na usioonekana una uhusiano

wa karibu. Shetani ndiye gwiji na mdanganyifu mkuu, na washirika wake katika uovu wako katika mafunzo chini yake ili wafanye kazi katika namna ile ile anayofanya kazi. Mtume anasema, "Kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili; juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu."— The Youth's Instructor, November 16, 1893. [TA 239.2; UM Aya ya 54]

Yule mfungwa mzee, Paulo, akisimama amefungwa minyororo na askari wake walinzi; hakuonesha chochote cha kuvutia katika mavazi au sura yake, ili dunia impe heshima yake. Bado mtu huyu, kwa sasa asiye na Rafiki, mali au cheo, alikuwa na ulinzi ambao walimwengu hawakuweza kuuona. Malaika wa mbinguni walikuwa wahudumu wake. Ikiwa utukufu wa mmoja wa wale wajumbe wenye kung'aa ungemulika, fahari na kiburi na majivuno vingeanguka mbele yake; mfalme na watumishi wangeangshwa chini.…Mbingu yote ilipendezwa na mtu huyu mmoja, ambaye sasa ni mfungwa kwa ajili ya imani yake katika Mwana wa Mungu.— Sketches from the Life of Paul, 254. [TA 240.1; UM Aya ya 55]

### Kuzingirwa kwa Yerusalemu

Ustahimilivu wa Mungu juu ya Yerusalemu uliwathibitisha tu Wayahudi katika ukaidi wao wa kutotubu. Katika chuki na ukatili wao kwa wanafunzi wa Yesu, waliukataa upendeleo wa mwisho wa rehema. Ndipo Mungu akawaondolea ulinzi Wake, na akaiondoa nguvu Yake ya kuzuia kutoka kwa Shetani na malaika zake, na taifa likaachwa chini ya udhibiti wa kiongozi waliyemchagua. Watoto Wake walikuwa wamekataa neema ya Kristo, ambayo ingewawezesha kuitiisha misukumo yao mibaya, na kisha kuwa washindi. [TA 240.2; UM Aya ya 56]

Shetani aliamsha chuki kali na shauku chafu sana kwenye roho za watu. Watu hawakufikiri; walikuwa nje ya fikra, hawakutumia akili tena nao-wakidhibitiwa kwa msukumo na hasira ya upofu. Wakawa mashetani katika ukatili wao ……..Shetani alikuwa mkuu wa taifa, na mamlaka za juu zaidi za kiraia na za kidini zilikuwa chini ya mamlaka yake.— The Spirit of Prophecy 4:29, 30. [TA 241.1; UM Aya ya 57]

Malaika wa Mungu walitumwa kufanya kazi ya kuangamiza/uharibifu, ili jiwe moja la hekalu lisiachwe juu ya jiwe pasipo kuondoshwa.— Manuscript Releases 21:66. [TA 241.2; UM Aya ya 58]

### Yohana wa Ufunuo

Kuhusu Gabrieli Mwokozi anena katika Ufunuo, akisema kwamba "Akamtuma malaika Wake akamwonesha mtumishi Wake Yohana." Ufunuo 1:1.

Na kwa Yohana malaika alisema, "Mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako manabii.” Ufunuo 22:9. Wazo la kustaajabisha—kwamba malaika anayesimama karibu kwa heshima, na Mwana wa Mungu Mwenyewe, ndiye aliyechaguliwa kufunua makusudi ya Mungu kwa watu wenye dhambi.—The Desire of Ages, 99. [TA 241.3; UM Aya ya 59]

Mungu alikuwa na kazi mahsusi kwa ajili yake kuikamilisha. Shetani alikusudiwa kuzuia kazi hii, na akawaongoza watumishi Wake kumwangamiza Yohana. Lakini Mungu alimtuma malaika Wake na akamhifadhi kwa njia ya ajabu. Wote walioshuhudia uweza mkuu wa Mungu uliodhihirishwa katika ukombozi wa Yohana, wakastaajabu, na wengi wakasadiki kwamba Mungu alikuwa pamoja naye, na ule ushuhuda alioutoa juu ya Yesu ulikuwa sahihi. Wale waliotaka kumwangamiza waliogopa tena kujaribu kumwua, naye akaruhusiwa kuteseka kwa ajili ya Yesu. [TA 241.4; UM Aya ya 60]

Alishitakiwa kwa uwongo na maadui zake, na punde si punde alipelekwa hadi kwenye kisiwa cha upweke, ambapo Bwana alimtuma malaika Wake kumfunulia mambo ambayo yangetukia juu ya nchi, na hali ya kanisa hadi mwisho; kurudi nyuma kwake, na nafasi ambayo kanisa linapaswa kuchukua ikiwa litampendeza Mungu, na hatimaye kushinda. [TA 242.1; UM Aya ya 61]

Malaika kutoka mbinguni alikuja kwa Yohana katika utukufu. Uso wake uking'aa kwa utukufu mkuu wa mbinguni. Alimfunulia Yohana matukio ya kina na ya kusisimua kuhusu kanisa la Mungu, na kuleta mbele yake mapambano ya hatari ambayo walipaswa kuyastahimili. Yohana aliwaona wakipita katika majaribu makali, na kufanywa weupe na kujaribiwa na, hatimaye, washindi, waliokolewa kwa utukufu katika ufalme ya Mungu. Muonekano wa malaika ukaangaza kwa furaha, na ulikuwa wa utukufu sana, alivyomwonesha Yohana ushindi wa mwisho wa kanisa la Mungu. [TA 242.2; UM Aya ya 62]

Yohana akanyakuliwa naye alipoona ukombozi wa mwisho wa kanisa, na alipokuwa amechukuliwa na utukufu wa tukio, pamoja na kicho cha kina na unyenyekevu, kisha akaanguka miguuni pa malaika huyo ili kumwabudu. Mara malaika akamwinua, akamkemea kwa upole; akisema, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu; mwabudu Mungu; kwani ushuhuda wa Yesu ndiyo roho ya unabii. [TA 242.3; UM Aya ya 63]

Kisha malaika akamwonesha Yohana jiji la kimbingu likiwa na uzuri wake wote na utukufu unaometameta. Yohana aliinuliwa na kutekewa/kuhemewa kwa utukufu wa mji. Hakukumbuka karipio lake la awali kutoka kwa malaika, lakini akaanguka tena kuabudu mbele ya miguu ya Malaika ambaye alimkaripia tena kwa upole, Angalia, usifanye hivi; kwa maana mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii, na wa hao wayashikao Maneno ya kitabu hiki; mwabudu Mungu.— Spiritual Gifts 1:130,131. [TA 242.4; UM Aya ya 64]

Kristo, mjumbe wa kifalme, alikuja kwa Yohana alipokuwa kwenye kifungo chake baharini kisiwani, na kumpa ufunuo wa ajabu sana wake Yeye Mwenyewe (Uturuki).— The Signs of The Times, March 3, 1890. [TA 243.1; UM Aya ya 65]

Malaika mwenye nguvu wa Ufunuo 10 aliyemwelekeza Yohana hakuwa mtu mwingine ila Yesu Kristo. Akiweka mguu wake wa kulia juu ya bahari, na wa kushoto juu ya nchi kavu, inaonesha sehemu ambayo Yeye anahusika katika matukio ya mwisho ya pambano kuu na Shetani. Nafasi hii inaashiria uwezo Wake mkuu na mamlaka juu ya dunia yote. Pambano limezidi kuwa na nguvu na kubwa zaidi kutoka kwa kipindi hadi kipindi, na litaendelea kuwa hivyo, hadi matukio ya mwisho ambapo kazi ya nguvu za giza itafikia kina chake. Shetani, akiungana na watu waovu, atadanganya ulimwengu wote na makanisa ambayo hayapokei upendo wa ile Kweli. Lakini Malaika mwenye nguvu wanahitaji umakini. Analia kwa sauti kuu. Ataonesha nguvu na mamlaka ya sauti Yake kwa wale ambao wameungana nao Shetani ili kuupinga Ukweli.— The S.D.A. Bible Commentary 7:971. [TA 243.2; UM Aya ya 66]

### Malaika katika Zama za Kati

Katika karne ya kumi na tatu kilianzishwa chombo cha kutisha kabisa katika akili na mamlaka ya upapa—Mahakama ya kanisa ya kukomesha uasi (inquistion/inkwizisheni). Mkuu wa giza aliwatawala viongozi wa kipapa. Katika mabaraza yao ya siri Shetani na malaika zake walitawala akili za watu waovu, pasipo kuonekana Malaika wa Mungu alisimama katikati yao, akichukua kumbukumbu za kutisha kuhusu uamuzi wao wa uovu na kuandika historia ya matendo ya kutisha sana hata yasiweze kuonekana katika macho ya wanadamu.— The Great Controversy, 59....

*.......(Baraza la Kuhukumu ‘Wazushi’ lilikuwa ofisi yenye nguvu iliyoanzishwa ndani ya Kanisa la Katoliki ili kung'oa na kuadhibu kitu wao walichokiita uzushi kotekote Ulaya na Marekani. Baraza la Kuhukumu; Wazushi’ lilikuwa na sifa mbaya kwa ukali wa mateso yake kwa waprotestanti. Nani alianzisha Baraza la Kuhukumu Wazushi na kwa nini?—Akiwa ameshtushwa na kuenea kwa Uprotestanti na hasa kwa kupenya kwake katika Italia, Papa Paulo lll mwaka 1542 alianzisha Kusanyiko la Baraza la Kuhukumu Wazushi huko Rumi. Taasisi hii pia ilijulikana kama Mahakama ya Kirumi ya Kuhukumu Wazushi na Ofisi Takatifu na, pia kwa kushirikiana na serikali za kilimwengu ili kupambana na kitu walichoita wao uzushi. Neno linatokana na kitenzi cha Kilatini inquiro (“uliza ndani”), jina hilo lilitumiwa kwa tume katika karne ya 13 na baadaye kwa miundo kama hiyo katika Ulaya ya kisasa ya awali. Mdadisi alikuwa afisa (kawaida akiwa na kazi za mahakama au uchunguzi) -mpango uliokusudiwa kuondoa uzushi na mambo mengine kinyume na fundisho au mafundisho ya*

*imani ya Kikatoliki. Watu zaidi ya milioni 50 waliuawa, soma zaidi kwenye historia, au google mtandaoni kuona hiyo historia)*

..... [TA 243.3; UM Aya ya 67]

### Matengenezo ya Kiprotestanti

Bendera ya mkuu wa sinagogi la Shetani iliinuliwa juu, na uasi ulielekea sasa kushinda, na wanamatengenezo kwa neema waliyopewa na Mungu, walipigana vita vilivyo na mafanikio dhidi ya majeshi ya giza. Matukio katika historia ya wanamatengenezo imewasilishwa mbele yangu. Ninajua kwamba Bwana Yesu na malaika Zake wametazama kwa shauku kubwa vita dhidi ya nguvu ya Shetani, ambaye aliunganisha majeshi Yake na watu waovu, kwa lengo la kuizima nuru ya Bwana.—Selected Messages 3:110. [TA 244.1; UM Aya ya 68]

### Luther

Siku moja alipokuwa akivichunguza vitabu katika maktaba ya chuo kikuu, Luther aligundua Biblia ya Kilatini....Kwa mkanganyiko na mshangao na hofu alifunua kurasa takatifu; kwa mapigo ya haraka ya moyo alijisomea Maneno ya uzima, akitulia mara kwa mara. kwa mshangao, Laiti Mungu angenipa kitabu kama hiki kwa ajili yangu mwenyewe!" Malaika wa mbinguni walikuwa kando yake, na miale ya nuru kutoka katika kile kiti cha enzi cha Mungu ilifunua hazina za Kweli katika fahamu zake.— The Spirit of Prophecy 4:96. [TA 244.2; UM Aya ya 69]

Maadui walipofuata desturi na mapokeo, au madai na mamlaka ya papa, Luther alikutana nao na Biblia na Biblia pekee. Hapa kulikuwa na hoja ambazo hawakuweza kuzijibu; kwa hiyo watumwa wa mila na ushirikina waliitamani damu yake……. Lakini Luther hakuangukia kwenye ghadhabu yao. Mungu alikuwa na kazi ili afanye, na malaika wa mbinguni walitumwa kumlinda.— The Spirit of Prophecy 4:108, 109. [TA 245.1; UM Aya ya 70]

Hapa palikuwa na mtu mmoja pekee ambaye alikuwa amechochea hasira ya makuhani na watu. Aliitwa Augsburg kujibu sababu za imani yake. Yeye alitii wito. Imara na bila woga alisimama mbele ya wale ambao walikuwa wamesababisha ulimwengu kutetemeka-mwana-kondoo mpole aliyezungukwa na simba wenye hasira— lakini kwa ajili ya Ukweli, na kwa ajili ya Kristo, alisimama bila woga, na kwa ufasaha mtakatifu, ambao Ukweli pekee ndiyo unaweza kutoa, alitoa sababu za imani yake. Walijaribu njia mbalimbali kumnyamazisha mtetezi shupavu wa Ukweli. Walimbembeleza, wakamsifia kwa kutia chumvi na kumshawishi; kuwa anapaswa kuinuliwa na kuheshimiwa; ila maisha na heshima hazikuwa na thamani kwake, kama vingetolewa kuwa dhabihu ya ile Kweli. [TA 245.2; UM Aya ya 71]

Kwa kung'aa zaidi na kwa ufasaha Neno la Mungu liliangaza juu ya ufahamu wake, na kumpa hisia ya wazi zaidi kuhusu makosa, upotovu, na. unafiki wa upapa. Maadui zake walitaka kumtisha, na kumfanya aikane imani yake, lakini alisimama kwa ujasiri kuitetea ile Kweli. Alikuwa tayari kufa kwa ajili ya imani yake, ikiwa Mungu alihitaji; lakini— kamwe, sio kuikana. Mungu alihifadhi maisha yake. Naye akawaagiza malaika wamhudumiie, na kumpeleka katika pambano lenye dhoruba, bila kudhurika, na alishangaa hasira na makusudi ya adui zake.—Spiritual Gifts 4b:118,119. [TA 245.3; UM Aya ya 72]

Kama macho ya mkutano huko Worms yangefumbuliwa, wao wangewaona malaika wa Mungu katikati yao, wakitoa miale ya nuru kuzuia giza la upotovu, na kufungua akili na mioyo ili kuipokea ile Kweli.—The Spirit of Prophecy 4:124. [TA 246.1; UM Aya ya 73]

### Melancthoni

Mwanamatengenezo, Simon Grynaeus alikuwa na uhusiano wa karibu na daktari mkuu wa papa; lakini, baada ya kushtushwa na moja ya mahubiri yake, akaenda kwake, na kumsihi asipigane tena kinyume na Ukweli. Huyu mfuasi wa papa alificha hasira yake, lakini haukupita muda na ikaonekana kwa mfalme, na kupata kutoka kwake mamlaka ya kumkamata mwanamatengenezo. Melancthon aliporudi nyumbani kwake, alifahamishwa kwamba baada ya kuondoka kwake maafisa kwa kusukumbwa Grynaeus walimtafuta kutoka juu hadi chini. Hakuamini kwamba Bwana alikuwa amemwokoa rafiki yake kwa kumtuma malaika mtakatifu kumpa onyo.—The Spirit of Prophecy 4:164, 165. [TA 246.1; UM Aya ya 74]

### Wazee Mahujaji na wasafiri

—(**waliotoka Ulaya kwa ajili ya mateso ya imani yao na kuja Marekani— miaka 1260 ya unabii**)

Katikati ya kuhamishwa na shida upendo na imani ya mahujaji iliendelea kuimarika. Waliamini ahadi za Bwana, na Yeye hakuwaangusha wakati wa mahitaji. Malaika Zake walikuwa kando yao,kuwatia moyo na kuwaunga mkono. Na wakati mkono wa Mungu ulipoonekana ukiwaelekeza ng'ambo ya bahari, kwenye nchi ambayo wangeweza kupata hali salama, na kuwaachia watoto wao urithi wa thamani wa uhuru wa dini, walisonga mbele, bila kunywea/kusita, katika njia ya majaliwa.— The Great Controversy, 291. [TA 246.2; UM Aya ya 75]

### Malaika Watatu wa Ufunuo 14

Kristo anakuja mara ya pili, akiwa na nguvu kwa wokovu. Kuwatayarisha wanadamu kwa tukio hili, Ametuma ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Malaika hawa wanawakilisha wale wanaoupokea Ukweli, na kwa

nguvu kuinua injili kwa ulimwengu.— The S.D.A. Bible Commentary 7:978, 979. [TA 246.3; UM Aya ya 76]

### William Miller

Niliona kwamba Mungu alimtuma malaika Wake kwenda juu ya moyo wa mkulima, William Miller, ambaye hakuwa ameamini Biblia, na kumsukuma kuuchunguza unabii. Malaika wa Mungu walimtembelea tena na tena huyu mmoja aliyechaguliwa, na kuiongoza akili yake, na kuufungua ufahamu wake kwa unabii ambao umekuwa giza kwa watu wa Mungu. Mwanzo alipewa mnyororo wa ile Kweli, naye akaongozwa kutafuta kifungu baada ya kifungu, mpaka akalitazama kwa mshangao na shauku Neno la Mungu…[TA 247.1; UM Aya ya 77]

Malaika wa Mungu waliandamana na William Miller katika utume wake. Alikuwa thabiti na asiye na hofu. Alitangaza ujumbe huo bila woga   Ingawa alipingwa na wale wanaodai kuwa Wakristo katika ulimwengu, na kuzuiwa na Shetani na malaika zake, hakuacha kuihubiri injili ya milele kwa umati popote alipoalikwa, na kilio kikasika, Mcheni Mungu na kumtukuza; kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja. Spiritual Gifts 1:128, 132. [TA 247.2; UM Aya ya 78]

Mchochezi wa maovu yote hakutafuta tu kupinga matokeo hayo ya ujumbe wa marejeo, bali kumwangamiza mjumbe mwenyewe. Miller ailifanya Kweli ya Maandiko kuwa sehemu ya Maisha katika mioyo wasikilizaji wake, akikemea dhambi zao na kuvuruga ubinafsi wao; na maneno yake ya wazi na yenye kuumiza, yaliamsha uadui wao. Upinzani uliodhihirishwa na washiriki wa kanisa juu ya ujumbe wake ulitia moyo matabaka na kwenda mbali zaidi; na maadui walipanga kuchukua maisha yake mara tu atakapoondoka mahali pa mkutano. Lakini malaika watakatifu walikuwa katika umati, na mmoja wao, katika umbo la mwanadamu, akaushika mkono wa mtumishi huyu wa Bwana, na kumwongoza salama kutoka katika umati wenye hasira.— The Great Controversy, 336, 33. [TA 248.1; UM Aya ya 79]

Watumishi wengi hawangeukubali ujumbe huu wa kuokoa wao wenyewe, na wale ambao wangeupokea, walizuiwa. Damu ya nafsi iko juu yao. Wahubiri na watu walijiunga kupinga ujumbe huu kutoka mbinguni. Walimtesa William Miller na wale ambao waliungana naye katika kazi. Uongo ulisambazwa kuharibu na kuzuia mvuto wake, na kwa nyakati tofauti baada ya kutangaza waziwazi shauri la Mungu, akitumia zile Kweli zenye kukata mioyoni mwa wasikilizaji wake, hasira kali ikawaka juu yake, na alipokuwa akipaacha pahali pa kukutania, wengine walimgonja njiani ili kuundoa uhai wake. Lakini malaika wa Mungu walitumwa kuuhifadhi uhai wake, nao wakamwongoza salama mbali na umati wenye hasira. — Spiritual Gifts 1:136. [TA 248.2; UM Aya ya 80]

## SURA YA 19

## MALAIKA KATIKA UZOEFU WA ELLEN WHITE

### Wito Wa Ellen White Kuwa Nabii

Nilipokuwa nikiomba kwenye madhabahu ya familia, Roho Mtakatifu alinishukia, na nilionekana nikiinuka juu zaidi na zaidi, mbali sana na dunia yenye giza. Niligeuka kuwatafuta Waadventista duniani, lakini sikuwaona, wakati sauti iliponiambia, "Tazama tena, na utazame juu kidogo." Katika hili niliinua macho yangu, nikaona njia iliyonyooka na nyembamba, iliyoinuliwa juu ya dunia. Katika njia hii Waadventista walikuwa wakisafiri kwenda mjini, mji uliokuwa mwisho wa njia. Walikuwa na mwanga mkali nyuma yao katika mwanzo wa njia, ambao malaika aliniambia ni kilio cha usiku wa manane. Nuru hii iliangaza njiani kote na kutoa nuru katika miguu yao ili wasijikwae. Ikiwa walikaza macho yao kwa Yesu, ambaye alikuwa mbele yao, akiwaongoza kwenda jijini, walikuwa salama.— Early Writings, 14. [TA 249.1; UM Aya ya 1]

Katika umri wa miaka kumi na saba ... mgeni wa mbinguni alikuja na

kuzungumza nami akaniambia, “Nina ujumbe kwako kuubeba.” “Kwa nini,” nilifikiria, “hakika lazima kuwe na kosa kubwa mahali fulani.” Tena maneno haya yalirudiwa: “Nina ujumbe kwako kuubeba. Andika kwa watu kile nilichokupa.”— Sermons and Talks 2:252. [TA 249.2; UM Aya ya 2]

### Sanduku la Agano Mbinguni

Bwana alinipa kuona muonekano wa Patakatifu pa mbinguni. Hekalu ya Mungu likafunguliwa mbinguni, nami nikaonyeshwa Sanduku la Agano la Mungu lililofunikwa kwa Kiti cha Rehema. Malaika wawili walisimama kila mwisho wa sanduku, na mabawa yao yametanda juu ya kiti cha rehema, na nyuso zao zimegeuka kulielekea. Huyu malaika aliyeandamana nami alinijulisha kuwa huliwakilisha jeshi lote la mbinguni likitazama kwa kicho cha heshima kuelekea Sheria ya Mungu ambayo ilikuwa imeandikwa kwa chanda cha Mungu.—Life Sketches of James White and Ellen G. White (1880), 236. [TA 250.1; UM Aya ya 3]

Sanduku la Agano la Patakatifu pa duniani lilikuwa ni kivuli/kielelezo cha Sanduku la Agano halisi (la kweli) mbinguni. Huko, kando ya Sanduku la Agano la mbinguni, wamesimama malaika walio hai, kila mmoja kwa bawa moja akifunika Kiti cha Rehema, na kuinuka juu, huku mabawa mengine yakiwa yamekunjwa juu ya maumbo yao kwa ishara ya heshima na unyenyekevu.—The Signs of the Times, Juni 24, 1880. [TA 250.2; UM Aya ya 4]

Laiti wote wangeweza kumwona Mwokozi wetu wa thamani jinsi alivyo, Mwokozi. Hebu mkono Wake na uondoe pazia ambalo huficha utukufu Wake kutoka kwenye macho yetu. Inamwonyesha katika ulimwengu wa roho pahali Pake na Patakatifu. Tunaona nini? Mwokozi wetu, si katika hali ya ukimya na utulivu pasipo kazi. Amezungukwa na viumbe wa mbinguni, makerubi, na maserafi, elfu kumi mara elfu kumi ya malaika. [TA 250.3; UM Aya ya 5]

Viumbe hawa wote wa mbinguni wana lengo moja juu ya mengine yote, ambayo wanavutiwa kwa kina sana—Kanisa Lake katika ulimwengu wa dhambi…….Wanafanya kazi kwa ajili ya Kristo chini ya agizo Lake, ili kuwaokoa kabisa wote wanaomtazamia na kumwamini. Hawa viumbe wa mbinguni wanaharakisha utume wao....Wanafanya hivyo wakiwa wameunganishwa katika muungano mtakatifu, katika umoja mkuu na uliotukuka wa kusudi, ili kuonesha uwezo na huruma na upendo na utukufu wa Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. [TA 250.4; UM Aya ya 6]

Katika huduma yao, majeshi haya ya mbinguni yanaonesha kile ambacho kanisa la Mungu linapaswa kuwa. Kristo anafanya kazi kwa ajili yao huko katika nyua za mbinguni, akiwatuma wajumbe Wake sehemu zote za dunia, ili kumsaidia kila mtu anayeteseka ambaye anamtegemea Yeye ili kupata msaada, kwa maisha ya kiroho na ujuzi.— The S.D.A. Bible Commentary 7:967,

968. [TA 251.1; UM Aya ya 7]

### Shetani Kabla Hajaanguka, na Alivyo Sasa

Shetani alikuwa malaika aliyeheshimiwa mbinguni, amfuataye kwa cheo Kristo. Muonekano wake, kama ule wa malaika wengine, ulikuwa mpole na wa kuonesha furaha. Paji la uso wake lilikuwa juu na pana, likionesha uwezo mkubwa wa akili. Umbo lake lilikuwa kamilifu; sifa yake ikiwa ya utukufu na ukuu. Early Writings, 145. [TA 251.2; UM Aya ya 8]

Nilioneshwa Shetani kama alivyokuwa zamani, malaika mwenye furaha, aliyeinuliwa. Kisha Nilioneshwa jinsi alivyo sasa. Bado ana umbo la kifalme. Muonekano wake bado ni mkuu na bora, kwa kuwa ni malaika aliyeanguka. Lakini muonekano wake umejaa wasiwasi, mashaka, fadhaa, kutokuwa na furaha, chuki, hasira, uovu, udanganyifu na kila uovu. Paji la uso ambalo hapo awali lilikuwa la kifahari sana, Nililtilia umakini. Paji la uso wake lilianza kushuka kwenye macho yake hadi kupungua. Niliona kwamba alikuwa amepinda kwa muda mrefu kwa uovu yaani kila ubora mzuri ulishushwa, na kila tabia mbaya ilikuzwa. Macho Yake yalikuwa ya ujanja, hila, na yalionesha kupenya sana. Umbo lake lilikuwa kubwa, lakini nyama ilining'inia vibaya juu ya mikono yake na uso. Nilivyoendelea kumtazama, kidevu chake kimeegemea juu ya mkono wake wa kushoto. Alionekana kuwa katika lindi la mawazo ya kina. Tabasamu lilikuwa juu ya uso wake, ambalo lilinifanya kutetemeka, lilikuwa limejaa uovu na hila za kishetani. Tabasamu hili ni lile analokuwa nalo kabla tu ya kujihakikishia windo lake, na kama akikamata windo katika mtego wake, tabasamu hili linakua la kutisha.— Early Writings, 152, 153. [TA 251.3; UM Aya ya 9]

### Malaika Aliowaona Ellen White Katika Maono na Ndoto

Niliota kwamba ndugu kadhaa huko California walikuwa katika baraza, wakijadili mpango bora wa kazi katika msimu ujao. Wengine waliona ni busara kuacha miji mikubwa, na kufanya kazi katika maeneo ya miji midogo. Mume wangu alikuwa akihimiza kwa dhati kuwekwa mipango mipana, na juhudi zilizopanuliwa zaidi zilizofanywa, ambazo zingelinganishwa vyema na sura ya ujumbe wetu. [TA 252.1; UM Aya ya 10]

Kisha kijana ambaye nilikuwa nimemwona mara kwa mara katika ndoto zangu, aliingia barazani. Alisikiliza kwa shauku sana maneno hayo ambayo yalisemwa, na kisha, akizungumza kwa kutafakari na kujiamini na mamlaka, akasema hivi: [TA 252.2; UM Aya ya 11]

"Miji na vijiji ni sehemu ya shamba la mizabibu la Bwana. Ni lazima wasikie jumbe za maonyo. Adui wa ukweli hufanya juhudi kubwa kuwageuza watu kutoka kwenye ile Kweli ya Mungu na kwenda kwenye uongo....Mnapaswa

kupanda kando ya maji yote."— Life Sketches of Ellen G. White, 208. [TA 252.3; UM Aya ya 12]

Katika kazi yangu, nimeunganishwa na wasaidizi wangu, na pia kuunganishwa na kuwasiliana kwa karibu na Mkufunzi wangu na viumbe wengine wa mbinguni. Wale walioitwa na Mungu wanapaswa kuwa katika mawasiliano Naye kwa utendaji wa Roho Wake Mtakatifu, ili waweze kufundishwa kumhusu Yeye.—Spalding and Magan Collection, 462. [TA 252.4; UM Aya ya 13]

Wakati nikipanda gari sikuweza kukaa. Mume wangu alifanya kitanda kwenye kiti, na nilijilaza huku kichwa na moyo vikiuma [TA 253.1; UM Aya ya 14]

Katika hali hii ya akili nililala na kuota malaika mrefu alisimama kando yangu, na kuniuliza kwa nini nilikuwa na huzuni. Nilimjulisha mawazo yaliyokuwa yamenisumbua, na kusema, "Siwezi kufanya vizuri sana, kwa nini tusiwe pamoja na watoto wetu, na kufurahia ushirika wao?" "Yeye akasema, "Umempa Bwana maua mawili mazuri, harufu nzuri ambayo ni kama uvumba mzuri mbele Zake, na yana thamani zaidi mbele Zake kuliko dhahabu au fedha, kwa maana ni zawadi ya moyo. Huvuta kila nyuzi za moyo kuliko dhabihu nyingine yoyote inavyoweza. Hupaswi tazama mwonekano wa sasa, lakini weka jicho lako katika wajibu wako, katika utukufu wa Mungu pekee, na kufuata katika majaliwa Yake, na njia itang'aa mbele yako. Kila kujinyima, kila dhabihu imeandikwa kwa uaminifu, na italeta thawabu yake."— Spiritual Gifts 2:129, 130. [TA 253.2; UM Aya ya 15]

Niliota kwamba kijana mwenye sura nzuri aliingia ndani ya chumba nilichokuwamo, mara baada ya kuzungumza. Huyu mtu ni huyo huyo amekuwa akinitokea katika ndoto muhimu ili kunielekeza mara kwa mara katika kipindi cha miaka ishirini na sita iliyopita. Alisema, Wewe umeelekeza umakini wa watu kwenye masomo muhimu, ambayo, kwa wengi, ni mageni na mapya. Kwa wengine ni ya kuvutia sana. Watenda kazi katika Neno na mafundisho wamefanya walichoweza katika kuuwasilisha Ukweli, ambao umezua uchunguzi katika akili na kuamsha shauku. Lakini isipokuwa kuna juhudi kamili zaidi iliyofanywa ili kusisitiza Kweli hizi akilini, juhudi zako zilizozofanywa sasa zitakuwa zisizozaa matunda.— The Review and Herald, November 4, 1875. [TA 253.3; UM Aya ya 16]

Kama maswali yameulizwa mara kwa mara kuhusu hali yangu katika maono, na baada ya kutoka, ningesema kwamba wakati Bwana anapoona inafaa kutoa maono, nachukuliwa katika uwepo wa Yesu na malaika, na kupoteza kabisa kuhusu mambo ya kidunia. Siwezi kuona mbali zaidi ya Malaika anavyonielekeza.— Spiritual Gifts 2:292. [TA 254.1; UM Aya ya 17]

## Vita vya Manassas

Niliona vita yenye msiba huko Manassas, Virginia. Lilikuwa tukio lenye kusisimua na kuhuzunisha sana. Jeshi la Kusini lilikuwa lina kila kitu kwa upande wao na walikuwa tayari kwa ajili ya mapambano ya kutisha. Jeshi la Kaskazini lilikuwa likisonga mbele kwa ushindi, bila shaka watakuwa washindi. Wengi walikuwa wazembe na walipigwa gwaride mbele kwa majigambo, kana kwamba ushindi tayari ni wao. Walipokaribia uwanja wa vita, wengi walikuwa karibu kuzirai kwa sababu ya uchovu na kutaka kuburudishwa. Hawakutarajia kukutana na hali hiyo kali. Walijikimbiza vitani na kupigana kwa ujasiri, kwa kukata tamaa. Wafu na waliokuwa wakifa walikuwa kila pande. Wote Kaskazini na Kusini waliteseka kwa ukali. Watu wa Kusini waliona vita, na katika muda kidogo wangeweza kurudishwa nyuma zaidi. Watu wa Kaskazini walikuwa wakikimbia kuendelea, ingawa uharibifu wao ulikuwa mkubwa sana. [TA 254.2; UM Aya ya 18]

Mara moja malaika alishuka na kutikisa mkono wake nyuma. Mara moja kulikuwa na mkanganyiko katika safu. Ilionekana kwa watu wa Kaskazini kwamba wanajeshi wao walikuwa wakirudi nyuma, wakati haikuwa hivyo kwa ukweli, na mafundo ya mvua yakaanza.—Testimonies for the Church 1:266, 267. [TA 255.1; UM Aya ya 19]

## Msimamizi wa Kituo cha tiba mbadala au tiba rahisi (Sanitarium)

Katika ndoto zangu nilikuwa kwenye Sanitarium ya Afya, na niliambiwa na mwongozaji wangu kuzingatia kila nilichosikia na kuchunguza kila nilichoona. Nilikuwa mahali pa kupumzika, ambapo sikuweza kuonekana, lakini naweza kuona kila kitu kinachoendelea chumbani. Watu walikuwa wanafanya hesabu na wewe, nami nikawasikia wakibishana nawe kuhusu zile fedha nyingi zilitozwa kwa malazi, chakula na matibabu. Nilikusikia kwa uthabiti, na sauti ya kimaauzi ukikataa kupunguza malipo. Nilishangaa kuona kwamba malipo yalikuwa makubwa sana. Ulionekana kuwa ndiwe nguvu ya kuyadhibiti.. [TA 255.2; UM Aya ya 20]

Niliona kwamba hisia zilizoletwa na mwenendo wako juu ya akili za waliokuwa wakilipa bili zao hazikuifaidisha taasisi hiyo. Nilisikia baadhi ya ndugu zako wakikusihi, wakikuambia kuwa mwendo wako haukuwa wa busara na usio na haki, lakini ulikuwa mgumu kama mwamba kufuata njia yako. Ulidai kuwa yale ulivyokuwa ukifanya, ulikuwa unafanya kazi kwa manufaa ya taasisi. Lakini niliona watu wanatoka kwenye Sanitarium bila kuridhika…….[TA 255.3; UM Aya ya 21]

Katika muda wa usiku nilikuona katika ukiwa na ushirika na mlezi wa kike wa taasisi. Kwa kadiri umakini wenu kwa kila mmoja ulivyokuwa ukihusika, mngeweza kuwa mume na mke. Mwenendo wenu kwa kila mmoja ulikuwa

mbaya mbele za Mungu, na moyo wangu ulihuzunishwa na hali ya mambo. Nikauliza, "Ni nani aliyewaloga, hata msiitii Kweli?" Mungu hafurahishwi. Mmemhuzunisha Roho Wake Mtakatifu. Dada H_____ hapaswi kuwa vile alivyokuwa zamani. Wote wawili mna hatia mbele za Mungu . [TA 255.4; UM Aya ya 22]

Mambo yaliyojiri katika kituo cha tiba mbadala cha... yalifunguliwa mbele yangu. Sauti ikasema, "Nifuate, Nami nitakuonesha dhambi zinazotendwa na wale wanaosimama katika nyadhifa zao." Nilipitia vyumbani, na nilikuona wewe, mlinzi juu ya kuta za Sayuni, ulikuwa karibu sana na mke wa mtu mwingine, ukikisaliti kiapo kitakatifu, ukimsulubisha tena Bwana wako. Je, ulizingatia kuwa kulikuwa na Mlinzi, Mtakatifu, ambaye alikuwa akishuhudia kazi yako ovu, na kuona matendo yako na kusikia maneno yako, na haya pia huandikwa katika vitabu vya mbinguni?— Manuscript Releases 8:315-317. [TA 256.1; UM Aya ya 23]

**Familia ya Brown**

Malaika wa Mungu akasema, "Nifuate." Nilionekana kuwa chumbani katika jengo lisilo na adabu, lenye ukorofi, na hapo kulikuwa na vijana kadhaa wakicheza karata. Walionekana kuwa na shauku sana katika burudani waliyokuwa wakijihusisha nayo, na walikuwa wamezama sana kiasi kwamba hawakuonekana kujua kuna mtu ameingia chumbani. Walikuwepo wasichana wadogo wakiangalia wachezaji, na maneno hapo hayakuwa yaliyotakaswa. Kulikuwa na roho na ushawishi ambao ulionekana kuwemo katika hicho chumba ambayo haikuwa ya tabia iliyohesabiwa kutakasa na kuinua akili na kuinua tabia.....[TA 256.2; UM Aya ya 24]

Niliuliza, "Hawa ni akina nani na tukio hili linawakilisha nini?" Neno likasemwa, "Subiri." ..... [TA 257.1; UM Aya ya 25]

Nilipokea maono mengine. Kulikuwa na unywaji wa kileo chenye sumu, na maneno na vitendo chini ya ushawishi wake vilikuwa si kitu chochote bali yaliyofaa kwa mawazo makini, mtazamo mzuri katika biashara, maadili safi, na kuwainua wahusika ... [TA 257.2; UM Aya ya 26]

Nikauliza tena, "Hawa ni akina nani?" [TA 257.3; UM Aya ya 27]

Jibu lilikuja, "Sehemu ya familia ambapo unatembelea. Adui wa roho, adui mkuu wa Mungu na mwanadamu, mkuu wa falme na mamlaka, na mkuu wa giza la ulimwengu huu anatawala hapa usiku wa leo. Shetani na malaika zake wanaendelea na majaribu yake kwa roho hizi maskini kwa uharibifu wao wenyewe.—Selected Messages 3:41,42. [TA 257.4; UM Aya ya 28]

## N. D. Faulkhead na Ishara ya Siri

Ndugu Faulkhead aliniita kuniona. Mzigo wa jambo lake ulikuwa akilini mwangu. Nilimwambia kuwa nina ujumbe kwa ajili yake na mkewe, ambao mara kadhaa nilikuwa tayari kuwatumia, lakini nilihisi kukatazwa na Roho wa Bwana kufanya hivyo. Nilimwomba ateue muda ambao ningeweza kuwaona. Akajibu, "Nimefurahi kuwa wewe hakunitumia mawasiliano ya maandishi; Ningependa kuwa na ujumbe kutoka katika midomo yako; ungekuja kwa njia nyingine sidhani kama ingenifanyia wema wowote." Kisha akauliza, "Kwa nini usinipe ujumbe sasa?" Nikasema, "Je, unaweza kukubali kubaki kuusikia?" Akajibu kwamba angefanya hivyo………[TA 257.5; UM Aya ya 29]

Nilikuwa nimechoka sana, kwa sababu nilikuwa nimehudhuria mazoezi ya kufunga shule siku hiyo; lakini sasa niliinuka kutoka kwenye kitanda nilichokuwa nimelala na kumsomea kwa saa tatu. Moyo wake ulilainishwa, machozi yalikuwa machoni pake, na nilipoacha kusoma, alisema, "Ninakubali kila neno; yote ni yangu." Mengi ya mambo niliyokuwa nimesoma yanahusiana na ofisi ya Echo na usimamizi wake tangu mwanzo. Na Bwana pia alinifunulia uhusiano wa Ndugu Faulkhead na dini ya Free Masons, na kuweka wazi kwamba isipokuwa amekata kila mnyonyoro unaomfunga katika vyama hivi angepoteza roho yake.. [TA 257.6; UM Aya ya 30]

Alisema, "Ninaikubali nuru ambayo Bwana ameniletea kupitia kwako. Nitaifanyia kazi. Mimi ni mshiriki wa vikundi vitano vya free mason (free mason lodges ndilo jina la mahali wanapokutania), na nyingine tatu ziko chini ya udhibiti wangu. Ninazifanyia biashara hizo zote. Sasa sitahudhuria tena mikutano yao, na nitafunga shughuli zangu zinazohusiana nao haraka iwezekanavyo." Nilirudia maneno yaliyozungumzwa na mwongozoji wangu kwa kuhusiana na vyama hivi. Kutoa harakati fulani ambazo zilifanywa na mwongozaji wangu, nilisema, "Siwezi kukujulisha yote niliyopewa." [TA 258.1; UM Aya ya 31]

Ndugu Faulkhead alimwambia Mzee Daniells na wengine kwamba nilitoa ishara maalum inayojulikana tu na mamlaka ya juu ya Free Masons*, ambamo alikuwa ameingia. Alisema kwamba sikujua ishara, na kwamba mimi sikujua kuwa nilikuwa nampa ishara. Huu ulikuwa ushahidi mahsusi kwake kwamba Bwana alikuwa akifanya kazi kupitia mimi kuokoa roho yake.— Manuscript Releases 5:148, 149. [TA 258.2; UM Aya ya 32]

*Nyongeza:*

**Siri za Freemason zinadaiwa kufichwa nyuma ya kila kitu kuanzia kupanga mji mkuu wa taifa la Marekani hadi mauaji. Wanachama wa undugu wa kimaajabu wa Kimasoni ni pamoja na wanasiasa mashuhuri, Mababa*

*Waanzilishi na wakuu wa biashara. Katika nyakati za kisasa, Masons wanajulikana kwa kutoa mamilioni ya misaada. Lakini Freemasons ni akina nani na wanasimamia nini? Hivi kweli kuna siri ya kupeana mikono ya Freemason? Ingawa Freemasonry yenyewe sio dini, washiriki wake wote wanaamini katika Mtu Mkuu, au "Msanifu Mkuu wa Ulimwengu." Wanachama wanatoka katika imani nyingi, lakini dhehebu moja hasa huzuia mgawanyiko wowote. Kanisa Katoliki lilishutumu Umasoni kwa mara ya kwanza mwaka wa 1738, likichochewa na wasiwasi juu ya mahekalu ya Kimasoni na mila ya siri iliyofanywa ndani yao. Katika karne ya 19, Vatikani iliwaita Wamasoni "sinagogi la Shetani." Kanisa lilienda mbali zaidi katika mwaka wa 1983, likitamka: "Kanuni zao sikuzote zimezingatiwa kuwa hazipatani na mafundisho ya Kanisa na kwa hiyo ushiriki wao bado umekatazwa. Waamini wanaojiandikisha katika vyama vya Kimasoni wako katika hali ya dhambi nzito na huenda wasipate Ushirika Mtakatifu."*

*Freemasons wamewasiliana kwa muda mrefu kwa kutumia alama za kuona kutoka kwa zana za uashi. "Jicho Linaloona Yote," au Jicho la Ufadhili, ingawa halijaundwa na Waashi, limetumiwa na kikundi kuwakilisha ujuzi wa Mungu. Ishara inayojulikana zaidi ya Freemason, "Mraba na Compasses," inaonyesha mraba wa wajenzi uliounganishwa na dira. "G" katika kituo chake bado chini ya mgogoro; baadhi ya wataalam katika Taasisi ya Teknolojia ya Massachusetts, kwa mfano, wanaamini kwamba "G" katika kituo cha alama hiyo inawakilisha jiometri, eneo muhimu kwa Freemasons wa kwanza, huku wengine wakiamini inawakilisha Mungu, "Msanifu Mkuu wa Ulimwengu." Mraba na Compass bado ni ishara maarufu kwenye pete za Masonic.*

### Uwepo wa Malaika Ellen White Alipokuwa Macho

Nilipoamka na kuchungulia dirishani, nikaona mawingu wawili meupe. Kisha nikalala tena; na katika ndoto yangu maneno haya yalisemwa kwangu: "Tazama mawingu haya. Yalikuwa ni mawingu kama haya yaliyofunika jeshi la mbinguni lililowatangazia wachungaji kuzaliwa kwa Mkombozi wa ulimwengu." Niliamka na kutazama nje ya dirisha la gari tena, na kulikuwa na mawingu mawili makubwa meupe, meupe kama theluji. Yalikuwa mawingu halisi tofauti, lakini moja lingekaribia na kugusa lingine, na kwa muda yangeweza kuungana pamoja; tena yangejitenga, na kubaki tofauti kama hapo awali. Hayakutoweka, lakini yaliendelea kuonekana hadi adhuhuri yote. Saa sita kamili tulibadilisha magari, na sikuyaona mawingu tena. [TA 258.3; UM Aya ya 33]

Wakati wa mchana nilivutiwa sana na wazo kuwa malaika wa Mungu, wakiwa wamefunikwa na mawingu haya, walikuwa wakitutangulia; ili tufurahie ungalizi wao, na pia yakini ili tuone wokovu wa Mungu katika mikutano itakayofanyika huko Brisbane. Na sasa mikutano imekwisha, na tumeona

shauku ya ajabu iliyooneshwa na watu, sasa mimi, zaidi ya hapo awali Napata hakika kwamba malaika wa mbinguni walikuwa wamefunikwa katika mawingu hayo—Malaika ambao walitumwa kutoka katika nyua za juu ili kuvuta mioyo ya watu watu, na kuzuia nguvu ile inayokengeusha ambayo wakati mwingine huingia katika maeneo yetu ya kambi, ambayo kwayo akili huelekezwa kutozingatia zile Kweli muhimu zinazotolewa kila siku. [TA 259.1; UM Aya ya 34]

Katika mkutano huu, maelfu wamesikia mwaliko wa injili, na wamesikiliza zile Kweli ambazo hawajawahi kuzisikia kabla. Wakati wote wa mkutano, hakujawa na upinzani wowote mkali, au mabishano makubwa kutoka kwa wale ambao mioyo yao inapinga sheria ya Mungu. Na katika jiji lote, hakukuwa na upinzani wa umma. Huu ni uzoefu usio wa kawaida; na tunaamini kwamba Malaika wa Mungu wamekuwapo ili kurudisha nyuma nguvu za giza.— The Review na Herald, March 21, 1899. [TA 259.2; UM Aya ya 35]

Nilikuwa na ugonjwa wa baridi yabisi katika upande wangu wa kushoto na sikuweza kupata kupumzika kwa sababu ya maumivu. Niligeuka kutoka upande hadi upande, nikijaribu kutafuta unafuu kutoka katika mateso. Kulikuwa na maumivu moyoni mwangu ambayo yalionesha kutokuwa mazuri kwangu. Hatimaye nililala. [TA 260.1; UM Aya ya 36]

Karibu saa tatu na nusu nilijaribu kujigeuza, na kadiri nilivyofanya hivyo, nikagundua kuwa mwili wangu haukuwa na maumivu kabisa. Kadiri nilivyogeuka kutoka upande hadi upande, na kusogeza mikono yangu, nilipata uzoefu wa uhuru wa ajabu na wepesi ambao siwezi kuuelezea. Chumba kilijazwa na mwanga, taa nzuri zaidi, laini, ya samawati ya kumetameta, na mimi nilionekana kuwa katika mikono ya viumbe vya mbinguni. [TA 260.2; UM Aya ya 37]

Nuru hii ya kipekee nimeipata siku za nyuma nyakati za baraka maalum, lakini wakati huu ilikuwa ya kipekee zaidi, ya kuvutia zaidi, na nilihisi amani kama hiyo, amani iliyojaa na tele, hakuna maneno yanayoweza kuieleza. Nilijiinua katika mkao wa kuketi, na nikaona kwamba nilikuwa nikizungukwa na wingu angavu, jeupe kama theluji, kingo zake zilikuwa zina na rangi ya waridi/pinki. Muziki laini na mtamu zaidi ulikuwa ukijaa hewani, na nikatambua muziki huo kuwa ni uimbaji wa malaika. Kisha Sauti ilinena nami, ikisema: "Usiogope; Mimi ni Mwokozi wako. Malaika watakatifu wako pote kukuzunguka."— Testimonies for the Church 9:65, 66. [TA 260.3; UM Aya ya 38]

## SURA YA 20

## MALAIKA KATIKA PAMBANO KUU LA MWISHO

### Malaika Wema na Waovu Watatokea

Washirika wa kishetani katika umbo la kibinadamu watashiriki katika hili pambano kuu la mwisho kupinga kujengwa kwa ufalme wa Mungu. Na malaika wa mbinguni katika sura ya kibinadamu watakuwa kwenye uwanja wa pambano. Pande mbili zinazopingana zitaendelea kuwepo hadi kufungwa kwa ukurasa wa mwisho katika historia ya ulimwengu huu.—The Review and Herald, Agosti 5, 1909. [TA 261.1; UM Aya ya 1]

Shetani atatumia kila fursa kuwapotosha wanadamu kutoka kwa uaminifu wao kwa Mungu. Yeye na malaika zake waovu walioanguka pamoja naye watatokea duniani kama wanadamu, wakitafuta kudanganya. Malaika wa Mungu pia wataonekana kama watu, na watatumia kila njia katika uwezo wao kushinda makusudi ya adui. Tuna sehemu ya kutenda.—Manuscript Releases 8:399. [TA 261.2; UM Aya ya 2]

Shetani analeta nguvu zake zote kwenye shambulio katika pambano la mwisho, lililo karibu, na uvumilivu wa mfuasi wa Kristo utaumizwa kwa kiwango cha juu kabisa. Wakati fulani itaonekana kwamba lazima wakate tamaa. Lakini maombi kwa Bwana Yesu yanaenda kama mshale kwenye kiti cha enzi cha Mungu, na malaika wa Mungu wanatumwa kwenye uwanja wa vita. Mawimbi yanageuzwa.—In Heavenly Places, 297. [TA 261.3; UM Aya ya 3]

Katika kipindi cha mwisho cha historia ya dunia Bwana atafanya kazi kwa

niaba ya wale wanaosimama kidete kwa ajili ya haki Malaika walio na nguvu nyingi zaidi, watawalinda.—Prophets and Kings, 513. [TA 262.1; UM Aya ya 4]

### Kazi ya Malaika Wabaya Kupitia Umizimu

Kwa muda mrefu Shetani amekuwa akijiandaa kwa ajili ya jitihada zake za mwisho za kuudanganya ulimwengu ....Kidogo kidogo ametayarisha njia kwa kazi yake bora ya udanganyifu katika uendelezaji wa umizimu. Bado hajafikia utimilifu kamili wa mbinu yake; lakini itafikiwa kwa masalia ya wakati wa mwisho....Isipokuwa wale waliohifadhiwa na nguvu ya Mungu, kwa njia ya imani katika Neno Lake, ulimwengu wote utafagiliwa katika aina za udanganyifu huu.— The Great Controversy, 561, 562. [TA 262.2; UM Aya ya 5]

Umizimu ni gwiji kuu la udanganyifu. Ni njia ya udanganyifu zaidi wa Shetani yenye mafanikio na wa kuvutia—ambayo imelenga kuteka huruma za wale ambao wameweka wapendwa wao kaburini. Malaika waovu huja kwa namna ya wapendwa hao, na kusimulia matukio kuhusiana na maisha yao, na kufanya vitendo walivyofanya wakati wa walipokuwa hai. Kwa njia hii huwaongoza watu kuamini kwamba marafiki wao waliokufa ni malaika, wakielea juu yao na kuwasiliana nao. Malaika hawa waovu, wanaodhaniwa kuwa marafiki waliokufa, wametazamwa kama vitu vya kuabudiwa (ibada ya sanamu), na neno lao limekuwa kwa wengi na uzito mkubwa kuliko Neno la Mungu.— The Signs of the Times,Agosti 26, 1889. [TA 262.3; UM Aya ya 6]

Kuja kwa Bwana kutatanguliwa na “kazi ya Shetani kwa uwezo wote na ishara na ajabu za uongo na kwa udanganyifu wote wa udhalimu.” Na mtume Yohana, akielezea nguvu ya kutenda miujiza ambayo itadhihirishwa katika siku za mwisho, anasema hivi: “Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu, naye atawakosesha wale wakaao juu ya nchi,kwa ishara zile alizopewa kuzifanya.” Hakuna upotovu wowote unaotabiriwa hapa. Watu wanadanganywa na miujiza ambayo watumishi wa Shetani wana uwezo wa kuifanya, si kile wanachojifanya kufanya.— The Great Controversy, 553. [TA 262.4; UM Aya ya 7]

Shetani ni adui mwenye hila. Na si jambo gumu kwa malaika waovu kuwawakilisha watakatifu na wenye dhambi wote waliokufa, na kuufanya huu uwakilishi kuonekana kwa macho ya mwanadamu. Maonesho haya yatakuwa ya mara kwa mara zaidi, na maendeleo ya namna ya kushangaza zaidi yatatokea tunapokaribia mwisho wa wakati.— The Review and Herald, Aprili1, 1875. [TA 263.1; UM Aya ya 8]

Shetani ana uwezo wa kuleta mbele ya watu mupnekano wa marafiki zao waliokufa. Muonekano bandia ni kamilifu; sura inayojulikana, maneno, sauti, vinatolewa tena kwa mkazo wa ajabu. [TA 263.2; UM Aya ya 9]

Wengi watakabiliwa na roho za mashetani wanaojifanya kuwa ndugu wapendwa au marafiki, na kutangaza hatari zaidi. Wageni hawa watadai huruma zetu za dhati, na kufanya miujiza ili kuendeleza kujidai wao. Ni lazima tuwe tayari kuwapinga kwa Ukweli wa Biblia kwamba wafu hawajui neno lolote, na kwamba hao wanaoonekana ni roho za mashetani. [TA 263.3; UM Aya ya 10]

Mbele yetu kuna "saa ya kujaribiwa ambayo itakuja juu ya ulimwengu wote, ili kuwajaribu wakaao juu ya nchi. Wote ambao imani yao haijaimarishwa kwa uthabiti juu ya Neno la Mungu watadanganyika na kushindwa.— The Great Controversy, 552, 560. [TA 263.4; UM Aya ya 11]

Mawasiliano kutoka kwa roho za kishetani zitatangaza kwamba Mungu amewatuma ili kuwasadikisha wanaoikanusha Jumapili juu ya upotovu wao, wakithibitisha kwamba sheria za nchi zinapaswa kutiiwa kama sheria ya Mungu. Wataomboleza uovu mkubwa uliopo duniani, na kuendeleza ushuhuda wa waalimu wa dini, kwamba hali iliyoharibika ya maadili inasababishwa na kudhalilishwa kwa Jumapili. Kutakuwa na hasira kubwa dhidi ya wote wanaokataa kukubali ushuhuda wao.—The Great Controversy,591. [TA 264.1; UM Aya ya 12]

### Miujiza Katika Wakati wa Mwisho

Kabla ya mwisho wa wakati Shetani atafanya kazi kubwa zaidi ya maajabu. Kadiri uwezo wake unavyoenea, atafanya miujiza halisi. Maandiko yanasema: "Yeye....naye atawakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya." Sio kitu anachojidai kufanya. Kitu zaidi ya maigizo tu kinaoneshwa katika andiko hili.—Testimonies for the Church 5:698. [TA 264.2; UM Aya ya 13]

Hatupaswi kudanganyika. Matukio ya ajabu, ambayo Shetani atahusika nayo kwa karibu, yatafanyika hivi karibuni. Neno la Mungu linasema kwamba Shetani atafanya miujiza. Atawafanya watu kuwa wagonjwa, na kisha ghafla ataondoa kutoka kwao nguvu zake za kishetani. Kisha wao wataonekana kama vile wameponywa. Kazi hizi za uponyaji dhahiri zitawaweka Waadventista wa Sabato katika kujaribiwa.—Selected Messages 2:53. [TA 264.3; UM Aya ya 14]

Wengine watajaribiwa kupokea maajabu haya kama yametoka kwa Mungu. Wagonjwa wataponywa mbele yetu. Miujiza itafanyika katika macho yetu. Je, tuko tayari kwa ajili ya jaribu ambalo linatungoja, wakati maajabu ya uongo wa Shetani yatakapooneshwa kikamilifu zaidi? Je, watu wengi hawatanaswa na kuchukuliwa? Kwa kujitenga na kanuni zilizo wazi na amri za Mungu, na kuzifuata hadithi na hekaya za uongo, akili za wengi zinajiandaa kupokea mijuiza hii ya uongo. Ni lazima sote sasa tutafute kujizatiti kwa ajili ya shindano ambalo ni lazima tulishirki hivi karibuni. Imani katika Neno la Mungu, tunapaswa kujifunza kwa sala na kulitumia kwa vitendo, kwa vitakuwa ngao yetu kutokana na nguvu za Shetani na itatufanya kuwa washindi kwa damu ya

Kristo.—Testimonies for the Church 1:302. [TA 265.1; UM Aya ya 15]

### Pepo Wabaya Wakitenda Miongoni mwa Masalia

Maumbo ya wafu yataonekana kupitia udanganyifu wa hila wa Shetani, na wengi wataungana na yule apendaye na kufanya uongo...Miongoni mwetu wengine watajitenga na imani na kuzifuata roho zidanganyazo na Mafundisho ya imani ya mashetani.— The Upward Look, 317. [TA 265.2; UM Aya ya 16]

Watu wa umizimu watashinikiza jambo hilo ili kubishana na watumishi wanaoufundisha ile Kweli. Ikiwa watakataa, Watawapa changamoto ya kuwaambia hebu na wathubutu au kujitosa. Watanukuu Maandiko, kama vile Shetani alivyomfanyia Kristo. "Thibisheni mambo yote," watasema. Lakini wazo lao la kuthibitisha ni kusikiliza hoja zao za udanganyifu na kuwashawishi. Lakini katika mikusanyiko yao malaika wa giza watachukua maumbo ya marafiki waliokufa, na kuwasiliana nao kama malaika wa nuru. [TA 265.3; UM Aya ya 17]

Wapendwa wao wataonekana wamevaa mavazi ya nuru, kama walivyozoea kuonekana walipokuwa duniani. Watawafundisha, na kuzungumza nao. Na wengi watadanganywa na jambo hili la ajabu la onesho la nguvu za Shetani. Usalama pekee kwa watu wa Mungu ni kuwa na mawasiliano kamili ya Mungu, katika kuzijua vyema kabisa Biblia zao, na kuwa na akili juu ya sababu za imani yetu kuhusu hali ya wafu.— The Signs of the Times, Aprili 12, 1883. [TA 265.4; UM Aya ya 18]

Malaika waovu katika maumbo ya waumini watafanya kazi katika safu zetu ili kuleta roho kali ya kutokuamini. Hebu hata hali hii isikukatishe tamaa, bali ilete moyo wa Kweli katika msaada wa Bwana dhidi ya nguvu za mawakala wa shetani. Nguvu hizi za uovu zitakusanyika katika mikutano yetu, si kupokea baraka, bali kukanusha ushawishi wa Roho wa Mungu……[TA 266.1; UM Aya ya 19]

Hatupaswi kamwe kupata maneno ambayo midomo ya wanadamu inaweza kusema kuthibitisha malaika waovu katika kazi yao, lakini tunapaswa kurudia Maneno ya Kristo. Kristo alikuwa Mwalimu katika makusanyiko ya malaika hawa kabla hawajaanguka kutoka katika hali zao za juu.— Selected Messages 3:410. [TA 266.2; UM Aya ya 20]

Shetani na malaika zake watatokea katika dunia hii kama wanadamu, na watachanganyikana na wale ambao Neno la Mungu linasema, "Wengine wataiacha imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani."— Manuscript Releases 8:345. [TA 266.3; UM Aya ya 21]

Wakati madanganyo haya ya kiroho yanapofunuliwa kuwa vile yalivyo halisi ni—kazi za siri za pepo wabaya—wale wanaoyashiriki watakuwa kama watu

waliopoteza akili zao.— Manuscript Releases 8:345. [TA 266.4; UM Aya ya 22]

Niliwaona watu wetu katika dhiki kubwa, wakilia na kuomba, wakiomba dua kwa ahadi za hakika za Mungu, wakati waovu walikuwa wametuzunguka pande zote wakitudhihaki, na kutishia kutuangamiza. Walitukejeli kwa udhaifu wetu, walidhihaki uchache wa idadi yetu, na wakatuzomea kwa maneno ya kuumiza. Walitushtaki kwa kuchukua nafasi binasfi kinyume cha wengine wote wa dunia. Walikata rasilimali zetu ili tusiweze kununua wala kuuza, na kuelekeza katika umaskini wetu uliokithiri na hali duni. Hawakuweza kuona jinsi ambavyo tungeweza kuishi bila ulimwengu; tulikuwa tunautegemea ulimwengu, na tunapaswa tukubali mila, desturi na sheria za ulimwengu, au kundolewa ndani yake. Ikiwa sisi tulikuwa watu pekee ulimwenguni ambao Bwana aliwapenda, maonesho hayo dhidi yetu yalikuwa ya kutisha sana. [TA 266.5; UM Aya ya 23]

Walitangaza kwamba wao walikuwa na Ukweli, kwamba miujiza ilikuwa miongoni mwao, kwamba malaika kutoka mbinguni walizungumza nao na kutembea nao, ule uweza mkuu, na ishara na maajabu zilifanyika miongoni mwao, na hii ilikuwa ni Milenia ya Muda, ambayo wao walikuwa wakiitarajia kwa muda mrefu. Ulimwengu wote uligeuzwa nao (uliongolewa kwa hiyo sumu) na kupatana na sheria ya Jumapili, na hawa watu wachache walio wanyonge wakajitokeza kwa kuasi sheria za nchi na sheria za Mungu, na kudai kuwa wao ndiyo pekee duniani ambao wako sahihi.—Maranatha, 209. [TA 267.1; UM Aya ya 24]

### Malaika Watafanya Kazi iliyopuuzwa na Wanadamu

Wakati nguvu ya Bwana inapounganishwa na juhudi za kibinadamu, kazi itatanda kama moto kwenye makapi. Mungu atatumia mawakala ambao asili ya mwanadamu haitaweza kupambanua; malaika watafanya kazi ambayo watu wangeweza kuwa na baraka kwa kuitimiza, kama hawatapuuza madai ya Mungu.— The Review and Herald, December 15, 1885.. [TA 267.2; UM Aya ya 25]

### Malaika Watatoa ugavi wa Mahitaji ya Watu wa Mungu

Niliwaona watakatifu wakiyaacha majiji na vijiji, na kujumuika pamoja katika makundi, na kuishi katika maeneo ya faragha zaidi. Malaika wakawaandalia chakula na maji, huku waovu wakiteseka kwa njaa na kiu.— Early Writings, 282. [TA 268.1; UM Aya ya 26]

Katika wakati wa taabu kabla tu ya kuja Kwake Kristo, wenye haki watahifadhiwa kupitia huduma ya malaika wa mbinguni; lakini hakutakuwa na usalama kwa mvunjaji wa sheria ya Mungu. Malaika hawawezi kamwe kuwalinda wale wanaodharau moja ya maagizo ya Bwana.— Patriachs and Prophets, 256. [TA 268.2; UM Aya ya 27]

Katikati ya wakati wa taabu—taabu ambayo haijapata kuwako tangu kuwapo kwa taifa—wateule Wake watasimama bila kutikiswa. Shetani pamoja na majeshi yote ya uovu hawezi kuwaharibu watakatifu wa Mungu walio dhaifu zaidi. Malaika walio na nguvu nyingi watawalinda, na kwa ajili yao Yehova atajifunua kuwa "Mungu wa miungu," awezaye kuokoa kabisa wale ambao wamemtumaini Yeye.— Prophets and Kings, 513. [TA 268.3; UM Aya ya 28]

**Kujigeuza kwa Shetani**

Katika wakati huu mpinga-Kristo atatokea kama Kristo wa kweli, na kisha sheria ya Mungu itabatilishwa kikamilifu katika mataifa ya ulimwengu wetu. Uasi dhidi ya sheria takatifu ya Mungu utakuwa umeiva kabisa. Lakini kiongozi wa kweli wa uasi huu wote ni Shetani aliyevikwa kama malaika wa nuru. Watu watadanganyika na kumwinua mpaka mahali pa Mungu, na kumfanya kuwa mungu. Lakini Mweza wa yote ataingilia kati, na kwa makanisa yaliyoasi wanaoungana katika kuinuliwa kwa Shetani, hukumu itatoka. "Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja katika siku moja, mauti na huzuni; na njaa; naye atateketezwa kwa moto; kwa maana Bwana Mungu aliyemhukumu ni Mwenye nguvu."— Testimonies to Ministers and Gospel Workers, 62. [TA 268.4; UM Aya ya 29]

Akiwa amejigeuza kuwa malaika wa nuru, Shetani, atatembea duniani kama mtenda miujiza. Kwa lugha nzuri atawasilisha hisia za hali ya juu hisia. Maneno mazuri yatasemwa naye, na matendo mema kutendwa. Kristo ataigwa, lakini katika hatua pointi/hoja moja kutakuwa tofauti. Shetani atawageuza watu kutoka katika sheria ya Mungu. Bila ya kujali hilo, yeye ataiga haki ya kughushi/feki, hata yumkini, atawapoteza wale walio wateule. Wakuu wenye taji, marais, watawala katika mahali pa juu, watazisujudia nadharia zake za uwongo.— The Review and Herald, Agosti 17, 1897. [TA 269.1; UM Aya ya 30]

Haiwezekani kutoa wazo lolote la uzoefu wa watu wa Mungu ambao watakuwa hai duniani wakati utukufu wa mbinguni na kurudiwa kwa yale mateso ya zamani vitakapochanganywa. Watatembea katika nuru itokayo katika kiti cha enzi cha Mungu. Kwa njia ya malaika kutakuwa na mawasiliano ya mara kwa mara kati ya mbingu na nchi. Na Shetani, akiwa amezungukwa na malaika waovu, na kujidai kuwa yeye ni Mungu atafanya miujiza ya kila namna, ili kuwapoteza, hata yamkini, walio wateule. Watu wa Mungu hawatapata usalama wao katika kufanya miujiza, kwa sababu Shetani ataiga ile miujiza itakayofanywa.—Testimonies for Church 9:16. [TA 269.2; UM Aya ya 31]

Shetani anatayarisha madanganyo yake ambayo katika kampeni yake ya mwisho dhidi ya watu wa Mungu, ili wasielewe kwamba ni yeye. "Wala si ajabu; maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru."... Shetani atafikia kadiri ya uwezo wake wa kuwasumbua, kuwajaribu, na

kuwapotosha watu wa Mungu.— The Review and Herald, May 13, 1862. [TA 270.1; UM Aya ya 32]

Shetani ... atamwigiza Yesu Kristo, akifanya miujiza mikubwa; na watu wataanguka chini na kumwabudu kama Yesu Kristo. Tutaamrishwa tumwabudu kiumbe huyu ambaye ulimwengu utamtukuza kama Kristo. Tutafanya nini basi?— Waambie kwamba Kristo ametuonya dhidi ya adui wa namna hiyo, ambaye ni adui mbaya zaidi wa mwanadamu, na ambaye hujidai kuwa ni Mungu.— The Review and Herald, Desemba 18,1888. [TA 270.2; UM Aya ya 33]

Wakati unakuja ambapo Shetani atafanya miujiza mbele ya macho yako, akidai kwamba yeye ni Kristo; na ikiwa miguu yako si imara yaani ile isiyoimarishwa juu ya ukweli wa Mungu, ndipo utaongozwa mbali kutoka katika msingi wako.— The Review and Herald, Aprili 3, 1888. [TA 270.3; UM Aya ya 34]

Katika siku za mwisho Shetani atatokea kwa namna ya kuwafanya watu wamwamini kuwa ni Kristo ajaye mara ya pili duniani. Hakika atajigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Lakini huku akichukua mwonekano wa Kristo katika kila jambo, kulingana na mionekano bandia inayoendelea, hatamdanganya mtu ila wale tu..... wanaotafuta kuupinga au kuusukuma mbali Ukweli.— Testimonies for the Church 5:698. [TA 270.4; UM Aya ya 35]

**Malaika Waovu Wachochea Mateso**

Shetani anafanya kazi kutoka chini ili kuzichochea nguvu zake za kuzimu za muunganiko wa uovu dhidi ya wenye haki. Huwapa mawakala wa kibinadamu sifa zake mwenyewe. Malaika waovu wakiungana na watu waovu wataweka jitihada zao kunyanyasa, kutesa, na kuharibu.— The Upward Look,262. [TA 270.5; UM Aya ya 36]

Kila wakati pale ambapo Ukweli unakataliwa, mawazo ya watu yanakuwa na giza zaidi, mioyo yao huzidi kuwa migumu zaidi, hadi mwelekeo na mazoea hupata nguvu na ugumu na kuendekeza maisha ya kikafiri. Kwa kudharau maonyo ambayo Mungu ameyatoa, wataendelea kukanyaga mojawapo ya maagizo ya Amri kumi katika Maandiko Matakatifu (Dekalojia), hadi waongozwe kuwatesa wale wanaoyashikilia kuwa matakatifu. Kristo Yuko tayari kwa ajili ya kukabili kudharauliwa kwa Neno Lake na Watu wake. Kadiri mafundisho ya umizimu yanavyokubaliwa na makanisa, kizuizi kilichowekwa juu ya moyo ya watu kinaondolewa; na kukiri dini itakuwa vazi la kusitiri uovu mbaya zaidi. Imani katika miujiuza ya kiroho hufungua mlango kwa roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani, na hivyo ushawishi wa malaika waovu utasikika katika makanisa.— The Great Controversy,603, 604. [TA 271.1; UM Aya ya 37]

Matukio ya usaliti, kukataliwa, na kusulubishwa kwa Kristo yatarudiwa tena, na yataigizwa tena kwa hali ya juu sana. Watu watajazwa na tabia za Shetani. Udanganyifu wa adui mkuu wa Mungu na mwanadamu atakuwa na nguvu nyingi.—Selected Messages 3:415. [TA 271.2; UM Aya ya 38]

Roho ya mapepo yaani kishetani huwamiliki wanadamu katika ulimwengu wetu Nguvu za pepo ... itamrarua na kumwangamiza mwanadamu aliyeundwa katika mfano wa Mungu kwa sababu ... kwa kuwa mtu hawezi kudhibiti dhamiri ya ndugu yake na kumfanya akose kuwa mwaminifu kwa sheria takatifu ya Mungu.— The Upward Look, 285. [TA 271.3; UM Aya ya 39]

Watakatifu walipokuwa wakiondoka mijini na vijijini, walifuatwa na kukimbizwa na waovu, waliotaka kuwaua. Lakini mapanga yaliyoinuliwa kuua watu wa Mungu yalivunjika na kuanguka bila nguvu kama majani makavu wanayokula ng'ombe. Malaika wa Mungu waliwalinda watakatifu.— Early Writings, 284, 285. [TA 272.1; UM Aya ya 40]

Katika siku ya majaribu makali Kristoatasema, "Njoni, watu wangu; ingia ndani ya vyumba vyako, na ufunge milango yako karibu nawe; jifiche mwenyewe kwa kitambo kidogo, hata ghadhabu hiyo itakapopita." Je, ni vyumba gani wanavyopaswa kujificha? Hivyo vyumba ni ulinzi wa Kristo na malaika watakatifu. Watu wa Mungu hawako kwa wakati huu wote katika sehemu moja. Wako katika makundi mbalimbali, na katika sehemu zote za dunia.—Historical Sketches of Foreign Missions of the Seventh -day Adventists, 158. [TA 272.2; UM Aya ya 41]

Katika matukio ya mwisho ya historia ya dunia hii, wakati nguvu inachukua miliki ya kila kipengele cha kidunia, Bwana anahitaji tuwe macho kwa ulinzi pasipo kutulia. Lakini hatujaachwa kupambana peke yetu. Huku kukiwa na hatari zinazoongezeka kwa kila upande, wale wanaotembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu, bila kutumaini hekima yao wenyewe, watakuwa na Malaika kama wasaidizi na walinzi wao. Wakati wa hatari kubwa watajua uwezo wa majaliwa na utunzaji wa Mungu.— The Review and Herald, Aprili 25, 1907. [TA 272.3; UM Aya ya 42]

Wakati wa usiku tukio la kuvutia sana lilipita mbele yangu. Kulionekana kuwa na machafuko makubwa na vita vya majeshi. Mjumbe kutoka kwa Bwana akasimama mbele yangu, akasema, waite wale wa nyumbani mwako. Nitakuongoza; Nifuate." Aliniongoza kupita gizani, kupitia msitu, kisha kupitia mapango ya milima, Naye akasema, "Hapa uko salama." Kulikuwa na wengine ambao walikuwa wameongozwa kufika hapa kupumzishwa haya. Mjumbe wa mbinguni alisema, "Wakati wa taabu umekuja kama mwivi wa usiku, kama Bwana alivyowaonya wakati huo utakuja."—Maranatha, 270. [TA 272.4; UM Aya ya 43]

## Utendaji Wa Shetani Wa Maigizo Baada Ya Kufungwa Kwa Mlango Wa Rehema

Ghadhabu ya Shetani huongezeka kadiri muda wake unavyopungua, na kazi yake ya udanganyifu na uharibifu inafikia kilele chake wakati wa taabu. Ustahimilivu wa Mungu umekwisha. Ulimwengu umekataa rehema Zake, umedharau upendo Wake, na kuikanyaga sheria Yake. Waovu wamevuka kiwango wa rehema yao, na Bwana anaondoa Ulinzi Wake, na kuwaachia rehema ya kiongozi waliyemchagulia. [TA 273.1; UM Aya ya 44]

Kama kitendo cha kutawazwa katika tamthilia kuu ya udanganyifu, Shetani mwenyewe atajaribu kujifananisha na Kristo. Kanisa limekiri kwa muda mrefu kutazamia ujio wa Mwokozi kama utimilifu wa matumaini yake. Sasa mdanganyifu mkuu atafanya ionekane kuwa Kristo amekuja. Katika sehemu mbalimbali za dunia, Shetani atajidhihirisha miongoni mwa wanadamu kama kiumbe mkuu mwenye mng'ao unaometameta, anayefanana na maelezo ya Mwana wa Mungu yaliyotolewa na Yohana katika Ufunuo. Utukufu unaomzunguka haufananishwi na chochote ambacho macho ya mwanadamu yamewahi kuona. Kelele ya ushindi inasikika hewani, "Kristo amekuja! Kristo amekuja!" [TA 273.2; UM Aya ya 45]

Watu wanamsujudia kwa kicho, huku akiinua mikono yake, na kutamka baraka juu yao, kama Kristo alivyowabariki wanafunzi Wake alipokuwa duniani. Sauti yake ni laini, imetulia, na imejaa muziki. Kwa sauti ya upole, za huruma anawasilisha baadhi ya Kweli zile zile za neema, za mbinguni ambazo Mwokozi alizitamka; anaponya magonjwa ya watu, na kisha, katika tabia yake ya kudhaniwa ya Kristo, anadai kuwa amebadilisha Sabato hadi Jumapili, na kuwaamuru wote kuitakasa siku ambayo ameibariki. Anatangaza kwamba wale wanaodumu katika kuitunza katika utakatifu siku ya saba wanalitukana jina lake kwa kukataa kuwasikiliza malaika waliotumwa kwao kwa nuru na Kweli. Huu ndio uongo wenye nguvu, wenye ustadi/ugwiji na usio na kipimo.—The Spirit of Prophecy 4:441,442. [TA 273.3; UM Aya ya 46]

Shetani anaona kwamba anakaribia kupoteza nafasi na kesi yake. Hawezi kuifagia dunia nzima. Hufanya juhudi ya mwisho ya kukata tamaa kuwashinda waaminifu kwa udanganyifu. Anafanya hivyo katika kujifananisha na Kristo. Anavaa mavazi ya kifalme ambayo yamekuwa kwa usahihi kama yalivyoelezwa katika maono ya Yohana. Ana uwezo wa kufanya hivi. Ataonekana kwa wafuasi wake waliodanganyika, ulimwengu wa Kikristo ambao hakuipoea ile Kweli, bali huufurahia ule udhalimu ... kama Kristo anayekuja mara ya pili. [TA 274.1; UM Aya ya 47]

Anajitangaza kuwa Kristo, na anaaminika kuwa Kristo, mzuri, mwenye fahari akiwa amevikwa adhama na, kwa sauti nyororo na maneno ya kupendeza, yenye utukufu unaopitwa na kitu chochote mwanadamu alichowahi

kuona.Kisha wafuasi wake waliodanganywa, na waliopotoshwa watapaza sauti ya ushindi, “Kristo amekuja mara ya pili! Kristo amekuja! Ameinua mikono Yake kama vile alivyofanya alipokuwa juu yake nchi, na kutubariki.” ……. [TA 274.2; UM Aya ya 48]

Watakatifu wanatazama kwa mshangao. Je, wao pia watadanganywa? Je, watamwabudu Shetani? Malaika wa Mungu wako pamoja nao. Sauti ya wazi, dhabiti na nzuri lkama muziki inasikika, “Tazameni juu.” [TA 274.3; UM Aya ya 49]

Kuna lengo moja mbele ya wanaosali—cha mwisho na cha milele wokovu wa roho zao. Lengo hili lilikuwa mbele yao kila wakati- kwamba uzima wa milele umeahidiwa wale wanaovumilia hadi mwisho. Tazama, inavutia jinsi gani matamanio yao yalivyokuwa ya dhati na makini!. Hukumu na umilele vilikuwa vikionekana. Macho yao kwa imani yalikazwa katika kiti cha enzi kinachowaka, ambacho mbele yake wale waliovaa mavazi meupe watasimama. Hili liliwazuia wasifanye dhambi. [TA 275.1; UM Aya ya 50]

Jitihada moja zaidi, na kisha udanganyifu wa mwisho wa Shetani utatumika. Anasikia kilio kisichokoma cha kuja kwa Kristo, ili Kristo awakomboe. Mbinu hii ndiyo ya mwisho ambayo inamwigiza Kristo, na kuwafanya wafikiri kuwa maombi yao yamejibiwa.— Last Day Events, 164, 165 .. [TA 275.2; UM Aya ya 51]

**Malaika na Amri ya Kifo kwa Ulimwengu wote**

Kama watu wangeweza kuona kwa maono ya mbinguni, wangeona makundi ya malaika walio hodari katika nguvu wakisimama juu ya wale ambao walishika Neno la subira ya Kristo. Kwa huruma, Malaika wameshuhudia dhiki zao, na wamesikia maombi yao. Wanasubiri Neno la Kamanda wao ili wawaondoe katika hatari yao. Lakini wanapaswa kusubiri kidogo. Watu wa Mungu wanapaswa kukinywea kikombe, na kubatizwa kwa ubatizo Wake. Ucheleweshaji huo, ulio wa uchungu kwao, ndio jawabu bora la maombi yao. Kadiri wanavyojitahidi kumngoja kwa uaminifu Bwana ili atende, wao wanaongozwa kuizoesha imani, tumaini, na subira yao, ambayo wamekuwa nayo kidogo sana wakati wa uzoefu wao wa kidini….[TA 275.3; UM Aya ya 52]

Walinzi wa mbinguni, waaminifu kwa dhamana yao, wanaendelea na uangalizi wao. Ingawa amri ya jumla imeweka tarehe maalum ambapo watunza-amri za Mungu wanaweza kuuawa, adui zao wakati fulani wataitarajia amri, na kabla ya muda maalum uliowekwa, watajitahidi kuchukua maisha yao. Lakini hakuna anayeweza kupita walinzi hodari waliowekwa kuizunguka kila nafsi ya mwaminifu.— The Great Controversy, 630, 631.. [TA 275.4; UM Aya ya 53]

### Mungu Aingilia Pale Waovu Wanapojaribu Kuwaua Watu wa Mungu

Watu wa Mungu—wengine wakiwa katika seli za gereza, wengine wakiwa wamefichwa katika maeneo ya siri msituni na milimani—bado wanaomba ulinzi wa Mungu, wakati katika kila mahali makundi ya watu wenye silaha, wakihimizwa na majeshi ya malaika waovu, wanajitayarisha kwa kazi ya mauaji. Ni sasa, katika saa ya uhitaji mkuu kabisa, ambapo Mungu wa Israeli ataingilia kati kuwaokoa wateule Wake…..[TA 276.1; UM Aya ya 54]

Ni katika usiku wa manane (saa sita usiku) ndipo Mungu anadhihirisha nguvu Zake kwa ajili ya ukombozi ya watu Wake. Jua linaonekana, linaangaza kwa nguvu Zake. Ishara na maajabu yanafuatana kwa haraka haraka. Waovu hutazama kwa hofu na mshangao juu ya tukio, wakati wenye haki wakitazama kwa furaha kuu ishara za ukombozi wao...Mawingu meusi, mazito yanatokea, na yanagongana. Katikati ya hasira mbingu kuna mwanya mmoja wenye utukufu usioelezeka, ambamo kunatokeaa sauti ya Mungu…..[TA 276.2; UM Aya ya 55]

Sauti hiyo inatikisa mbingu na ardhi. Kunatokea tetemeko kubwa sana la ardhi, "ambalo jinsi halijakuwapo tangu wanadamu wawe juu ya nchi hapakuwa namna ile, jinsi lilivyokuwa kubwa tetemeko hilo." Anga linaonekana kufunguka na kufunga. Utukufu kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu unaonekana kumetameta. Milima inatikisika kama mwanzi katika upepo, na miamba iliyopasuka inatawanyika kila upande. Kuna kishindo kama tufani inayokuja. Bahari inachafuka kwa hasira. Kunasikika mlio wa yowe la tufani, kama sauti ya mapepo waliotumwa kwa misheni ya kuangamiza. Dunia nzima inanyumbuka ikipanda na kushuka kama mawimbi ya bahari. Uso wake unavunjika. Misingi yake milima, yenyewe inaonekana kuong'oka. Vilele vya mlima vinazama. Visiwa vinavyokaliwa na watu vinatoweka. [TA 276.3; UM Aya ya 56]

Radi kali zinapiga kutoka mbinguni, na kuifunika dunia kama shuka la ndimi za moto. Juu ya kishindo kikali cha ngurumo, sauti za ajabu na za kutisha, zinatangaza adhabu na ole ya waovu. Wale ambao hapo kabla walikuwa wakorofi, wasiojali, wenye majivuno, wasiotii na wenye kudharau, wakifurahia ukatili wao kwa watu wa Mungu wanaozishika amri, sasa wanazidiwa na fadhaa, na kutetemeka kwa hofu. Mayowe yao yanasikika juu ya sauti ya vitu vya asili. Mashetani wanakiri uungu wa Kristo, na kutetemeka mbele ya uwezo Wake, wakati wanadamu wanatetemeka kwa kuomba rehema, na kutetemeka kwa hofu kuu.—Great Controversy, 635-638. [TA 277.1; UM Aya ya 57]

### Ujio wa Pili wa Kristo

Kristo anakuja na nguvu na utukufu mkuu. Anakuja na utukufu Wake Mwenyewe, na utukufu wa Baba. Anakuja na Malaika watakatifu wote pamoja

Naye. Wakati ulimwengu wote ukiwa na giza, kutakuwa na nuru katika kila makao ya watakatifu. Wao wataiona nuru ya kwanza ya kutokea Kwake mara ya pili.—Christ's Object Lessons, 420. [TA 277.2; UM Aya ya 58]

Punde macho yetu yalivutwa kuelekea mashariki, kuna wingu dogo jeusi lilikuwa limetokea, karibu nusu ya ukubwa wa mkono wa mtu, nasi sisi sote tulijua hiyo ilikuwa ni ishara ya Mwana wa Adamu. Kwa ukimya mzito sote tulitazama juu ya wingu lilipokaribia zaidi, na kuwa jepesi, tukufu, na utukufu zaidi, hata likawa wingu kubwa jeupe. Chini ilionekana kama moto; upinde wa mvua ulikuwa juu ya wingu, na pande zote, makumi elfu ya malaika, wakiimba wimbo wa kupendeza sana; na juu yake Mwana Adamu ameketi.—Testimonies for the Church 1:60. [TA 277.3; UM Aya ya 59]

Hakuna lugha ya kibinadamu inayoweza kueleza matukio ya ujio wa pili wa Mwana wa Adamu katika mawingu ya mbinguni …..Atakuja akiwa amevaa vazi la nuru, ambalo amelivaa tangu milele huko nyuma.— The Review and Herald, September 5, 1899. [TA 278.1; UM Aya ya 60]

Msafara mtakatifu wa malaika, wakiwa na taji zao angavu, zinazometa juu ya vichwa vyao, wakamsindikiza katika njia Yake.— Spiritual Gifts 1:206,207. [TA 278.2; UM Aya ya 61]

Katikati ya msukosuko wa dunia, mwanga wa radi na ngurumo, sauti ya Mwana wa Mungu inawaita watakatifu waliolala. Anayatazama makaburi ya watu wema, kisha akiinua mikono yake juu mbinguni, analia, "Amkeni, amkeni, amkeni, ninyi mlalao mavumbini; na msimame!" …...[TA 278.2; UM Aya ya 62]

Wote wanatoka makaburini mwao wakiwa na kimo kilekile walichoingia nacho kaburini. Adamu, ambaye anasimama kati ya umati uliofufuka, ni wa kimo kikubwa na umbo la fahari, ila kimo chake kipo chini kidogo ya Mwana wa Mungu. Anawasilisha tofauti kubwa ya watu wa vizazi vingine vya nyuma; katika hili jambo moja linaonyeshwa uchakavu mkubwa wa jamii ya wanadamu. Lakini wote huinuka na upya na nguvu za ujana wa milele. Mwili wa kufa, wa kuharibika, usio na uzuri, uliokuwa umetiwa unajisi na dhambi, unakuwa mkamilifu, mzuri, na usiokufa. Kasoro zote na ulemavu huachwa kaburini.—The Great Controversy, 644,645. [TA 278.4; UM Aya ya 63]

Yeye Kristo alikufa kwa ajili yetu, na kufufuka kwa ajili yetu, ili sisi tupate kutoka kaburini hadi kwenye ushirika mtukufu na malaika wa mbinguni, kukutana na wapendwa wetu na kutambua nyuso zao, kwani. Kufanana na Kristo hakujaharibu sura yao, bali kuibadili kuwa kama Sura Yake ya tukufu. Kila mtakatifu aliyeunganishwa katika uhusiano wa familia hapa watajuana huko.—Selected Messages 3:316. [TA 279.1; UM Aya ya 64]

Wenye haki walio hai watabadilishwa "kwa dakika moja, kufumba na kufumbua." Kwa sauti ya Mungu walitukuzwa: sasa wamefanywa kuwa na hali

ya kutokufa, na pamoja na watakatifu waliofufuka wananyakuliwa ili kumlaki Bwana wao hewani. Malaika "huwakusanya wateule kutoka pepo nne, kutoka mwisho mmoja wa mbingu hadi mwisho mwingine."— The Great Controversy, 645. [TA 279.2; UM Aya ya 65]

Watoto wadogo huchukuliwa na malaika watakatifu hadi kwenye mikono ya mama zao.—Great Controversy ,645. [TA 279.3; UM Aya ya 66]

Kadiri watoto wachanga wanavyotoka katika hali ya kutoweza kufa kutoka kwenye vitanda vyao vyenye vumbi, mara moja wanapaa kuelekea kwenye mikono ya mama zao. Wanakutana tena, na kamwe hawataachana tena. Lakini wengi wa watoto wadogo hawa, hawana mama zao pale. Tunasikiliza bure wimbo wa kunyakuliwa wa ushindi kutoka kwa mama. Malaika huwapokea watoto wasio na mama na kuwaongoza kwenye mti wa uzima.— The Youth's Instructor, April 1, 1858. [TA 279.4; UM Aya ya 67]

Marafiki waliotenganishwa kwa muda mrefu na kifo wameunganishwa, nao kamwe hawatatengana tena, na kwa nyimbo za furaha wanaelekea pamoja katika mji wa Mungu. [TA 279.5; UM Aya ya 68]

Kila upande wa gari la wingu kuna mabawa, na chini yake kuna magurudumu hai; na magari yanapopaa juu, magurudumu yanapaza sauti yakisema; "Mtakatifu," na mbawa, zinapopaa, hulia, "Mtakatifu," na mfuatano ya malaika wanapiga kelele, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mwenyezi." Na waliokombolewa wanapaza sauti, "Haleluya!" gari linaposonga kuelekea Yerusalemu Mpya.— The Great Controversy, 645. [TA 280.1; UM Aya ya 69]

Sisi sote tuliingia lile wingu pamoja, tukasafiri siku saba kwenda kwenye bahari ya kioo, wakati Yesu alipoleta taji, na kwa mkono Wake wa kuume akaziweka juu ya vichwa vyetu. Pale Alitupa vinubi vya dhahabu na mitende ya ushindi.— Early Writings, 16. [TA 280.2; UM Aya ya 70]

Kuna nguzo za malaika kila upande, na waliokombolewa wa Mungu hutembea katikakati ya makerubi na maserafi. Kristo anawakaribisha na kuweka juu yao baraka Zake. [TA 280.3; UM Aya ya 71]

"Vema, mtumwa mwema na mwaminifu: ... ingia katika furaha Bwana wako."—The S.D.A. Bible Commentary 6:1093. [TA 280.4; UM Aya ya 72]

### Shetani na Malaika Wake Wabaya Kufungwa Katika Dunia Hii

Dunia yote inaonekana kama jangwa lenye ukiwa. Magofu ya miji na vijiji vilivyoharibiwa na tetemeko la ardhi, miti iliyong'olewa, miamba chakavu iliyotupwa nje na bahari au iliyong'olewa kutoka kwenye ardhi yenyewe, yametawanyika juu ya uso wake, wakati mashimo na mapango makubwa yanaashiria mahali milima ilipong'olewa misingi yake. Hapa patakuwa nyumba

ya Shetani pamoja na malaika wake waovu kwa muda wa miaka elfu moja. Hapa atafungiwa, akitangatanga juu na chini ya uso uliovunjika wa dunia, na kuona matokeo ya uasi wake dhidi ya sheria ya Mungu. Kwa miaka elfu moja ataweza kufurahia matunda ya laana ambayo ameisababisha. Akiwa peke yake duniani, hatakuwa na nafasi hiyo ya kwenda sayari nyingine, kuwajaribu na kuwaudhi wale ambao hawajapata kuanguka.— The Spirit of Prophecy 4:474, 475. [TA 280.5; UM Aya ya 73]

Kwa njia yake mwenyewe ya utendaji Shetani ametengeneza mnyororo ambao kwa huo atafungwa …..Viumbe wote ambao hawajaanguka sasa wameungana katika kudai Sheria ya Mungu haibadiliki. Wanaiunga mkono serikali Yake, Yeye ambaye, ili kumkomboa mdhambi, hakumzuilia Mwanawe. Sheria Yake imethibitishwa kuwa haina makosa. Serikali Yake iko salama milele.— The Signs Of the Times, Agosti 27, 1902. [TA 281.1; UM Aya ya 74]

Hapa patakuwa ni makazi ya Shetani pamoja na malaika wake waovu kwa miaka elfu moja. Akiwa amezuliwa kukaa hapa katika dunia hii peke yake, hatakuwa na ufikiaji wa ulimwengu mwingine kuwajaribu na kuwaudhi wale ambao hawajawahi kuanguka. Ni kwa dhana hii ndiyo atakuwa amefungwa.— The Great Controversy, 659. [TA 281.2; UM Aya ya 75]

Nilisikia kelele za ushindi kutoka kwa malaika na kutoka kwa watakatifu waliokombolewa, ambayo ilisikika kama ala elfu kumi za muziki, kwa sababu hawakusumbuliwa tena na kujaribiwa na Shetani, na kwa sababu wakazi wa dunia nyingine walikombolewa dhidi ya uwepo wa majaribu yake (adui).— Early Writings, 290. [TA 281.3; UM Aya ya 76]

## SURA YA 21

## MALAIKA KATIKA ULIMWENGU UJAO MBINGUNI

### Tujapofika Mbinguni

Nikaona idadi kubwa sana ya malaika wakileta kutoka katika mji ule wenye utukufu taji kwa kila mtakatifu, na jina lake huyo mtakatifu likiwa limeandikwa juu yake. Yesu alipoita taji, malaika walizikabidhi Kwake, na kwa Mkono Wake

wa kuume, Yesu mpendwa aliweka taji juu ya vichwa vya watakatifu. Kwa namna ile ile malaika walivyoleta vinubi, na Yesu alivikabidhi pia kwa watakatifu. Malaika viongozi wakaanza kupiga nota, na kisha kila sauti ikapazwa kwa shukrani, furaha na sifa, na kila mkono ukazipiga nyuzi za kinubi kwa ustadi; wakitoa muziki mzuri kwa wingi na ukamilifu. Kisha nalimwona Yesu akiongoza kundi la watu waliokombolewa hadi kwenye lango la mji. Akalishika lango na kulirudisha nyuma kwa ya bawaba zake zinazometameta, na kuyasihi mataifa ambayo yalikuwa yameihifadhi Kweli yaingie.— Early Writings, 288. [TA 283.1; UM Aya ya 1]

Kutoka katika midomo ya Mfalme wa utukufu, baraka itayafikia masikio yao kama muziki mzuri zaidi, “Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Hivyo waliokombolewa watakaribishwa kwenye makao ambayo Yesu anayaandaa kwa ajili yao. Hapo marafiki zao hawatakuwa wanyonge wa dunia, bali wale ambao kwa msaada wa Bwana wameunda tabia kamilifu. Kila mwelekeo wa dhambi, kila kutokamilika, na udhaifu kumeondolewa kwa damu ya Kristo; na ubora na mwangaza Wake wa utukufu, upitao sana mng'ao wa jua katika mng'aro Wake wa kupendeza, unatolewa kwao. Na uzuri wa maadili, ukamilifu wa tabia Yake, unang'aa kupitia kwao, kwa thamani kubwa kupita hii fahari ya nje. Hawana hatia mbele ya kile kiti cha enzi kikubwa cheupe, wakishiriki adhama na faida za malaika.— The Watchman,March 31, 1908. [TA 283.2; UM Aya ya 2]

Waliokombolewa watakutana na kutambua wale ambao umakini wao umewaelekeza kwa Mwokozi aliyetukuka. Ni baraka ya jinsi gani watakayosema watu hawa! “Nilikuwa mwenye dhambi,” watasema, “bila Mungu na bila tumaini katika ulimwengu, na ulikuja kwangu na kuvuta umakini wangu kwa Mwokozi wa thamani kama tumaini langu la pekee ” Wengine watasema, “Nilikuwa mpagani katika nchi za makafiri. Ukawaacha marafiki zako na ukaja kunifundisha jinsi ya kumpata Yesu, na kumwamini Yeye kama Mungu wa pekee na wa Kweli. Nilibomoa sanamu zangu, na kumwabudu Mungu, na sasa ninamwona uso kwa uso. Nimeokoka, nimeokolewa milele, daima kumtazama Yeye nimpendaye…” [TA 284.1; UM Aya ya 3]

Wengine watatoa shukrani zao kwa wale waliolisha wenye njaa na kuwavika walio uchi. “Wakati nikiwa nimekata tamaa katika kutokuamini, Bwana alikutuma kwangu,” watasema “kuniambia maneno ya tumaini na faraja. Uliniletea chakula kwa mahitaji yangu ya kimwili, na ulinifungulia Neno la Mungu, ukiamsha mahitaji yangu ya kiroho. Ulinichukulia kama ndugu/dada. Ulinionea huruma katika huzuni yangu, na kurejesha nafsi yangu iliyojeruhiwa na kuumizwa, ili niweze kuushika mkono wa Kristo ulionyooshwa kuniokoa. Katika ujinga wangu ulinifundisha kwa uvumilivu kwamba nilikuwa na Baba wa mbinguni ambaye ananijali. Ulinisomea ahadi zenye thamani za Neno la Mungu.

Ulinipa imani kwamba Yeye angeniokoa. Moyo wangu ulilainishai, ukatiishwa, na kuvunjika, kadiri nilivyotafakari sadaka ambayo Kristo alikuwa ameitoa. Mimi niko hapa, nimeokolewa, nimeokolewa milele kuishi mbele Zake, na kumsifu Yeye aliyetoa uhai Wake kwa ajili yangu." [TA 284.2; UM Aya ya 4]

Je, kutakuwa na furaha ya namna gani hao waliokombolewa wanapokutana na kuwasalimia na wale ambao wamekuwa na mzigo moyoni kwa ajili yao!—Review na Herald, January 5, 1905. [TA 285.1; UM Aya ya 5]

Ikiwa vijana watampokea Kristo na kumwamini, wataletwa katika uhusiano wa karibu na Mungu. Atawapa nguvu kuwa wana wa Mungu, kushirikiana na wakuu wa juu katika ufalme wa mbinguni, kuungana na Gabrieli, na makerubi na maserafi, pamoja na malaika wa kawaida na malaika mkuu. "Na alinionesha mto safi wa maji ya uzima, angavu kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu na Mwana-Kondoo. Katikati ya barabara zake, na kando ya mto ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda ya namna kumi na mbili, na kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti yalikuwa ya kuwaponya mataifa. Na hakutakuwa na laana tena; lakini kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwa ndani yake; na watumishi Wake watamtumikia. Nao watamwona uso Wake, na Jina Lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. Wala hapatakuwa na usiku huko; na hawana haja ya taa, wala mwanga wa jua; kwa kuwa Bwana Mungu hutoa mwanga kwao; nao watatawala milele na milele."—Spalding and Magan Collection, 52. [TA 285.2; UM Aya ya 6]

Sio mpaka majaliwa ya Mungu yaonekane katika nuru ya umilele ndipo tutaelewa nini tunadaiwa kwa utunzaji na uingiliaji kati wa Malaika Zake Bwana. Viumbe wa mbinguni wameshiriki kikamilifu katika maisha na mambo ya wanadamu.—Education, 304. [TA 286.1; UM Aya ya 7]

Katika maisha ya baadaye tutaelewa mambo ambayo yalituchanganya sana hapa. Tutatambua msaidizi tuliyekuwa naye alikuwa na nguvu gani, na jinsi gani Malaika wa Mungu walitumwa kutulinda tulipokuwa tukilifuata shauri la Neno la Mungu.— The Signs of the Times, Januari 3,1906. [TA 286.2; UM Aya ya 8]

Katika ulimwengu ujao, Kristo atawaongoza waliokombolewa kando ya mto wa uzima, na atawafundisha masomo ya ajabu ya ile Kweli. Atawafunulia siri za asili. Wataona kwamba Mkono ule wa msanifu mkuu unashikilia malimwengu katika nafasi yake. Watatazama ustadi ulioonyeshwa na Msanii mkuu katika kupaka rangi maua ya kondeni, na watajifunza makusudi ya Baba Mwenye rehema, ambaye husambaza kila mionzi ya nuru, na pamoja na malaika watakatifu, wale waliokombolewa watakubali katika nyimbo za sifa na shukrani upendo mkuu wa Mungu kwa ulimwengu usio na shukrani. Ndipo wataelewa kuwa "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima

wa milele."— The Review and Herald, January 3, 1907. [TA 286.3; UM Aya ya 9]

Warithi wa neema hapo wana uhusiano mtakatifu zaidi na Mungu kuliko malaika ambao hawajaanguka.—Testimonies for the Church 5:740. [TA 286.4; UM Aya ya 10]

Kwa uwezo wa upendo Wake, kwa njia ya utii, mwanadamu aliyeanguka, na mnyoo/mdudu katika vumbi, yeye anapaswa kugeuzwa, ili kufaa kuwa mwana-familia ya mbinguni, mshiriki katika enzi za milele za Mungu na Kristo na malaika watakatifu. Mbingu itashinda, kwani nafasi iliyoachwa wazi kwa anguko la Shetani na jeshi lake itajazwa na waliokombolewa wa Bwana.-The Upward Look, 61. [TA 287.1; UM Aya ya 11]

Mungu alimuumba mwanadamu kwa ajili ya utukufu Wake, kwamba baada ya mtihani na majaribu familia ya kibinadamu iweze kuwa moja na familia ya mbinguni. Lilikuwa Kusudi la Mungu la kujaza tena mbingu kwa familia ya kibinadamu, ikiwa wangejionyesha kuwa watiifu kwa kila Neno Lake. Adamu alipaswa kujaribiwa ili kuona kama atakuwa mtiifu, kama malaika waaminifu, au atakuwa yule asiyetii.— The S.D.A. Bible Commentary 1:1082. [TA 287.2; UM Aya ya 12]

Upendo na huruma ambazo Mungu Mwenyewe amezipanda rohoni, zitapata mazoezi ya kweli na matamu zaidi huko. Ushirika safi na viumbe watakatifu, maisha ya kijamii yenye usawa pamoja na malaika waliobarikiwa na waaminifu wa zama zote ambao wameosha mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo, mahusiano matakatifu yanayounganisha pamoja "familia yote ya mbinguni na duniani" (Waefeso 3:15)—haya hukamilisha furaha ya waliokombolewa.— The Great Controversy, 677. [TA 287.3; UM Aya ya 13]

**Hukumu ya Miaka Elfu Moja**

Wakati wa miaka elfu katika ufufuo wa kwanza na ufufuo wa pili, hukumu ya waovu hufanyika. Danieli anatangaza kwamba alipokuja Yule Mzee wa siku, "watakatifu wa Aliye Juu wakapewa hukumu." Kwa wakati huu wenye haki wanatawala kama wafalme na makuhani kwa Mungu. Yohana katika Ufunuo anasema, "Nikaona viti vya enzi, nao wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu." "Watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja Naye miaka elfu." Ni wakati huu ambapo, kama ilivyotabiriwa na Paulo, "Watakatifu watauhukumu ulimwengu." Wakiungana na Kristo kuwahukumu waovu, wakilinganisha matendo yao na kitabu cha sheria, yaani Biblia, na kuamua kila kesi kwa kadiri ya matendo yaliyofanyika kimwili. Shetani pia na malaika waovu wanahukumiwa na Kristo na watu Wake.— The Southern Watchman, March 14, 1905. [TA 287.4; UM Aya ya 14]

**Ujio wa Tatu wa Kristo**

Mwishoni mwa ile miaka elfu moja, Kristo atarudi tena duniani. Anaambatana na jeshi la waliokombolewa, na kusindikzwa na msururu wa malaika. Anaposhuka kwa utukufu wa kutisha, anaamuru waovu waliokufa waamke ili kupokea adhabu na ole yao. Linatoka, jeshi kubwa, lisilohesabika kama mchanga wa bahari. Ni tofauti iliyoje ukilinganisha na wale waliofufuliwa katika ufufuo wa kwanza! Wenye haki walivikwa ujana na uzuri usioweza kufa. Waovu hubeba athari ya ugonjwa na hali ya kifo. [TA 288.1; UM Aya ya 15]

Kila jicho katika umati huo mkubwa limegeuzwa kutazama utukufu wa Mwana wa Mungu. Kwa sauti moja majeshi ya waovu yanapaza sauti, "Amebarikiwa Yeye ajaye kwa Jina la Bwana!" Sio upendo kwa Yesu ambao unawahamasisha kufanya tamko hili. Nguvu ya Ukweli inawahimiza kutamka Maneno haya kutoka katika midomo isiyotaka. Kama waovu walivyoingia makaburini mwao, ndivyo wanavyotoka, wakiwa na uadui uleule kwa Kristo, na roho ile ile ya uasi. Hawapewi rehema mpya ya kurekebisha kasoro za maisha yao yaliyopita. Hakuna lolote la maana ambalo lingepatikana kwa njia hii. Maisha yote ya uasi hayakulainisha mioyo zao. Kama wangepewa nafasi ya pili ya rehema, basi ingetumiwa kama ilivyokuwa ile mara ya kwanza, yaani watajishugulisha katika kukwepa matakwa ya Mungu na kuchochea uasi dhidi Yake. [TA 288.2; UM Aya ya 16]

Kristo anashuka juu ya Mlima wa Mizeituni, ambapo kutokea huko, baada ya ufufuo Wake, alipaa, na ambapo malaika walirudia ahadi ya kurudi Kwake. Nabii asema hivi: "Bwana Mungu wangu atakuja, na watakatifu wote pamoja Naye." "Na siku hiyo miguu Yake itasimama juu ya Mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki, nao Mlima wa Mizeituni utapasuka katikati Yake, ... na litakuwako huko bonde kubwa sana." "Na Bwana atakuwa mfalme juu ya dunia yote; katika siku hiyo Bwana atakuwa Mmoja, na Jina Lake Moja." Zekaria 14:5, 4,9.—The Great Controversy, 662, 663. [TA 289.1; UM Aya ya 17]

Kisha tukatazama juu na kuona Jiji kubwa na zuri, pamoja Misingi kumi na miwili, milango kumi na miwili, mitatu kila upande, na Malaika kwenye kila lango. Tulipiga kelele, Jiji! Mji mkuu! Unakuja chini kutoka kwa Mungu mbinguni! Nao Ukashuka katika fahari yake yote,na utukufu unaing'aa, na kukaa katika uwanda mkubwa ambao Yesu alikuwa ameuweka tayari kwa ajili yake.— Spiritual Gifts 1:213. [TA 289.2; UM Aya ya 18]

Sasa Shetani anajitayarisha kwa pambano kuu la mwisho kwa ajili ya ukuu. Wakati amenyimwa uwezo wake, na kukatiliwa mbali na kazi yake ya udanganyifu, mkuu huyu wa uovu alikuwa na hali mbaya, huzuni, uharibifu na; lakini waovu wanapofufuliwa, na anaona umati mkubwa wa watu ubavuni mwake, matumaini yake yanafufuka, na anaamua kutoacha pambano kuu ..Waovu ni mateka wa Shetani...Wako tayari kupokea mapendekezo yake na

kutimiza matakwa yake. Walakini, kulingana na ujanja wake wa awali, hajikiri kuwa yeye ni Shetani. Anadai kuwa yeye ni mkuu ambaye ndiye mmiliki halali wa ulimwengu, na urithi wake amepokonywa kutoka kwake kinyume cha sheria. Anajiwakilisha mwenyewe kwa raia wake waliodanganyika kama mkombozi, akiwahakikishia kwamba ni uweza wake ndiyo amewatoa makaburini mwao (amewafufua), na kwamba yuko karibu kuwaokoa kutoka katika utawala wa kikatili zaidi...Anapendekeza kuwaongoza dhidi ya kambi ya watakatifu, na kuuteka Mji wa MUNGU.... [TA 289.3; UM Aya ya 19]

Katika umati huo mkubwa kuna watu wengi wa kizazi cha watu walioishi muda mrefu waliokuwepo kabla ya Gharika (antedeluvian) ......kuna jemadari walioshinda mataifa, watu mashujaa ambao hawakushindwa vitani, Shetani anashauriana pamoja na malaika zake, na kisha pamoja na wafalme hawa na washindaji na watu wenye nguvu. Wanatathimini nguvu na hesabu ya upande wao, na kutangaza kwamba jeshi lililoko ndani ya mji ni dogo kwa kulinganisha na wao na kwamba wanaweza kushinda. Wanaweka mikakati yao ya kiumiliki utajiri na utukufu wa Yerusalemu Mpya. Wote huanza mara moja kujiandaa kwa vita. Mafundi stadi wanatengeneza zana za vita. Viongozi wa kijeshi, wanaosifika kwa mafanikio yao, wanaongoza umati wa watu wapenda vita katika vikosi na migawanyiko mbalimbali. [TA 290.1; UM Aya ya 20]

Hatimaye agizo la kusonga mbele linatolewa, na wapiganaji wasiohesabika wanasonga mbele Shetani, shujaa hodari zaidi, anaongoza msafara wa vita, na malaika zake wanaunganisha nguvu zao kwa ajili ya mgogoro na pambano hili la mwisho.— The Great Controversy, 663, 664. [TA 290.2; UM Aya ya 21]

Sasa Kristo tena anaonekana mbele ya adui Zake. Juu sana ya mji, juu ya msingi ya dhahabu iliyosuguliwa, kuna kiti cha enzi, kirefu na kuinuliwa sana. Juu ya kiti hiki cha enzi ameketi Mwana wa Mungu, na raia wa ufalme Wake wamemzunguka.— The Great Controversy, 665. [TA 291.1; UM Aya ya 22]

Mbele ya wakazi wa duniani na wa mbinguni, wanakusanyika ili kutawazwa kwa mwisho kwa Mwana wa Mungu kufanyike. [TA 291.2; UM Aya ya 23]

Shetani ameona taji ikiwekwa juu ya kichwa cha Kristo na malaika wa kimo kilichoinuka na uwepo wa fahari, naye anajua kuwa hicho cheo cha juu cha malaika huyo kingeweza kuwa chake.— The Great Controversy, 666, 669. [TA 291.3; UM Aya ya 24]

### Hukumu ya Mwisho

Sasa, akiwa amekabidhiwa ukuu na mamlaka ya juu kabisa, Mfalme wa wafalme anatangaza hukumu juu ya waasi dhidi ya serikali Yake, na anatekeleza haki juu ya wale walioivunja Sheria Yake na kuwatesa watu Wake. [TA 291.4; UM Aya ya 25]

Mara tu vitabu vya kumbukumbu vinapofunguliwa, na jicho la Yesu kuwatazama waovu, wanapata ufahamu wa kila dhambi waliyowahi kuifanya katika maisha yao. Wanaona mahali ambapo miguu yao iliteleza na kuondoka katika njia ya usafi na utakatifu, jinsi kiburi na uasi vilivyowapeleka mbali katika uvunjaji wa sheria ya Mungu...[TA 291.5; UM Aya ya 26]

Juu ya kiti cha enzi unafunuliwa msalaba; na kama onesho la filamu kunaonekana matukio ya majaribu na kuanguka kwa Adamu, na mfululizo wa hatua katika mpango mkuu wa ukombozi. Kuzaliwa katika hali duni kwa Mwokozi; Maisha Yake ya awali ya usahili na utiifu; Ubatizo Wake katika Yordani; ...Huduma Yake ya umma/hadhara; ... kusalitiwa Kwake...; Mwana wa Mungu kwa kushangiliwa akioneshwa mbele ya Anasi, akahukumiwa katika jumba la kuhani mkuu, jumba la hukumu la Pilato, mbele ya Herode mwoga msaliti na katili ...— vyote vinaoneshwa kwa uwazi. [TA 291.6; UM Aya ya 27]

Na sasa mbele ya umati unaomanganga kwa kutokuwa na msimamo unafunuliwa katika mandhari za mwisho (pale msalabani)—Mtesekaji mvumilivu akiikanyaga njia ya kwenda Kalvari; Mfalme wa mbinguni akining'inia juu ya msalaba. [TA 292.1; UM Aya ya 28]

Tukio la kutisha linaonekana kama lilivyokuwa. Shetani, malaika zake, na wafuasi wake hawana uwezo wa kugeuka ili wasiione picha ya kazi yao wenyewe. Kila mhusika anakumbuka sehemu aliyofanya.—The Great Controversy, 666, 667. [TA 292.2; UM Aya ya 29]

Wakati utakuja ambapo wote lazima wasimame mbele ya malaika na mbele ya watu, wakifunuliwa katika nuru yao ya Kweli. Kama vile msanii anavyoweka katika kibao au sahani iliyonakshiwa sifa za sura ya binadamu, ndivyo tabia zao zinavyohamishiwa kwenye vitabu vya mbinguni Katika hukumu kila mtu atasimama akifunuliwa jinsi alivyo, ama ameumbwa kulingana na mfano wa kimbingu au kuharibiwa na dhambi za kuabudu sanamu na ubinafsi na choyo.— Manuscript Releases 17:288. [TA 292.3; UM Aya ya 30]

Katika siku ambayo kila mtu atalipwa sawa na kazi yake ilivyokuwa, wakosaji wataonekanaje machoni pao wenyewe kama kwa muda mchache wataruhusiwa kuona kumbukumbu ya maisha yao kama walivyoamua kuyaishi.. [TA 292.4; UM Aya ya 31]

Katika siku ya hukumu watu wataona vile ambavyo wangeweza kuwa kwa uwezo wa Kristo. Wao Waliyajua madai ya Mungu, lakini walikataa kuyafuata masharti yaliyowekwa ndani ya Neno Lake. Kwa uchaguzi wao wenyewe waliungana na mapepo... [TA 292.5; UM Aya ya 32]

Katika siku ya hukumu, haya yote yanafunuliwa mbele ya wale wasiotubu. Tukio baada ya tukio linapita mbele yao. Kwa uwazi kama katika mwanga wa jua la mchana, wote wanaona vile ambavyo wangekuwa kama wangeshirikiana

na Mungu badala ya kumpinga Yeye. Picha haiwezi kubadilishwa. Kesi zao zimeamuliwa milele... [TA 293.1; UM Aya ya 33]

Na malaika walioanguka, waliopewa akili ya juu kuliko mwanadamu, watatambua wamefanya nini katika kutumia mamlaka yao kuongoza wanadamu kuchagua udanganyifu na uwongo kutoka kwenye ushawishi wao.—The Upward Look, 203. [TA 293.2; UM Aya ya 34]

Lakini wakati umekuja ambapo uasi huo hatimaye utashindwa na historia na tabia ya Shetani kufichuliwa. Katika juhudi zake za mwisho za kumwondoa Kristo madarakani, kuwaangamiza watu Wake, na kuumiliki mji wa Mungu, mdanganyifu mkuu ameondolewa barakoa yake kikamilifu. Wale ambao wameungana naye wanaona kushindwa/kufeli kabisa kwa kusudi lake. Wafuasi wa Kristo na malaika watakatifu huona kiwango chake kamili cha hila dhidi ya serikali ya Mungu. Yeye ndiye mlengwa wa chukizo la ulimwengu wote... [TA 293.3; UM Aya ya 35]

Shetani aona kwamba uasi wake wa hiari/makusudi ulimwondoa mbinguni Mashtaka yake dhidi ya rehema na haki ya Mungu sasa yamenyamazishwa. Aibu ambayo amejaribu kuitupa juu ya Yehova inakaa juu yake mwenyewe. Na sasa Shetani anainama chini, na kukiri haki ya hukumu yake. Kila swali la Ukweli na kosa katika pambano la muda mrefu sasa limewekwa wazi... [TA 293.4; UM Aya ya 36]

Ingawa Shetani analazimika kukiri haki ya Mungu, na kusujudu ukuu wa Kristo, tabia yake inabaki isiyobadilika. Roho ya uasi, kama kijito chenye nguvu, inaibuka tena. Akiwa amejawa na wasiwasi, anaamua kutokubali kushindwa pambano kuu. Wakati umefika wa mapambano ya mwisho dhidi ya Mfalme wa mbinguni. Anakimbilia katikati ya raia wake, na anajaribu kuwatia moyo kwa ghadhabu yake mwenyewe, na kuwaamsha kwa vita vya papo hapo. Lakini kati ya mamilioni yote yasiyohesabika ambayo amewavutia katika uasi, hakuna hata mmoja sasa ambaye anayetambua ukuu wake. Nguvu zake ziko mwishoni. Hasira yao inawaka dhidi ya Shetani na wale ambao wamekuwa mawakala wake katika udanganyifu, na kwa hasira ya pepo wanawageukia... [TA 293.5; UM Aya ya 37]

Moto washuka kutoka kwa Mungu mbinguni. Dunia yavunjika....Miali ya moto yalipuka kutoka katika kila mpenyo wa ardhi...Siku imekuja ambayo inawaka kama tanuru. Vitu vya asili vinayeyuka kwa joto kali, dunia pia, na kazi zote zilizomo ndani yake zitaunguzwa. Malaki 4:1; 2 Petro 3:10. Uso wa dunia waonekana kama donge moja kubwa lililoyeyuka—ziwa kubwa la moto... [TA 294.1; UM Aya ya 38]

Waovu wanapokea malipo yao Wengine wanaangamizwa kama kwa nukta moja tu, huku wengine wanateseka kwa siku nyingi. Wote wanaadhibiwa "kulingana na matendo yao." Dhambi za wenye haki zimekuwa zikihamishwa

kwa Shetani, hivyo anateswa si kwa ajili ya uasi wake tu, bali kwa ajili ya dhambi zote ambazo amesababisha watu wa Mungu kuzitenda. Adhabu yake ni kubwa zaidi kuliko ya wale ambao amewadanganya. Baada ya wote wale walioanguka kwa udanganyifu wake na kuangamia, yeye ataendelea kuishi na kuteseka zaidi. Katika miali moto utakasao waovu hatimaye wanaangamizwa.— The Great Controversy, 670-673. [TA 294.2; UM Aya ya 39]

Kwa maisha ya uasi, Shetani na wote wanaoungana naye hujiweka wenyewe nje ya upatanifu na Mungu hivi kwamba uwepo Wake kwao ni moto ulao. Utukufu Wake Yeye aliye Upendo utawaharibu.— The Desire of Ages, 764. [TA 295.1; UM Aya ya 40]

Malimwengu yote yatakuwa mashahidi wa asili na matokeo ya dhambi. Na ukatili wake mkubwa, ambao hapo mwanzo ulileta hofu kwa malaika na fedheha kwa Mungu, sasa utathibitisha upendo Wake na kuweka heshima Yake mbele ya ulimwengu wa viumbe wanaopendezwa kufanya mapenzi Yake, na ambao mioyoni mwao mna sheria Yake.— Great Controversy, 504. [TA 295.2; UM Aya ya 41]

Moto unaowateketeza waovu huisafisha dunia. Kila kielelezo cha laana kinafagiliwa mbali. Hakuna jehanamu iwakayo milele itakayohifadhi mbele ya waliokombolewa matokeo ya kutisha ya dhambi. [TA 295.3; UM Aya ya 42]

Kumbukumbu moja pekee itasalia: Mkombozi wetu atabaki na alama za kusulubishwa Kwake. Juu ya kichwa Chake kilichojeruhiwa, ubavuni Mwake, Mikono na miguu Yake, ndizo alama pekee zilizobakia, za kazi ya kikatili ambayo dhambi ilisababisha.- The Great Controversy, 674. [TA 295.4; UM Aya ya 43]

Dhambi ni siri na fumbo lisiloweza kuelezeka. Hakukuwa na sababu ya uwepo Wake; kutafuta kuielezea ni kutafuta kuitolea udhuru, na hiyo itakuwa ni kuihalalisha. Dhambi ilionekana katika ulimwengu (mbinguni na dunia yetu) mkamilifu, jambo ambalo lilionyeshwa kuwa haina udhuru na uovu huo basi umepitiliza kiasi. Sababu ya kutokea kwake au maendeleo yake hazikuelezwa kamwe na kamwe pia hazitaweza kuelezwa, hata katika siku kuu ya mwisho wakati hukumu itakapoketi na vitabu vitakapofunguliwa Siku hiyo itadhihirika kwa wote, kuwa kamwe hakukuwa na sababu yoyote ya dhambi kuwepo. Katika hukumu ya mwisho ya Shetani na malaika zake na ya watu wote ambao hatimaye wamejitambulisha wao wenyewe kuwa pamoja naye kama wavunjaji wa sheria ya Mungu, kila kinywa kitanyamazishwa. Wakati majeshi ya uasi, kutoka kwa mwasi mkuu wa kwanza hadi mkosaji wa mwisho, watakapoulizwa kwa nini wamevunja sheria ya Mungu, watakuwa hawana cha kusema, watanyamaza tuli. Hakutakuwa na jibu la kutoa, wala sababu ya kutoa ambayo itabeba uzito.-The Signs of the Times, April 28, 1890. [TA 295.5; UM Aya ya 44]

Wakazi wa ulimwengu wote watasadikishwa juu ya uadilifu wa sheria katika kuangusha uasi na uondoaji wa dhambi. Utekelezaji wa mpango wa wokovu haudhihirishi tu kwa wanadamu bali kwa malaika, tabia ya Mungu, na katika nyakati za milele, tabia ya kutisha ya dhambi itaeleweka kwa gharama ya Baba na Mwana ya ukombozi wa jamii ya waasi. Katika Kristo, Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, walimwengu wote wataona alama za laana, na malaika na wanadamu pia watatoa heshima na utukufu kwa Mkombozi ambaye kupitia Kwake wote wamewekwa salama dhidi ya uasi. [TA 296.1; UM Aya ya 45]

Ufanisi wa msalaba hulinda jamii ya waliokombolewa kutoka katika hatari ya anguko la pili. Uhai na kifo cha Kristohufichua kwa ufanisi udanganyifu wa Shetani, na kukanusha madai yake. Dhabihu ya Kristo kwa ajili ya ulimwengu ulioanguka huwavuta si wanadamu tu, bali malaika Kwake. katika vifungo vya muungano usioweza kufutwa. Kupitia mpango wa wokovu haki na rehema ya Mungu imethibitishwa kikamilifu, milele na hata milele uasi hautatokea tena milele, kamwetaabu haitaugusa tena ulimwengu wa Mungu.—The Messenger, June 7, 1893. [TA 296.2; UM Aya ya 46]

### Dunia kufanywa upya

Mungu atapoitakasa dunia hatimaye itaonekana kama ziwa la moto. Kama alivyoihifadhi katikakati ya Gharika, kwa sababu ilikuwa na watu wanane wenye haki, ataihifadhi Yerusalemu mpya, yenye waaminifu wa nyakati zote…..Ingawa dunia nzima isipokuwa hiyo sehemu ambapo jiji limetua itafunikwa katika bahari ya moto, lakini mji utahifadhiwa kama ilivyokuwa Safina, kwa muujiza wa uweza mkuu. Utasimama bila kudhurika katikakati ya vitu vya asili vinayoungua.— Spiritual Gifts 3:87. [TA 297.1; UM Aya ya 47]

### Dunia Mpya na Urithi Wetu wa Milele

Musa aliiona nchi imesafishwa kwa moto na kusafishwa kutoka katika kila mabaki ya dhambi, kila alama ya laana, na kukarabatiwa na kupewa watakatifu kuimiliki milele na milele.— Manuscript Releases 10:158. [TA 297.2; UM Aya ya 48]

Mpango wa ukombozi hautaeleweka kikamilifu, hata waliokombolewa watakapoona jinsi wanavyoonekana na kujua jinsi wanavyojulikana; lakini kupitia enzi za milele Ukweli mpya utaendelea kufunuliwa katika kustaajabisha na akili zenye furaha.— The Great Controversy, 651. [TA 297.3; UM Aya ya 49]

Katika mpango wa ukombozi kuna miinuko na vilindi ambavyo uzima wa milele wenyewe hauwezi kuvimaliza, maajabu ambayo malaika wanatamani kuyatazama. Waliokombolewa pekee, kati ya viumbe vyote vilivyoumbwa, ndiyo wana uzoefu unaojulikana wa mapambano halisi na dhambi; wamefanya kazi

pamoja na Kristo, na, kwa jinsi ile ambayo hata malaika wasingeweza kufanya, wameingia ndani ya ushirika wa mateso Yake; Malaika hawatakuwa na ushuhuda wa sayansi ya ukombozi—hakuna kitu ambacho kitakuwa na thamani kwa viumbe wasioanguka?—Education, 308. [TA 297.4; UM Aya ya 50]

Kuna siri katika mpango wa ukombozi ... ambayo malaika wa mbinguni wamepigwa bumbuazi kwa mshangao daima. Mtume Petro, akizungumzia mafunuo yaliyotolewa kwa manabii ya "mateso ya Kristo, na utukufu utakaofuata," asema kwamba hayo ni mambo ambayo "malaika hutamani kuyatazama."— Testimonies for the Church 5:702. [TA 298.1; UM Aya ya 51]

Umati uliokombolewa utazunguka ulimwengu hadi ulimwengu, na wakati wao mwingi utatumika katika kujifunza na kuchunguza siri za ukombozi. Na katika kipindi chote cha umilele, somo hili litaendelea kufunuliwa akilini mwao milele.— The Review and Herald, March 9, 1886. [TA 298.2; UM Aya ya 52]

Sayansi ya ukombozi ndiyo sayansi ya sayansi zote; ni sayansi ambayo huchunguzwa na malaika na viumbe wote wa ulimwengu usioanguka; sayansi ambayo inahusisha usikivu wa Bwana wetu na Mwokozi; Sayansi ambayo inaingia katika kusudi la Yule Asiye na ukomo...; Sayansi ambayo itakuwa ikichunguzwa na watu wa Mungu walikombolewa katika nyakati zote milele.—Education, 126. [TA 298.3; UM Aya ya 53]

Kusudi la kushangaza la Mungu la neema, siri ya upendo wa ukombozi, ndiyo mada ambayo "malaika hutamani kuitazama," na itakuwa ndiyo masomo yao katika enzi zote milele. Wote waliokombolewa na wale viumbe wasioanguka watapata katika msalaba wa Kristo Sayansi yao na Wimbo wao. Itaonekana kuwa utukufu unaong'aa katika uso wa Yesu, ni ule utukufu wa upendo wa kujitoa. Katika nuru kutoka Kalvari itaonekana kuwa sheria ya upendo wa kujinyima ni sheria ya uzima kwa nchi na mbingu; kwamba upendo "usiotafuta mambo yake" una chanzo chake katika moyo wa Mungu; na kwamba katika Yule Mmoja aliye mpole na mnyenyekevu anaiidhihirisha tabia yake Yeye akaaye katika nuru ambayo hapana mwanadamu anayeweza kuifikia.— The Desire of Ages, 19, 20. [TA 298.4; UM Aya ya 54]

Na miaka ya umilele, inavyoendelea, italeta mafunuo makubwa na yenye utukufu zaidi kumhusu Mungu na Kristo. Uelewa utakuwa endelevu, kadhalika upendo, kicho, na furaha vitaongezeka. Kwa kadiri watu wanavyojifunza zaidi juu ya Mungu, ndivyo wanavyozidi kuipenda tabia Yake. Yesu alipofungua mbele yao upana wa ukombozi, na mafanikio ya kushangaza katika pambano kuu dhidi ya Shetani, mioyo ya waliokombolewa ilizizima kwa furaha kwa kujiweka wakfu na kumpenda Yesu zaidi, na kwa shangwe tele wanapiga vinubi vyao vya dhahabu; na sauti elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu huungana kuimba kibwagizo cha sifa. [TA 299.1; UM Aya ya 55]

“Na kila kiumbe kilichoko mbinguni, na juu ya nchi chini, na juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake; nalivisikia vikisema, Baraka, na heshima, na utukufu, na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo hata milele na milele milele.” Ufunuo 5:13. [TA 299.2; UM Aya ya 56]

Pambano kuu limekwisha. Dhambi na wenye dhambi havipo tena. Ulimwengu wote ni safi. Mdundo wa muafaka na furaha hupiga kupitia uumbaji Wake wote. Kutoka kwa Yeye aliyeumba vyote, unabubujika uzima na nuru na furaha, katika maeneo yote na nafasi isiyo na kikomo. Kutoka kwa atomu ndogo sana hadi ulimwengu mkubwa sana, vitu vyote, vyenye uhai na visivyo na uhai, katika uzuri wao usio na kivuli na furaha kamilifu, vinakiri kuwa Mungu ni pendo.— The Great Controversy, 678. [TA 299.3; UM Aya ya 57]

**Hitimisho**

Mada ya ukombozi ni ile ambayo malaika wanatamani kuiangalia;itakuwa sayansi na wimbo wa waliokombolewa kote katika milele zote. Je, sio vema kuwa wimbo wa kufikiriwa kwa makini na kuujifunza sasa?— Bible Echo, January 1, 1888.

Mwanafunzi anapojifunza Biblia na kutafakari juu ya mada ambazo “malaika hutamani kutazama” (1 Petro 1:12), atakuwa na ushirika nao. Anaweza kufuata hatua za Mwalimu wa mbinguni, na kuyasikiza maneno Yake kama alipokuwa akifundisha mlimani na tambarare na baharini. Anaweza kukaa katika ulimwengu huu katika angahewa ya mbinguni, akiwapa watu wenye huzuni na majaribu mawazo ya tumaini na shauku ya utakatifu; akija karibu na karibu zaidi katika ushirika na Asiyeonekana; kama yule wa zamani aliyetembea na Mungu, akikaribia na kukaribia kizingiti cha ulimwengu wa milele, mpaka malango yatakapofunguka naye akaingia humo. Atajikuta mwenyewe si mgeni. Sauti zitakazomsalimu ni sauti za watakatifu, ambao, bila kuonekana, walikuwa marafiki zake duniani—sauti ambayo hapa alijifunza kuitambua na kuipenda. Yeye ambaye kupitia Neno la Mungu aliishi katika ushirika na mbinguni, atajikuta nyumbani katika ushirika wa mbinguni.—Education, 127.

Bwana angetaka akili zetu ziwe na shauku ya kuelewa kuwa hawa wenye nguvu wanaozuru ulimwengu wetu wana sehemu kubwa katika kazi zote ambazo tumeziita ni zetu. Viumbe hawa wa mbinguni ni malaika wahudumu, na mara nyingi huonekana katika umbo la kibinadamu. Kama wageni wanazungumza na hao ambao wanajishughulisha na kazi ya Mungu. Katika maeneo ya upweke wamekuwa marafiki wa msafiri katika hatari. Katika meli zinazopeperushwa na tufani malaika katika umbo la kibinadamu wamezungumza maneno ya kutia moyo kutuliza hofu na kuleta matumaini katika saa ya hatari, na abiria walidhani kwamba ni mmoja wao ambaye hawajawahi kamwe kuzungumza naye.— The Upward Look, 84.

Hebu tudumishe mioyo iliyojaa ahadi za Mungu zenye thamani, ili tuweze kusema maneno ambayo yatakuwa ya faraja na nguvu kwa wengine. Hivyo tunaweza kujifunza lugha ya malaika wa mbinguni, ambao, kama tukiwa waaminifu, watakuwa wenzetu katika umilele.— The Youth’s Instructor, January 10, 1901.

Katika maisha ya baadaye tutaelewa mambo ambayo hapa sana yanatuchanganya. Tutatambua msaidizi tuliokuwa nao walivyo na nguvu na jinsi gani Malaika wa Mungu walitumwa kutulinda tulipokuwa tukifuata shauri la Neno la Mungu.—In Heavenly Places, 257.

Kila aliyekombolewa ataelewa huduma ya malaika katia maisha yake mwenyewe. Malaika ambaye alikuwa mlinzi wake tangu wakati wake wa utoto; malaika aliyetazama hatua zake, na kufunika kichwa chake wakati wa hatari; malaika aliyekuwa pamoja naye katika bonde la uvuli wa mauti, ambaye aliashiria mahali pake pa kupumzika, ambaye alikuwa wa kwanza kumsalimia asubuhi ya ufufuo-itakuwaje kuzungumza naye, na kujifunza historia ya mwingiliano wa kiungu katika maisha ya mtu binafsi, ya ushirikiano wa mbinguni katika kila kazi kwa ajili ya wanadamu -Education, 305.

‘Eben-ezeri...Hata sasa Bwana ametusaidia’
1 Samweli 7:12